Ustaarabu Wa Watu wema

Othman Nuri TOPBASH

Istanbul – 2022

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

Ustaarabu wa watu wema - 1

Othman Nuri Topbash

Jina la Asili : Asr-ı Saadet'ten Günümüze Faziletler Medeniyeti - 1

Mwandishi : Othman Nuri Topbash

Msimamizi Mkuu : Abdi Mohamed Adam

Mfasiri : Hemedi Dhuli Hemedi

Mhariri : Ibrahimu H. Kabuga

Msanifu jalada : Sarkhan Isgandarov

Kupangiliwa vizuri na Sarkhan Isgandarov
Nijat Garibov

ISBN: 978-9944-83-713-2

Mchapaji: Erkam Printhouse

Anuani: Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi Mah.
Atatürk Bulvarı, Haseyad 1. Kısım
No: 60/3-C Başakşehir, Istanbul, Turkey

Simu: (+90-212) 671-0700 pbx
(+90-212) 671-0748

Barua pepe: info@islamicpublishing.org

Tovuti: www.islamicpublishing.org

Language : Swahili / Kiswahili

ERKAM PUBLICATIONS

Ustaarabu Wa Watu wema

- 1 -

Othman Nuri TOPBASH

ERKAM PUBLICATIONS

YALIYOMO

DIBAJI **7**

SEHEMU YA KWANZA

IMANI NA IBADA / 17

1. Kuishi kwa imani na upendo 19
2. Usafi wa moyo 46
3. Taqwa (Uchamungu na kumfahamu Mwenyezi Mungu) 63
4. Tawba na Istighfar 76
5. Kutii maamrisho ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake 88
6. Umakini katika ibada 103
    a. Ibada za ziada 116
    b. Kuswali katika jamaa 126
    c. Ibada za usiku 143
    d. Swala na Dua 156
    e. Unyenyekevu na utulivu (khushu) 177
7. Kuifahamu Qur'an tukufu 188
8. Dhikrullah na Swalawat-i Sharifa 205
9. Hofu na maandalizi ya kifo na maisha ya Akhera 223

DIBAJI

Sifa zote njema na utukufu ni wake Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ambaye amevipa thamani viumbe vyote hasa mwanadamu, na kumfanya afikie kilele cha ubora kwa kupitia Mtume Mtukufu, na ambaye kwa kuapa juu ya uhai wa tumaini hili la ulimwengu, amemfanya awe chanzo cha utu na heshima na kuubashiria umma wake bishara njema.

Amani ya milele na baraka ziwe juu ya kiongozi wa mitume, Mtume wetu Muhammad ﷺ, ambaye ni rehema kwa walimwengu wote na chanzo cha baraka. Mtume ambaye alikuwa ni mwenye tabia njema na aliyeonyesha mifano mingi ya tabia njema na ambaye alijaaliwa tabia za kipekee juu ya walimwengu wote.

Vitu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini ni kwa ajili ya mwanadamu. Hivyo hana budi kuishi kulingana na hadhi aliyopewa. Hili litafikiwa kwa yeye kuwa mwema na kumtumikia Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu. Utii na unyenyekevu utafikiwa kwa kuwa na tabia yenye kukubalika na kutukuzwa.

Mtume Muhammad ﷺ[1] anasema:

"Sikutumwa kwa sababu nyingine ila kukamilisha tabia njema." (Muwatta, Tabia Njema, 8)

Hivyo alionyesha misingi ya busara katika majukumu yake na alisisitiza umuhimu wa tabia njema. Tukiangalia maisha yote ya

1. ﷺ katika kiarabu ni kifupi cha "*sallallahu alayhi wa sallam*" na tafsiri yake ni "rehema na amani ziwe juu yake". Linasemwa pale jina la Mtume linapotajwa. (Maelezo ya mfasiri).

Mtume tutaona kuwa ni mfano wa maadili ya hali ya juu, sifa na tabia njema .

Mwenyezi Mungu Mtukufu analithibitisha hili kwa kusema:

"Na hakika wewe una tabia tukufu" (Al-Qalam, 68:4)

Hivyo Mtume alikuwa si mwalimu wa kufundisha Qur'an kwa maneno tu. Badala yake alitekeleza kila alichokifundisha na hivyo alikuwa ni mfano halisi wa Qur'an na kiongozi mzuri ambaye alifundisha ukweli wa Mwenyezi Mungu kwa njia ya matendo yake. Hii ndiyo sababu iliyopelekea maisha yake kuwa mfano bora kwa vizazi vijavyo mpaka siku ya malipo.

Kwa kuja kwake Mtume, nuru ya kuumbwa kwake ilifunika viza vya dunia, asubuhi mpya ya neema iliyokuwa ikisubiriwa na watu iliwadia, nyoyo ziliangazwa na utambuzi ukaenea. Kwa ufupi yeye ndiye aliyewezesha wanadamu kuchunga utu wao, heshima, ukweli, haki na maadili mema. Yeye ndiye aliyefundisha siri ya maisha ya hapa duniani na kesho Akhera.

Kwa sababu hakuna nabii mwingine atakayekuja mpaka siku ya Malipo, hakuna uzuri na wema wowote ila mwanadamu anauhitaji, na vyote hivi vimewekwa juu yake. Kutokana na sababu hizi yeye ndiye kilele cha wema.

Hivyo:

Yeye ni kilele cha upendo. Yeye ni kilele cha matumaini. Yeye ni kilele cha subira na uvumilivu. Yeye ni kilele cha ukarimu, kujitolea kwa ajili ya wengine na kuweka wengine mbele. Yeye ndiye kilele cha kijizuilia na maovu, msimamo, kuridhika na unyenyekevu licha ya kuwa neema kubwa kubwa za kidunia zilikuwa mbele yake. Yeye ni kilele cha huruma na kuwasaidia wahitaji. Yeye ni kilele cha ukweli na uchamungu. Yeye ni kilele cha kupata radhi za Mwenyezi Mungu na yeye ni kilele cha shukrani. Yeye ni kilele cha ufahamu juu ya Mwenyezi Mungu, na hekima, neema na

fadhila. Yeye ni kiongozi wa manabii. Yeye ni kilele cha mafundisho na elimu ya adabu na tabia njema. Yeye ni kiongozi wa madaktari wa mioyo iliyojeruhiwa. Yeye ni kilele cha uadilifu na uaminifu. Yeye yuko juu ya marafiki wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake. Yeye ni kiongozi wa watu wote siku ya malipo. Yeye ni mwombezi wa wakosaji. Yeye ni kilele cha kila aina ya fadhila na tabia njema na huduma. Kwa maneno mengine, ni yeye pekee ambaye anaweza kuwa katika nafasi ya juu ya utumishi.

Kila sifa, tabia na maadili ambayo Mwenyezi Mungu anayaridhia vimeletwa kwa mwanadamu kwa kupitia ulimi uliobarikiwa wa Mtume. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameonyesha mfano wa 'mwanadamu kamili' kwa kupitia kwa Mtume. Hiki ndicho alichokusudia katika Uislamu ndiyo maana akamfanya Mtume awe mfano wa kuigwa na wanadamu wote.

Tofauti na hili wale wanafalsafa ambao akili zao hazijapata ufunuo na mawazo hasi au chanya kuhusu amani na utulivu katika jamii wameachwa katika safu zenye vumbi ndani ya maktaba. Na maisha ya wale walioyatumia mawazo yao yamekuwa mafupi. Hawa wanafalsafa hawakuweza kwa kiwango chochote kufanyia kazi yale waliyoyafundisha na kuonyesha mfano kwa watu wengine. Mawazo yao yamebakia kuwa nadharia tu.

Kwa mfano Aristotle amesimamisha misingi ya baadhi ya sheria na kanuni za falsafa ya maadili, lakini haya yaliondolewa katika ufunuo wa Mungu. Hivyo hatuwezi kuona hata mtu mmoja ambaye hii falsafa inatumika katika maisha yake binafsi na kupata furaha. Hata kitabu muhimu cha Farabi, ambacho kinabeba mawazo yake ya kufikirika kwenye mji wa watu wema na jamii kwa ujumla hayakupata nafasi ya kutumika na hata kujitokeza katika mistari ya vitabu. Kwa sababu ukweli huu haukuwa umeandikwa wala kusemwa kutokana na uzoefu, na wala hazikutumika baada ya kuwa zimeandikwa.

Mtume alikuwa amependwa na kila mtu hata kabla ya wajibu wake wa unabii kuanza na alikuwa na utu wa hali ya juu kiasi kwamba watu wakasema "Wewe ni mwenye kuaminika na muaminifu". Hivyo akaanza wajibu wake wa kuhubiri baada ya uthibitisho huu wa wazi wa utambulisho wake na tabia yake.

Na hivyo ni kwa kupitia tabia yake njema na mafunzo ya kiroho yaliyosababisha karne na vizazi kujitengeneza kimaadili, na kwa wanadamu ilikuwa imewafikia ' enzi ya neema'. Moja ya majina muhimu katika mbinu za sheria za kiislamu ni Karafi (toleo 684), yeye ana yafuatayo ya kusema:

"Kama Mtume wa Mwenyezi Mungu angelikuwa hana muujiza mwingine, kizazi cha maswahaba watukufu kingetosha kuthibitisha kuwa yeye alikuwa mtume".

Dhati ya Mtume, maneno yake na kila hali yake kuanzia mwanzo mpaka mwisho, ni mambo yenye kuonyesha uzuri wa tabia yake ambayo imejificha ndani ya Quran Tukufu. Mifano kamili ya tabia njema ilionekana katika maisha yake.

Aliye juu ya viumbe vya Mwenyezi Mungu ni mwanadamu. Na kilele cha ukamilifu wa imani miongoni mwa viumbe vyake ni Mtume mtukufu. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu ameweka kuwa baada ya utii kwake unafuatia utii kwa Mtume, na kumuasi Mtume ni sawa na kumuasi Mwenyezi Mungu.

Ndani ya Quran tukufu tunaelezwa:

"Sema:Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu" (Al'i Imran, 3:31)

Pia kumtukuza Mtume kunaruhusiwa hali ya kuwa hutovuka mipaka kwa kufikia kwenye *shirk* au kumfanyia Mwenyezi Mungu

wasaidizi. Si hivyo tu bali kumsifu kwetu hakuna budi kuishia kwenye upeo wetu wa kumtambua.

Aliye juu katika orodha ya wale wanaomtambua Mtume kwa kiwango cha juu ni maswahaba wake. Ni wao ambao wamepelekea vizazi vilivyofuatia kumjua Mtume. Ni hawa maswahaba waliobarikiwa ambao wamepelekea vizazi baada ya Mtume kujua namna sahihi ya kufanya ibada, mahusiano ya kijamii na mambo mengine ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Walipata heshima kwa kuongea naye. Mtume mtukufu aliwafananisha 'kama nyota mbinguni'.

Kwa sababu maswahaba walipokea na kuiga tabia za Mtume wa Mwenyezi Mungu walielewa kuwa utajiri wa kweli wa mtu ulisababishwa na kiwango cha amali njema alizozitanguliza kwa ajili ya kesho Akhera. Hivyo waliweza kuonyesha wema wa kipekee kama vile ukarimu, kuwafikiria wengine na kujitolea kwa lengo la kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Waliendesha maisha yao kwa kutarajia radhi za Mwenyezi Mungu, hivyo waliishi kwa huruma na unyenyekevu na kupelekea kufikia kilele cha haki.

Katika nyakati zenye kuvutia na kuleta maana ni wakati maswahaba wanasambaza ujumbe wa umoja wa Mwenyezi Mungu kwa wanadamu kwa shauku kubwa.

Baada ya kizazi cha maswahaba, *awliyaullah* (marafiki wa Mwenyezi Mungu) wote ambao wataendelea mpaka siku ya mwisho na ambao wamefuata kikamilifu misingi yao ya maadili watatukuka kutokana na baraka zitokazo kwenye nuru ya wema ambayo ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Uzuri ulioje namna Jalaladdin Rumi alivyoelezea hali hii:

"Njoo ewe moyo! Sherehe ya kweli ni ya kuungana na Mtume aliyebarikiwa. Kwani kuelimika kwa dunia kumekuja kutoka kwenye nuru ya uzuri wa mtu huyo aliyebarikiwa".

Wanazuoni na wenye elimu ambao ni marafiki wa Mwenyezi Mungu na ambao wamepata heshima ya kuwa ni warithi wa Mitume wana nafasi ya juu katika uongozi wa kinabii na tabia njema katika umri wao wote, ndiyo maana nao pia ni viongozi wema kwa umma wote uliobaki ambao haukupata heshima ya kumuona Mtume na maswahaba wake.

Kwa kifupi bila ya shaka yoyote Mitume inaonyesha mifano ya wema ambayo inaupa moyo uhai, na tunamkuta Mtume Muhammad ﷺ kama kiongozi wao. Baada yao zinafuatia safu za wanavyuoni wema, waja wema, wenye elimu, wapenzi na kadhalika kulingana na namna walivyoshikamana nao. Wao ni watu wakubwa kwa sababu ya kuishi kwao katika maisha ya wema na kumtumikia Mwenyezi Mungu. Waliishi maisha ya wema ambayo yalibakia katika kumbukumbu za watu waliowazunguka ambazo hazitafutika kamwe. Kwa njia hii wameunda 'Ustaarabu wa watu wema'. Visa vya maadili ambayo yanatoka kwao vinatoa utulivu wa moyo na vinahuisha nyoyo zenye maradhi.

Imepelekea Abu Hanifa kusema yafuatayo juu ya kutaja visa vinavyohusu watu wema vinavyosimuliwa ndani ya Qur'an:

"Visa ambavyo vinaelezea uzuri wa watu wema vinanivutia zaidi kuliko vile vya sheria. Kwa sababu visa hivi vinatufundisha desturi na tabia za wale walio karibu na Mwenyezi Mungu".

Ni kweli kwamba mtu hawezi kuelewa vizuri jambo bila kupewa mfano. Mazuri na mabaya yanabainishwa wazi kwa mifano. Mapenzi yanakuwa hai zaidi na kuongezeka kwa kupitia mifano. Mtu kushikamana na tabia za kipenzi chake kutaonekana kwa kupitia mifano mizuri wanayoionyesha. Kwa kuzingatia haya mifano mizuri ni fadhila inayompelekea mtu kufikia utu na heshima ya kweli.

Katika haya, Malik bin Dinar anasema yafuatayo:

"Visa vizuri vya watu wema ni kama zawadi zitokazo mbinguni"

Matokeo yake kila kisa cha mtu mwema ni kama lulu ya bure tuliyopewa kama zawadi. Kwa kifupi ni muhimu kujenga tabia nzuri na maadili mema. Kwa kumalizia haya Mtume ﷺ ana haya ya kusema:

"Siku ya kiama hakuna kitakachokuwa na uzito zaidi ya tabia njema. Mwenyezi Mungu hapendezwi na watu wanaofanya matendo mabaya na kusema maneno mabaya". (Tirmidhi, Birr, 62/2002)

Bila shaka tabia njema inapatikana kwa kujenga urafiki na Mtume mtukufu na waja wema ambao walifuata nyayo zake. Hili ni sharti la kwanza ili kuingia katika msururu wa watu wema. Tabia mbaya zinasababishwa na kupoteza urafiki nao na kujiharibu mwenyewe kwa ujinga. Kwa kuzingatia ukweli huu, Mwenyezi Mungu mtukufu ana haya ya kusema katika *hadith Qudsi* [2] :

"Nimetangaza vita dhidi ya wale wanaofanya uadui na marafiki zangu(ambao wananitumikia kikweli kweli). Mja wangu anajikurubisha kwangu si kwa kingine bali kwa kutekeleza mambo ya faradhi kwake, kisha anajikurubisha kwangu zaidi kwa kutekeleza mambo ya sunna mpaka ninampenda;na nikimpenda nakuwa ni kusikia kwake pale anaposikiliza, kuona kwake kwa kile anachokiangalia, mkono wake ambao anapigia, mguu wake anaotembelea, ikapelekea kwa ajili Yangu anasikia, kwa ajili yangu anaona, kwa ajili yangu anapiga na kwa ajili yangu anatembea. Hatoniomba jambo lolote ila nitampa, Hatoniomba ulinzi ila nitamlinda. Kamwe sisiti[3] *kufanya jambo lolote zaidi ya ninavyosita kutoa roho*

2. Hadith qudsi ni hadith ambayo maneno yake yanatoka kwa Mtume lakini maana yake ama ameshushiwa au amefunuliwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. (Maelezo ya mfasiri).
3. Mwenyezi Mtukufu yuko juu ya tabia za kibinadamu kama vile kusita kufanya jambo. Kifungu hiki kimetumika hapa ili kuonyesha namna

ya mja wangu muumini; hapendi kifo na Mimi sipendi kumuudhi…"
(Angalia Bukhari, Rikak, 38; Ahmad, VI, 256; Haythami, II, 248).

Ili sisi tufikie wema wa hali ya juu ambao utatufanya tukubalike kwa Mwenyezi Mungu hatuna budi tuwapende marafiki wa Mwenyezi Mungu na Mtume mtukufu ﷺ ambaye wamemfuata, na ni yeye tu wa kufuatwa.

Kwa sababu hii inatarajiwa kuwa kadri tunavyofungamana na Mtume ﷺ na kumfanya mfano wa tabia njema ambazo zimesifiwa na Mwenyezi Mungu tutakuwa na heshima ya kuwa miongoni mwa wale waliobashiriwa bishara njema na Mtume.

Kama tutamtambua yeye leo, Yeye ﷺ atatutambua katika mkusanyiko mkubwa wa kesho kiama. Ikifikia hatua tunamuona yeye kikweli naye atatuona. Kama tunamsikiliza na kufanya yale aliyotuagiza naye atasikia vilio vyetu na kutushika mkono. Kwa njia hii tutakuwa ni mfano wake mzuri kwa wengine. Huu ni wema wa hali ya juu.

❁

Kitabu hiki kimeandikwa ili kuonyesha kwa wastani mifano ya watu wema. Mifano iliyoainishwa inatoka kwanza kabisa kwa Mtume Muhammad ﷺ kutokana na wasifu wake mtukufu na kisha maswahaba wake, watakatifu, wanavyuoni na watu wema ambao ni kama vioo vinavyoakisi mfano wake mzuri.

Kwa kuongezea tu ni kwamba hatujakwamia kwenye mifano kutoka kwa Mtume wala wale marafiki wa Mwenyezi Mungu ambao wamepitia njia ya uchamungu pekee. Bali mara nyingi tumetoa mifano kutoka kwenye takwimu za kihistoria zilizotokana na matukio ya kisiasa na kijamii na mashujaa waliokuwa na wajibu

Mwenyezi Mungu anavyowajali na kuwasikiliza waja wake anaowapenda na kusaidia mwanadamu kuelewa vizuri zaidi.

kwa kidunia. Haya ni ili wale watakaojikuta katika mazingira hayo wapate watu wenye tabia njema ambao wanawahitaji.

Ili kufikisha vizuri ujumbe wa kiongozi wa maisha ya hapa duniani na kesho Akhera ﷺ, ambaye minyororo ya maadili inajikusanya kwake na ambaye wasifu wake mkubwa umesambaa kwa watu wengine wema, ni vigumu kwetu kuwafikia. Kwa namna yoyote ile tunajua kuwa hatuwezi kumuiga kwa ukamilifu. Lengo ni kuonja angalau tone kutoka kwenye bahari ya maarifa, ili kumkaribia kwa hatua chache, kufufua shauku na mapenzi yetu kwake, kuonyesha kujitoa kwa ajili yake, kukimbilia baraka zake nyingi na kukimbilia maombezi yake…

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutupa heshima sisi waja wake dhaifu kuwa miongoni mwa watu wa umma wa kipenzi chake Mtume ﷺ. Kwa kuelewa ukweli wa fadhila hii, njia pekee ya kuthamini mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kupongeza nafasi ya kuwa miongoni mwa marafiki zake ni kushikamana na mafundisho yake na kupenda warithi wake watakatifu na kuiga tabia yake kadri ya uwezo wetu.

Ndiyo sababu tunahitajika kujipamba na mapenzi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuwa watafutaji wa mafunzo ya tabia yake tukufu kama maswahaba na marafiki wa Mwenyezi Mungu walivyofanya. Lazima tupiganie kuiga uzuri wao katika maisha yetu, uzuri ambao hautafifia wala kupitwa na wakati, bila kujali ni karne ngapi zimepita. Hii ni zawadi ya kutoa ili kuthaminisha heshima na bahati ya kuwa mmoja katika umma wa Mwenye kuvuniwa na ulimwengu.

Ningependa kuwashukuru ndugu zangu katika taaluma, hasa Murat Kaya ambaye alichangia katika kuandaa kazi hii. Namuomba Mwenyezi Mungu azikubali juhudi zao kama sadaka yenye kuendelea.

Mwenyezi Mungu atupe maisha yaliyomulikwa na tabia njema na mifano ya maadili ambayo itatupelekea kupata radhi zake. Mwenyezi Mungu atujaalie tuwe rafiki wa karibu wa Mtume wake katika maisha ya dunia na kesho Akhera. Na atujaalie tupate maombezi yake makubwa siku ya kiama…

Amin...

Othman Nuuri Topbash

Mei 2006 - Uskudar

Sehemu ya 1

Imani na Ibada

1. Kuishi kwa imani na upendo

Imani ni nuru ya akili, kinoleo cha ufahamu na utulivu wa hisia ndani ya moyo. Kupita katika maisha haya mafupi ya dunia kwa furaha wakati wa kuelekea maisha ya milele itawezekana tu pale tutakapokuwa chini ya uongozi wa imani.

Viongozi wa imani ni mitume, vitabu vitakatifu na marafiki wa Mwenyezi Mungu ambao wameishi kulingana na hivyo viwili vya kwanza. Ni kwa neema ya imani tu ndiyo iliyowafanya Mitume, watakatifu na watu wema katika historia yote kuwa mifano hai ya mafanikio ya maadili mema.

Imani ni fadhila ya Mwenyezi Mungu; mitihani katika maisha ni kipimo cha imani ya mtu. Kuichunga imani kwa subira na unyenyekevu, mambo ambayo yanatarajiwa kutoka kwa muumini, ndiyo thamani ya kulipa zawadi hii tukufu. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anapenda waja wake walipe fadhila hii ili wapate utukufu na thamani halisi ya fadhila za imani aliyowapa.

"Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao [maisha] **na mali zao ili awalipe pepo".** (Tawba, 9:111).

Aya hii ni uthibitisho dhahiri wa ukweli huu.

Hivyo njia za kuimarisha imani ya mtu ni kwa yeye kujitolea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (uhai wake, mali, alivyovimiliki n. k) ili kupata fadhila zake.

Kwa kuyashinda magumu yote na tabu za mitihani ya maisha kwa kuridhika na kunyenyekea na kufuata njia ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni ishara muhimu kwa waumini.

Kila muumini hana budi kulipa fadhila kwa Mwenyezi Mungu aliye juu kwa neema ya imani. Kudhania umiliki au kutarajia malipo ya kitu ambacho hujalipa fadhila zake ni kupoteza muda.

Kuelekea kwenye kilele cha imani kunategemea matendo mema, kuishi kwa nia nzuri, kufanya ibada na tabia njema ambazo zinampendeza Mwenyezi Mungu. Ndiyo maana ndani ya Quran na *Ahadith*[4], imani na matendo mema vimekuwa vikitajwa pamoja. Kuishi kwa imani hakuwi kwa nadharia bali kwa ukweli uliozama ndani ya moyo na kuthibitishwa kwa tabia za mtu. Kuwaza na kutafakari juu ya mtiririko wa nguvu ya Mwenyezi Mungu katika ulimwengu ndani ya moyo ambao unafaa kwa ajili ya ibada, na inapelekea waumini kuonja ladha ya imani ya kweli na kudhihirisha wema katika maisha yao yote.

Imani iko juu ya namna zote za kuabudu, kwani kuabudu kunawezekana tu kwa kupitia imani. Kuabudu kunafanywa katika nyakati maalum. Swala pia ambayo ni nzito juu ya mambo yote mema ni faradhi yenye kufanywa mara tano kwa siku. Imani inahitajika wakati wote wa maisha ya mtu, ndiyo maana inatubidi kujiepusha na mitego yote ya madhambi ambayo yatapelekea nyoyo zetu kutokujali na kulinda imani zetu kwa matendo mema (ambayo ni kama silaha ya kiroho).

Tunu ya imani kwa muumini ni kubwa kuliko mali nyingine zote. Shetani ambaye ndani ya Quran ametangazwa kama adui yetu wa wazi, pamoja na wafuasi wake wanajaribu kuiiba tunu hiyo ya imani kutoka katika nyoyo za waumini kwa kutumia hila na

4. *Ahadith* ni wingi wa neno *hadith* linalomaanisha mkusanayiko wa maneno ya Mtume Muhammad ﷺ. (Maelezo ya mfasiri).

miito mbali mbali. Kwa msingi huu hatuna budi daima kuwa macho na kukumbatia imani zetu kwa upendo mkubwa na bidii. Lazima tupiganie kuzilinda zisitikiswe na hawa maadui kwa kufanya matendo mema.

Ili tunu yetu ya imani iakisi maelekezo ya Mwenyezi Mungu kana kwamba ni kioo kipya chenye kung'aa, tunahitaji *dhikrullah* (kumkumbuka Mwenyezi Mungu). *Dhikrullah* ni kama kushonea neno *'Allah'* katika nyoyo zetu kwa mapenzi na tamaa. Kwa njia hii kutu ya madhambi na machafu nyoyoni mwetu itafutwa na utaonja ladha ya imani ya kweli kwa kutosheka na kupata amani kamili.

Furaha inayotokana na imani ya wale waliobarikiwa na waja maalum ambao wamefikia ukomavu wa kiroho inapita raha na starehe zote za hapa duniani, cha zaidi ni kwamba maumivu yote na mahangaiko yote ya dunia hii yanapotea machoni mwao.

Sasa ngoja tuangalie mifano mingi ya subira, ustahamilifu, ujasiri, busara, kujitolea na matumaini yaliyoonyeshwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye alitufundisha imani yetu, na wale waja wema ambao huduma yao imefanikisha neema hii kutufikia:

Maeneo ya wema

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokuwa mtoto wa takriban miaka 12, mtawa aitwae Bahira alimuambia:

"Mtoto mpendwa, nakuuliza kwa jina la Lat na Uzza[5] unijibu".

Akamjibu: "Usiniulize jambo lolote kwa jina la Lat na Uzza. Naapa kwa jina Mwenyezi Mungu! Sichukii jambo lingine lolote zaidi ya ninavyochukia masanamu hayo mawili".

5. Lat na Uzza yalikuwa ndio masanamu makubwa pale Makka. (Maelezo ya mfasiri).

Hata katika umri huu mdogo Mtume alijiweka mbali na masanamu na imani potofu kwa imani ya asili iliyo ndani yake.

Azimio la kipekee na juhudi aliyoonyesha katika kuishi kwa imani na upendo, kuisambaza na kuifundisha kwa watu baada ya kuwa Mtume ni wazi kwa kila mtu.

Wachawi katika kipindi cha Firauni walikataa uungu wake, matokeo yake wakapata mateso makubwa. Hata hivyo waliweza kumpa changamoto kutokana na msukumo wa imani zao:

"Uonevu wako ni wa hapa duniani tu. Una uhuru wa kuhukumu na kufanya utakalo. Vyovyote iwavyo tutarejea kwa Mola wetu".

Kwa amri ya Firauni walikatwa mikono yao na miguu yao kwa kubadilishana. Kabla hawajatundikwa kwenye matawi ya mitende, walinyanyua mikono yao mbinguni wakionyesha udhalili. Kwa shauku kwamba wangalikuwa na udhaifu wa imani wakaomba:

" ... Ewe Mola Mlezi wetu! Tumiminie uvumilivu na utufishe hali ya kuwa ni Waislamu" (A'raf 7:126).

Hivyo walitafuta ulinzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na walikutana na Mola wao katika raha isiyo na mipaka kwa kufa mashahidi.

Wakristo wa mwanzo ambao walikuwa wanyenyekevu walihifadhi imani zao kati ya magego ya simba wa sarakasi na wao pia walionja ushahidi kwa mapenzi ya imani yao.

Kundi lingine lililo juu ya orodha ya mashujaa waliokuwa wakiishi kwa imani na upendo ni wale waumini waliochomwa moto wakiwa hai na 'watu wa ukhdud'. Myahudi aitwae Dhu Nawas, aliyekuwa mfalme wa Yemen katika karne ya nne baada ya Nabii Issa عليه السلام aliwalazimisha watu wa Najran, Wakristo waliofungamana na imani ya Mungu mmoja kubadili imani yao. Walipo-

kataa, wengi wao walichomwa moto wangali hai kwa kurushwa ndani ya mashimo ya moto. Inasimuliwa kuwa watu waliokufa kwa njia hii wanafikia elfu ishirini.

Waonevu hawa waliitwa 'watu wa mashimo' kutokana na mashimo (yaliyoitwa *'ukhdud'*) waliyoyachimba ili kuwachoma waumini. Lakini hawa waonevu ambao walijaribu kuharibu imani ambazo zimezama na kugota ndani ya nyoyo za waumini walishindwa na badala yake wakastahiki kisasi na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Hivyo walikamatwa na kuadhibiwa na kulaaniwa milele. Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Wameangamizwa watu wa mahandaki yenye moto wenye kuni nyingi" (Al-buruj, 85:4-5).

Swahaba wa kike aitwae Sumayya ﷺ[6] ambaye aliishi kwa imani na upendo katika zama za furaha, alibahatika kupewa cheo cha 'shahidi wa kike wa kwanza katika Uislamu'. Sumayya ﷺ alikuwa akiogopa hata ncha kali ya sindano. Hata hivyo baada ya kuonja raha ya imani alionyesha uvumilivu wa hali ya juu mbele ya vyuma vyekundu vya moto ambavyo washirikina[7] walimuweka juu yake kutokana na imani yake. Baada ya mateso haya makubwa, alifungwa mguu mmoja kwenye farasi mmoja na mwingine kwenye farasi wa pili, kisha akachanwa katikati kinyama, hivyo akawa shahidi kwa kupitia njia yenye maumivu makali. Mume wake pia aitwae Yasir alionyesha uvumilivu wa hali ya juu japokuwa alikuwa mzee na dhaifu. Yeye pia alionja ushahidi. Ikapelekea familia ya

6. ﷺ kifupi cha *radiyallahu anhu* (kwa wanaume) *anha* (kwa wanawake). Linamaanisha 'Mwenyezi Mungu awe radhi naye' na linatumika kama ishara ya heshima kwa maswahaba wa Mtume Muhammad ﷺ. (Maelezo ya mfasiri).

7. Katika kiarabu 'mushrik', mtu ambaye amefanya dhambi kubwa kuliko zote, inayoitwa 'shirk', ikimaanisha kumshirikisha Mwenyezi Mungu na wengine. Watu wengi wa Kiquraysh, ambalo ni kabila la Mtume Muhammad walikuwa washirikina. (Maelezo ya mfasiri).

Yasir (Mwenyezi Mungu awe radhi nayo) ni mashahidi wa kwanza katika Uislamu. Walilipa thamani ya imani yao kwa kuishi kwa imani na upendo.

❁

Hata pale damu ya Bilal ﷺ ilipomwagika kutoka katika mwili wake, damu ambayo ilikuwa kama mafuta yatokanayo na mateso mazito ya washirikina wenye hasira na unyama, aliendeleza kauli yake ya Umoja wa Mwenyezi Mungu:" *Ahad, Ahad, Ahad*: Mwenyezi Mungu ni mmoja, Mwenyezi Mungu ni mmoja, Mwenyezi Mungu ni mmoja". Kando ya maumivu na mateso, Bilal alikuwa akihisi raha ya kukutana na Mwenyezi Mungu akiwa ameonja furaha kubwa ya imani.

❁

Omar ﷺ katika Ukhalifa wake alimuuliza mmoja wa Waislamu wa mwanzo aitwae Habbab bin Arat ﷺ:

"Unaweza kutuelezea kidogo mateso uliyoyapata katika njia ya Mwenyezi Mungu".

Habbab akajibu:

"Ewe kiongozi wa waumini! Hebu angalia mgongo wangu".

Omar akastaajabu alipoangalia mgongo wake. Akasema:

"Sijapata kuona katika maisha yangu mgongo wa mwanadamu umeharibika kiasi hicho".

Habbab akaendelea:

"Makafiri walikuwa wakiwasha moto na kuniweka humo nikiwa uchi. Moto ulizimwa na mafuta yaliyoyeyuka na kuvuja kutoka mwilini mwangu".

Washirikina walikuwa wakiweka mawe yaliyochomwa kwenye mgongo wa Habbab na kusababisha ngozi ya swahaba huyu

aliyebarikiwa kubanduka kutokana na uzito wa mateso haya. Licha ya haya alikataa kusema maneno waliyoyataka makafiri. Haya ni kwa sababu furaha ya kukutana na Mwenyezi Mungu ambayo imetokana na imani yake inafutilia mbali mahangaiko ya dunia.

Habbab bin Arat anasimulia:

Siku moja wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu akiwa katika kivuli cha Ka'bah tulienda kwake na kulalamika juu ya mateso tunayoyapata kutoka katika mikono ya washirikina. Baada ya hayo tulimtaka kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu ili kutuokoa kutokana na mateso haya. Mtume ﷺ akajibu:

"Miongoni mwa vizazi kabla yenu kulikuwa na waumini ambao walichomwa na kutupwa ndani ya mashimo ya moto na kisha wakakatwa na msumeno vipande viwili kutoka kichwani hadi kwenye kidole gumba, waumini ambao nyama yao ilichanwa kwa vitana vya chuma lakini hawakuipa mgongo imani yao. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwa atakamilisha dini hii kiasi cha mtu kusafiri kutoka San'a mpaka Hadramat bila kumuogopa yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu na kuogopa kondoo wake kushambuliwa na mbwa mwitu. Kwa hayo tu bado hamna uvumilivu…" (Bukhari, Manakibu'l Ansar 29, Manakib 25, Ikrah 1; Abu Dawud, Jihad 97/2649)

❁

Maadui wa Uislamu walikuwa wakimpiga Suhayb رضي الله عنه mpaka anazimia. Mateso haya yaliendelea mpaka alipohamia Madina. Matokeo yake Suhayb aliweza kuanza safari yake kwa lengo la kuhamia Madina baada ya Mtume kuhamia. Baadhi ya watu wa Makka walimfuata na walipomfikia walisema:

"Ulikuja hapa ukiwa mtu masikini na dhaifu. Ukapata utajiri mkubwa kuliko sisi. Na sasa unaondoka na utajiri wako? Kwa jina la Mwenyezi Mungu hatuwezi kukuruhusu!

Suhayb akashuka upesi juu ya mnyama wake na huku akitoa mishale kwenye podo lake akawaambia:

"Enyi Makuraishi! Mnajua mimi ni mpiga mishale bora kati yenu. Kwa jina la Mwenyezi Mungu nitatumia mishale yangu yote niliyonayo na kama ikiisha nitachomoa upanga wangu, nikiwa na vyote hivi hakuna atakayeweza kunisogelea. Baada ya vyote hivi kuisha ndiyo mnaweza kunifanya mtakavyo. Sasa nikiwaambia nilipoiacha hazina yangu mtaniacha niende?

Washirikina wakakubali wazo lake. Kisha Suhayb akawaambia ilipo hazina yake na kuendelea na safari. Alifika Quba (kijiji karibu na Madina) katikati ya mwezi wa Rabiul awwal na akaungana na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipomuona alitabasamu na kwa kuwa aliacha utajiri wake kwa ajili ya imani yake akasema:

"Suhayb ameshinda! Suhayb ameshinda! Ewe baba wa Yahya. Biashara yako imethibitisha faida. Biashara yako imethibitisha faida".

Kwa mujibu wa masimulizi, Aya ifuatayo ilishuka kutokana na tukio hili:

"Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake" (Baqara, 2:207).

❁

Zinnura Hatun رضي الله عنها alikuwa ni swahaba mwingine wa kike ambaye alitaabika kwa maelfu ya mateso na ukatili mikononi mwa washirikina. Alisababishiwa upofu kutokana na mateso ya Abu Jahl.

Abu Jahl alimuambia:

"Unaona? Lat na Uzza wamekupofusha"

Zinnura Hatun akajibu:

"Hapana! Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu siyo wao walionipofusha. Si Lat wala Uzza ambao wanaweza kunifaidisha au kunidhuru. Mungu wangu ndiye anayeweza kunirudishia uoni wangu!"

Ilipofika asubuhi, Washirikina ambao roho zao zilikuwa zimefunikwa na kiza walishangazwa kuona Zinnura Hatun anaona kwa rehema za Mwenyezi Mungu.

❁

Waislamu wengi wa mwanzo walitaabika kwa mateso na maumivu hayo. Maswahaba hao watukufu kama vile Amir bin Fuhayra, Abu Fukayha, Mikdad bin Amr, Ummu Ubeys, Lubeyna Hatun, Nahdiye Hatun na binti yake walipata mateso makubwa mno. Washirikina walifikia kuwafunga minyororo miguu yao wakiwa uchi na kuwaburuza, pia walikuwa wakiwalaza chini jangwani wakati wa jua kali na kuwawekea mawe makubwa juu yao. Walipitia mateso hayo kiasi cha kupoteza fahamu wasijue wanalosema. Waliwakaba mpaka wahakikishe wamekufa.

Maswahaba hawa watukufu waliweza kulinda imani zao mbele ya mateso na ukandamizaji wa hali ya juu waliokuwa wakifanyiwa. Walipambana kwa mali zao na nafsi zao ili neema hii tukufu itufikie. Haya ni kwa sababu walikuwa na uelewa wa kweli juu ya neema ya Uislamu. Hivyo walifahamu namna ya kufungua mlango wa neema hii tukufu hapa duniani na kesho Akhera. Maisha yao magumu yalifikia mwisho na kuingia katika furaha ya milele wakiwa wameshikamana na amri ifuatayo:

"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu" (Al-Imran, 3:102)**.**

❁

Saad bin Abi Waqqas alikuwa ni mtoto anayemuheshimu sana mama yake. Alipoingia kwenye Uislamu mama yake akamuambia:

"Ewe Saad! Umefanya nini? Kama huachi dini hii mpya naapa sitakula wala kunywa mpaka nife, na kwa sababu hii utajulikana kama mtoto aliyemuua mama yake".

Saad akajibu:" Samahani mama, Sitaacha dini hii kwa sababu yoyote ile". Aliposikia haya mama yake hakula kwa siku mbili na kupoteza nguvu nyingi. Ili kumfanya mama yake aliyempenda sana kuachana na msimamo wake, Saad akamuambia mama yake kwa azimio imara:

"Mama mpendwa! Lijue hili: Hata kama ulikuwa na roho mia moja na zote zikafa moja baada ya nyingine sitaacha dini hii…"

Mama yake alipoona azimio la mtoto wake akaachana na msimamo wake na kuanza kula tena. Baada ya tukio hili, Aya ifuatayo ilishuka:

"Na tumemuusia mtu kwa wazazi wake wawili. Mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha ziwa baada ya miaka miwili. (Tumemuusia): Nishukuru Mimi na wazazi wako. Ni kwangu Mimi ndiyo marudio. Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwatii. Lakini kaa nao kwa wema duniani, nawe ishike njia ya anayeelekea kwangu. Kisha marejeo yenu ni kwangu Mimi, na Mimi nitakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda" (Luqman, 31:14-15).

❁

Wakati Mtume anataka kuhamia Madina alimuita Ali ﷺ na kumuambia amri tukufu ya kuhama. Akamuambia kuwa anataka kumpa dhamana ya kurudisha amana zote alizokuwa anazihifadhi kwa ajili ya watu. Hii ilikuwa ni kwa sababu kulikuwa hakuna mtu

ndani ya Makka ambaye ana kitu cha thamani na kuacha kumpa Mtume amuhifadhie kwa kujua ukweli na uaminifu wake.

Kama tahadhari dhidi ya mipango ya washirikina, Mtume ﷺ alimuambia Ali:

"Ewe Ali! Leo lala katika kitanda changu na jifunike kwa joho langu. Usiogope hakuna kibaya kitakachokutokea".

Kwa ujasiri mkubwa wa imani aliokuwa nao Ali رضي الله عنه alilala katika kitanda cha Mtume chini ya kivuli cha mikuki mikali ya washirikina ambayo ilikuwa tayari kumshukia mwilini mwake. Washirikina wenye hasira ambao walikuja kwenye nyumba ya Mtume kumuua walipomuona Ali ndiye aliyejifunika pale kitandani wakakasirika sana:

Wakapiga kelele "Ewe Ali! Yuko wapi mtoto wa mjomba wako?".

Ali Akasema:

"Sijui. Sijui kabisa. Na mimi si mwangalizi wake. Mlimwambia aondoke Makka na yeye amefanya hivyo".

Kutokana na haya wakamsema Ali رضي الله عنه kwa hasira na kumsumbua; Wakamchukua na kumpeleka katika msikiti wa Al Haram na kumuweka jela kwa muda na kumuachia.

❁

Wakati Fulani watu wa Najd walimuendea Mtume wakitaka kujifunza Uislamu, wakaomba waalimu. Juu ya hili Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwatumia *mahafidh*[8] 70 ambao walitokana na *Ahl as-Suffah*[9]. Wote walikuwa wanaujua Uislamu vizuri.

8. *Hafidh* ni muislamu ambaye amehifadhi Qur'an yote. (Maelezo ya mfasiri).
9. Kwa maneno mengine "watu wa benchi". Ahl as-Suffah lilikuwa ni kundi la waislamu wa mwanzo ambao hawakuwa na sehemu ya kuishi na

Wakati Waislamu wamekuja Bi'r-i Mauna ili kupumzika ndani ya pango walivamiwa. Mshirikina aitwae Jabbar bin Sulma alirusha mkuki ambao uliingia mgongoni mwa Amir bin Fuheyra na kutokea kifuani. Alipoona anakaribia kuwa shahidi, Ibn Fuheyra ambaye alikuwa na umri wa takriban miaka 40 wakati ule akapiga kelele kwa furaha kubwa:

"Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu! Nimeshinda!"

Ibn Tufayl, ambaye alikuwa kiongozi wa wale walioandaa mtego ule wa kilaghai alimchukua muislamu mmoja ambaye alipona katika yale mauaji na kumleta mbele ya mmoja wa mashahidi na kumuuliza:

"Huyu ni nani?"

Yule muislamu akajibu:

"Ni Amir bin Fuheyra".

"Niliona mwili wake ukipandishwa kwenda angani kisha ukatulia baina ya mbingu na ardhi na kisha ukarudishwa chini".

Pamoja na kuwa shuhuda wa tukio lile, Ibn Tufayl aliyekuwa Mshairi mkubwa alishindwa kuwa muislamu. Sauti za mtu aliyemfanya afe shahidi, "Nimeshinda" ziligonga masikioni mwake kwa masiku kadhaa. Maneno haya yakawa ya kumshangaza. "Nimemuua lakini anasema ameshinda, linawezekanaje hili?" aliwaza mwenyewe kwa wiki kadhaa. Siku moja akamuuliza Dahhak bin Sufyan, maarufu kwa uwerevu wake na mfuasi wa Mtume ambaye alimfikiria kuwa na watu 100. Swahaba wa Mtume alimaanisha nini aliposema: "Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu nimeshinda?" Aliposema hivyo alimaanisha" nimefika peponi",

hawakuwa na namna ya kupata kipato. Hivyo walikuwa wakikaa kwenye benchi lililokuwa nje ya msikiti wa Mtume. (Maelezo ya mfasiri).

Jabbar akaamka katika usingizi mzito wa kupuuzia na kuingia katika Uislamu.

❁

Mwishoni mwa vita vya Uhud, Safiyya alitamani kumuona kaka yake aitwaye Hamza ambaye mwili wake ulikuwa ni vipande vipande, akiwa na nia hii kichwani mwake akaelekea ilipowekwa miili ya mashahidi. Mtoto wake wa kiume aitwae Zubayr akamkuta na kusema:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anakuamrisha urudi".

Safiyya akasema:

"Kwa nini? Ili nisimuone kaka yangu? Najua namna alivyochanwachanwa na kuparaganyika. Alifikwa na maafa haya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na hata hivyo hakuna kitu kingine zaidi ya hiki kitakachotupa faraja. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitavumilia na kusubiri malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu".

Zubayr alienda kwa Mtume na kumjulisha kile mama yake alichokisema. Mtume akasema:

"Kama ni hivyo mruhusu akamuone kaka yake".

Safiyya akaenda kwenye maiti ya kaka yake aliyeheshimika kwa kuwa mkuu wa mashahidi na kumuombea kwa unyenyekevu.

❁

Imani ya kijasiri ya maswahaba watukufu ambao walichukua barua zilizoandikiwa viongozi mbalimbali wa wakati ule kutoka kwa Mtume ni maarufu sana. Walipeleka ujumbe wa Mtume bila kuhofia yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu mbele ya wakandamizaji ambao walikuwa maarufu duniani kote ambao walikuwa

tayari kukata vichwa vya watu. Hawakusita kuongea kwa uwerevu mbele ya kivuli cha mikuki. Baadhi ya mifano ni hii ifuatayo:

Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu aliuliza:

"Enyi watu. Ni nani atachukua barua hii aipeleke kwa Muqawqis wa

Alexandria kwa kutarajia malipo ya Mwenyezi Mungu na thawabu?"

Hatib bin Abi Beltaa akanyanyuka na kwenda mbele ya Mtume:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi nitachukua" alisema.

Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema:

"Ewe Hatib! Mwenyezi Mungu akubariki katika wajibu huu".

Hatib bin Abi Beltaa alipowasili Alexandria akamsomea mfalme barua ya Mtume. Muqawqis akamuita Hatib upande wake, pia walikusanyika pamoja naye watu wake wa dini. Akawaambia hebu tusikilize habari iliyobaki kutoka kwa Hatib:

Muqawqis akaniambia:

"Nitazungumza na wewe kuhusu baadhi ya mambo ambayo ninataka kuyaelewa.

"Hebu tuongee tafadhali" nikamwambia.

Muqawqis aliuliza:

"Je, mwalimu wako si nabii?"

"Ndiyo. Yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu" nikajibu.

"Kama yeye ni nabii kweli basi kwa nini asiwashitaki kwa Mwenyezi Mungu watu wake ambao wamemfanya akimbilie ardhi nyingine?"

Nikajibu:

"Nadhani unashuhudia kuwa Yesu mwana wa Mariam alikuwa mtume, ni sawa? Kama kweli alikuwa Mtume mbona hakumuomba Mwenyezi Mungu awaangamize wale watu waliomkamata na kutaka kumsulubu badala ya kupaishwa mbinguni?"

Muqawqis hakupata jibu. Baada ya kimya kifupi aliniambia nirudie maneno yangu. Nilipoyarudia yale maneno Muqawqis akafikiria tena kwa muda. Kisha akasema:

"Umeongea vizuri. Wewe ni mtu mwenye busara, unaongea ipasavyo na umetoka kwa mtu ambaye lazima ni mwenye busara".

Kufuatia hayo nikamuambia Muqawqis:

"Kabla yako kulikuwa na mtu ambaye alidai kuwa yeye ndiye mungu mkuu. Mwenyezi Mungu mtukufu alimkamata Firauni huyo na kumuadhibu hapa duniani na Akhera. Chukua fundisho kwa wale waliokuwa kabla yako na liwe somo kwa wale wajao".

Muqawqis akasema:

"Tuna dini yetu na hatuwezi kuiacha mpaka tupate kitu bora kuliko hii"

Kutokana na hili nikasema:

"Uislamu ndiyo dini iliyo juu ya hiyo uliyonayo. Tunakualika katika Uislamu, dini ambayo Mwenyezi Mungu aliye juu ameichagua kwa ajili ya watu wake. Mtume Muhammad ﷺ hakualiki wewe tu bali wanadamu wote. Watu waliokuwa wabaya na wakatili kwake walikuwa ni Maquraish. Na watu ambao walikuwa na uadui mkubwa kwake ni Wayahudi. Hata hivyo walio karibu naye ni

Wakristo. Kama nabii Musa alivyombashiria Yesu, vivo hivyo na Yesu naye alitoa habari njema za kuja kwa Muhammad ﷺ. Kukuita kwetu kwenye Qur'an ni kama nyinyi mnavyowaita kwenye Injili watu wanaofuata Taurat. Kila mtu ni lazima amfuate mtume aliyetumwa katika wakati wake. Wewe pia ni mmoja wa wanaoishi wakati wa Muhammad ﷺ, matokeo yake kukuita kwetu kwenye Uislamu hatukutenganishi na dini ya Yesu. Kinyume chake tunakusihi ufanye lililo sawa kutokana na ujumbe aliokuja nao".

Muqawqis akasema:

"Nimejifunza dini ya huyu Mtume. Nimeona kuwa haamrishi kuiacha dunia wala hakatazi yanayopendwa na kukubalika na watu. Yeye si mchawi wala aliyepotea njia, wala si muongo anayedai ana ujuzi wa yasiyoonekana. Kinyume chake ana dalili zinazoonyesha kuwa yeye ni mtume kwa kuwa kafichua habari za yasiyoonekana. Hata hivyo bado nahitaji kufikiria zaidi".

Baadaye alijibu barua ya Mtume... Hata hivyo hakukufanya zaidi ya hili na wala hakuingia katika Uislamu, na alitoa tahadhari ifuatayo kwangu:

"Kuwa makini! Usiruhusu watu wa dini za Misri kusikia hata neno moja kutoka kwako wasije kukusababishia madhara".

Haya maneno ya Hatib ni mfano mzuri kwetu. Uzuri ulioje wa mfano huu wa kimtazamo na ujasiri wa muumini ambaye aliishi kwa imani na upendo na ambaye alizungumza mbele ya Mfalme kwa ujasiri utokanao na imani yake. .

Barua aliyoandikiwa Chosroes wa Iran ilichukuliwa na Abdullah bin Huzafa. Alipoona jina la Mtume limeandikwa kabla ya jina lake alikasirika na akararua ile barua tukufu vipande vipande. Pia alimtukuna mjumbe kwa maneno makali.

Kwa ujasiri na heshima kutokana na imani yake, Abdullah alimhutubia Chosroes na watu wake kama ifuatavyo:

"Enyi watu wa Uajemi! Mnapitisha siku bila ya nabii au kitabu. Mnadhibiti sehemu ndogo ya nchi mikononi mwenu. Mnaishi kana kwamba mko ndani ya ndoto. Sehemu ya ardhi ambayo haipo katika udhibiti wenu ni kubwa mno.

"Ewe Chosroes! Watawala wengi walikuja kabla yako na wakatawala na kutaka ama dunia au Akhera. Wale ambao walitaka Akhera walipata sehemu yao katika dunia hii vilevile. Wale ambao walitaka hii dunia walipoteza Akhera yao. Unadharau dini hii ambayo tunaipendekeza kwa ajili yenu, lakini kwa jina la Mwenyezi Mungu mahali popote mtakapokuwa, wakati jambo hili mnalolidharau litakapowasibu, mtakuwa na hofu na hamtaweza kujilinda".

Katika kujibu haya Chosroes alisema kuwa mali na ufalme ni vyake peke yake na kuwa hakuwa na hofu ya kushindwa wala mtu yeyote asingeweza kudai ushirika pamoja naye. Kufuatia hayo aliamrisha watu wake kumtoa Abdullah bin Huzafe nje.

Mara tu baada ya kutoka kwa Chosroes, Abdullah alipanda farasi wake na kufunga safari ya kuelekea Madina, mawazo yafuatayo yalimpitia kichwani mwake:

"Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu sina wasiwasi juu ya matokeo yoyote juu yangu(kama kuuawa au kubaki hai). Nimetekeleza wajibu wangu wa kuifikisha barua ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, na hilo ndilo la muhimu".

Hii ni hali ya amani juu ya dhamiri ya mmoja wa mashujaa wa Uislamu ambaye alihatarisha maisha yake ili kutimiza nia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Ifuatayo ni hadith nyingine iliyojaa masomo ambayo yanafaa kuchukuliwa, na kuonyesha maadili ya kipekee na ujasiri wa imani ya Abdullah bin Huzafe:

Wakati wa Ukhalifa wa Omar, jeshi la Waislamu lilitumwa kwenda kupambana na Warumi katika wilaya ya Qaysariyye ya Dameski. Abdullah bin Huzafe alikuwa katika jeshi hilo. Warumi walimchukua mateka na kumpeleka kwa mfalme wao na kusema:

"Huyu ni swahaba wa Muhammad".

Kisha Abdullah akafungwa katika chumba bila chakula wala kinywaji, baada ya hapo wakampelekea kiasi kidogo cha mvinyo na nyama ya nguruwe na kumuangalia kwa siku tatu. Abdullah hakuweka mkono juu ya divai wala nyama ya nguruwe. Walimuambia Mfalme:

"Amepoteza nguvu nyingi, kama hutamtoa atakufa".

Mfalme aliamuru aletwe kwake kisha akamuuliza:

"Ni kipi kilichokuzuia kula na kunywa?

Abdullah akajibu:

"Kwa hakika juu yangu lazima imefanywa juu ya ulaji wa vitu halali, lakini sitaki kujisababishia mimi wala Uislamu kuwa kichekesho mbele yako".

Kulingana na msimamo huu, Mfalme akasema:

"Vipi ukiwa mkristo na nikakupa nusu ya utajiri wangu, na vipi nikikufanya mshirika wangu katika ufalme wangu wote na kisha nikatoa binti yangu umuoe?"

Abdullah akajibu:

"Hata ukinipa utajiri wako wote na utajiri wote wa waarabu, sitaiacha dini ya Muhammad hata kwa kiasi cha kupepesa jicho".

Mfalme akasema:

"Kama ni hivyo nitaamuru uuawe".

Juu ya hilo Abdullah akajibu:

"Hilo ni juu yako".

Kisha Abdullah akatundikwa msalabani. Kwanza akafyatuliwa mishale kwa nia ya kumkosa ili aogope. Kisha akapewa nafasi nyingine ya kuritadi. Swahaba yule mtukufu hakuonyesha hata chembe ya muelekeo. Kutokana na haya mfalme akasema:

"Ama uwe mkristo au nitakuingiza ndani ya chungu cha maji yenye kuchemka".

Alipokataa tena kililetwa mbele yake chungu cha shaba chenye kuchemka. Mfalme akaamuru mtumwa mmoja wa kiislamu aletwe. Akamshauri yule mtumwa aingie katika ukristo, alipokataa akadumbukizwa ndani ya kile chungu huku Abdullah anaangalia. Mara ngozi ya yule mtumwa ikabanduka kutoka mwilini mwake na akafa pale pale.

Mfalme akamshauri Abdullah tena aingie katika ukristo. Alipokataa akaamuru arushwe ndani ya kile chungu. Alipotaka kurushwa ndani ya chungu akaanza kulia. Kwa kudhani kuwa amebadilisha msimamo wake, mfalme akaamuru aletwe kwake na akampa nafasi nyingine ya kuingia kwenye ukristo. Alipoona namna Abdullah alivyokataa tena kwa nguvu zote, kwa mshangao akamuuliza:

"Sasa kwa nini ulilia?"

Abdullah akatoa jibu zuri lifuatalo:

"Msidhani kwamba nililia kwa hofu ya ulichotaka kunifanyia. Hapana. Nililia kwa sababu nina roho moja ya kufa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Nikajisemea moyoni:" Una roho moja tu na ndiyo unataka kurushwa ndani ya chungu. Mara tu utakufa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Nilitamani ningelikuwa na roho kiasi cha kufikia idadi ya nywele mwilini mwangu ili zote zife kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kupata radhi zake".

Kitendo hiki cha kuvutia alichokionyesha Abdullah kutokana na hadhi na ushupavu wa imani yake kilimvutia mfalme kiasi cha kutamani kumuachia huru.

"Busu kichwa changu nikuache huru", mfalme akamuambia.

Kwa zawadi hii ambayo isingelikuwa na kipingamizi, Abdullah alijibu kwa ombi lake binafsi:

"Utawaruhusu watumwa wengine wa kiislamu wawe huru pamoja na mimi?"

Mfalme alipojibu kuwa angelifanya kama alivyoomba, Abdallah akasema:

"Kama ni hivyo nitafanya".

Baadae Abdullah akasema:

"Nikajiambia:Kuna kikwazo gani kwa mimi kubusu kichwa cha mmoja wa maadui wa Mwenyezi Mungu ili kuokoa maisha yangu na maisha ya watumwa wa Kiislamu? Kibusu na uwe huru"

Siku ile waislamu 80 waliachwa huru. Waliporudi kwa Omar walimueleza kilichotokea. Omar akasema:

"Kubusu kichwa cha Abdullah bin Huzafe ni wajibu wa kila muislamu! Nitakuwa wa kwanza kutekeleza wajibu huu". Akasimama na kwenda kwa Abdullah na kubusu kichwa chake.

Waislamu wenye ufahamu na utambuzi wanachunguza matukio kwa kupitia dirisha la maisha baada ya kufa. Wanaweza kufanya hivi kwa sababu imani yao inawapa mtazamo mpana. Kwa njia hii wao daima huchukua tahadhari juu ya hasi na chanya, yani faida na hasara. Hii ni kwa sababu maumivu yote ya kidunia, mateso, majaribu na dhiki havina nafasi dhidi ya mapenzi yao katika imani.

Shujaa mwingine ambaye aliishi kwa imani na upendo ni Wahb bin Kabshah ﷺ. Kaburi la swahaba huyu mtukufu lipo China. Mtume alimpa jukumu la kwenda China kueneza Uislamu. Wakati huo ilichukua mwaka mmoja kufika China kutoka Madina. Baada ya kufika China na kukaa huko kwa muda mrefu na kueneza Uislamu akaamua kupanga safari ya kwenda Madina ili kutosheleza angalau kidogo hamu kubwa aliyokuwa nayo ya kumuona Mtume wa Mwenyezi Mungu. Baada ya safari ngumu ambayo ilichukua mwaka mmoja kufika Madina, kwa bahati mbaya hakuweza kumuona Mtume kwa kuwa alikuwa tayari ameshafariki. Alirudi China huku hamu yake ya kumuona Mtume ikiwa imeongezeka zaidi. Alifanya hivyo ili kukamilisha jukumu tukufu alilopewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mauti yalimkuta akiwa anatekeleza wajibu huu. Kutokana na haya Wahb bin Kabshah alipewa heshima ya kuwa mwakilishi wa kwanza wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika nchi ya China. Mwili wake ulibakia China lakini roho yake ilikwenda Madina kuwa pamoja na roho ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Matukio ambayo yalifanyika kati ya Sultani Bayazid II na ndugu yake Jem Sultan yalionyesha wazi ujasiri wa imani za baba zetu na uzuri na wema ambao ulitokana na Uislamu:

Alipokuwa sultani katika mwaka 1481, Bayazid II (ambaye pia alikuwa akijulikana kama Bayazid mtakatifu kutokana na uchamungu wake) alitumia miaka 14 ya kwanza ya utawala wake kushughulikia matatizo yaliyotokana na ndugu yake Jem Sultani kudai kiti cha enzi cha dola ya Uthmaniyya. Hali hii ilimzuia Bayazid II kushiriki kikamilifu katika ulimwengu wa Kikristo. Jem Sultan alipendekeza yafuatayo kwa Bayazid II:

"Hebu tugawe nchi yetu mara mbili. Utawale nusu na mimi nitatawala nusu nyingine".

Bayazid II akajibu huku akikataa ombi hili:

"Ndugu yangu, nchi hii ni mali ya watu. Kama tutaigawa, serikali itapoteza nguvu. Tutakuwa ni miongoni mwa watawala dhaifu, jambo ambalo litakuwa na madhara makubwa. Niko tayari kuugawa mwili wangu lakini ardhi ya watu wangu haiwezi kugawanywa".

Muda mfupi baadae Jem Sultan alialikwa kwenda Rhodes na mashujaa wa Rhodes. Alivutiwa na maneno yao ya upole na bila ya kipingamizi alikubali mwaliko wao. Hata hivyo mashujaa wale walivunja ahadi waliyoiweka na kumuuza kwa Papa wa Rumi kama mtumwa. Papa alikuwa na mipango ya kumtumia katika vita vijavyo vya msalaba dhidi ya dola ya Uthmaniyya. Hata hivyo kwa kutambua kuwa asingefanikiwa katika hili, Papa Innocent alipendekeza Jem Sultan awe mkristo. Hili ombi lilimpa mashaka sana Jem Sultan. Kwa masikitiko makubwa alimwambia Papa:

"Hata kama utanipa dunia nzima na si tu uongozi wa dola ya Uthmaniyya nisingelibadili dini yangu".

Dua aliyoomba Jem Sultan kwa Mwenyezi Mungu alipoona kuwa askari wa vita vya msalaba wanataka kumtumia yeye dhidi ya Uislamu inatosha kuonyesha juhudi yake juu ya dini yake:

"Ewe mlezi wangu! Kama makafiri wanataka kunitumia kama chombo cha kuleta madhara katika ulimwengu wa kiislamu basi usiruhusu mtumwa wako huyu kuishi tena. Chukua nafsi yangu uipeleke kwenye makazi yako ya heshima haraka iwezekanavyo..."

Maombi yake yatakuwa yalijibiwa katika umri wa miaka 36 alipofia Naples. Agano lake la mwisho kwa watu wa karibu naye katika masiku yake ya mwisho ni hili lifuatalo:

"Hakikisheni mnatangaza habari ya mauti yangu nchini kote. Kufanya hivyo kutapelekea baadhi ya michezo wanayotaka kucheza wasioamini juu ya Waislamu kwa kunitumia mimi kama chom-

bo chao inaweza kuisha. Baada ya hilo nendeni kwa kaka yangu Sultan Bayazid na mumuambie asafirishe maiti yangu mpaka nchini kwetu licha ya ugumu wowote atakaokutana nao.

Sitamani kuzikwa kwenye ardhi ya makafiri. Kilichotokea kimetokea. Hakikisheni hakatai ombi langu. Mwambieni anilipie madeni yangu yote, kwani sitaki kwenda sehemu takatifu nikiwa na madeni. Mwambieni aisamehe familia yangu, watoto wangu na wote walionitumikia. Mwambieni awashawishi waridhike katika hali zao".

Ndugu yake Bayazid II akafanya agano lake la mwisho.

Hizi ni sifa ambazo Uislamu humpa mwanadamu. Uhusiano wa dhati kati ya hawa ndugu wawili unaonyesha kujitolea kwao katika imani na mapenzi ya nchi yao. Pia inaonyesha kujitolea kwao muhanga kwa ajili ya amani ya watu wao, na ni mfano wa uvumilivu na dhamiri njema inayotokana na kutambua makosa ya mtu, kujizuia kukiuka haki za mwingine, msamaha, huruma na mapenzi katika mambo mengine ya kimaadili.

Ndugu Ilyas, Oruc na Hizir walikuwa na nafasi muhimu katika kikosi cha maji cha Uthmainiyya. Walishughulishwa na biashara za baharini kabla hawajafungua bendera ya jihad katika bahari ya Mediterranea. Hata hivyo biashara hii ilionyesha hatari kubwa kwa watu wa Mediterranea. Wakati Oruc Reis alipofungwa na maharamia wa Rhodesia, ndugu yake Hizir Reis akaanza kutafuta ufumbuzi wa suala hili. Licha ya kuwa alituma kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kuachiwa kwa kaka yake, ndugu yake alibakia mtumwa kwa muda mrefu kutokana na mbinu za hila za maharamia ambao hawakutekeleza ahadi zao. Kwa kutoridhika na hili, makafiri walimtuma kuhani aliyekuwa jasiri kwenda kwa Oruc

Reis kumshawishi awe mkristo. Hata hivyo jibu la Oruc Reis lilikuwa ni kama kofi katika nyuso zao:

"Enyi wajinga na wapuuzi! Nitaachaje dini ya kweli ili kuingia katika dini ya uongo?"

Maharamia wakaghadhibika juu ya hili na kusema:

"Kama ni hivyo muache Muhammad wako aje kukusaidia" na kumfunga minyororo katika boti na kumfanya mtumwa wa maonyesho.

Oruc Reis alijikinga kwa Mwenyezi Mungu na kuomba:

"Subiri tu na uone namna mlezi wangu atakavyonisaidia".

Baadaye kidogo mikono na miguu yake ilikuwa imefunguliwa na kuachwa huru katikati ya bahari kwa usaidizi wa kikundi cha watu waliovalia kanzu nyeupe na vilemba ambao pia walionekana kwa makafiri. Namna hii akapata fadhila ya unyenyekevu na utegemezi kwa Mwenyezi Mungu kutokana na nguvu za imani aliyokuwa nayo. Baada ya tukio hili Oruc Reis pamoja na ndugu yake Hizir Reis walianzisha vita dhidi ya maharamia wa Mediterranea bila huruma.

Mapigano ya Dardanels ni mfano mwingine mkubwa ambao unaelezea vipaji vya kuishi kwa imani na upendo.

Kanali mstaafu ambaye alikuwa ni kamanda katika vita vya Dardanels na ambaye alikuwa amejeruhiwa katika mchakato huo anaelezea katika kumbukumbu yake kama ifuatavyo:

"Ilikuwa ni siku ambayo vita vya Dardanels vilipiganwa. Siku ile vita ambavyo vilidumu mpaka jioni, ilibaki kidogo tushinde, licha ya vifaa vingi vya kivita kwa maadui. Nilikuwa nikishuhudia kwa furaha hatua za mwisho za vita. Sauti za "Allah, Allah" kutoka

kwa askari wa kiislam zilirindima na kufunika milio ya mizinga iliyofunika eneo la vita".

Wakati fulani nilisikia hatua za miguu karibu yangu. Nilipogeuka nikakutana uso kwa uso na sajini Ali. Kulikuwa na maumivu makubwa katika uso wake uliogeuka njano. Nilipata nafasi ya kumuuliza kuwa tatizo ni nini, alinionyesha mkono wake ambao ulitosha kuonyesha kila kitu. Nilitetemeka kwa hofu. Mkono wake wa kushoto ulikuwa ukining'inia kwa urefu wa vidole vinne kutoka kiunoni na pale alipopigwa. Ilikuwa na kipande chembamba cha ngozi ndicho kilichozuia mkono wake kudondoka chini. Sajini Ali alikuwa anang'ata meno ili kujaribu kupunguza maumivu. Akanipa panga aliloshika katika mkono wa kulia:

"Kamanda ukate!" alisema.

Kauli hii ya maneno matatu tu ilionyesha uhitaji mkubwa na ulazima kiasi kwamba nikachukua kisu bila ya kujitambua wala kufikiria na kutenga mkono uliokuwa ukining'inia kwa kingozi chembamba. Wakati nikifanya jambo hili nilijaribu kuinua ari yake:

"Usihuzunike Sajini Ali. Mwenyezi Mungu akurudishie afya mwilini mwako".

Si muda mrefu baada ya Sajini Ali kupoteza mkono wake kwa ajili ya watu wake, lakini pia mwili wake uliobarikiwa. Wakati anafumba macho yake na kutoa pumzi yake na huku amezungukwa na bwawa la damu alirudia sentensi zifuatazo:

"Naomba taifa langu la kiislamu liishi muda mrefu! Namuomba Mwenyezi Mungu alihifadhi lisiiache imani…. Naomba maisha yangu yapotee kwa ajili ya dini yangu!"

Na hivyo ndivyo askari wa dola ya Uthmainiyya ndani ya Dardanels walivyochukulia kwa imani zao kuwa kulilinda taifa lao ni deni na hitajio la dini yao na hawakusita kulipa deni hili kwa uhai

wao. Ndiyo maana askari hawa waliikumbatia dini yao kama walivyokumbatia bunduki zao na walikumbatia bunduki zao kama walivyokumbatia imani zao.

❁

Wakati wa vita kwa ajili ya Dardaneles ngome za kirumi za Mecidiye zilikuwa zimefutwa karibia zote kutokana na kushambuliwa vibaya na maadui. Silaha zao nyingi zililipuliwa na wanamizinga kumi na sita waliuawa. Ni kapteni tu na wanajeshi wawili ndiyo waliobaki kati ya jeshi lote pamoja na mzinga wao ambao ulivunjika kiasi cha kutoweza kuchukua mizinga tena.

Kapteni alienda kuvijulisha vikosi vilivyokuwa vinawazunguka juu ya hali ile. Koca Sayyid, aliyekuwa mmoja wa maaskari aliziangalia meli za maadui zilizokuwa zikiwasogelea kwa kupitia baharini huku zikitoa moto na kuua alihuzunika sana. Macho yake yalijaa machozi. Moyo wake wenye huzuni ulidunda kwa maumivu ya kutoweza kutoa msaada wowote mbele ya maadui na alinyanyua mikono yake na kuomba:

"Ewe mlezi wangu! Ewe Mwenyezi Mungu ambaye ni mmiliki wa utukufu! Nipe nguvu sasa hivi ambayo hakuna mja wako mwingine atakayekuwa nayo".

Mara ikawa kana kwamba Koca Sayyid amefariki dunia…Ilikuwa kana kwamba yuko mbele ya Mola wake na hakuna mwingine. Machozi yakatiririka usoni mwake. Baaada ya muda akapaza sauti:" *Hakuna nguvu wala utukufu ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu*".

Mara akapiga kelele "Allah!" na huku rafiki yake akimshangaa alienda na kunyanyua tufe la mzinga lenye uzito wa takriban kilo 276, kisha akapanda na kushuka ngazi za chuma mara tatu. Mlio wa mifupa ya kifua na mabega yake iliweza kusikika. Huku akitoa jasho kwa mkono wake wa kulia alimuomba Mwenyezi Mungu:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Tafadhali usichukue nguvu zangu".

Mara mwelekeo wa vita ukabadilika baada ya kuweka tufe la mzinga lililokuwa la tatu kwa umaarufu kwenye mdomo wa mzinga. Alipoufyatua uliipiga meli ya kivita ya Waingereza iliyoitwa Bahari na kuisababishia moto mkubwa.

Kutokana na tukio hili Cevat Pasha akamtukuza Mwenyezi Mungu mtukufu, kisha akampongeza Koca Sayyid na kumuomba anyanyue mpira mwingine wa mzinga wenye uzito uleule. Koca Sayyid akatoa jibu lifuatalo:

" Pasha wangu! Niliponyanyua ule mpira wa mzinga moyo wangu ulijawa na mafanikio ya Mwenyezi Mungu na mwili wangu ulikuwa katika msaada mtukufu. Nilikuwa mtu mwingine. Msaada wa Mwenyezi Mungu mtukufu na mwongozo ulikuwa kwangu kutokana na dua niliyomuomba. Hili lilikuwa ni tukio kwa wakati ule pekee. Siwezi kuinua sasa, Kapteni; inabidi unisamehe tafadhali..."

Kwa maneno haya ya Sayyid, Cevat Pasha alisema:

"Mwanangu! Umefanya kazi yenye mafanikio makubwa, niombe zawadi".

Huyu shujaa aliyejitolea ambaye alifuta yote ndani ya moyo wake na kuacha unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, alionyesha ushujaa zaidi kwa maneno yafuatayo:

"Kiongozi wangu! Mimi sina ombi; hata hivyo kutokana na nguvu zangu ambazo ni kama mcheza mieleka, mkate mmoja kwa siku haunitoshi. Unaweza kutoa amri kwamba wanipe mikate miwili ili niwe na nguvu zaidi dhidi ya adui?"

Cevat Pasha huku akitabasamu juu ya ombi hili alimkubalia matakwa yake. Wakati wa jioni kila mtu alipata mkate mmoja lakini Kanali Sayyid alipewa mikate miwili, moyo wa shujaa huyu mkubwa mwenye imani haukuweza kukubali hili. Wakati huu wa

uhaba wa chakula hakutaka kuwa tofauti na rafiki zake. Alirudisha mkate mmoja kati ya ile miwili aliyopewa na kamwe hakuchukua tena mikate miwili.

Usafi wa moyo ulioje.. ! Hakika hali hii ya Koca Sayyid ilikuwa ni kielelezo cha ukweli wake na kujitolea kulikotokana na ujasiri wa imani yake.

❁

Kwa kumalizia, imani si tamko kavu tu. Imani ni ushahidi wa ukamilifu wa moyo wa muumini, na ishara yake ni kujitolea nafsi yako juu ya dini. Kwani imani ni mji mkuu wa milele, maisha ya watu wengi yamekuwa yakitolewa na kupata mateso makubwa na magumu ambayo yameifunika historia ili kuilinda na kuiimarisha hiyo imani. Mifano mbalimbali ya maadili na ushujaa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imekuwa ikitolewa. Na leo tunachohitaji zaidi ni hii furaha ya kuishi kwetu kwa imani na upendo. Kama deni la neema ya imani tuliyojaaliwa, tunahitajika kufanya juhudi kualika watu wote kwenye Dar-us Salaam au nyumba ya amani. Muumini ambaye anaishi kwa mapenzi ya imani yake atajihisi kuwa na jukumu juu ya jamii. Kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu atatu-unganisha kesho Akhera kwa kujitolea kwetu ili kuithibitisha imani yetu hapa duniani.

Mwenyezi Mungu mtukufu atujaalie tuwe miongoni mwa wa-takaosafisha imani zao na utujaalie kuwa waja wako wanaoen-desha maisha yao kwa namna hii…Amin!

2. Usafi wa moyo[10]

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema: "V*itendo vya mtu vinatokana na nia yake"* (Bukhari, Faith, 41; Muslim, Imare, 155).

10. Katika kiarabu ikhlas, linatokana na neno khalasa lenye kumaanisha kuwa msafi, bila ya kuchanganyika na uchafu wowote. (Maelezo ya mfasiri).

Hivyo asili ya mambo yote mema na mwanzo wa kuabudu ni ili kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Haya yanaweza kupatikana ikiwa yatafanywa kwa moyo safi tu. Kwa maneno mengine, ni kuwa kwa kupitia moyo safi na kufungamana na lengo kubwa ambalo litapandisha hadhi ya matendo ya mtu kufikia daraja la ibada. Matokeo yake sharti la kukubalika kwa matendo ya mtu mbele ya Mwenyezi Mungu ni moyo safi.

Moyo safi ni kufanya matendo kwa lengo pekee la kumridhisha Mwenyezi Mungu na kujizuia kuyaharibu kwa matamanio ya mwili na malengo ya kidunia. Matendo yasiyofanywa kwa moyo safi yatapelekea kutopata kitu zaidi ya kupoteza muda.

Moyo safi inamaanisha kuuhifadhi moyo kutokana na mafanikio ya kidunia kwa lengo la kuwa karibu na Mwenyezi Mungu mtukufu. Moyo safi ni kusafisha matendo ya mtu kutokana na dosari za nafsi kama vile kujionyesha (*riya*) na majivuno (*ujub*), kwani haya ni magonjwa ya moyo ambayo yanaharibu na kuchafua moyo wa mtu.

Kufuta malengo yote mengine moyoni ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu ni wajibu muhimu kwa kila Muislamu. Hata hivyo ni lazima kuwa makini kwani wale ambao wana moyo safi daima wako katika hatari ya kupoteza hali hii nzuri kama matokeo ya ushindi wa *nafsi* [11]. Kama ilivyo vigumu kubakia katika daraja la juu, ndivyo pia ilivyo vigumu kuhifadhi usafi wa moyo wa mtu. Maneno yanayohusiana na suala hili kutoka kwa Dhunnun wa Misri ni maarufu:

'Watu wote ni maiti, isipokuwa kwa wanavyuoni (wale ambao wana ujuzi). Wanavyuoni wote wamelala, isipokuwa wale ambao wanafanyia kazi maarifa yao. Wale ambao wanafanyia kazi maarifa yao wako katika hatari ya kudanganywa, isipokuwa wale ambao

11. Nafsi ni roho ya mwanadamu ambayo imeegemea kwenye maasi. Hii ni asili ya kiunyama na matamanio ya mwanadamu. (Maelezo ya mfasiri).

wana moyo safi. Na wale ambao wana moyo safi wako katika hatari kubwa ndani ya dunia hii... '[12]

Hata hivyo wale watumishi ambao wana uwezo wa kudumisha nyoyo zao safi licha ya kila namna ya shida, wako katika neema kubwa ya Mwenyezi Mungu.

Kwa ufupi, moyo safi unamuwezesha mtu kufikia wema mkubwa, uitwao radhi ya Mwenyezi Mungu. Kwani lengo la Mwenyezi Mungu katika matendo ya watu ni kutafuta radhi zake. Imeelezwa katika Qur'an tukufu:

"Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa Haki. Basi muabudu Mwenyezi Mungu ukimsafia Dini Yeye tu" (Az- Zumar, 39:2)

"Sema: Hakika mimi nimeamrishwa nimuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia Dini Yeye tu" (Az-Zumar, 39:11)

Moyo safi unamuokoa muumini kutokana na shambulio la shetani ambaye ni adui yake mkubwa, kwani shetani anaweza kumuathiri yule ambaye ni dhaifu katika moyo wake. Mwenyezi Mungu anasema yafuatayo ndani ya Qur'an tukufu:

"Akasema: Mola wangu Mlezi! Ilivyo kuwa umenitia makosani, basi nahakikisha nitawazaini hapa duniani na nitawapoteza wote, Ila waja wako walio safika" (Al-Hijr, 15: 39-40).

Wale ambao wana moyo safi wataokolewa na moto. Mwenyezi Mungu mtukufu anatoa bishara njema juu ya ukweli huu katika aya ifuatayo:

"Hakika nyinyi bila ya shaka mtaionja adhabu chungu…. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu walio khitariwa" (As-Saffat, 37: 39-40)

12. Bayhaki, ShuAbu'l- Iman, Beirut 1990 V 345

Hata kama amali ni ndogo, ikifanywa kwa moyo safi, inatosha kumuokoa ambaye kaifanya. Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema:

"Kuwa na moyo safi katika dini yako! Kama ukifanya hivi, hata amali ndogo zitakutosha" (Hakim, IV, 341)

Moyo safi huvuta msaada wa Mwenyezi Mungu. Pia Mtume anasema:

"Mwenyezi Mungu anasaidia umma huu kutokana na dua, swala za faradhi na moyo safi kwa walio dhaifu" (Nasai, 43).

Mtu hapaswi kuwa na shaka kwamba moyo safi utaleta ushindi. Kwani jitihada za dhati daima hutunzwa na kamwe si bure. Katika historia kumekuwa na majeshi mengi madogo yakijumuisha watu wenye moyo safi na uvumilivu ambayo yaliyashinda majeshi mengine mengi zaidi yao katika idadi na vifaa bora kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Hali hii inaonyesha kwamba moyo safi ni msingi wa ushindi.

Matukio ya wema

Maisha ya Mtume wa Mwenyezi Mungu yamejaa mifano ya hali ya juu ya usafi wa moyo. Haya yanaweza kuonekana vizuri katika tukio lifuatalo lililotokea katika siku zake za mwanzo za utume:

Washirikina walitaka kumtumia habari Mtume kwa kupitia mjomba wake, Abu Twalib ili kuachana na kazi yake ya kuhubiri dini. Mtume alimpa mjomba wake jibu lifuatalo:

"Ewe mjomba wangu! Kwa jina la Mwenyezi Mungu, hata kama wakiweka jua mkono wangu wa kulia na mwezi mkono wa kushoto ili kunifanya niachane na dini ya Mwenyezi Mungu, kamwe sitoachana

na kazi hii! Ama Mwenyezi Mungu mtukufu aieneze duniani kote na wajibu wangu kumalizika au mimi kufa katika njia hii”

Huku washirikina wakichukia kuzaliwa kwa Uislamu, na vitimbi vyao kwa kupitia Abu Twalib kushindwa waliamua kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu moja kwa moja kwa ujasiri na kutoa maombi yafuatayo:

“Kama unataka utajiri, sisi tutakupa utajiri wowote unaotaka kiasi kwamba hakutakuwa na mtu yeyote miongoni mwa makabila yetu atakayekuwa tajiri kuliko wewe”

“Kama unataka uongozi, tutakufanya kiongozi wetu na mtawala mkuu wa Makka”.

“Kama unataka kuoa wanawake wenye kuheshimika, sisi tutakupa yeyote utakayempenda kati ya wanawake wazuri wa kiquraysh”.

“Tutafanya chochote utakacho ilhali uachane na kazi hiyo”

Katika kujibu mawazo yenye kuvutia ya wale watu wasiojali kitu ambayo wangeendelea kuyatoa, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisema yafuatayo:

“Sitaki chochote kutoka kwenu. Sitaki utajiri, mali, ufalme, uongozi na wala mwanamke! Ninachotaka ni kwa nyinyi kuachana na ibada zenu za masanamu na kumuabudu Mwenyezi Mungu pekee”.

Mtume aliishi katika maisha yake huku akifanya juhudi ya kusambaza dini ya Mwenyezi Mungu na kwa sababu hii hakutegemea watu na kamwe hakutaka kitu kutoka kwao. Mtume Muhammad na manabii wengine wote walirudia maneno yafuatayo:

"Sikuombeni ujira wowote kwa ajili ya hili. Ujira wangu ni jukumu la si mwingine zaidi ya Mola wa walimwengu wote"[13].

Eneo lifuatalo kutoka katika maisha ya nabii Musa ni kielelezo kingine kikubwa cha moyo safi:

Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Na alipoyafikia maji ya Madyan alikuta umati wa watu wananywesha (wanyama wao), na akakuta karibu yao wanawake wawili wanawazuia wanyama wao. Akasema: Mna nini? Wakasema: Hatunyweshi sisi mpaka wamalize hao wachungaji. Na baba yetu ni mzee sana" (Al-qas'as, 28:23).

Wanawake hawa wawili walikuwa ni Safura na Sufayra ambao ni binti za nabii Shuayb. Pamoja na kukaa na njaa kwa muda wa siku nane, Musa alichota maji na kunywesha wanyama wao licha ya ugumu mkubwa. Wanawake wale walimshukuru na kuondoka.

Baadae Shuayb alimualika Musa katika nyumba yake kwa ajili ya chakula. Musa alikataa kula ingawa alikuwa na njaa kwa siku kadhaa. Shuayb aliuliza sababu. Musa akajibu:

"Sisi ni familia ambayo kama tungelipewa dunia nzima kamwe tusingeliweza kuichukua ili kuachana na amali moja ya heri. Sikutoa msaada kwenu ili kutarajia chakula hiki bali kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu".

Shuayb alifurahishwa sana na jibu hili, akasema:

"Hili ombi letu si kwa sababu wewe ulitusaidia sisi bali kwa sababu wewe ni mgeni wetu. Hebu njoo tule".

Kwa hili, Musa akiwa na uchovu na njaa akakubali kula.

Mfano huu unaonyesha umuhimu wa kujizuilia kuchafua moyo wa mtu katika nia yake kwa matarajio yoyote ya kidunia ili

13. (As-Shu'ara verses 109, 127, 145, 164, 180. Jonah verse 72, Hud verse 29).

kutokupoteza malipo ya matendo mema yaliyofanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

❁

Wasila bin Aska ﷺ anahaditha mfano wa moyo safi uliopatikana katika kampeni za vita vya Tabuk:

Sikuwa na utajiri wa vifaa wala mnyama ulipofika muda wa kwenda Tabuk. Sikutaka kukosa nafasi hii takatifu, nikiwa ndani ya Madina nikalalamika:

"Ni nani atakayeniruhusu nipande mnyama wake kwa malipo ya sehemu ya ngawira (mali zinazookotwa baada ya vita)?"

Mzee mmoja wa kiansar akakubali tuendeshe mnyama wake kwa zamu mpaka vitani. Niliposema kwa haraka:" Tumekubaliana" akasema:

"Kama ni hivyo njoo twende kwa rehema za Mwenyezi Mungu".

Hivyo nikawa nimepata rafiki mzuri niliyeenda naye vitani. Matokeo yake Mwenyezi Mungu akanijaalia ngawira, baadhi ya ngawira zikaangukia kwangu. Nikazichukua na kumpelekea yule mzee wa kiansar, akaniambia:

" Ondoka na ngawira zako"

"Lakini kutokana na makubaliano yetu ya mwanzo hizi ni zako" nikamwambia. Ansar akajibu:

"Ewe ndugu yangu! Chukua ngawira zako kwani sikuzitaka hizi. Nia yangu ilikuwa ni kupata malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, nilitaka kuwa mshirika katika faida yako ya kiroho" (Abu Dawud, 113/2676)

Wale maswahaba watukufu ambao walichangia vyote walivyokuwanavyo kwa ukarimu ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu,

walifungamana na siri ya moyo safi kwa kiwango cha juu, ama walipoenda vitani kwa jina la Mwenyezi Mungu, au walipowasaidia waumini wenzao.

Walionyesha kujali kwa hali ya juu katika kuhakikisha kuwa hata faida ndogo ya kidunia haifuniki matendo mema waliyoyafanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

❁

Aisha ﵂ kila alipowasaidia masikini aliwaombea dua za heri juu ya dua walizomuombea wao. Aliulizwa kuhusu hili:

"Unawapa na kisha unawaombea dua, kwa nini unafanya hivi?"

Akajibu:

"Nahofia dua wanazoniombea zisije zikawa ni fidia ya sadaka nayowapa. Nawaombea dua ileile wanayoniombea ili nipate malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu tu".

Uzuri ulioje wa mfano wa moyo safi!... Watu hao watukufu walionyesha uangalifu wa hali ya juu katika kulinda usafi wa nyoyo zao.

❁

Uzuri ulioje wa mfano ufuatao ambao unaonyesha undani na unyeti wa moyo safi kwa Ali ﵁.

Wakati wa vita Ali alimkamata askari wa maadui na kutaka kumuua. Yule askari akautemea mate uso mtukufu wa Ali kutokana na ubaya wake.

Ungelikuwa ni kama mchezo wa kitoto kwa 'simba wa Mwenyezi Mungu' ambaye ni mwerevu na shupavu kukata kichwa cha yule adui mara moja. Badala yake akaacha ghafla, akihisi kuwa wakati ule nafsi yake imechafua nia yake ya kupigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu na si vinginevyo. Aliacha na polepole akawe-

ka chini panga lake ambalo liliitwa Zulfikar, alilokuwa amepewa kama zawadi kutoka kwa Mtume, akaamua kutomuua adui yake.

Kwa mshangao yule mtu akalala chini akisubiria kifo chake. Alifikiria kuwa Ali angelitumia juhudi nyingine kubwa kutokana na hasira na chuki iliyotokana na yeye kumtemea mate usoni. Hata hivyo haikuwa kama alivyotarajia. Akaja kujua kuwa asingelimfikiria Ali vile. Adui ambaye kitendo hiki cha shujaa wa Uislamu na shujaa wa nyoyo za watu hakikumuingia akilini alimuuliza Ali kwa mshangao na hamu kubwa ya kutaka kujua:

"Ewe Ali! Kwa nini umeacha kuniua wakati ulikuwa unataka kuniua? Nini kilibadilisha mawazo yako? Nini kimetokea mpaka kikakufanya utoke kwenye chuki kubwa mpaka kwenye utulivu wa hali ya juu…Ulikuwa kama radi inayotaka kupiga mahali kabla ya kutulia.."

Ali akajibu:

"Natumia upanga huu wa Mtume katika njia ya Mwenyezi Mungu. Siruhusu kamwe nafsi yangu kuingilia kati... Wakati uliponitemea mate kwenye uso wangu ulitaka kunikasirisha na kunitukana. Kama ningeshindwa kuzuia hasira yangu ningeshakuua kwa kuingilia matashi yangu binafsi, ambacho ni kitu kisichomnufaisha muumini. Ambapo mimi napambana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na si kwa ajili ya kujivuna".

Matokeo yake moyo wa yule adui ukapata uhai tena kutokana na tabia tukufu ya mtu aliyekuja kumuua. Alijifunza kutokana na imani ya Ali, moyo wake safi na namna alivyopambana na matashi ya nafisi yake. Matokeo yake yule askari akawa muislamu.

Wakati fulani moto ulilipuka katika soko la shaba la Baghdad. Watoto wawili walishindwa kutoka katika duka moja lililokuwa likiungua. Licha ya vilio vya kuomba msaada hakuna mtu jasiri

aliyethubutu kuingia kuwaokoa. Mwangalizi wao alikuwa nje akilia huku amekata tamaa:

"Nitatoa vipande 1000 vya dhahabu kwa atayeokoa watoto wangu"

Wakati ule Abu'l Hussain Nuur alikuwa akipita, akajitupa ndani ya moto. Moto ukawa kama bustani la mawaridi kwake. Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu mtu huyu mtukufu aliweza kuwaokoa watoto wale kutokana na ule moto huku kila mtu akishangaa.

Kwa furaha muangalizi wao akatoa vipande vya dhahabu kumpa Abu'l Hussain Nuur ambaye ghafla alighadhibika na kusema:

"Chukua dhahabu yako na umshukuru Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi! Kama ningelikuwa nimefanya vile si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu bali kwa ajili ya matumaini ya kupata zawadi, kamwe nisingeliweza kuwaokoa watoto hao kutoka kwenye ule moto"

❁

Kama tunavyoweza kuona katika mfano huu, Moto mkubwa unaweza kuwa bustani la mawaridi kwa baraka za moyo safi. Lakini kuingia kwenye moto kunawezekana pale tu mtu atakapokuwa kama Ibrahim, yaani rafiki wa Mwenyezi Mungu. Kwani Ibrahim kukosa woga mbele ya moto ilikuwa ni neema kubwa aliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu kutokana na kunyenyekea kwake kwa Mwenyezi Mungu kwa mapenzi.

Moyo safi una athari katika kila kitu. Hali ya kuwa umesababishwa na nia safi, mtu atakayetoa sadaka atalipwa kutokana na kiwango cha usafi wa moyo wake, hata kama sadaka inamuendea mtu ambaye haithamini. Kutokana na kiwango cha usafi wa moyo

wa mtu litazalika jambo zuri kwa yule aliyepewa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ameonyesha ukweli huu kama ifuatavyo:

"Wakati mmoja mtu alisema:" Nitatoa sadaka".

Usiku ule akachukua sadaka na bila kujua akampelekea mwizi. Siku iliyofuata watu wa mji wakaanza kusema:

"Ni jambo la kustaajabisha! Jana usiku mtu mmoja alimpa sadaka mwizi!"

Yule mtu akasema:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Sifa njema ziwe juu yako. Nitatoa sadaka leo pia"

Mara nyingine tena akachukua fedha zake na bila kujua akaziweka mikononi mwa kahaba. Siku iliyofuata watu wa mji wakaanza kusema tena:

"Haiwezekani! Jana usiku mtu mmoja alitoa sadaka kwa kahaba".

Yule mtu akasema tena:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Sifa njema ziwe juu yako hata kama nimetoa sadaka kwa kahaba. Nitatoa sadaka tena"

Mara nyingine tena yule mtu akachukua alichoandaa kwa ajili ya sadaka na kuondoka nyumbani kwake. Wakati huu ikaanguakia kwenye mikono ya tajiri. Siku iliyofuata watu wa mji wakaanza kusema tena kwa mshangao:

"Hiki nini! Jana usiku sadaka alipewa tajiri!"

Yule mtu akasema tena:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Ninakushukuru kwa kuwa na uwezo wa kutoa sadaka ikiwa ni kwa mwizi, kahaba au tajiri".

Matokeo ya moyo safi wa mtu huyu, alimuona mtu katika ndoto akimwambia:

"Labda sadaka uliyompa mwizi itamsuta na kumfanya aache kuiba. Na kahaba pengine itakuwa ni majuto kwake juu ya alichokuwa akifanya na kuwa mwanamke mtulivu. Na labda tajiri atachukua tahadhari na kutoa sadaka kwa masikini kutokana na mali alizopewa na Mwenyezi Mungu. *(Bukhari, Zakat, 14)*

Na hizi ndizo Baraka za kuwa na moyo safi na kujitolea kwa kweli…Kinachoonekana katika hadith hii ni ulazima wa moyo safi na kujitolea kutoka ndani ya moyo wa mtu anayetoa sadaka. Pia inaonyesha kuwa nia ni bora kuliko matendo. Isieleweke kuwa mtu utoe sadaka bila uangalifu. Kinyume chake ukitoa sadaka ni muhimu uzingatie wenye kuhitaji, na lazima uwatafute wenye kuhitaji zaidi na uwape.

Tukio lifuatalo linaonyesha wazi mafunzo ya hadith iliyotajwa hapo juu.

Wakati wa safari ya Shaykh Sami Ramazanoglu ya kwenda Anatolia, mtu mmoja alisimamisha gari lake ndani ya Urgup na kuomba fedha za kununulia sigara. Licha ya upinzani – ambao haukusemwa, lakini ulikuwa ndani ya mioyo ya baadhi ya wasafiri wenzake, Shaykh Sami, ambaye alikuwa ni bahari ya ukarimu alisema:

"Kwa sababu anaomba, [ni sawa] tukimpa" na kwa mshangao wa wale waliokuwepo karibu naye alimpa yule mtu fedha bila kusita. Kwa kuvutiwa na hili, yule masikini alibadilisha nia yake na kusema:

"Sasa nitaenda kununua mkate kwa fedha hii" na akaondoka.

Huu ni mfano dhahiri wa umuhimu wa wema unaotokana na kiwango cha usafi wa nia ya mtu na chanzo cha halali cha mali ya mtu.

❁

Wakati wa miaka ya mwanzo katika historia ya Uislamu mtu mmoja asiyejulikana alikuwa akiacha gunia la chakula katika milango ya masikini mbalimbali wa Madina kila asubuhi. Siku moja wale masikini waliamka bila ya kukuta mfuko wa vitu milangoni mwao. Wakati wanajiuliza ni kwa sababu gani wakasikia tangazo la kuhuzunisha la kifo cha mjukuu wa Ali aitwae Zayn-al-abideen. Mji wa Madina ulitikiswa na habari hizi na watu wake walihuzunika sana.

❁

Maandalizi ya mwisho yakaanza kufanywa kwa yule mrithi wa Mtume kwa uangalifu. Ilipofika wakati wa kumuosha mwili wake, mtu aliyekuwa akimuosha aliona majipu mgongoni mwa maiti. Alistaajabishwa na kushindwa kuelewa sababu. Mtu mmoja kutoka *ahl'lul bayt*[14] ambaye alijua siri alielezea:

"Kila asubuhi Zayn-al-abideen alikuwa akichukua magunia ya vyakula aliyoyaandaa na kuyapeleka kwenye milango ya masikini. Alikuwa akirudi bila ya mtu yeyote kumuona. Hakuna mtu aliyejua kuwa ni yeye aliyekuwa akiwapelekea vile vitu. Hivi vidonda mnavyoviona ni matokeo ya kuyabeba yale magunia" (Ibn-i Kathir, al-Bidaya, IX, 112, 133; Abu Nuaym, Hilye, III, 136)

Huu ni udhihirisho wa usafi ndani ya moyo wa muumini uliojaa huruma. Huu ni unyeti ulioonekana katika kipindi cha maisha ambao ni kukataa kukosa zawadi ya wema kwa pongezi za binadamu wa kawaida.

❁

14. ahl'ul bayt ni familia ya Mtume. (Maelezo ya mfasiri).

Ufuatao ni mfano mwingine mzuri wa moyo safi ulioonyeshwa na Sultani Alparslan ambaye moyo wake ulikuwa pamoja na mola wake.

Mwaka 1071 kabla ya kuingia katika vita ya Malazgirt, Alparslan alivaa nguo safi na nyeupe na alisema: "Hii ni sanda yangu". Kwa maneno mengine, alikuwa tayari amejiandaa si kwa ajili ya umaarufu wa kidunia bali kwa kufa shahidi kwa furaha iliyotokana na imani safi. Kabla ya kwenda vitani alitoa hotuba hii fupi kwa askari wake:

"Ama napata ushindi na kufikia lengo langu, au nakuwa shahidi na kwenda mbinguni. Wale ambao wanachagua kunifuata mimi, wafanye hivyo. Wale ambao wanachagua kuondoka, basi waondoke. Hapa hakuna Masultani wanaotoa amri, na wala hakuna askari wanaohitaji kutii. Leo mimi ni mmoja kati yenu. Ni askari anayeenda vitani pamoja nanyi. Wale watakaonifuata na kuwa mashahidi wakawa wamejitolea nafsi zao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mtukufu – mtaenda mbinguni; wale watakaobaki hai watakuwa ni mashujaa wa vita. Na kwa wale ambao watatukimbia, moto wa Akhera na aibu katika dunia hii vitawasubiri".

Kutokana na usafi ndani ya moyo wa Sultani Alparslan, Mwenyezi Mungu mtukufu alimfanya kuwa mshindi dhidi ya Diyogen wa Rumi, ambaye jeshi lake lilikuwa mara tano ya ukubwa wa jeshi lake.

Kama ilivyotajwa kabla wale watu wenye moyo safi ndiyo watakaopata uongofu wa kweli. Hata hivyo wenye moyo safi wako katika hatari kubwa na mitihani. Vilevile mauaji yaliyolengwa kwa kamanda mkubwa wa Uislamu, Sultani Alparslan ilikuwa ni mtihani. Hili ndilo lililotokea:

Mwaka 1072 baada ya ushindi ndani ya Malazgirt, Sultani Alparslan aliandaa safari kuelekea Maveraunnehir. Alikuwa na

farasi wengi. Aliizingira himaya ya Hana ambayo ilikuwa kwenye mto wa Amuderya. Kamanda wa himaya hiyo alikuwa ni Yusuf al-Harazmi ambaye alikuwa ni mwanachama wa kikundi cha urithi kiitwacho *Batiniyye*. Alipoona himaya yake haiwezi tena kushindana na upinzani alimjulisha Alparslan kuwa amejisalimisha. Hata hivyo huyu mhalifu mwenye hila alipoletwa mbele ya Alparslan, mara akamjeruhi kwa kisu. Haraka akauawa na sultani Alparslan hakujali kitu juu yake. Tarehe 25 Octoba, 1072 akawa amerudi kwa Mola wake. Maneno yake ya mwisho yalikuwa kama ifuatavyo:

❁

"Wakati wowote nilipokuatana na adui nilijikinga kwa Mwenyezi Mungu aliye juu na kuomba msaada wake. Jana nilipopanda mlima, ilikuwa kana kwamba ule mlima chini ya mguu wangu unatikisika kutokana na namba na ukubwa wa jeshi langu. Ndani ya moyo wangu nikafikiria:" Mimi ni mtawala wa dunia, nani anayeweza kunishinda?" Kwa matokeo yake Mwenyezi Mungu mtukufu akaniadhibu kwa kupitia mmoja wa waja wake dhaifu. Naomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu mtukufu kwa fikira hizi zilizonijia kichwani na kwa makosa niliyofanya huko nyuma, na ninarudi kwake. Hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu mmoja na Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu…"

Bila shaka hii ni hali ya wema wa kweli na moyo safi unaojiwajibisha.

Mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu aliulizwa kama aliwahi kutokewa na tukio ambalo lilihusu moyo safi na likaacha mvuto katika maisha yake, akajibu:

"Ndiyo ninalo" na akaelezea:

"Wakati mmoja nilipoteza mfuko wangu ndani ya Makka na nikaachwa bila fedha. Nilikuwa natarajia fedha kutoka Basra lakini

zilishindwa kufika. Nywele zangu na ndevu zilikuwa ni ndefu kiasi fulani. Nikaenda kwa kinyozi na kumuuliza:

"Sina fedha, unaweza kuninyoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?"

Wakati ule kinyozi alikuwa akinyoa mtu. Akionyesha kiti kinachofuata akamwambia:" kaa hapa" na akamuacha yule mtu na kuanza kumnyoa yeye. Yule mtu akakataa. Kinyozi akamgeukia na kusema:

"Samahani bwana. Nilikuwa nikikunyoa kwa fedha lakini huyu mtu ameniomba nimnyoe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Mambo yanayofanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu yanapewa kipaumbele na hayana ushuru. Waja hawawezi kujua gharama za mambo yaliyofanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kamwe hawawezi kuyalipia".

Baada ya kuninyoa aliingiza vipande kadhaa vya dhahabu ndani ya mfuko wangu:

"Unaweza kukidhi mahitaji yako muhimu kwa hivi, hivi ndivyo nilivyonavyo, samahani".

Siku chache zikapita. Zile fedha nilizokuwa nikizisubiria kutoka Basra zikawasili. Nikachukua pochi ndogo ya dhahabu nikampelekea kinyozi lakini akakataa:

"Sitachukua kamwe! Hakuna mja wa Mwenyezi Mungu awezae kulipa thamani ya amali iliyofanywa kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Unaweza kwenda. Mwenyezi Mungu akupe amani".

Nikakubaliana naye na kwenda zangu lakini kwa miaka 40 sasa ninaamka katikati ya usiku na kumuombea.

Hivyo Mwenyezi Mungu atalipa kwa zile amali njema kwa wema utokanao na utukufu wake ilimradi ziwe zimefanywa kwa moyo safi, yaani kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

❁

Katika kipindi cha mfungo wa Ramadhani matajiri wengi ndani ya dola ya Uthmainiyya walikuwa wakitangatanga kwenye malisho yasiyotambulika katika mavazi ya kawaida. Wakienda masokoni, grosari na maduka ya mji na kuwaomba kuchukua vitabu vyao vya mahesabu. Waliwaambia wajumlishe madeni katika vitabu vyao bila ya mpangilio kuanzia mwanzo, katikati na kurasa za mwisho. Baada ya kujumuishwa walilipa kiwango kilichopatikana. Kisha waliondoka bila kujitambulisha huku wakisema:

"Futa madeni haya! Na tunamuomba Mwenyezi Mungu atukubalie amali hii".

Ikawa mwenye deni hajui nani aliyemlipia, na aliyefuta madeni yale hakujua ni nani aliyewalipia wadaiwa. Watu wale walijua kuwa sadaka iliyotolewa kwa siri inakubalika zaidi ya ile iliyotolewa hadharani, hivyo walijaribu kuwasaidia watu kwa siri kadri iwezekanavyo. Baba zetu waliotangulia walikuwa na moyo safi mno kiasi kwamba ilichotoa mkono wa kulia hakikujulikana na mkono wa kushoto na mara moja walisahau jema walilolifanya.

Marafiki watukufu wa Mwenyezi Mungu wamewashauri watu kusahau vitu viwili:

1. Amali njema ulizozifanya ili zisipelekee kujiona na kujivuna.

2. Mambo mabaya uliyofanyiwa ili hasira na kisasi visije vikatawala moyo wako.

Kwa ufupi moyo safi ni tunu ambayo ni ngumu kuipata na kuitunza ambapo hakuna awezaye kuilipa ila Mwenyezi Mungu

pekee, moyo safi ni ubora mkubwa ambao unampandisha mja daraja katika hii dunia na kesho Akhera na kumfanya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi hakubali amali zilizofanywa bila moyo safi. Siku ya kiama zile amali zilizofanywa kwa kujiridhisha mwenyewe na kujiona ambayo ni magonjwa ya moyo zitatupwa usoni mwa watendaji. Hivyo moyo safi unafanya kidogo kuwa kikubwa kwa rehema za Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi. Pia inafanya maisha ya mtu kuwa marefu na neema zake na mafanikio kuendelea.

3. *Taqwa*[15] (Uchamungu na kumfahamu Mwenyezi Mungu)

Taqwa inamaanisha kuulinda moyo dhidi ya kitu chochote kile asichokiridhia Mwenyezi Mungu au kitu chochote kinachokuweka mbali na Mwenyezi Mungu, hivyo kupelekea moyo kuwa ni kioo cha mambo mema. *Taqwa* inapatikana pale muumini anapojiweka kwenye ulinzi wa Mwenyezi Mungu na kujizuia na mambo ambayo yatasababisha madhara na maumivu ya hapa duniani na kesho Akhera, na kumuweka mbali na madhambi ili kupenda amali njema.

Mtume Muhammad ﷺ katika kumhutubia Abu Dharr alisema kwamba *taqwa* ndiyo kipimo pekee cha thamani ya mtu na kukubalika kwake mbele ya Mwenyezi Mungu:

"Jua kwamba wewe si bora zaidi ya mtu mwekundu wala mweusi. Ni *taqwa* pekee ndio inayokufanya kuwa na hadhi ya juu" (Ahmad, V, 158)

Mtume ﷺ alisema:

15. Neno *Taqwa* linatokana na neno waqa'a lenye kumaanisha kulinda, kutunza, kuzuia. Lina maana ya usafi, kujitolea na uchamungu. (Maelezo ya mfasiri).

"Mimi ndiye ninayemuogopa Mwenyezi Mungu zaidi miongoni mwenu". (Bukhari, Iman, 13; Muslim, Siyam, 74). Katika kila hatua ya maisha yake alifanya mambo katika kiwango cha *taqwa*. Ndiyo maana ni muhimu kushikamana na *sunnah*[16]za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ili kuwa muumini mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu.

Nabii Issa عليه السلام ameonyesha *taqwa* kwa vizuri zaidi kama ifuatavyo:

Wakati fulani mtu alimuendea Yesu na kumuuliza:

"Ewe Mwalimu wa wema na uongofu! Ni namna gani mja anapata *taqwa* mbele ya Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi?"

Yesu akajibu:

"Ni rahisi. Kwa kumpenda Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anavyostahiki kupendwa, kwa moyo wako na roho, na kwa kufanya amali njema kwa uwezo wako wote ili kumridhisha Yeye, na kuonyesha huruma na mapenzi kwa wana wote wa Adam kama ambapo ungelionyesha kwako".

Kisha akasema:

"Kamwe usimfanyie mwenzako usilopenda kufanyiwa wewe! Kisha utakuwa ni mtu mwenye *taqwa* ya kweli kwa Mwenyezi Mungu". (Ahmad, Az-Zuhd pg 59).

Siku moja Omar alimuomba Ubayy bin Ka'b afafanua *taqwa*. Ubayy bin Ka'b akamjibu:

"Ewe Omar, umewahi kutembea kwenye njia yenye miba?"

Wakati Omar alipojibu "Ndiyo nimewahi" kisha akamuuliza:

"Kwa hiyo ulifanya nini?"

16. Sunnah ni mkusanyiko wa mwenendo wa Mtume Muhammad. (Maelezo ya mfasiri).

Omar akajibu:

"Nilinyanyua mavazi yangu na kufanya juhudi zote ili kuzuia miba isinidhuru"

Juu ya hili Ubayy bin Ka'b alisema:

"Hiyo ni *taqwa*" (Ibn-i Kathir, Tafsir" ul Qur'an al Azim, Beirut 1988, I, 42).

Hali ya *taqwa* ni kutoka kwenye ukafiri na kumfanyia Mwenyezi Mungu washirika kana kwamba unakimbia moto. Dalili ya hili ni kwa mtu kufanya mambo ya faradhi sawasawa na kujizuia na madhambi yote.

Mtume mtukufu alisema:

"Mche Mwenyezi Mungu popote utakapokuwa, na fanya tendo jema baada ya baya ili lilifute hili baya. Na ishi na watu kwa tabia nzuri" (Tirmidhi, Bir, 55/1987)

Kilele cha *taqwa* ni wakati mja analinda moyo wake kutokana na kila kitu ambacho kitaufanya kughafilike na Mwenyezi Mungu na unarudi kwake kwa ukamilifu, kwa kiwango ambacho hakina kikomo. Hii hatua ya mwisho ndiyo *taqwa* ya kweli ambayo inaamrishwa katika aya zifuatazo:

"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu" (Al- Imran, 3: 102)

Ili kufikia kilele cha *taqwa* ni lazima mtu kuepuka mambo yenye kutia mashaka kwa gharama zote. Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema:

"Mtumwa wa Mwenyezi Mungu hawezi kufikia kiwango cha *taqwa* ya kweli isipokuwa aache mambo ambayo yana mashaka ili kuhofia kufanya kitu kilichokatazwa" (Tirmidhi, Qiyama, 19/2451, ibn - Maja, Zuhd, 24)

Abdullah ibn Omar anatuonya juu ya yafuatayo:

"Mtu hawezi kufikia daraja la kweli la *taqwa* bila kuachilia mambo yanayomfanya awe na wasiwasi na kusumbua moyo wake" (Bukhari, Iman, 1)

Ili kupata *taqwa* ni lazima mja daima aiwajibishe nafsi yake. Hii ni kwa sababu inawezekana tu kuimarisha *taqwa* ya mtu kwa kupinga tamaa kali ya nafsi inayoamrisha uovu, ambayo ni adui mkubwa wa moyo, na kuulinda kutokana na udanganyifu wake.

Ili kujizuia kuangukia katika mapambo yenye kuvutia aliyowekewa mbele yake, nabii Yusuf عليه السلام alionyesha kuwa tiba pekee ni kujikinga kwa Mwenyezi Mungu kwa kiwango kikubwa cha *taqwa*. Na hii inaonyesha kuwa ni lazima kuwa na *taqwa* ili kupata msaada wa Mwenyezi Mungu.

Mtume Muhammad ﷺ alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu mtukufu amjaalie *taqwa*:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie uchamungu katika moyo wangu, uutakase, kwani wewe ni mbora wa watakasao na uwe mlinzi na kiongozi wangu" (Muslim, Dhikr, 73)

"Ewe Mwenyezi Mungu! Nakuomba uongofu, uchamungu, uvumilivu na utajiri wa moyo" (Muslim, Dhikr, 72)

Aliye mbora zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule mwenye kiwango cha juu cha *taqwa* au uchamungu[17]. Mwenyezi Mungu mtukufu anawapenda waja wake wema[18] na daima yuko pamoja nao[19]. Amewaahidi waja wake wema pepo ambayo upana wake ni baina ya mbingu na ardhi[20]. Mwenyezi Mungu mtukufu anawapa waja wake wema uwezo wa kutofautisha mema na maovu na ana-

17. Angalia Al Hujurat, aya ya 13.
18. Angalia Al Imran, aya ya 76.
19. Angalia An Nahl, aya ya 128
20. Angalia Al Imran, aya ya 133

samehe madhambi yao[21]. Anawaonyesha njia wakati wa dhiki na anawapa kutoka wasipokutarajia. Anawarahisishia mambo yao, anawasamehe maovu yao na kuwaandalia malipo makubwa[22].

Kwa mujibu wa masimulizi ya Abu Dharr Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema:

"Naijua Aya, kama watu watashikamana nayo itawatosha".

Maswahaba wake wakamuuliza:

"Ni Aya ipi hiyo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?"

Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwasomea kifuatacho kutoka katika Qur'an tukufu:

"Na anayemcha Mwenyezi Mungu humtengezea njia ya kutokea" (Talaq, 65: 2) (ibn Majah, Zuhd, 24)

Wale ambao wana ucham ngu ndiyo walio karibu zaidi na Mtume kiroho. Muadh bin Jabal anasema yafuatazo:

"Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu aliponituma kwenda Yemen kama gavana, akanisindikiza mpaka nje kidogo ya Madina kwa kuniaga. Nilikuwa juu ya mnyama wangu wakati yeye alikuwa akitembea. Baada ya kunipa ushauri alisema:

"Ewe Muadh! Unaweza usinione tena baada ya mwaka huu. Inawezekana ukirudi kwenye msikiti wangu huu ukakuta kaburi langu".

Niliposikia hayo, nilianza kulia kutokana na huzuni ya kutengana na rafiki kama Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema:

21. Angalia Al Anfal, aya ya 29
22. Angalia Al Talak, aya ya 2-5

"Usilie ewe Muadh!". Na huku akigeuza uso wake kuelekea Madina, alisema:

"Wale ambao wako karibu na mimi ni wale ambao wana uchamungu mbele ya Mwenyezi Mungu popote watakapokuwa" (Ahmad, V, 235 Haythami, Majmua'z - Zawaid, Beirut, 1988, IX, 22)

Mtume akasema pia:

"Bila shaka rafiki zangu ni wale wema zaidi" (Abu Dawud, Fiten, I/4242).

Moyo ulio na *taqwa* unatukuzwa kwa kuwa chini ya usimamizi wa Mwenyezi Mungu na unakuwa ni mahala pa mwangaza wa hekima na siri ya Mwenyezi Mungu.

❁

Matukio ya wema

Wanazuoni wa kweli na marafiki wa Mwenyezi Mungu kama vile Abu Hanifa, Imam Shafii', Ahmad bin Hanbal waliishi kwa *taqwa.* Wakati mmoja Imam Abu Hanifa akijaribu kusafisha doa dogo katika nguo yake aliulizwa:

"Ewe Imam! Kutokana na *fatwa*[23] uliyoitoa hili doa dogo si kizuizi cha swala; sasa kwa nini unafanya juhudi kubwa kulitoa?"

Abu Hanifa akajibu:

"Hiyo ni *fatwa*, na hii kwa upande mwingine ni *taqwa"* …

Kama inavyoweza kuonekana *taqwa* ni kuonyesha kujali na kuzingatia kwa hali ya juu maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu.

23. Fatwa ni hukumu ya kisheria inayohusiano na mambo ya uislamu inayotolewa na mwanachuoni aliyebobea. (Maelezo ya mfasiri).

Hadith ifuatayo inaonyesha vizuri uchamungu wa mwanamke ambaye alikuwa hazungumzi ila Aya za Qur'an kwa kuhofia kuangukia kwenye dhambi:

Abdullah bin Mubarak anasimulia:

Wakati mmoja nilitoka kwa lengo la kwenda kuhiji katika nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu, Al-kaaba na kutembelea kaburi la Mtume, nikaona kitu cheusi katikati ya njia. Nikaangalia kwa makini nikamuona mwanamke aliyevalia koti lililotengenezwa kwa pamba na nikabu ya pamba kichwani mwake…Nikamsalimia:

"Asalaamu alaykum Wa rahmatullahi Wa barakatuhu (amani, rehema na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako)".

Akajibu kutoka surat Yasin ndani ya Qur'an:

"Amani!" Neno kutoka kwa Mola Mlezi Mwenye kurehemu".

"Mwenyezi Mungu akujaalie wema! Unafanya nini hapa?" aliuliza.

Akajibu kwa Aya ya 186 ya Surat A'raf:

"Aliyemwacha Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumwongoa".

Nikatambua kuwa alikuwa amepotea njia. Hivyo nilimuuliza:

"Unataka kwenda wapi?"

Akajibu kwa sehemu ya Aya ya kwanza ya Surat Isra:

"Ametakasika ambaye alimchukua mja wake katika safari ya usiku kutoka katika Msikiti wa al - Haram na kuelekea Msikiti wa al - Aqsa".

Nilimuelewa kwamba alikuwa amefanya Hija na alitaka kwenda Yerusalemu. Nilimuuliza:

"Umekuwa hapa kwa siku ngapi?"

Akajibu na Aya ya 10 ya Surat Mariam:

"Kwa masiku matatu, na hali ni mzima"

"Je, una kitu chochote cha kula" nilimuuliza.

Yeye akasoma Aya ya 79 ya surat Shu'ara:

"Yeye anipaye chakula na kinywaji"

"Jinsi gani unaweza kuchukua udhu katika jangwa hili kavu?" Nikamuuliza.

Yeye akajibu na Aya ya 43 ya Surat Nisaa:

"(Kama) huwezi kupata maji yoyote, basi tayammam[24] [jisafishe] na udongo safi".

"Nina chakula. Je, unaweza kula?" niliuliza. akajibu kwa sehemu ya Aya ya 187 ya surat Baqara:

" ... kisha timiza funga mpaka usiku uonekane".

"Huu si mwezi wa Ramadhani "Nikasema. Akajibu kwa sehemu ya Aya ya 158 ya surat Baqara:

"Kama mtu atafanya jema, Mwenyezi Mungu ni mwenye shukurani na mjuzi"

"Kuvunja funga ni halali wakati uko safarini" nilisema. Akajibu kwa sehemu ya Aya ya 184 ya surat Baqara:

"Lakini kufunga ni bora kwenu, ikiwa mnajua".

24. Tayammam ni namna ya kujitwaharisha wakati hakuna maji. Inatekelezwa kwa kupangusa uso na mikono kwa kutumia udongo safi, au kilicho sawa na hiki. (Maelezo ya mfasiri).

"Kwa nini huzungumzi na mimi kwa namna ninavyozungumza na wewe?" nilimuuliza. Akajibu kwa kusoma Aya ya 18 ya surat Qaf:

"Hatoi neno hata moja, bila ya muangalizi juu yake, kalamu mkononi!"

"Je, naweza kukuchukua kwenye ngamia wangu na kukupeleka kwenye kabila lako?" niliuliza. Akajibu kwa sehemu ya Aya ya 197 kutoka katika surat Baqara:

"Chochote kizuri unachokifanya, Mwenyezi Mungu anakijua".

Nikaandaa ngamia wangu tayari kwa yeye kupanda. Akasoma sehemu ya Aya ya 30 ya surat Nur:

"Waambie waumini kwamba wanapaswa kuinamisha macho yao".

Wakati alipopanda juu ya ngamia, akasoma sehemu ya Aya ya 13 ndani ya surat Zuhruf:

"Ametakasika aliyemfanya huyu atutumikie, na tusingeliweza kufanya haya wenyewe".

Tulipoanza kusogea akasoma kutoka katika Aya ya 20 ya Surat Muzammil:

"Basi someni kilicho chepesi katika Qur'ani".

Kwa kuongozwa na Aya ya 269 ya surat Baqara nikasema:

"Aliyepewa hekima bila ya shaka amepewa heri nyingi".

Nikamuambia:

"Umepewa heri nyingi". Akamalizia Aya hii:

"Hakuna anayezingatia ila watu wenye akili".

Mwisho tukafikia msafara wake.

"Huu ni msafara wako. Una nani ndani yake?" nikauliza.

Akasoma Aya ya 46 ya Surat Kahf:

"Mali na watoto ni pambo la maisha ya dunia"

Nikaelewa kwamba alikuwa na watoto katika lile kundi. Nikauliza:

"Ni upi wajibu wao katika kundi la Hijja?

Akasoma Aya ya 16 ya surat Nahl:

"Na alama nyingine. Na kwa nyota wao wanajiongoza"

Nikaelewa kwamba watoto wake walikuwa viongozi wa msafara huo. Nikionyesha mahema nikamuuliza:

"Nani kati ya hao ni watoto wako? akajibu:

"Mwenyezi Mungu alimchukulia Ibrahim kama rafiki yake wa karibu sana, na Mwenyezi Mungu aliongea moja kwa moja na Musa. Yahya, chukua kitabu kwa nguvu".

Kisha nikaupigia kelele msafara:

"Ewe Ibrahim, ewe Musa, ewe Yahya". Vijana watatu wenye kung'aa kama mwezi wakaja. Walipokuja na kukaa chini, mama yao aliwasomea Aya ya 19 kutoka Surat Kahf:

"Hebu mtumeni mmoja wenu na hizi fedha zenu aende mjini, akatazame chakula chake kipi kilicho bora kabisa akuleteeni kwa ajili ya kula" (Kahf, 50:19)

Mmoja wa vijana alikwenda kununua chakula na kukiweka mbele yao. Yule mwanamke alisoma Aya ifuatayo kutoka katika Surat Haqqa:

"Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya mlivyotanguliza katika siku zilizo pita!" (69:24).

Niliwaambia watoto wa mwanamke yule:

"Chakula chenu kiwe haramu kwangu kama hamtaniambia hali ya mama yenu"

Juu ya hili vijana walisema:

"Kwa miaka 40 sasa, mama yetu hasemi kitu ila Aya za Qur'an kwa kuhofia kuanguka katika makosa mbele ya Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema".

Kisha nikasoma kutoka Surat Jumu'ah:

"Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu anayompa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kubwa" (62:4)

Matakwa ya *taqwa* ni kwamba mtu anaacha ambayo yanatia mashaka na hata ya halali kutokana na hofu ya kufanya jambo la haramu. Mfano wa hili ni kama ifuatavyo:

Sultani Abdulaziz Han, ambaye alilifanya jeshi lake na meli zake kuwa katika nafasi ya juu na yenye kuvutia, alitatua migogoro ya ndani kwa ujuzi mkubwa wa siasa, na ambaye alipandisha hadhi ya serikali yake na kufikia ufahari wake kama zamani, aliivutia dunia nzima. Matokeo yake sultani alialikwa Ufaransa na Uingereza.

Abdulaziz Han, ambaye alikuwa mtu wa dini zaidi ya masultani wengine alichukua wapishi kutoka Bolu na kwenda nao, akifikiria kuwa chakula cha watu wa Ulaya kingelikuwa kinatia mashaka chini ya viwango vya sheria za Kiislamu.

Abdulaziz Han alikuwa ni mtu mwema na aliyeishi katika maisha mazuri ya dini. Alikuwa na uchamungu wa hali ya juu kiasi kwamba hakunywa maji mengine yoyote katika maisha yake yote

isipokuwa maji ya *zamzam*[25]. Alikuwa akiswali kwa namna ya kipekee na akisoma Qur'an mara kwa mara. Alipouawa kikatili, Qur'an tukufu ikiwa imefunguliwa katika surat Yusuf ilikutwa juu ya meza ndogo ndani ya chumba chake. Hii Qur'an tukufu ambayo ilikuwa na matone ya damu iliyobarikiwa imehifadhiwa katika kasri la Topkapi.

Mtume anasema katika *hadith*:

"Mtu anakufa juu ya hali aliyokuwa akiishi nayo na atahukumiwa juu ya hali aliyokufa nayo" [26].

Mtu mwingine katika historia ambaye aliishi kwa *taqwa* ya hali ya juu ni sultani Abdulhamid II. Aliamuru aamshwe muda wowote usiku kama jambo lolote litatokea, hakukubali kuacha jambo lifike siku inayofuata. Mwandishi wake aitwae As'ad Bey anahaditha katika kitabu cha kumbukumbu:

"Usiku mmoja niligonga mlango wa sultani katika usiku wa manane ili kumuomba asaini nyaraka muhimu lakini hakufungua mlango. Nilisubiri kidogo kabla ya kugonga tena, lakini hakufungua mlango. Nilihofu na kudhani ikiwa sultani ameshaitwa na Mwenyezi Mungu. Nikagonga tena kwa kirefu ndiyo sultani akafungua mlango akiwa na taulo mkononi. Alikuwa anafuta uso wake. Alitabasamu na kusema:

"Mwanangu! Nadhani saa hii umekuja kwa jambo muhimu sana. Niliamshwa kwa wito wako wa kwanza lakini nilichelewa kujibu kwa sababu nilienda kuchukua udhu. Hii ni kwa sababu kamwe sijasaini nyaraka yoyote kwa ajili ya watu wangu bila ya

25. *Zamzam* ni maji kutoka kwenye kisima kilichoko Makka, ambacho kiligunduliwa na Hajar, mke wa Ibrahim. (Maelezo ya mfasiri).
26. Angalia Muslim, Jannah, 83; Munawi, Fayzu"l Qadir, Beirut 1994, V, 663)

kuchukua udhu kwanza. Niletee nisaini…" na alisaini ili nyaraka kwa kuanza na *Bismillah*[27]".

Mke wa Abdulhamid II alisimulia yafuatayo katika kuonyesha kiwango chake cha hekima:

"Abdulhamid Han daima alikuwa akiweka kigae kisafi katika mguu wa kitanda chake. Kila akiamka alikuwa akitayammam kwa kigae kile kabla ya kwenda kwenye beseni na kuchukua udhu kwa maji ili kujizuia asikanyage chini bila ya udhu. Siku moja nikamuuliza sababu ya kufanya hivi. Akanijibu kama ifuatavyo:

"Kama Khalifa wa Waislamu wengi sitakuwa makini katika viwango vya kutekeleza sunna, itasababisha umma wa Muhammad kuathirika…"

Maisha yake ya kiuchamungu yalimfanya awe na kipaji katika nyanja za siasa pia. Maono yake yamerikodiwa katika historia ya dunia kutokana na kanuni yake katika miaka ya hatari na ugumu.

Kwa kifupi *taqwa* iko juu ya mema yote ambayo ndiyo misingi ya dini na ambayo yanatakasa maisha ya mtu. Mtaji mkubwa ambao mtu anaweza kuwa nao ili kupata furaha katika maisha ya kesho Akhera ni *taqwa*. Maisha bila *taqwa* yamejaa hatari kubwa. Maisha bila misingi ya *taqwa* yatasababisha hasara ya milele katika pumzi ya mwisho kama ilivyoonyeshwa katika hadith isemayo "Vyovyote utakavyoishi, ndivyo utakavyokufa". (Munavi, V, 663) -Mwenyezi Mungu atulinde. Ili tujilinde kutokana na uovu unaosababishwa na matamanio ya mwili ndani ya dunia hii yenye kupita, ni muhimu kuishi kwa uangalifu kana kwamba tunatembea kwenye eneo lililopandwa milipuko.

27. Bismillah ni neno linalorudiwa mara kwa mara na waislamu wanapotaka kuanza jambo lolote na lina maanisha 'Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu'.

Vita vinapiganwa na vinafika mwisho baada ya muda fulani na mahali fulani. Na mapambano kati ya *taqwa* na nafsi inayoamrisha maovu lazima viendelee bila kusimama kwa kipindi chote cha maisha. Qur'an inatujulisha:

"Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini (kifo)". (Hijr, 15:99).

Mwenyezi Mungu mtukufu atujaalie kumtumikia yeye kwa taqwa na kuendeleza umakini dhidi ya kupuuzia maamrisho yake ambapo kunafungua milango ya kudanganywa na nafsi zetu.

Amin

4. Tawba na Istighfar

Mwanadamu ana tabia ya kuegemea kwenye dhambi atakaposhindwa na matamanio ya nafsi yake na anapopoteza nuru ya imani. Wakati msaada wa dhamira ya maadili mema unapopungua unasababisha busara na imani kutoweka. Udhaifu mkubwa unajitokeza katika njia ya kuelekea kwenye maadili. Madhambi yanakuwa kama muziki mtamu katika nafsi na yanafanywa bila ya kujali uzito wa matokeo yake mabaya.

Wakati mwanadamu anakuja katika dunia hii akiwa msafi bila ya dhambi yoyote kama kioo safi. Kisha akadhihirishiwa na Mwenyezi Mungu rehema ya dini ili kuulinda huu usafi. Kwa matokeo yake kama mja ataweza kuuhifadhi usafi wa asili na kufaidika na imani ya dini ataweza kujivua kizuizi cha kutozingatia maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Hii itamfanya akifanya dhambi ahisi ukubwa wa dhambi yake kutokana na maadili yake. Akiwa amejeruhiwa ataamka kutokana na hisia za wema ambazo zimejificha ndani yake. Moyo wake utajuta kwa huzuni kubwa na ataufungua kwa

mola wake huku akitoa machozi. Huku kuumia na kujuta kunaitwa *"Tawba"*. Kilio cha kuomba msamaha ambacho kinatoka moyoni kinaitwa "I*stighfar*".

Madhambi ni kikwazo cha kuingia peponi, kinyume chake *tawba* ambayo inaimarishwa kwa matendo mema na moyo wenye kutubia ni mambo yenye kukuokoa na moto:

Mtume Muhammad anasema:

"Mja atakapofanya dhambi doa jeusi linawekwa katika moyo wake. Akiachana na dhambi hiyo na kujiegemeza kwenye tawba, moyo wake husafishwa. Kama hatoacha ile dhambi madoa meusi yataongezeka na kufunika moyo wote. Hii ni hali ambayo Mwenyezi Mungu mtukufu ameitaja katika Qur'an:

"La hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao hao waliokuwa wakiyachuma" (Mutaffifin, 83:14) (Tirmidhi, Tafsir, 83/3334).

Imeelezwa katika hadith nyingine:

"Jambo kubwa na la kuzingatiwa na mtu ni kuhofia madhambi, dawa yake ni kufanya istighfar katika giza la usiku" [28].

Mtu yeyote akifanya dhambi ambapo inaweza kumtokea kila mtu kwa kuwa yeye ni mwanadamu, ni lazima atubu na kuomba msamaha haraka sana na kurudi kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu mtukufu anawasifu waja wake anaoridhika nao kama ifuatavyo:

"Na ambao pindi wafanyapo uchafu au wakajidhulumu nafsi zao humkumbuka Mwenyezi Mungu na wakamwomba msamaha kwa dhambi zao - na nani anayefuta dhambi isipo kuwa Mwenyezi Mungu? - na wala hawaendelei na waliyoyafanya na hali wanajua" (Al-Imran, 3:135).

28. Deylemi, al Firdaws bi Me"suri"l Hıtab, Beirut, 1986, I, 136

"Walikuwa wakilala kidogo tu usiku. Na kabla ya alfajiri wakiomba maghfira" (Adh-Dhariyat, 51:17-18).

Mwenyezi Mungu mtukufu anatufahamisha katika Aya nyingi kwamba atawasamehe wale waja wake ambao wanatubu kwa moyo safi. Anasema atabadilisha madhambi ya wale wanaorudi kwake kikweli kuwa thawabu:

"Isipokuwa atakayetubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema. Basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, mwenye kurehemu" (Furqan, 25:70).

Mtume mtukufu anasema:

"Mwenyezi Mungu aliye juu anafungua mikono yake nyakati za usiku ili kukubali toba za wale waliofanya madhambi mchana wake. Na anawafungulia mikono wale waliofanya madhambi nyakati za usiku. Inaendelea hivi mpaka jua lichomoze upande lilipozamia, ikimaanisha mpaka siku ya hukumu" (Muslim, Tawba, 31).

Sharti kuu la *tawba* ni kuwa na moyo safi. Mtu ambaye anavunja tawba yake mara kwa mara anakuwa ni mtu mwenye kuchezewa na shetani. Mwenyezi Mungu mtukufu anaeleza:

"Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala asikudanganyeni kuhusu Mwenyezi Mungu mdanganyifu" (Luqman, 31:33).

Kwa upande mwingine *tawba* na *istighfar* ni matendo ambayo yatamuweka mtu huru na maumivu ya hapa duniani na kesho Akhera. Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema kwamba:

"Katika aya zifuatazo Mwenyezi Mungu aliye juu amenifunulia uhakika wa mambo mawili kwa ajili ya umma wangu:

1. Mwenyezi Mungu si wa kuwaadhibu nawe umo pamoja nao.

2. Mwenyezi Mungu si wa kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha. (Anfal, 8:33)

"Nikiondoka ninawaachia uhakika wa pili, yani istighfar ambayo itazuia adhabu ya Mwenyezi Mungu na kuwalinda mpaka siku ya hukumu". (Tafsiri ya Tirmidhi, 8/3082)

Tawba na *istighfar* ni mambo mawili yenye ufanisi mkubwa katika kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, kwani asili yake ni kuwa yanaashiria majuto ya kweli na kujikinga kwa Mwenyezi Mungu. *Istighfar,* ambayo ina nafasi muhimu katika kumuelekea Mwenyezi Mungu na kupandisha hadhi ya moyo ni njia ya kipekee ya kujitakasa kutokana na dosari za kiimani. *Tawba* iliyokubalika inanyanyua pazia na kuondoa vikwazo vilivyopo kati ya mja na Mola wake na itaacha mapenzi kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi. Kwa namna hiyo Mwenyezi Mungu mtukufu anatueleza:

"Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanao jisafisha" (Baqara, 2:222)

Mtume Muhammad ﷺ alitoa mfano ufuatao katika kuelezea furaha ya Mola wetu wakati watu wanafanya *tawba* kwake:

"Mwenyezi Mungu alifurahikiwa sana na tawbah ya mja wake aliyekuwa katika msafara kwenye jangwa (la joto kali hakuna mtu) Akapotelewa na mnyama wake, chakula na maji, akakata tamaa ya kuvipata tena, akapumzika kidogo chini ya mti kupata kivuli chake, baada ya muda hivi mara kamuona mnyama wake kamsimamia (na vitu vyake) kwa ile furaha akasema, "Ewe Mwenyezi Mungu, Wewe ni mja wangu na mimi ni Mola wako" (Muslim, Tawba 7: Tirmidhi, Qiyamah, 49, Deawat, 99)

Katika hadith nyingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaelezea faida za *istighfar:*

"*K*ama mtu kamwe haachi kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atamuonyesha njia

katika magumu, furaha katika huzuni, na atamruzuku kutoka asipopatarajia" (Abu Dawud, Vitir, 26/1518; Ibn-i Maja, Adab, 57)

Hivyo jambo la muhimu kwa mja ni kutakasa nafsi yake na kuusafisha moyo wake. Yaliyoelezewa mpaka sasa kuhusu *tawba* na *istighfar* ni mwanzo tu wa hali hii. Pindi mtu atakapoingia ndani matendo mema ni lazima. Baada ya mtu kufanya matendo ya faradhi na ya sunna kwa usahihi ni lazima awe na maadili mazuri kama vile kuchunga haki za wengine, kuchunga haki za wazazi, kutoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kutafuta ukaribu na viumbe wengine kwa kuonyesha huruma na kuwasamehe.

Matukio ya wema

Mtume Muhammadﷺ anasema:

"Enyi watu! Tubieni kwa Mwenyezi Mungu na kumuomba msamaha, kwani mimi nafanya *tawba* kwake mara mia moja kwa siku" (Muslim, Zikir, 42)

❁

Ukweli kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu aliendelea kufanya *tawba* na *istighfar* kwa Mwenyezi Mungu wakati dhambi zake zote na zijazo zimesamehewa ni somo muhimu kwa umma wake na pia ni shukurani kwa neema alizopewa na Mwenyezi Mungu.

Mtume mtukufu ambaye alijua kuwa jukumu kubwa kwa mja ni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kumuabudu yeye wakati wote, alifanya *tawba* na alipenda *istighfar* kila wakati akiamini kuwa anahitaji kuongeza kiasi chake cha kuabudu. Pia alikuwa akifanya *tawba* na *istighfar* kwa ajili ya umma wake.

Ibn-i Omar ﵁ anasema:

Tulikuwa tukimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akisema maneno yafuatayo mara 100 katika kikao kimoja:

رَبِّ اغْفِرْ لِى وَتُبْ عَلَيِّ إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ

"Ewe Mwenyezi Mungu! Nisamehe na ukubali *tawba* yangu. Kwani wewe ni mwingi wa kupokeo *tawba* na mwingi wa kurehemu" (Abu Dawud, Vitir, 26/1516; Tirmidhi, Deawat, 3434)

Tawba na *istighfar* zilizofanywa na Mtume hazikuwa kwa sababu ya makosa au kasoro zake bali ilikuwa ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi na kupata radhi zake. Kwa kuwa Mtume alikuwa katika hali ya kujiongezea imani alikuwa akiendelea kufanya *istighfar* kila mara.

❁

Mtume wa Mwenyezi Mungu katika siku zake za mwisho alikuwa akisema mara kwa mara:

سُبْحَانَ اللهِ وَبِحَمْدِهِ أَسْتَغْفِرُ اللهَ وَأَتُوبُ اِلَيْهِ

"Ametakasika Mwenyezi Mungu na sifa zote njema ni zake, ninaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na ninatubu kwake"

Siku moja mke wa Mtume, Aisha رضي الله عنها alimuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ninakusikia ukisema maneno haya mara kwa mara, ni ipi sababu yake?

Mtume akajibu:

"Mola wangu alinijulisha kuwa nitaona ishara katika umma wangu. Tangu niione hii ishara nimekuwa nikisema haya maneno ya kutukuza. Niliiona hiyo ishara katika aya ifuatayo ndani ya surat Nasr, ambayo inaasharia kuikomboa Makka:

"Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi, na ukaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi, zitakase sifa za Mola wako Mlezi, na umwombe msamaha; hakika Yeye ndiye anayepokea toba" (Muslim, Salat, 220).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliufundisha umma wake njia mbali mbali za kufanya *istighfar*. Iliyo muhimu zaidi ya zote ni *Sayyid'ul Istigfar*, ambayo ameielezea katika hadith ifuatayo:

"Namna ya juu ya kufanya istighfar ni kwa mja kusema yafuatayo:

اَللَّهُمَّ اَنْتَ رَبِّى لاَاِلَهَ اِلاَّ اَنْتَ خَلَقْتَنِى وَاَنَا عَبْدُكَ وَاَنَا عَلَى عَهْدِكَ وَوَعْدِكَ
مَااسْتَطَعْتُ اَعُوذُبِكَ مِنْ شَرِّ مَا صَنَعْتُ اَبُوءُ لَكَ بِنِعْمَتِكَ عَلَىَّ اَبُوءُ ذَنْبِى
فَاغْفِرْلِى فَاِنَّهُ لاَيَغْفِرُ الذُّنُوبَ اِلاَّ اَنْتَ

"Ewe Mwenyezi Mungu! Wewe ni Mola wangu. Hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ila wewe. Umeniumba mimi na mimi ni mja wako. Nitachunga ahadi yangu niliyoiweka kwako hapo mwanzo kwa uwezo wangu wote katika maisha yangu yote. Najikinga kwako kutokana na uovu wa makosa niliyoyafanya. Nakiri mbele yako kwa shukurani juu ya neema ulizonijaalia na nakiri madhambi yangu. Basi nisamehe, kwani hakuna anayesamehe madhambi ila wewe"

❁

Mtume mtukufu akaendelea:

"Yeyote atakayesoma hii *Sayyad'ul istighfar* mchana kwa kukubali moyoni matunda yake na thamani yake ataingia peponi kama atakufa kabla ya usiku. Na yeyote atakayeisoma usiku akiamini kwa uhakika matunda yake na thamani yake basi ataingia

peponi kama atakufa kabla ya asubuhi" (Bukhari, Dawat, 2, 16; Abu Dawud, Adab, 100-101)

Ni muhimu kufanya *tawba* na *istighfar* na kisha kuziimarisha upesi kwa kufanya amali njema. Ibn Omar anaelezea:

"Siku moja mtu alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kuuliza:

❁

"Nimefanya dhambi kubwa, je nina nafasi ya kufanya tawba?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akauliza:

"Mama yako bado yupo hai?"

Swahaba akajibu "Hapana".

"Sawa, unaye shangazi?", akauliza.

Swahaba akajibu:

"Ndiyo ninaye".

Mtume aliposikia hivi akasema:

"Kama ni hivyo kaa naye vizuri. Shangazi wa upande wa mama ni kama mama". (Tirmidhi, Birr, 6; Ahmad, II, 13-14)

Hapa Mtume alimshauri swahaba wake ambaye alikuwa katika majuto makubwa na akifanya *istighfar* ili kuimarisha *tawba* yake kwa matendo mema. Alimjulisha kuwa amali njema na matendo mazuri vinaweza kuwa kifuto cha matendo mema na kuyafuta kabisa.

❁

Usiku mmoja Mtume Muhammad ﷺ alimuona Bilal رضي الله عنه katika ndoto. Siku iliyofuata akamuita Bilal aliyekuwa muadhin na kumuambia:

"Bilal! Jana usiku nilisikia milio ya viatu vyako mbele yangu. Niambie ni amali gani zilizokutanguliza peponi kabla yangu?"

Bilal akajibu:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Endapo nitafanya dhambi ndogo haraka sana ninanyanyuka na kuswali rakaa mbili nikiomba. Na nikipoteza udhu wangu haraka sana ninachukua udhu tena".

Juu ya hili Mtume alisema:

❁

"Hii ndiyo sababu".

Hivyo endapo tutafanya kosa lolote ni muhimu kufanya *tawba* haraka bila kupoteza muda na kufanya amali njema.

Ka'b bin Malik ﷺ ambaye kutokana na uzembe wake alikosa kushiriki kwenye msafara wa Tabuk kutokana na kuchelewa kwake kufika, haraka sana alifanya *tawba* na *istighfar* na kujutia kutokana na kosa lake hili na kuona kuwa dunia imekuwa nyembamba sana kwake. Alipopata taarifa kuwa tawba yake imekubaliwa akasujudu kutokana na furaha aliyokuwa nayo (Ibn'i Majah, Salat, 192). Baadaye akaamua kutoa sadaka kwa kutoa mali zake zote na kumpa Mtume. Lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu akamshauri kutoa nusu ya amali yake na kuacha sehemu iliyobaki kwa ajili ya familia yake (Bukhari, Megazi, 79).

Hii ni kwa sababu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akikubali sadaka za watu kulingana na hali zao. Hakutaka waje kujuta baadaye kutokana na walichokitoa na kufanya malipo yao yapungue.

❁

Mwenyezi Mungu mtukufu anawatoa kutoka katika magumu wale waja wake wanaofanya *tawba* na *istighfar* na anawapa neema nyingi. Wakati mmoja watu wanne walikuja kulalamika kwa Hassan al Basri. Mmoja alilalamika kuhusu ukame, mwingine kuhusu njaa, mwingine kuhusu upungufu wa mavuno na wa mwisho alilalamika kuwa hana watoto. Walimuomba msaada. Huyu mtakatifu mkubwa aliwashauri kila mmoja kufanya istighfar. Watu waliomzunguka wakasema:

"Matatizo na magumu ya hawa watu ni tofauti lakini wewe unawashauri wote wafanye kitu kimoja". Hassan al Basri akawajibu kwa kuwasomea Aya ifuatayo kutoka katika Qur'an:

"Ombeni msamaha kwa Mola wenu Mlezi; hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe. Atakuleteeni mvua inyeshe mfululizo. Na atakupeni mali na wana, na atakupeni mabustani na atakufanyieni mito". (Nuh, 71:10-12) (Ibn-i Hajar, Fethu'l-Bari, XI, 98; Ayni, Umdetu'lKari, Beirut ts. XXII, 277-278)

Kuchelewa kufanya *tawba* kutokana na kushindwa na vitimbi vya Shetani ni sawa na kupoteza maisha ambayo ni jambo baya mno kwa mtu kulipoteza. Muumini mwerevu ni lazima aharakishe kutubia madhambi yake na kujiandaa na pumzi yake ya mwisho.

Kutokana na masimulizi fulani fundi cherehani alimuuliza mtu mwema:

"Unasema nini kuhusu hadith ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu inayosema:" Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anakubali tawba ya mtu kabla ya roho yake kufika kooni" (Tirmidhi, Dawat, 98/3537). Yule mtu mwema akamuuliza fundi cherehani:

❁

"Ndiyo hivi ni kweli. Lakini niambie, unafanya kazi gani?"

"Mimi ni fundi cherehani, ninashona nguo".

"Ni kitu gani kirahisi sana katika kushona nguo?"

"Kuchukua mkasi wangu na kukata kitambaa".

"Kwa muda gani sasa umekuwa ukifanya shughuli hii?"

"Kwa miaka 30".

"Je, roho yako ikifika kooni utaweza tena kukata kitambaa?"

"Hapana, sitoweza".

"Ewe fundi cherehani! Ikiwa utashindwa kufanya ulichokuwa unakifanya kwa miaka 30 ambacho umejifunza kwa muda mrefu, sasa utawezaje kufanya tawba wakati huo ikiwa kamwe hujawahi kufanya hivyo katika maisha yako? Fanya tawba wakati huu ukiwa na nguvu zako na uimara! Vinginevyo wakati wa pumzi yako ya mwisho hutapata msamaha wala mwisho mwema... Haukuwahi kushauriwa kufanya tawba haraka kabla mauti hayajakufika?" (Munawi, V, 65).

Kutokana na haya haraka sana fundi cherehani akatubu kwa moyo safi na kuwa mtu mwema.

Mtume alitujulisha kuwa namna mtu anavyoishi ndivyo atakavyokufa na namna anavyokufa ndivyo atakavyofufuliwa." [29]

Siku moja Bayazid-i Bistami alipopita mahali na kumuona daktari akiandaa dawa alimuuliza:

"Ewe daktari! Una tiba ya ugonjwa wangu?"

Daktari akamuuliza:

"Una ugonjwa gani?"

"Ugonjwa wa dhambi" akajibu.

Daktari akanyanyua mikono yake yote na kusema:

29. Angalia Muslim Jannah, 83 Munavi, V, 663

"Sijui tiba ya ugonjwa wa dhambi".

Wakati ule kijana mwendawazimu (majzuub) aliyekuwa pale aliwakatisha:

"Ninajua tiba ya ugonjwa wako" alisema. Bayazid akamuambia Kwa furaha:

"Niambie kijana".

Kijana ambaye watu walifikiria ni mwendawazimu lakini kiukweli ni mtu mwenye elimu, aliwaelezea tiba ya ugonjwa wa dhambi kama ifuatavyo:

"Chukua dram 10 za mzizi wa *tawba* na majani 10 ya *istighfar*. Yaweke ndani ya kinu cha moyo wako, vitwange kwa mchi wa *tawheed,* chekecha katika chekecheo la usawa, ifinyange kwa machozi yako, ipike katika oveni ya upendo na majuto. Kunywa vijiko viwili vya mchanganyiko huu kila siku, hakitabaki chochote katika ugonjwa wako".

Bayazid'i Bistami akiwa anasikiliza kwa makini alivuta pumzi na kusema:

"Masikitiko kwa wale wanaodhani ni werevu na kuwaita wendawazimu watu wenye busara kama wewe".

Kwa kifupi mwanadamu hawezi kujizuilia moja kwa moja kutofanya makosa, hivyo ni lazima wakati wote *tawba* na *istighfar* viwe mdomoni mwake. Pia ni lazima aisajili na kuiwajibisha nia yake kwa amali njema. Istighfar na amali njema ni mambo muhimu yatakayomfanya mtu awe mja mwema wa Mwenyezi Mungu. Tunaambiwa yafuatayo katika Qur'an:

"Enyi watu! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala mdanganyifu asikudanganyeni juu ya Mwenyezi Mungu" (Faat'ir, 35: 5)

Kucheleweshа kutubu madhambi mpaka sehemu ya mwisho ya uhai wa mtu kwa kufuata matamanio ya nafsi na shetani ni hadaa kubwa ambayo mwisho wake ni hasara. Hivyo ni muhimu kutubia na kuomba msamaha na kuwa mkweli wa nafsi na kusimama katika matendo mema. Kama hali inavyomlinda mtu na mabalaa na matatizo, vilevile inamuwezesha kupata neema na fadhila za Mwenyezi Mungu.

5. Kutii maamrisho ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake

Daraja la kiimani la muumini linatokana na kiwango chake cha kutii maamrisho ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake. Na ukamilifu wa imani ya mtu unaongezeka kutokana na kiwango cha umakini, sensitivity, upendo na hamasa katika utii huu. Wale watu wanaopanda daraja katika upendo wao na utii wapo katika neema za Mwenyezi Mungu hapa duniani na kesho Akhera. Imeelezwa katika Aya ndani ya qur'an:

"Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!" (Nisaa 4:69)

Mtume wa Mwenyezi Mungu ametujulisha:

"Mola wenu mwenye kutukuzwa anasema:" Kama mja wangu angelinitii namna inavyostahiki kunitii, Nilingeliifanya mvua inyeshe usiku na jua liwachomozee mchana. Na Nisingeliruhusu wasikie hata mngurumo wa radi". *(*Ahmad, II, 359; Hakim, IV, 285/7657)

Nyoyo za wale wanaotii maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa upendo na unyenyekevu na ambao wanatunza hali yao hii ya uvumilivu katika hali mbali mbali watakuwa ni mifereji ya hekima, wema na mafanikio. Kinyume chake zile nyoyo na miili ambayo

haijalindwa kutokana na mambo haramu na yenye kutia wasiwasi vitaelekea katika maasi na viota vya uovu.

Matukio ya wema

Kabla ya kuingia kwenye vita vya Badr, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitaka kujua mawazo ya maswahaba wake. Mikdad bin Aswad رضي الله عنه alisimama na kutoa hotuba ifuatayo:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Fanya uliloamrishwa kufanya. Tupo pamoja na wewe. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa hatutakwambia yale wana wa Israel waliyomuambia Musa عليه السلام. Walisema:"...Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa". (Maida 5:24).

❁

Naapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye amekutuma wewe kama Mtume wa kweli ambaye tukiwa na wewe tunaweza kuvumilia magumu makubwa hata kama tutatembea mpaka Birku'l Gimad[30]30. Wakati wote tupo tayari kupambana na maadui tukiwa kuliani kwako, kushotoni kwako, mbele yako na nyuma yako mpaka mwisho wa mapambano[31]. (Bukhari, Megazi 4, Tafsir 5/4; Wakidi, I, 48) Baada ya Mikdad kuongea Sa'd bin Muadh akasimama:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Tumekuamini na kukubali. Tumeshuhudia kuwa Qur'an uliyokuja nayo na *sunnah* ni vya kweli. Tumeahidi kwa dhati kwamba tutakusikiliza kwa kila neno

30. Birku'l Gimad ni sehemu yenye umbali wa siku kumi kutoka Makka al Mukarrama, karibu na bahari nyekundu. Pia imepokewa kuwa ni jina la mji uliopo Yemen.

31. Ibn -i Masud amesema: "Nilikuwa shahidi katika neno lile la Mikdad bin Aswad kwamba kumiliki maneno hayo kunanivutia zaidi kuliko maneno yote mengine ambayo yangelikuwa sawa na hili"...(Bukhari, Megazi, 4, Tafsir, 5/4)

na kukutii. Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Fanya utakalo! Naapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye amekutuma wewe kama Mtume wa kweli kwamba hata kama ungetuonyesha bahari na kuzama ndani yake na sisi tungelizama pamoja na wewe na hakuna hata mmoja ambaye angelibaki nyuma. Na hatutahisi vibaya ukitukutanisha uso kwa uso na maadui zetu kesho. Kuwa na subira na uvumilivu na kuwa na utii wa kweli wakati wa mapambano ndiyo sifa yetu. Tunatumaini Mwenyezi Mungu atakuonyesha kitu kutoka kwetu ambacho kitakuangazia macho yako. Njoo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, tupeleke katika neema ya Mwenyezi Mungu".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliposikia maneno haya ya utii na unyenyekevu uso wake mtukufu ulifunikwa na tabasamu na akafanya dua akiomba heri:

"Kama ni hivyo njooni mtembee na neema ya Mwenyezi Mungu. Iwe bishara njema kwenu, Mwenyezi Mungu ametuahidi moja kati ya makundi mawili[32]*. Naapa kwa Mwenyezi Mungu, ni kana kwamba naona sehemu ambayo maquraish watashindwa katika uwanja wa mapambano..."* (Muslim, Jihad, 83; Wakidi, I, 48-49; Ibn-i Hisham, II, 253-254).

❁

Uzuri ulioje maneno ya maswahaba namna yalivyoonyesha upendo na utii kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Anas ﵁ anasimulia *hadith* ifuatayo ambayo inaonyesha kwa uzuri ukweli wa moyo, uhalisi, unyeti na uharaka wa utii wa maswahaba watukufu juu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake:

32 Moja kati ya makundi mawili yaliyoahidiwa katika aya ya saba ndani ya surat Al Anfal lilikuwa ni la maquraysh wenyewe, kutokana na kushindwa kwao na kuchukuliwa kama mateka, na lingine ni la msafara mkubwa wa maquraysh kutoka Syria.

"Nilikuwa ni mhudumu katika nyumba ya Abu Talha. Nilikuwa nikiwahudumia wageni kwa kuwajazia bilauri zao pombe. Mara pombe ikaharamishwa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akaamuru mnadi awatangazie watu kuhusu kuharamishwa huku. Tulisikia habari wakati bado tupo ndani ya nyumba. Abu Talha akaniambia:

"Nenda nje usikilize hilo tangazo linahusu nini". Nikaenda nje na kurudi na kumuambia:

"Ni mnadi ananadi:" Fahamuni, fahamuni, pombe imeharamishwa". Akanigeukia na kusema:

"Kama ni hivyo chukua na mwaga pombe yote nje".

Tokea pale pombe ikawa inamwagwa katika mitaa ya madina (Bukhari, Tafsir, 5/11)

Hawa maswahaba walitii amri mara tu waliposikia kuwa pombe imeharamishwa. Hawakutafuta kisingizio na wala hawakusema: Ngoja nimalizie kilichoko mkononi kisha nitaacha". Hawakuchelewa, waliweza kuimwaga pombe yote iliyokuwa katika milki yao ikiwemo ile waliyokuwa wakiinywa wakati ule.

❁

Kijana mmoja kutoka kabila la Aslam alikuja kwa Mtume na kusema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nataka kujiunga na vikosi vya vita lakini sina kifaa chochote muhimu katika vita"

Mtume ﷺ akamuambia:

"Nenda kwa mtu yule; alijiandaa na vita lakini anaumwa". Yule kijana akaenda kwa yule mtu na kumuambia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anakutakia amani na anasema unipatie kile ulichoandaa kwa ajili ya vita".

Juu ya hili yule mtu akamgeukia mke wake:

"Mke wangu mpendwa! Mpe kijana huyu kila kitu nilichoandaa kwa ajili ya vita. Usiache chochote. Usiache chochote kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ili tuweze kubarikiwa katika hili". (Muslim, Imare, 134)

Huyu swahaba alitii amri ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa upendo na hamasa kubwa na kusisitiza mke wake atoe kila kitu alichoandaa na asiache chochote. Kwa namna hii ameonyesha mapenzi, kujitolea na utii wake kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na pia ameonyesha ari na shauku kubwa aliyonayo katika kutenda mambo mema.

❁

Ibn omar ﵁ amesimulia:

"Katika siku ya ushindi Mtume ﷺ alipoingia Makka alimuomba mmoja wa *hajib*[33] wa al Ka'aba aitwaye Othman bin Talha ﵁ kuleta funguo pale kwenye al Ka'aba.

Othman akaenda kwa mama yake ambaye alikuwa akiilinda funguo. Hata hivyo yule mwanamke ambaye alikuwa ni mpagani alikataa kutoa funguo. Othman akamuambia:

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu! Ama unipe funguo au hili panga litatoka kwenye ala yake".

❁

Yule mwanamke akampa ile funguo, kisha akaipeleka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Mtume akafungua mlango na kuingia ndani ya nyumba ya Mwenyezi Mungu. Usama ﵁, Bilal ﵁, Othman ﵁ waliingia pamoja naye. Mtume ﷺ alibakia ndani ya

33. *Hajib* ni mtu aliyechaguliwa na kupewa jukumu la '*hijaba*', linalohusiana na majukumu muhimu kama vile kuiangalia Al-Ka'bah, kuzisimamia funguo na milango yake, kufungua milango yake wakati fulani kwa ajili ya wageni, kutunza na kusafisha sehemu aliposimama nabii Ibrahim, vitu vya thamani, mapazia ya ndani na nje.

al Ka'aba kwa muda mrefu kabla ya mwishowe kutoka. Baada ya hapo watu wengi wakashindana kuingia.

❁

Mtu wa kwanza kuingia ndani alikuwa ni Abdullah bin Omar ﵁. Alipoingia tu akamkuta Bilal amesimama nyuma ya mlango.

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ameswalia wapi? Akauliza. Bilal akaonyesha mahali ambapo Mtume aliswalia. Abdullah baadaye akasema:

❁

"Nimesahau kuuliza amezunguka mara ngapi wakati anaswali". (Bukhari, 127, Salat 30, 81, 96, Tahajjud 25, Hajj 51, 52, Megazi 77, 48; Muslim, Hajj 389)

Katika mfano huu tunaona namna Othman alivyoonyesha utii kwenye amri ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na namna Abdullah bin Omar alivyomfuata Mtume kwa umakini wa hali ya juu.

Mtume alisema:

"M*tu yeyote asinyanyuke pale alipokaa na kumpisha mtu mwingine akae. Tanueni mduara ili kuongeza nafasi ili Mwenyezi Mungu awazidishie*" (Bukhari, Isti'zan, 32; Muslim, Salam, 29)

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

"Ukialikwa mahali, itikia mualiko".

Ibn Omar ﵁ aliposikia hili alihakikisha anakubali mialiko yote, ya harusi au mingineyo, hata kama amefunga. (Bukhari, Nikah 71, 74; Muslim, Nikah 103).

Ni kusema kwamba akiwa amefunga funga ya sunna alikuwa akifungulia na kuilipiza siku nyingine. Kama amefunga funga ya

faradhi au muhimu alikuwa akihudhuria mualiko bila ya kufungulia ili tu kuendana na amri ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Siku moja Mtume Muhammad ﷺ aliuchagua mlango mmoja utumike kwa ajili ya wanawake. Ibn Omar رضي الله عنه aliposikia haya kamwe hakuutumia tena mlango ule mpaka alipokufa. (Abu Dawud, Salat, 53/571)

Tufay ambaye ni mtoto wa Ubayy bin Ka'ab رضي الله عنه anasemekana kuwa *Tabi'een*[34]*34*. Alikuwa akikutana na maswahaba ili kunufaika na ufahamu wao. Mara kwa mara alikuwa akimtembelea Abdullah bin Omar رضي الله عنه na kwenda naye sokoni.

❁

Tufay anaelezea umakini wa Abdullah katika kutii maamrisho ya Mtume:

"Tulipokuwa tukienda sokoni, Abdullah bin Omar alikuwa akimtolea salamu kila anayekutana naye. Ama mtu aliyekuwa akiuza bidhaa zilizokwishatumika au za thamani, masikini au yeyote mwingine asiyemjua, alikuwa akiwapa salamu wote. Siku moja nilienda kumuona tena, akashauri twende sokoni kwa mara nyingine tena:

"Unaenda kufanya nini sokoni?" Nikamuuliza. "Hujui lolote kuhusu kuuza na kununua. Huulizi bei za bidhaa wala hununui kitu chochote. Hukai pale watu wengine wanapokaa na kuongea. Kinyume na kwenda sokoni ni bora tukae hapa na kuongea".

Abdullah aliposikia haya aliniambia:

34. Tabi'een ni karne ya pili ya waislamu baada ya maswahaba. Ni wale waislamu waliowaona maswahaba katika uhai wao, lakini sio Mtume. (Maelezo ya mfasiri).

"Ndugu yangu! Tunaenda sokoni kutoa salamu ya Mwenyezi Mungu kwa kila tutakayekutana naye. Hatutakuwa na lengo lingine zaidi ya hili" (Muwatta, Salam, 6; Bukhari, al-adab'ul Mufrad, s 348)

Maswahaba wote watakatifu walionyesha hisia za hali ya juu katika kutii maamrisho ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake. Kwa kutawanya amani miongoni mwa watu na kuongeza mapenzi walijenga msingi imara ambao juu yake udugu wa kiimani ulijaa ndani ya nyoyo za waumini. Shauku na fadhila za Abdullah bin Omar ﷺ ndani ya mada hii vinavuta umakini wa watu wengi kutokana na asili yake ya utukufu. Ushahidi wake unaonekana katika mifano iliyotangulia.

❁

Siku moja aya ifuatayo iliyoko ndani ya Qur'an tukufu ilishushwa: **"Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii... "** (Hujurat, 49: 2)

Thabit bin Kays ﷺ aliposikia Aya hii alikaa nyumbani kwake na kulia. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipoacha kumuona Thabit kwa muda aliulizia aliko. Mtu aliyekuwa pale akamuambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ninajua aliko". Akaenda moja kwa moja nyumbani kwake na kumkuta kainamisha kichwa chini huku analia.

❁

"Kuna tatizo gani?Kwa nini unalia?" akamuuliza.

"(Usiulize). Nimefanya maovu mengi. Nimenyanyua sauti yangu juu ya sauti ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Matendo yangu yote yamekuwa ni bure. Ninastahiki moto", alijibu. Yule swahaba akarudi na kumjulisha Mtume yale maneno ya Thabit. Mtume akasema:

"Nenda na umuambie kuwa yeye si kwa ajili ya moto bali kwa ajili ya pepo" (Bukhari, Manaqib, 25, Tafsir 49/1; Muslim, Iman 187).

Thabit ambaye kwa asili alikuwa na sauti kubwa alichanganyikiwa na kuhuzunika huku akidhani kuwa ameasi amri ya Mwenyezi Mungu. Hata hivyo kwa kuwa sauti yake ya juu ilikuwa ndiyo asili yake na kwa sababu alikuwa na moyo safi, hali yake ilikuwa ni dharura na yule swahaba aliyemjia mwanzo kumuuliza alimrudia na kumpa bishara njema za pepo.

Pia yule swahaba aliyeenda kufahamu hali ya Thabit alikuwa ni mfano mzuri wa namna maswahaba watukufu walivyokuwa wakichukua maelekezo yote ya Mtume kama amri na kuwa tayari kujitolea kwa ajili yake.

Mke wa Abdullah bin Rawaha ﵁ anasimulia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alkuwa amepanda juu ya mimbari (kutoa khutba). Wakati ule ule Abdullah ﵁ alikuwa njiani akielekea msikitini na kusikia kwa mbali Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema "Kaa chini". Ijapokuwa alikuwa hajafika msikitini haraka akakaa pale alipo. Jambo hili lilipomfikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuambia Abdullah:

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akuzidishie moyo wa kumtii yeye na Mjumbe wake".

❁

Abdullah bin Abbas ﵁ anasimulia:

"Siku moja Uyayna bin Hisn alikuja Madina kumtembelea mpwa wake Hur bin Kays ﵁. Hur bin Kays alikuwa ni mmoja wa wanakamati ya ushauri kwa Omar ﵁. Haikujalisha ujana au utu uzima bali wanachuoni wote waliingizwa katika kamati hii. Kwa sababu hii Uyayna alimuambia mpwa wake Hur bin Kays:

"Mpwa wangu, nafasi yako kwa kiongozi wa dola ni kubwa, naomba upange mkutano kati yetu".

Hur akamuomba Omar ﷺ ruhusa. Uyayna alipokutana na Omar akamuambia:

"Ewe mtoto wa Khattab! Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika hututoshelezi na wala hutuongozi kwa uadilifu".

❁

Omar akapandwa na hasira na akataka kumuadhibu Uyayna. Hur alipoona vile haraka akaingilia kati:

"Ewe kiongozi wa waumini! Kumbuka nini Mwenyezi Mungu alimuambia Mtume- **"Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili"**. (A'araf 7:199). Mjomba wangu ni miongoni mwa majahili".

Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika Hur aliposoma Aya hii Omar ﷺ haraka akabadilisha msimamo wake wa kumuadhibu Uyayna. Omar alikuwa amefungamana na kitabu cha Mwenyezi Mungu. (Bukhari, Tafsir 7/5, I'tisam 2)

Omar alipokumbushwa amri ya Mwenyezi Mungu haraka alidhibiti hasira zake. Hakuchelewa kutii amri tukufu ya Mwenyezi Mungu na aliachana na kile alichotaka kukifanya kwa matakwa yake. Kwa namna hii alionyesha uwajibikaji wa muumini wa kweli katika kutii maamrisho ya Mwenyezi Mungu.

Wakati mmoja Hisham bin Hakim ﷺ ambaye ni miongoni mwa maswahaba wa Mtume alikuwa Palestina. Aliona kikundi cha wakulima wasiokuwa waislamu ambao wamefungwa kwa kosa la kutolipa kodi na wakawa wanaadhibiwa kwa kumwagiwa mafuta ya zaituni na kuwekwa juani. Akaenda moja kwa moja kwa gavana na kumuambia kuwa hili analofanya ni jambo baya sana. Kisha

akamsimulia hadith ambayo aliisikia moja kwa moja kutoka kwa Mtume:

❁

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu atawatesa wale ambao wanawatesa wengine bila haki"

Kwa kusikia haya yule Gavana akawaacha huru wale wakulima. (Muslim, Birr, 117-119; Abu Dawud, Imare, 32; Ahmad III, 403, 404, 468).

Watu hawa watukufu hawakusita hata kidogo katika kufanyia kazi maelekezo ya Mtume na waliwajibika kwa haraka.

Abdullah bin Abi Awfa ﷺ katika mazishi ya binti yake alitoa *takbir* (*Allahu Akbar*) mara nne. Baada ya *takbir* ya nne alinyamaza kwa muda kati ya *takbir* mbili na kumuombea msamaha binti yake na kumswalia.

Wale waliokuwa naye wakadhani kuwa ataleta *takbir* ya tano. Kisha akatoa salamu upande wa kulia na kushoto. Baada ya swala wakamuuliza:

❁

"Ni nini hiki ulichofanya?". Akajibu:

"Hivi ndivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alivyokuwa akifanya". (Hakim, I, 360; Ibn-i Majah, Janaiz, 24).

Jibu la Abdullah bin Abi Awfa ﷺ ni muhimu katika kuonyesha umakini wa maswahaba watukufu katika kumfanya Mtume wa Mwenyezi Mungu kama mfano katika kila kitu. Kipimo chao kilikuwa ni *sunnah* za Mtume. Ndiyo maana utetezi wao na ufafanuzi wao ulikuwa umeegemea kwenye uthibitisho kutoka kwenye Qur'an na *sunnah*. Waliishi kulingana na Qur'an na *sunnah*. Na wameonyesha namna gani leo hii tuishi kulingana na Qur'an na *sunnah* na kufaidika kutokana na mafanikio yake ili midahalo na

uthibitisho wa mambo yetu uendane na muongozo huu mtukufu. Ubora wa tabia na utu wetu na ukamilifu wa Uislamu wetu unaendana na kiwango chetu cha kushikamana na Qur'an na *sunnah.*

Usiku mmoja ulipofika wakati wa swala ya I'sha Mtume ﷺ aliwaambia maswahaba zake:

"J*ikusanyeni kwa ajili ya swala kesho, kuna kitu nataka niwaambie*". Swahaba mmoja akawaambia rafiki zake:

"Ewe fulani na fulani. Wewe shika jambo moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu atakachokisema, na kisha wewe (fulani na fulani) shika jambo la pili na kisha wewe (fulani na fulani) shika linalofuata ili tusikose chochote atakachokisema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu". (Haythami, I, 46).

❁

Huu umakini ulioonyeshwa na maswahaba katika kujifunza na kutekeleza maamrisho ya Mtume Mtukufu ni wa kutukuzwa mno. Kwani ni jitihada hizi kubwa za kizazi hiki kitukufu ndizo zilizopelekea leo hii tukawa na fursa ya kushikamana na mwenendo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu awaridhie...

Abu Burda anasimulia:

Wakati fulani Abu Musa al Ash'ari رضي الله عنه alikuwa mgonjwa na akazimia wakati ameweka kichwa chake juu ya paja la mkewe. Hili lilipotokea mkewe akalia kwa sauti na kupiga kelele. Hata hivyo wakati ule Abu Musa hakuwa katika nafasi ya kuweza kumnyamazisha mkewe. Alipopata nafuu akamuambia mkewe katika hali ya kumuonya:

❁

"Chochote ambacho kilikuwa hakimridhishi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na ambacho alijiweka nacho mbali pia mimi siridhiki nacho na najiweka nacho mbali. Mtume alijitenga na wanawake ambao wanalia na kuvuta nywele zao na kuchana nguo zao kutokana na huzuni ya kufiwa" (Bukhari, Janaiz, 37, 38; Muslim, Iman, 167; Nasai, Janaiz, 17)

Uzuri ulioje wa imani kwa mtu kutii maamrisho ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hata kama yupo katika mahangaiko yanayokaribia kifo.

❁

Dihya bin Khalifa رضي الله عنه alipoona watu wanaenda kinyume na *sunnah* aliwaambia:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu, Nimekutana uso kwa uso na tukio ambalo kamwe nisingelifikiria kulifanya;Watu fulani wamezipa kisogo sunnah za Mtume na maswahaba zake. Ewe Mwenyezi Mungu! Chukua uhai wangu sasa hivi ili nije kwako". (Abu Dawud, Sawm, 47/2413).

Bishr-i Hafi (q.a) anaelezea kuwa:

"Usiku mmoja nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu ndani ya ndoto, akaniambia:

"Ewe Bishr! Je unajua kwanini Mwenyezi Mungu amekupandisha daraja?"

❁

"Hapana, sijui ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nikasema. Akaendelea:

"Ni kwa sababu unafuata sunnah yangu na unawatumikia watu wema. Unawashauri ndugu zako juu ya dini, na unawapenda

maswahaba zangu na watu wa familia yangu, ndiyo maana Mwenyezi Mungu amekupandisha daraja sawa na watu wema[35]".

Uzuri ulioje wa maelezo ya Abdulhalik Gujduvani (q.a) juu ya kumtumikia Mwenyezi Mungu:

Siku moja aliulizwa:

"Je tufanye yale nafsi zetu inayotuamrisha kufanya au twende kinyume na matakwa ya nafsi zetu?"

Mwema huyu alijibu kama ifuatavyo:

"Ni vigumu kutofautisha vitu hivi viwili. Wakati wote nafsi zinawapoteza watu katika kujua ama matamanio haya yanatoka kwa Mwenyezi Mungu au kwa Shetani. Ndiyo maana mtu hana budi kufanya kile tu Mwenyezi Mungu alichokiamrisha na kujizuia kufanya yale anayotukataza. Huu ndiyo utumishi bora kwa Mwenyezi Mungu".

Wasafiri katika njia ya haki ni lazima wafanye kutii maamrisho ya Mwenyezi Mungu kama kanuni yao ya msingi. Hizi ni njia za kufikia furaha ya milele na lazima zitumike kama jitihada za kufikia radhi za Mwenyezi Mungu. Siku moja mtu ambaye alikuwa ana kawaida ya kuhudhuria katika mazungumzo ya David Tai alimuambia Maruf Kerhi:

"Hakikisha huachi matendo mema kwa kuwa yatakuweka karibu ya radhi za Mwenyezi Mungu mtukufu". Maruf Aliuliza:

"Nifanye matendo gani?" Yule mtu akajibu:

"Wakati wote jiweke katika hali ya kumtii Mola wako; wahudumie Waislamu na washauri..."

Kwa kifupi utii ni alama kubwa ya mapenzi. Kuna kanuni kuwa "Anayependa atatii", hivyo waumini ambao wanampenda

35. Mahir Iz, Tasawwuf, Istanbul 1969, s. 184)

Mola wao watakuwa katika hali ya utii kwake. Jambo dogo la ibada litakalofanywa kwa utii na unyenyekevu linakubalika zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko milima ya ibada iliyofanywa bila utii na nia. Haya ni kwa sababu utumishi unaanza kwa utii na unyenyekevu. Shetani alifukuzwa mbele ya Mwenyezi Mungu si kwa sababu ya mapungufu yake katika ibada bali kwa kukataa kwake kutii na kunyenyekea maamrisho ya Mwenyezi Mungu.

Maswahaba watukufu walifikia hali ya juu ya ubora kutokana na daraja lao la mapenzi, kujitolea na kumtii Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake. Kwa kunyenyekea bila kusita katika maamrisho matukufu ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi na unyenyekevu waliweza kuwa mfano wa kuigwa miongoni mwa watu wote.

Katika Mathnawi yake Jalaluddin Al Rumi anaonyesha vizuri utii wa viumbe visivyo na uhai juu ya amri ya Mwenyezi Mungu:

"Je huoni? Mawingu, jua, mwezi na nyota vyote vinatembea katika utaratibu maalum. Kamwe jua , mwezi na nyota havichelewi kuchomoza wala havizami kabla ya muda vilivyowekewa. Kwa nini hatuelewi maajabu haya kwa kuangalia miujiza ya Mitume? Walivipa utambuzi milima na vinginevyo. Angalia haya na linganisha na vile vitu vingine visivyo na uhai na vitu vya Musa na vilinganishe na vipande vingine vya mawe.

Vipande vya mawe vilivyomtii Mtume Muhammad ﷺ na utii wa vile vipande vya Musa kwa Nabii Musa, ni kiashirio tosha cha namna viumbe vingine ambavyo tunavidhania kuwa havina uhai vinavyotii amri za Mwenyezi Mungu.

Viumbe hivi vinasema kwa kupitia ndimi zao zisizoonekana: "Tunamjua Mwenyezi Mungu na tunamtii. Hatukuumbwa bila sababu. Tunafanana na bahari nyekundu. Hata kama ilikuwa ni bahari tu lakini iliweza kumtambua Firauni na kumuepusha na kuzama miongoni mwa wana wa Israel...

Popote pale miti na mawe vilipomuona Mtume Muhammad ﷺ vilimtolea salamu. Hivyo fahamu kwamba kila kitu ambacho uliona hakina uhai, kikweli ni kwamba kina uhai kamili".

Inamaanisha kuwa si tu watu na majini ambao wanamtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bali ni wanyama wote na viumbe vyote visivyo na uhai. Huzuni iliyoje wakati viumbe wengine wote wanaharakisha kumtii Mwenyezi Mungu lakini mwanadamu anajitumbukiza kwenye mashimo ya uasi. Hivyo hatuna budi kuchukua mazingatio kwenye utii wa viumbe vyote vilivyoumbwa na Mwenyezi Mungu. Lazima tujifunze na kubadili muelekeo wetu mbele ya Mwenyezi Mungu.

❁

6. Umakini katika ibada

Ulimwengu huu ni kama kazi ya mikono iliyofanywa na Mwenyezi Mungu na kuipamba kwa ukubwa Wake na nguvu zake. Katikati kuna mwanadamu ambaye ameumbwa na kufanywa kuwa juu ya viumbe vyote, na amepewa jukumu la ibada ili kumpa uhakika wa kuwa karibu na Mwenyezi Mungu.

Katika Aya nyingi ndani ya Qur'an Mwenyezi Mungu anamuamrisha Mwanadamu ashikamane na matendo mema ili ajiokoe kutokana na hasara yenye kudumu na kumuwezesha kuwa na moyo safi na *qalb-i munib*[36].

Ibada ni dalili ya mtu kutekeleza ahadi iliyowekwa na mja kwa Mola wake kabla ya kuumbwa. Ibada ni jambo linalomleta muumini karibu na Mwenyezi Mungu mtukufu. Kwa maana nyingine ibada ni tiba bora na chanzo cha amani na utulivu ambayo itamu-

36. *qalb-i munib* ni moyo ambao unamgeukia Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu ili kuwa mbali na vishawishi.

weka mwanadamu huru kutokana na hofu ya litakalompata baada ya kufa. Ibada ni chimbuko muhimu la mafanikio ambayo yatampandisha mja daraja na kumhakikishia amani na usawa ndani ya moyo wake.

Ni lazima tuipe ibada kipaumbele na umuhimu mkubwa miongoni mwa mambo yetu mengine muhimu.

Matukio ya wema

Kabla ya yote ni muhimu kugusia umakini unaohitajika wakati wa kuchukua udhu kutokana na umuhimu wake. Kwani kwa kukosa umakini na uzingatiaji wakati wa kuchukua udhu itaashiria ni namna gani ibada iliyo mbeleni itakavyokuwa.

❁

Wakati fulani Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliongoza swala ya Alfajiri. Yalitokea makosa madogo wakati surat Rum inasomwa. Swala ilipoisha Mtume aliwageukia watu na kusema:

"Baadhi ya watu wanakuja kuswali bila udhu ndiyo maana shetani ameingilia katika kisomo chetu. Mkija kuswali chukueni udhu kwa umakini kadri iwezekanavyo".

Hivyo kujitwaharisha na kuchukua udhu kwa umakini kabla ya swala ni mambo muhimu katika kukubaliwa swala zetu.

Pia ni wema mkubwa kuwa na udhu wakati wote kadri iwezekanavyo. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akitekeleza majukumu yake yote akiwa na udhu.

Imesimuliwa na Abu Juhaym رضي الله عنه kuwa , Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikutana na mtu mmoja aliyekuwa akitokea katika kisima cha Jamal. Mtu yule alimtolea salamu mtume lakini hakumuitikia. Mara Mtume akaenda kwenye ukuta na kupangusa

mikono yake kisha akapangusia uso wake na mikono yake kama *tayammam* (kuchukua udhu kwa udongo mkavu), kisha akajibu maamkizi ya amani ya yule mtu.

Kwa kitendo hiki Mtume wa Mwenyezi Mungu ameonyesha namna inavyowezekana kwa mtu kuwa na udhu muda wote. Pia kinaashiria namna ilivyo wema kuchukua udhu kabla ya kutekeleza jukumu lolote lile hata kama si la lazima.

Ibn-i Abbas ﷺ anasimulia:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akitoka msalani anajimiminia maji mikono na kuosha mikono yake kisha anafanya *tayammam* kwa udongo mkavu. Siku moja nikamuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, maji yanapatikana, kwa nini ulifanya vile?". Mtume akajibu:

"Nitakuwaje na uhakika kuwa roho yangu haitachukuliwa kabla sijayafikia maji?" (Ahmad, I, 288, 303; Haythami, 263).

Kutokana na masimulizi mengine pale alipotaka kuondoa josho kubwa. Mtume ﷺ alikuwa akipangusa ukutani kwa mikono yake na kufanya *tayammam* ili asibaki bila udhu mpaka atakapooga kuondoa josho kubwa. (Haythami, I, 264).

❁

Huu ni upeo wa usafi alioonyesha Mtume kwa umma wake...

Siku moja Mtume ﷺ pamoja na maswahaba zake walitembelea eneo la makaburi na akasema:

"Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yenu enyi wakazi wa makaburi haya ya waumini! Mwenyezi Mungu akipenda siku moja tutaungana nanyi. Tamaa iliyoje ya kuwaona ndugu zangu. Namna gani nawakumbuka"

Maswahaba zake wakauliza:

"Je sisi si ndugu zako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!"

Mtume akajibu:

"Nyinyi ni maswahaba zangu. Ndugu zangu bado hawajafika hapa duniani".

Kisha maswahaba zake wakauliza:

"Utawatambuaje hao ambao bado hawajaja kuwa wanatoka katika umma wako?".

❁

Mtume ﷺ akasema:

"Chukulieni mtu ambaye ana farasi ambaye paji lake na miguu yake ni meupe sana. Je mtu huyu atashindwa kumtambua farasi wake akiwa ndani ya kundi la farasi wengine ambao ni weusi mno?"

Maswahaba zake wakajibu:

"Ndiyo atawatambua ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu". Kisha Mjumbe ﷺ aliyebarikiwa akasema:

"Na kwa namna hiyo ndugu zangu ni wale watakaokuja huku nyuso, mikono na miguu yao inang'aa kutokana na udhu. Nitakuwa ninawasubiri juu ya mnara tayari kwa kuwapa wanachohitaji. Lakini fahamuni! Baadhi ya watu watafukuzwa kwenye bwawa langu kama ngamia pori wanavyofukuzwa kwenye zizi na kusogezwa mbali. Nitawaita:

❁

"Njooni". Nitaambiwa:

"Walibadilika ulivyoondoka. (Hawakufuata sunna *yako na walijiweka mbali nayo)"*. Kisha nitasema:

"Wawekwe mbali na mimi. Wawekwe mbali na mimi".

❁

Hivyo wale waumini ambao wapo makini na udhu wao wataingia kwenye mapenzi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na watakuwa ni wale ambao Mtume atawaita 'ndugu' zake. Wale ambao hawapo makini katika udhu wao na ibada zao, na ambao wanaelekea kwenye njia ya upotofu watafukuzwa kama ngamia pori siku ya kiama. Watakuwa wamepata hasara kubwa sana, hasara ya kuwekwa mbali na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Siku moja bwana mmoja wa Tabieen aitwae Abu Hazim alimuona Abu Hurayra ﷺ akichukua udhu na akiosha mikono yake mpaka kwapani.

"Abu Hurayra, huu ni udhu wa namna gani?" Akamuuliza. Abu Hurayra ﷺ akajibu:

"Ewe Bani Ferruh! Sikujua kama upo hapa. Kama ningelijua upo hapa nisingelichukua udhu kama hivi".

❁

Akaendelea kuelezea:

"Nilimsikia rafiki yangu, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akisema:

"Siku ya kiama nuru ya waumini itang'arisha mpaka ile sehemu ya kiungo itakayofikiwa na maji ya udhu" (Muslim, Taharat, 40)

Uzuri ulioje wa maneno yafuatayo ya Ali ﷺ namna yanavyoonyesha mapenzi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika ibada zake:

"Siku ya Badr hakubaki muendesha farasi yeyote isipokuwa Mikdad. Nakumbuka siku hii hakulala mtu yeyote isipokuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ambaye alikuwa akiswali chini ya mti huku akilia mpaka asubuhi" [37].

37. Ibn-i Huzayma, Sahih, Beirut 1970, II, 52

Huu ni mfano wa mapenzi katika ibada ambayo kamwe haya-kufifia ama katika hali ya amani au vita...

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini (kifo)" (Hijir, 15:99).

"Nawe sujudu na ujongee" (Alaq, 96:19)

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akimsifu Abdullah bin Rawaha رضي الله عنه kwa kuonyesha kwake umakini mkubwa katika ibada na akampendelea kwa kumuita 'ndugu yangu':

❁

"Mwenyezi Mungu amrehemu ndugu yangu, Abdullah bin Rawaha! Ilikuwa muda wa swala ukifika anasimama upesi na kuswali" (Haythami, IX, 316)

Jarh bin Abdullah رضي الله عنه anasimulia:

"Usiku mmoja tulikuwa tumekaa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Akaangalia mwezi uliokuwa umekamilika na kusema:

"Namna mnavyoweza kuuona mwezi ule kwa urahisi bila ya kusukumana, ndivyo mtakavyomuona Mola wenu. Fanyeni bidii katika kutekeleza ibada zenu kabla ya jua kuchomoza na kabla ya kuzama kwake".

Baada ya hapo akasoma Aya ifuatayo:

"...Na umtakase Mola wako Mlezi kwa kumsifu kabla ya kuchomoza jua, na kabla halijachwa, na nyakati za usiku pia umtakase, na ncha za mchana ili upate ya kukuridhisha". (Taha, 20:130) (Bukhari, Mawakit 16, 26, Tafsir 50/1, Tawheed 24; Muslim, Masajid 211).

❁

Hivyo njia ya pekee ya kumuona Mola wetu ni kuonyesha umakini wa hali ya juu tunapotekeleza ibada zetu.

Kila kitendo cha ibada kinachofanywa ni lazima kionekane kama viza ya kuingilia peponi, hivyo ni lazima kifanywe kwa umakini na kwa shauku inayotoka ndani ya moyo safi.

❁

Mtume ﷺ anasema:

"Kama mtu ataswali vizuri kwa kurukuu na kusujudu vizuri, swala yake itamuambia:

"Mwenyezi Mungu akuhifadhi kama ulivyonihifadhi. Swala itamnyanyua daraja.

Kama mtu hataswali vizuri kwa kurukuu na kusujudu vizuri, swala yake itamuambia:

"Mwenyezi Mungu akupuuze kama ulivyonipuuza". Swala yake itakunjwa kunjwa na kutupiwa usoni mwake" [38].

Imeelezwa katika Aya ndani ya Qur'an:

"Basi, ole wao wanaoswali, ambao wanapuuza Swala zao" (Al-Maau'n, 107:4-5).

Ni mazoea mabaya kucheleweshа swala mpaka muda wake wa mwisho na kunyanyuka kuswali kwa uvivu kana kwamba unataka kuepukana nayo tu na pia kufanya yale matendo ya lazima tu. Kitendo hiki ni kibaya kwani kinaweza kumpelekea mtu kwenye unafiki, jambo ambalo Mwenyezi Mungu amelikemea. Ala bin Abdurrahman رضي الله عنه anasimulia:

❁

38. Suyuti, Al Jamiu"s Sagir, Egypt 1321,I,58/364

"Mchana mmoja tulienda kumuona Anas bin Malik ﷺ. Tulipofika Anas alinyanyuka upesi na kuswali swala ya Adhuhur. Alipomaliza kuswali tukamuambia ameswali swala ile mapema mno. Alielezea kwa nini aliiswali mapema:

"Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema:

"Hii ni swala ya wanafiki. Hii ni swala ya wanafiki. Hii ni swala ya wanafiki[39]. Mmoja wao anakaa na kukaa mpaka aone jua limegeuka na kuwa manjano na linataka kuzama, wakati jua linataka kuingia kati ya pembe mbili za shetani, ndipo anaponyanyuka na kurukuu mara nne upesi upesi kana kwamba ni kuku anayedonoa. Anamkumbuka Mwenyezi Mungu kidogo katika swala yake". (Muwatta, Qur'an al Kareem, 46; Muslim, Masajid 195)

Siku moja Omar ﷺ aliwashauri magavana wake kama ifuatavyo:

"Wajibu wenu muhimu kwangu ni swala. Yeyote atakayeihifadhi na kuwa makini katika nyakati zake, ataihifadhi dini yake na yeyote atakayeiacha na kuipuuzia, atapoteza dini yake ndani ya muda mfupi".

❁

Miswar bin Mahrama ﷺ anasimulia:

"Omar bin Khattab ﷺ alipopigwa alipoteza fahamu na kulala chini bila ya kujitambua. Wakati fulani nikamtembelea kwenye chumba chake. Alikuwa amelala chini huku wamemfunika. Nikawauliza wale waliokuwa wamemzunguka:

❁

"Anaendeleaje?"

"Kama unavyomuona, hajitambui", wakajibu.

39. Unafiki uliotajwa katika hadith hii ni ule wa matendo yasiyo ya kiimani.

"Je, mmemuita kwa ajili ya swala?" Kama yuko hai hakuna kitu kitakachomhofisha na kumuamsha zaidi ya swala". Waliposikia haya wakasema:

"Ewe kiongozi wa waumini! Swala, swala imeshaswaliwa. Omar akaamka na kusema:

"Je hayo ni kweli? Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, yeyote anayeacha swala hatakuwa na chochote katika Uislamu". Akasimama na kuswali huku damu zikivuja kutoka katika majeraha yake". (Haythami, I, 295; Ibn-i Sa'd, III, 35; Muwatta, Taharet, 51)

Wakati Ali ﷺ anahutubia ndani ya mji wa Kufa alirudia alichokisikia kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

❁

"Kwenye siku za Ijumaa, Shetani huenda kwenye maduka na masoko na kujaribu kuwazuia watu kwa kutumia vikwazo elfu moja na moja. (Akishindwa kwa haya) hujaribu angalau kuwachelewesha kwenda msikitini. Kwa upande mwingine malaika huenda misikitini na kuwasubiri milangoni. Wanawaandika wale wanaowahi kama ifuatavyo:wale wanaokuja katika saa ya kwanza, kisha wale waliokuja katika saa ya pili, n. k. Wanaendelea hivi mpaka imamu apande kwenye mimbari. Kama mtu atakaa mahali ambapo atamuona na kumsikiliza imamu kwa makini huku amenyamaza, ataandikiwa thawabu mara mbili. Na ikiwa mtu atakaa mbali kiasi cha kutomsikia imamu lakini akawa kimya, ataandikiwa thawabu mara moja. Ikiwa mtu atakaa mahali ambapo atamuona imamu vizuri lakini atakuwa anaongea maneno ya upuuzi, ataandikiwa dhambi mbili...

❁

Wale ambao wanakuja msikitini mapema kwa heshima ya swala ya Ijumaa na kukaa pale ambapo utamsikia na kumsikiliza imamu vizuri na kuzingatia yale yatakayosemwa kwa heshima

kubwa watatoka pale na faida kubwa kinyume na wale ambao hawafanyi hivyo.

Mmoja wa wanazuoni wanaoongoza katika kusoma na kusherehesha Qur'an kutoka Tabieen aitwaye Mujahid ﷺ anasema:

"Abdullah bin Zubayr ﷺ alikuwa amefikia kilele katika kumuabudu Mwenyezi Mungu, nafasi ambayo hakuna mtu aliyekuwa ameifikia. Wakati fulani eneo linalozunguka Ka'bah lilikuwa limefurika watu kiasi cha kushindwa kufanya *tawaf* kwa wiki moja. Kwa upande mwingine Abdullah alifanya *tawaf* kwa wiki moja kwa kujipenyeza kwenye lile kundi la watu vile vile".

❁

Shaykh Sadi katika kazi yake inayoitwa Gulistan anaonyesha umuhimu wa kutodhoofisha ibada ya mtu kwa makosa ya nafsi:

"Nilipokuwa mdogo nilikuwa na bidii kubwa katika kujitenga na dunia na kufanya ibada za usiku. Usiku mmoja nilikuwa nimekaa karibu na baba yangu. Sikufunga macho yangu wala kuweka chini Qur'an usiku mzima. Watu wengine walionizunguka walikuwa wamelala, nikamwambia baba yangu:

"Hakuna hata mmoja katika watu hawa anayenyanyua kichwa chake na kuswali hata rakaa mbili za usiku;wamelala kana kwamba wamekufa". Baba yangu aliposikia haya alikunja uso na kujibu:

❁

"Mtoto wangu Sadi! Kwa nini usingelikuwa umeenda kulala kuliko kuwateta wenzako. (Kwani huenda wale unaowaona wako chini kwa muda huu wanapata rehema ya Mwenyezi Mungu, angalau hawaandikiwi kitu chochote kibaya na Malaika. Lakini nini wewe umeandikiwa katika kitabu chako cha amali? Umeandikiwa kuwa umewadharau ndugu zako katika dini na dhambi ya kuteta".

Waislamu waliendelea na umakini katika ibada zao hata katika nyakati za vita na matokeo yake walipata msaada wa Mwenyezi Mungu. Trajivani wa Venice analielezea jeshi hodari la Yildirim Bayazid kama ifuatavyo:

"Katika jeshi la Dola ya Uthmainiyya hakukuwa na pombe, kamari wala wanawake kama yalivyo majeshi yetu. Zaidi ya mafunzo yao ya kijeshi ambayo yalikuwa imara, pia walilikumbuka jina tukufu la Mwenyezi Mungu, na walifungamana na ibada usiku na mchana. Hii ndiyo sababu walikuwa wakiibuka washindi daima".

❁

Msikiti wa Bayazid ulifunguliwa kwa ajili ya ibada siku ya Ijumaa na wa kwanza kuongoza Swala alikuwa ni mtoto wa Fatih, ambaye ni Bayazid II mwenyewe. Evliya Chelebi analielezea tukio hili kama ifuatavyo:

"Baada ya msikiti kujengwa ulifunguliwa rasmi siku ya Ijumaa kwa sherehe kubwa. Bayazid II aliuambia ule mkusanyiko:

"Yeyote ambaye hajawahi kuacha swala ya *sunnah* ya kabliya katika swala za *asr* na *'isha* aje mbele ili awe imamu wetu katika muda huu uliobarikiwa".

Ilipokuwa hakuna mtu yeyote katika mkusanyiko ule (ambao ulikuwa kama bahari) aliyenyanyuka, ilibidi Bayazid Han anyanyuke:

"Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu! Kamwe hatujawahi kujitenga na swala hizi za sunnah ama katika vita au katika amani... "Na akawa imamu na kuongoza swala".

Safiye Hanim, ambaye alijulikana pia kama Muallima'i Selatin alikuwa ni mwalimu wa masultani ambaye aliteuliwa na Sultani Mehmed Rashad ili kuwalea na kuwafundisha watoto ndani ya

kasri la dola ya Uthmainiyya. Moja ya amri za Mehmed Rashad kwake ilikuwa ni kama ifuatavyo:

"Nitawanyima chumvi na mkate wale ambao hawaswali na kufunga. Watangazie wanafunzi wako jambo hili" [40].

Heshima na cheo cha kidunia havikuwafanya watu hawa wasahau umakini wao katika ibada, wala kuwazuia kufanya juhudi katika maandalizi ya kesho Akhera kama vile swala na funga katika majukumu yao.

❁

Mfano mzuri kabisa wa umakini katika ibada unatoka kwa m*ujahid wa* Caucasus aitwae Shaykh Shamil. Alijeruhiwa na singe, panga na risasi wakati wa kuihami Gimri mwaka 1829. Singe ambayo ilikuwa imemchoma kifuani na kutokea mgongoni ilikuwa imetoboa mapafu yake, na kuvunja mbavu zake na mtulinga wa kulia. Alitibiwa na baba yake wa kufikia ambaye pia alikuwa ndiye daktari wake wa upasuaji, na ilichuka karibia miezi 6 kabla ya kupona kabisa. Kijana huyu *mujahid* alikuwa amezimia kwa siku 25 kuanzia siku aliyojeruhiwa. Alipofungua macho katika siku ya 25 alimuona mama yake amekaa pembeni yake. Maneno yake ya kwanza kwa mama yake ni:

"Mama mpendwa! Je, nimepitwa na muda wa swala?".

Ilikuwa ni katika sherehe za *Eid* ya baada ya mwezi wa Ramadhani vita kwa ajili ya Dardanelles vilipiganwa. Kamanda wa mbele aitwae Wahip Pasha alimuita imamu wa batalioni ya tisa na kumuambia kwa huzuni:

❁

"Ewe Hafiz! Kesho ni *eid* ya mwezi wa Ramadhani. Askari wanatamani kuswali swala ya *eid* katika jamaa. Kadri nilivyojita-

40. Safiye Unuvar, Saray Hatiralarim, Istanbul 1964, p 21.

hidi kuwashawishi wabadili mawazo yao nilishindwa. Lakini jambo hilo ni la hatari mno kwani litawapa maadui nafasi ya kutumaliza kabisa. Tafadhali unaweza kuwaelezea jambo hili katika njia nzuri..."

Yule imamu alimuacha Pasha alipotokewa na mtu aliyekuwa anang'aa na kumuambia:

"Mwanangu! Hakikisha huwaambii kitu wanajeshi! Ngoja tusubiri tuone nini kitatokea. Chochote atakachosema Mwenyezi Mungu kitakuwa".

Asubuhi iliyofuata utukufu mkubwa ulionekana na kumuacha kila mtu kwenye mshangao. Mawingu makubwa yalikuwa yamening'inia angani kana kwamba ni vichanga vya matunda, vimewafunika askari waumini wakati wanaswali kwa mapenzi kwa Mwenyezi Mungu. Askari wa maadui ambao walikuwa wanawaangalia kwa darubini hawakuweza kuona chochote isipokuwa mawingu meupe. Asubuhi ile sauti za *takbir* (Allahu Akbar) za swala ya *eid* zilipaa angani. Yule mzee mwenye kung'aa alipokuwa akisoma baadhi ya Aya kutoka surat Fath ndani ya Qur'an, Umoja wa Mwenyezi Mungu kutoka katika nyoyo za askari ulisikika kwa maadui.

Yalipotokea yale vikosi vya Waingereza viliparaganyika. Waingereza walikuwa wamewadanganya askari mbalimbali wa Kiislamu katika koloni zao na kuwapeleka wapigane kwa ajili yao. Hawa askari wa kiislamu waliposikia sauti za takbir (Mwenyezi Mungu ni mkubwa) na tawheed (La ilaha illallah) wakajua kuwa walikuwa wanapigana na waislamu wenzao, hivyo wakaasi. Wakiwa hawajui la kufanya, Waingereza ambao walikuwa wakatili waliwaadhibu baadhi yao na wengine kurudishwa nyuma.

Mtume mtukufu ﷺ alisema kuwa kasi atakayokuwa nayo mtu wakati anapita juu ya daraja la Sirat itakuwa ni kulingana na namna alivyozipa umuhimu ibada zake.

"Watu watakuja kwenye moto siku ya kiama na kuuvuka kulingana na amali zao:kundi la kwanza litapita kwa kasi ya radi, la pili kama upepo, linalofuata kama waendesha farasi na linalofuata kama muendesha ngamia. Linalofuata litakimbia na lingine baada ya hili litakuwa likitembea". (Tirmidhi, Tafsir, 19/3159).

Kwa kifupi lengo la ibada na utumishi ni kuufanya moyo uwe karibu na Mwenyezi Mungu. Inamaanisha ni lazima uwe na ufahamu (ufahamu wa kiroho) na mapenzi kwa Mwenyezi Mungu. Ibada itammiminia mtu baraka na wema kiasi kwamba imani itagota katika moyo wake. Ibada iliyofanywa kwa shauku na hamasa itasafisha nafsi ya mtu na kumsogeza karibu na Mwenyezi Mungu. Itaruhusu hisia za huruma na ukarimu kujengeka moyoni mwake. Mwenyezi Mungu mtukufu atakuwa kama jicho la kuonea na sikio la kusikilizia kwa mja huyo. Ni kusema kwamba, anachoona, anachosikia, anachofikiria na kukisema vitakuwa vinamridhisha Mwenyezi Mungu.

Mola wetu tujaalie haya yawezekane kati yetu sote. Amin!...

a. Ibada za ziada

Ibada za ziada zinasaidia kufanya ibada za wajibu na ni njia ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Kama mwanadamu huwezi kutekeleza ibada za faradhi kwa ukamilifu kiasi cha kumridhisha Mwenyezi Mungu. Hata hivyo ni lazima uchukuliwe umakini mkubwa ingawa makosa hayataepukika kutoka muda hadi muda. Matokeo yake hakuna dawa nyingine zaidi ya ibada za sunnah kufidia mapungufu yatakayotokea. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ametujulisha kuwa:

"Siku ya kiama amali ya kwanza ya mja kuhesabiwa ni swala. kama swala yake itakuwa imekamilika na mambo yake mengine yatakuwa sawa na atakuwa ni mwenye kufaulu. Kama swala yake itakuwa haijakamilika atakuwa amepoteza na kupungukiwa. Kama kutakuwa na mapungufu katika ibada zake za faradhi, Mwenyezi Mungu aliye Mkuu na Mtukufu atasema:

"Angalieni muone kama mja wangu ana swala zozote za sunnah". Swala za sunnah zitafidia mapungufu ya zile za faradhi. Na kisha atahesabiwa vivi hivi amali zake nyingine zilizosalia". (Tirmidhi, Salat, 188/413).

Hata hivyo isieleweke kuwa ni sahihi kuachana na faradhi na kushikamana na sunnah tu. Kama ilivyo makosa kufanya juhudi katika kutekeleza ibada za faradhi tu na kupuuzia zile za sunnah, vilevile ni makosa kufanya juhudi katika kutekeleza ibada za sunnah tu na kupuuzia zile za faradhi. Njia sahihi ni kutekeleza ibada za faradhi na kufanya juhudi katika kutekeleza ibada za sunnah kadri iwezekanavyo. Matendo ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na maswahaba zake ndiyo muongozo pekee katika jambo hili.

Kwa upande mwingine si sahihi kwa wale wenye madeni katika faradhi kuzilipizia na kuachana na sunnah kabisa. Hii ni kwa sababu mtu anaweza kulipia swala za faradhi katika muda wowote ndani ya siku isipokuwa ile mida iliyokatazwa kwa uwazi kabisa. Kwa kuwa swala zote za sunnah kama vile tahajjud (swala za usiku), ishrak, kusluk (swala za mwishoni mwa asubuhi) na awabeen (swala za mwishoni mwa jioni) zinategemea muda maalum, inashauriwa kuzitekeleza katika hii mida yake[41].

41 Wanavyuoni *Mujtahid* wa dhehebu la Hanafi wameshikilia kuwa swala za *sunnah* ni lazima. Ni katika *sinn-i kibar*, yani uzee, wakati mtu hana nguvu ya kutekeleza tena faradhi na sunnah, hivyo zile za sunnah zitafidia zile za faradhi.

Mja hawezi kumkurubia Mwenyezi Mungu kwa amali nyingine bora zaidi ya faradhi. Anaweza kuendelea na safari hii muhimu kwa kutekeleza ibada za sunnah. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaelezea katika *hadith* tukufu kuwa mwenyezi Mungu anasema:

"Natangaza vita dhidi ya wale wanaofanya uadui na marafiki zangu ambao wananitumikia kwa moyo safi. Mja wangu anajikurubisha kwangu si kwa kingine bali kwa kutekeleza mambo ya faradhi, kisha anajikurubisha zaidi kwangu kwa kutekeleza mambo ya sunna mpaka ninampenda;na nikimpenda nakuwa ni kusikia kwake pale anaposikiliza, kuona kwake kwa kile anachokiangalia, mkono wake ambao anapigia, mguu wake anaotembelea, ikapelekea kwa ajili Yangu anasikia, kwa ajili yangu anaona, kwa ajili yangu anapiga na kwa ajili yangu anatembea. Hatoniomba jambo lolote ila nitampa, Hatoniomba ulinzi ila nitamlinda. Kamwe sisiti kufanya jambo lolote zaidi ya ninavyosita kutoa roho ya mja wangu muumini;hapendi kifo na Mimi sipendi kumuudhi" (Bukhari, Rikak, 38; Ahmad, VI, 256; Haythami, II, 248).

Ibada za sunnah zinahuisha utumishi wa mtu kwa Mola wake na kulainisha moyo wake. Zinasafisha moyo na kuleta nuru ya wema. Imani ya wale wanaoendelea na ibada za sunnah kwa utii, uvumilivu na utambuzi wa moyo ni kubwa na kutamani kwao umoja kunaongezeka. Na furaha yao ya maisha ya Akhera inakuwa kubwa.

Matukio ya wema

Nyakati zote za usiku na mchana kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ zilifunikwa kwa muendelezo wa ibada za sunnah ili kuongezea katika ibada za faradhi. Swala zake za sunnah alizoziswali kabla na baada ya swala za faradhi, swala ya tahajjud aliyoendelea

kuiswali usiku, ibada kama vile kumkumbuka na kumtukuza Mwenyezi Mungu, kusoma kwake Qur'an kila siku, swala zake mbalimbali kama vile zile za mwisho wa asubuhi na jioni, funga zake za sunnah, kutoa kwake sadaka kwa masikini, mahangaiko yake katika njia ya Mwenyezi Mungu, tabasamu lililoenea sura yake kama waridi, yote yalikuwa ni ishara za amani aliyokuwa nayo kwa kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Alipofurahia jambo lolote au alipopokea habari za kufurahisha alikuwa akisujudu[42]42 na kuomba[43]43 ili kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ile. Yalipotokea matukio makubwa kama vile kupatwa kwa jua na mwezi alikuwa akiswali ili kumtukuza Mwenyezi Mungu[44]44. Alipokuwa na shida alimuomba Mwenyezi Mungu kwa kuswali. Katika mwezi wa Ramadhani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akizidisha ibada zaidi kama vile swala ya *taraweh*, *itikaf* (kujitenga kwa ajili ya ibada) na ukarimu wake katika kutoa. Baada ya Ramadhani aliendelea kutekeleza ibada za sunnah mara kwa mara. Alikuwa akifunga Jumatatu na Alhamisi na kutoa sababu ifuatayo:

❁

"Ni ndani ya jumatatu na alhamisi ambamo amali za mtu zinawasilishwa kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi. Napenda amali zangu zipelekwe nikiwa ndani ya funga". (Tirmidhi, Savm, 44/747).

❁

42. Sijda ya shukurani ni kama sijda ya kisomo. Wakati mtu ana udhu atanuia kuleta sijda ya shukurani, mikono itanyanyuliwa na kutamka takbir, "*Allahu Akbar*", kisha mtu anasujudu na kubakia katika sijda kwa kitambo, kisha ananyanyuka.
43. Ibn-i Majah, Salat, 192
44. Bukhari, Kusuf, 2-4; Ibni Hibban, Sahih, Beirut, 1993, VII, 8, 100

Mtume ﷺ alikuwa akifunga na kuwashauri maswahaba zake wafunge ndani ya tarehe 13, 14 na 15 katika kalenda ya *hijri*, yaliyoitwa *'masiku meupe'* (kutokana na kukamilika kwa mwezi). Ibn-i Abbas رضي الله عنه anasema:

❁

"Mtume alikuwa akifunga katika masiku ya mwezi kamili akiwa katika vita au amani na kamwe hakuacha kufanya hivi"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akifunga siku sita ndani ya mwezi wa *Shawwal*[45] na funga ya *Ashura* katika mwezi 9 na mwezi 10 au 10-11 ndani ya mwezi wa Muharram[46].

Mtume alikuwa akielezea ubora wa hija kubwa na ndogo (Hijja na umra) na alibakia katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu, na kamwe hakuacha kumsifu, kumtukuza na kumuomba msamaha. Alikuwa akichinja kwa ajili yake na kwa wale ambao hawakumudu kufanya hivyo[47].

Rabia bin Ka'ab رضي الله عنه anasimulia:

"Nilikuwa nikimuandalia Mtume ﷺ maji ya kuchukulia udhu na kumpelekea mlangoni kwake vitu alivyohitaji katika nyakati za usiku. Mara nilikuwa nikimsikia akisema '*Sami Allahu liman hamida*' na kisha akisema '*Alhamdulillahi Rabb al alamin*'. (Ibn-i Sa'd, IV, 313).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliniambia:

"Niombe chochote unachotaka" Nikasema:

"Nataka kuwa pamoja na wewe peponi". Mtume akajibu:

45. Muslim, Siyam, 204
46. Muslim, Siyam, 115
47. Abu Dawud, Edahi, 3-4/2792: Ibn-i Sa'd, I, 249

"Huwezi kuuliza kitu kingine?". Nikasema:

"Hili ndilo jambo pekee ninalotaka". Kwa kusikia haya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema:

"Kama ni hivyo sujudu sana ili unisaidie mimi nikusaidie wewe". (Muslim, Salat, 226).

❁

Hapa sijda inamaanisha swala ya faradhi. Hivyo wale wanaotaka kuingia peponi na kuwa majirani wa kipenzi cha Mwenyezi Mungu ni lazima waswali sana na waongeze sijda zao sehemu ambazo unakuwa karibu na Mwenyezi Mungu.

Sehemu ya Mtume Muhammad ﷺ peponi ni kubwa kuliko zile za mitume wengine. Hivyo kama mtu anataka kuwa karibu na Mtume peponi hana budi kufuata *sunnah* yake na kuswali swala za faradhi kwa unyenyekevu mkubwa.

Ummu Habiba ؓ anasimulia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu atamjengea nyumba peponi yeyote atakayeswali rakaa 12 za sunnah kwa kuongezea kwenye faradhi" . Baada ya kusikia habari hizi njema kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kamwe sikuacha swala hizi hata moja". (Muslim, Musafirin, 103).

Siku ilipotekwa Khaibar mtu mmoja alimjia mtume na kusema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, leo nimepata faida ambayo katika bonde hili hajapata mtu kuifikia". Mtume akamuuliza:

❁

"U*meingiza faida gani?*" Swahaba akajibu:

"Niliendelea kuuza na kununua bila kusimama kiasi kwamba nikapata *ukiyye* 300[48].

Mtume ﷺ akajibu:

"N*ikuambie jambo ambalo ni bora kuliko faida zote?*"

Swahaba akajibu:

"Ni lipi hilo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Mtume akatoa jibu lifuatalo:

❁

" Rakaa mbili za sunnah unazoswali baada ya swala ya faradhi". (Abu Dawud, 168/2785).

Wakati fulani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alituma kikosi cha jeshi kwenda kwenye mji fulani. Ndani ya muda mfupi sana askari wa Uislamu wakarudi na kiasi kikubwa cha ngawira. Mtu mmoja akasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hatujapata kuona kikosi kinarudi mapema hivi pamoja na ngawira nyingi kiasi hiki".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akauliza:

"Niwaambie jambo ambalo lina faida ya haraka sana na kuleta ngawira nyingi zaidi?" na kisha akaendelea:

❁

"Mtu akichukua udhu wake vizuri na kisha akafika msikitini na kuswali swala yake ya alfajiri, na kufuatanisha na rakaa mbili za swala ya katikati ya asubuhi (dhuha), atakuwa ametengeneza faida ya haraka na kupata zaidi". (Ibn-i Hibban, VI, 276/2535).

48. Ukiyye- kipimo cha zamani cha uzito sawa na gramu 1283.

Ibn-i Omar ﷺ anasimulia:

Nilimuambia Abu Dharr ﷺ:

"Mjomba mpendwa, unaweza kunipa ushauri?"

Akajibu:

"Unaniuliza nilichomuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliniambia:

❁

"Ukiswali rakaa mbili za swala ya mwishoni mwa asubuhi hautaandikwa kama miongoni mwa wajinga;kama utaswali rakaa 4 utaandikwa kama mwenye kuabudu;kama utaswali rakaa 6 utaandikwa kama 'qanitin' *(anayefanya ibada zaidi);kama utabahatika kuswali rakaa 10 utajengewa nyumba peponi".*

Hakuna mchana, usiku wala sekunde ambayo Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi hawapi waja wake kile wanachotaka na kuwaridhisha. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi hajamshushia mja yeyote neema kubwa zaidi ya anavyomshushia yule anayemkumbuka moyoni mwake. (Haythami, II, 236; Ali al-Muttaki, VII, 809/21511).

❁

Mtume ﷺ anasema:

"Kuna mlango wa kuingilia peponi uitwao Dhuha. Siku ya kiama mnadi atanadi:

"Wako wapi wale waliokuwa wamedumu kwenye swala ya Dhuha? Huu ni mlango wenu, ingieni peponi kwa rehma ya Mwenyezi Mungu". (Suyuti, I, 355/2323).

Kuswali rakaa mbili kila baada ya kuchukua udhu na kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa neema ya Uislamu na furaha ya kuchukua udhu ni jambo zuri.

Kama Othman ﷺ aliposema baada ya kuchukua udhu kabla ya kuwafundisha watu:

"Nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akichukua udhu kama hivi, kisha alipomaliza alisema:

"Yeyote atakayechukua udhu kama nilivyofanya mimi na kuswali rakaa mbili na kujitenga na vishawishi vya nafsi wakati wa swala, atafutiwa madhambi yake yote yaliyopita". (Bukhari, Wudu, 24).

Wakati fulani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuambia Bilal ﷺ:

"Ewe Bilal! Ni ibada gani uliyoifanya baada ya kuwa muislamu ambayo kwayo unatumaini malipo makubwa?Kwani nilisikia sauti ya viatu vyako mbele yangu kule peponi".

Bilal akajibu:

"Baada ya kuchukua udhu wangu huwa ninaswali kadri niwezavyo mchana na usiku. Hii ndiyo ibada ambayo kwayo ninatumaini malipo makubwa". (Bukhari, Tahajjud 17, Tawheed 47, Fadailus – Sahaba 108).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimuona Bilal akitembea mbele yake peponi ndani ya ndoto. Mwenyezi Mungu mtukufu alimuotesha Mtume ndoto hii ili amfahamishe ubora wa swala za sunnah.

❁

Siku moja Abu Qatada alikuja kwenye msikiti wa Mtume. Alipomuona Mtume mtukufu amekaa pamoja na maswahaba zake akaenda na kukaa karibu yake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipoona hili akamgeukia na kumuambia:

"Ni kipi kilichokuzuia kuswali rakaa mbili kabla ya kukaa?" Abu Qatada akajibu:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Niliona wewe na watu wako mmekaa (hivyo sikuswali)" Kisha Mtume akasema:

"Yeyote atakayeingia msikitini na asikae chini mpaka aswali rakaa mbili". (Muslim, Musafirin, 70).

Pale maswahaba walipohitaji kitu chochote au walipokuwa katika mfadhaiko haraka sana waliswali swala za sunnah na kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu. Katika kipindi fulani cha kiangazi mtunza bustani wa Anas ﷺ alikuja kwake na kulalamika kuwa mvua haijanyesha hivyo bustani imekauka. Anas akaomba maji na kuchukua udhu kisha akaswali. Baada ya kumaliza alimuuliza yule mtunza bustani:

"Je unaona kitu chochote angani?" Mtunza bustani akamjibu:

"Hapana sioni kitu".

Anas ﷺ akarudi tena ndani na kuendelea kuswali. Akamuuliza tena kwa mara nyingine:

"Unaweza kuona chochote angani?" Mtunza bustani akajibu:

"Naona wingu lenye ukubwa wa bawa la ndege". Kisha Anas akaendelea na swala na dua. Baada ya muda mfupi mtunza bustani akamuendea na kumuambia:

"Anga imejaa mawingu na mvua imeanza kunyesha". Anas akasema:

"Njoo, panda farasi tuliyetumiwa na Bishr bin Shagaf na uende kuangalia mvua imefika mpaka wapi".

Mtunza bustani alipopanda farasi na kuzunguka naye alikuta mvua haikunyesha pengine zaidi ya kwenye bustani ya Anas. (Ibn-i Sa'd, VII, 21-22).

Umuhimu wa ibada za sunnah kwa maswahaba ulienda mpaka kwa watoto wao. Rubayyi' bint-i Muawwiz ﵂ ambaye ni mmoja wa maswahaba wa kike anasema:

" ... Tulikuwa tukifunga katika siku ya Ashura na kuwaamrisha watoto wetu wadogo nao wafunge. Tulikuwa tukiwapeleka msikitini na kuwatengenezea midoli kwa kutumia pamba. Yeyote aliyelia kwa ajili ya njaa tulimpa mdoli mmoja wapo ili kumsahaulisha mpaka wakati wa kufuturu ufike". (Bukhari, Sawm, 47; Muslim, Siyam, 136).

Kwa kifupi ibada za faradhi pekee hazitoshi. Ili kuziboresha waumini hawana budi kuendelea na kuzidisha ibada za sunnah kadiri ya uwezo wao. Wafanye hivi kwa tamaa ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na kama shukurani kwa neema zote zilizowafikia katika nyakati za wepesi na ugumu. Kwani maana ya ibada ni kuwa mbele ya Mwenyezi Mungu na kuongea naye. Hili ni jambo lisilo na ugumu ambalo linauingiza moyo kwenye raha ya ajabu na kumuongezea imani.

Uzoefu unaopatikana katika ibada za sunnah na juhudi zilizoonyeshwa katika ibada hizi, vyote vinampelekea mja kufikia daraja la *'ihsan'*, ambapo mja anakakuwa karibu na mwenyezi Mungu wakati wote.

Ibada za sunnah ndiyo mwenendo unaomfaa mtu katika kuendea lengo lake la kuumbwa. Pia ni msaada mkubwa katika kuendea maisha ya kesho Akhera.

b. Kuswali katika jamaa

Mafunzo ya kijamii ni mojawapo ya misingi muhimu ya Uislamu. Na somo la kwanza kwa muislamu ni kuswali katika jamaa. Hili ni jambo muhimu ambalo linaimarisha umoja na ushirikiano katika jamii ya kiislamu, ambayo yenyewe imesimamia katika

Mungu mmoja. Sehemu ambayo swala inaswaliwa katika jamaa ndipo lilipoanzia chimbuko la mfumo wa jammii ya kiislam.

Uislamu unaamrisha waumini kuishi katika jamii kwa kusaidiana katika mambo yote na kushikamana kana kwamba ni wako katika daraja moja ndani ya njia ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaopigana katika Njia yake kwa safu kama jengo liliokamatana". (As Saff, 61:4).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

" ... Napenda muwe jamii moja yenye nguvu na kujiepusha na utengano na mgawanyiko. Hili ni kwa sababu shetani yupo pamoja na wale wanaojitenga. Lakini anakaa mbali na watu wanaoishi pamoja hata kama ni wawili. Mtu anayetaka kuwa katikati ya pepo na aendelee kuswali katika jamaa...". (Tirmidhi, Fiten, 7/2165).

Katika kila rakaa ndani ya swala tunairudia Aya isemayo **"Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada"** (Al-Faatih'a, 1:4), hivyo kuonyesha kwa mola wetu kwamba sisi ni sehemu ya jamii ya kiislamu, angalau mara 40 kwa siku.

Jambo la kwanza alilolifanya Mtume mara tu baada ya kuingia katika miji ya Quba na Madina ni kujenga msikiti. Yeye mwenyewe alisaidia katika ujenzi wa msikiti hivyo kuweka misingi ya udugu wa kiislamu.

Baba zetu waliotangulia walifuata mwenendo huu wa Mtume. Walipotaka kujenga miji kwanza kabisa walijenga misikiti katikati na kuendeleza miji kwa kuizunguka misikiti kuwa kama duara la nuru.

Hivyo kuswali katika jamaa ni jambo linalopendeza katika Uislamu na ni amri ya Mwenyezi Mungu.

Mtume ﷺ anasema:

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anapendezwa na kufurahishwa na muislamu ambaye anaenda mara kwa mara msikitini kwa lengo la kumtaja Mwenyezi Mungu au kuswali kama inavyopendezwa familia ambayo wanafamilia wenzao walio mbali na nyumbani watakaporudi". (Ibn-i Majah, Masajid, 19).

"Yeyote atakayejenga urafiki na msikiti, Mwenyezi Mungu atajenga urafiki na yeye". (Suyuti, II, 143).

"Je niwafahamishe namna Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anavyofuta makosa ya watu na namna anavyopandisha daraja la mtu?kuchukua udhu katika siku yenye baridi, kwenda kwenye jamaa kutoka maeneo ya mbali na msikiti na kusubiri swala inayofuata baada ya kuswali swala ya nyuma yake. Huku ndiko kujitoa kwa kweli! Huku ndiko kujitoa kwa kweli! Huku ndiko kujitoa kwa kweli!". (Muwatta, Kasru's Salat, 55).

❁

Aisha ﵂ anaelezea:

"Yeyote atakayesikia adhana na asiende msikitini, inamaanisha kuwa hapendi wema na wala hajaandikiwa kupata wema". (Bayhaki, AS Sunan al Kubra, III, 57).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakumridhia mtu ambaye alipuuza kuswali katika jamaa. Siku moja alisema:

"Yeyote atakayesikia adhana na asiende msikitini, na hana dharura inayomzuia kufanya hivyo haitakubaliwa swala yake(kwa ukamilifu). Maswahaba wema wakamuuliza:

"(Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu) ni ipi hiyo dharura?"

Mtume akajibu:

"Hofu ya hatari au ugonjwa". (Abu Dawud, Salat, 46/551).

Kuacha kuswali katika jamaa kutapelekea kuvunjika kwa umoja wa kiislamu. Mwenyezi Mungu mtukufu anamkemea yule anayewagawa watu kama ifuatavyo:

"Hakika walioigawa Dini yao na wakawa makundi makundi, huna uhusiano nao wowote". (An'am, 6:159).

❁

Matukio ya wema

Abu Hurayra ﷺ anasimulia:

"Wakati fulani tulipokuwa katika msafara Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alibaki sehemu kati ya Dacnan na Usfan. Washirikina wakasema:

"Waislamu wana swala ambayo ina thamani kwao zaidi ya baba zao na watoto wao. Swala hii ni swala ya *al-asr*. Jiandaeni na muwashambulie wote kwa wakati mmoja (wakati wanaswali hii swala)"

Kutokana na hili malaika Jibril alimjia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na Aya ya 102 kutoka katika *surat Nisai* ambayo inafafanua namna ya kutekeleza swala ya jamaa katika vita. (Tirmidhi, Tafsir, 4/21).

Hivyo hata katika vita, bila kujali hali iliyopo, waislamu hawakuweza kucheleweshа swala wala kuacha kuswali katika jamaa.

Jafar bin Amr anasimulia maneno aliyosikia kutoka kwa baba yake:

"Nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akikata mguu wa mwana kondoo na kuanza kuula. Wakati ule ule akasikia adhana, upesi akanyanyuka na kuacha kisu kilichokuwa mkononi mwake na bila ya kuchukua udhu mwingine akasimama kuswali". (Bukhari, Adhan, 43).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa makini juu ya kuswali katika jamaa hata ikafikia kuacha chakula upesi na kunyanyuka kwa ajili ya kuswali katika mwito wa kwanza, ambapo angeweza kusubiri mpaka amalize kula.

Yazid bin Amir ﷺ anasimulia:

"Nilifika karibu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wakati anaswali. Nikakaa chini bila ya kujiunga na jamaa. Mtume alipomaliza swala na kugeuka akaniona nimekaa katika pembe, akaniambia:

❁

"Ewe Yazid! Je wewe si muislamu?"

"Kwa hakika mimi ni muislamu ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu", nikasema.

"Kwa hiyo ni kipi kilichokuzuia kujiunga na jamaa?" Akamuuliza.

"Nilidhani mmeshaswali hivyo nikaswalia nyumbani", nikasema. Kisha Mtume akasema:

"Kama kwa bahati unakuja katika swala na kuwakuta watu wanaswali ungana nao. Kama tayari umeshaswali ile swala basi itahesabika kama sunnah. Ile uliyoswali nyumbani itahesabika kama faradhi". (Abu Dawud, Salat, 56/577).

Hata wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ana maradhi ambayo ndiyo sababu ya kifo chake, jambo la muhimu zaidi kwake lilikuwa ni kuswali katika jamaa. Imesimuliwa kutoka kwa Anas ﷺ kuwa Mtume hakuweza kujiunga na jamaa katika siku tatu pekee za mwishoni mwa maradhi yake. (Bukhari, Athan, 46).

Aisha ﷺ anasema:

"Mtume alipozidiwa na maradhi aliuliza:

"Je, Maswahaba zangu wameshaswali?"

"Hapana ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wanakusubiri wewe" Nikasema.

"Kama ni hivyo niandalie maji" akaniambia. Nikampa maji kisha akajisafisha mwenyewe. Alipojaribu kunyanyuka akazimia. Baadaye kidogo akapata fahamu na kuuliza tena:

"Je, Maswahaba zangu wameshaswali?"

"Hapana ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wanakusubiri wewe" Nikasema.

❁

"Kama ni hivyo niandalie maji" akaniambia. Nikampa maji kisha akajisafisha mwenyewe. Alipojaribu kunyanyuka akazimia. Baadaye kidogo akapata fahamu.

Jambo hili likajirudia mara kadhaa. Baada ya muda mfupi watu waliopo msikitini walikuwa wakimsubiri Mtume ili waswali swala ya *'isha* (swala ya usiku). Kisha Mtume akaagiza Abu Bakar aongoze swala. Abu Bakar ﷺ alikuwa ni mtu mwenye upole sana hivyo akamuambia Omar ﷺ:

"Ewe Omar, Je unaweza kuongoza swala?" Omar hakuweza kukubali ombi lake hivyo akasema:

"Wewe unastahiki zaidi hili". Kuanzia pale Abu Bakar ﷺ akawa anaongoza swala. Baadaye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipopata nafuu kidogo alienda msikitini kuswali swala ya mchana akiwa ameshikilia mikono ya wanaume wawili. (bado naweza kumuona akiwa mbele yangu huku miguu yake iliyobarikiwa ikiwa inaburuta chini wakati anatembea kutokana na kukosa nguvu)[49].

49. Bukhari, Athan, 67

Wakati ule Abu Bakar ﷺ alikuwa anaongoza swala. Alipoona Mtume amefika akataka kusogea nyuma. Hata hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuashiria abakie pale alipo. Kisha akaenda na kukaa karibu na Abu Bakar. Abu Bakar akawa anamfuata Mtume, wakati watu wanamfuata Abu Bakar mpaka wakamaliza swala yao. (Bukhari, Athan, 51).

❁

Anas ﷺ anasimulia:

"Wakati fulani Abu bakar alikuwa anaswali. Ilikuwa ni jumatatu na tulikuwa katika safu zilizonyooka. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alinyanyua pazia la mlango wake na kutuangalia. Alikuwa amesimama huku uso wake unang'aa. Kisha akatabasamu mpaka meno yake yakaonekana. Tulipomuona Mtume aliyebarikiwa tukajawa na furaha kiasi cha kutaka kuacha swala. Abu Bakar akaanza kusogea nyuma ili akae katika safu ya kwanza huku akidhani kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu angelijiunga na swala. Hata hivyo Mtume alimuashiria amalizie swala kisha akarudishia pazia lake. Ile ilikuwa ndiyo siku ya mwisho kumuona na pia ndiyo siku aliyoenda kwenye maisha ya milele". (Bukhari, Adhan, 46).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alifurahi kwa kuwa ameacha watu ambao wanasimama katika safu zilizonyooka ndani ya swala na wanaendelea kuswali katika jamaa kana kwamba ni jengo lililoimarishwa kwa madini ya risasi. Alipowaangalia uso wake uliobarikiwa ulitabasamu. Tabasamu ambalo liliangaza dunia nzima lillikuwa ndiyo chanzo cha matumaini kwa maswahaba wake waliobarikiwa, (lakini walikuwa hawana budi kukubali kuwa) amerejea kwa Mwenyezi Mungu kwa amani na anasubiri kukutana nao.

Maneno ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kabla ya kufa kwake yalikuwa:

❁

"Swala zenu! Swala zenu! Kuweni makini na swala zenu na muogopeni mwenyezi Mungu katika juu ya vile vilivyo chini ya usimamizi wenu" (Abu Dawud, Adab, m 123-4/ 5156; Ibn-i Majah, Wasaya, 1)

Jabir bin Abdullah ﷺ anasimulia:

"Makazi ya kabila langu la Bani Salim yalikuwa mbali na msikiti. Kulikuwa na maeneo yenye nafasi pembezoni mwa msikiti wa Mtume, hivyo tukataka kuiuza nyumba yetu ili tusogee karibu na msikiti. Wakati ule Aya ifuatayo ikashushwa:

❁

"Hakika Sisi tunawafufua wafu, na tunayaandika wanayoyatanguliza, na wanayo yaacha nyuma. Na kila kitu tumekihifadhi katika daftari lenye kubainisha" (Yasin 36:12)

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliposikia nia yetu akasema:

"Nimesikia kuwa mnatakakusogea karibu na msikiti, je ni kweli?" Wakasema:

"Ndiyo, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Kwa hakika tunataka kufanya hivyo"

Kisha Mtume aliyebarikiwa akasema:

❁

"Enyi Bani Salim! Bakieni mlipo ili mpate malipo kwa kila hatua mnayopiga mkija msikitini. Kwa hakika bakieni mlipo ili muandikiwe malipo kwa kila hatua mnayopiga mkija msikitini" (Muslim, Masajid, 280, 281; Tirmidhi, Tafsiru'l Qur'an, 36/1).

Siku moja Abdullah bin Ummi Maktum ﷺ alimuuliza Mtume:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Ndani ya Madina kuna wadudu wengi wenye sumu na wanyama mwitu wengi. Nahofia madhara ambayo yanaweza kunipata kutokana na wanyama hawa. Je nina ruhusa ya kuswalia nyumbani badala ya kuja msikitini?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

❁

"Je unaweza kusikia maneno:" hayya ala's-swalah" (njooni kwenye swala) na "Hayya ala'l falah" (njooni kwenye mafanikio)? Kama ndivyo basi hamna budi kuja msikitini" (Abu Dawud, Salat, 46/553).

Hivyo Mtume aliweka msisitizo mkubwa katika kuhudhuria kwenye jamaa kwa hali yoyote ile hata ikibidi kufanya jitihada kubwa ili kuipata.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitumia njia mbalimbali katika kuwausia watu wahudhurie katika swala za jamaa. Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه anasimulia:

"Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliongoza swala ya alfajiri kisha akasema:"

"Je fulani amekuja kwenye swala?"

"Hapana, hakuja" Tukajibu.

"Je fulani amekuja?" Aliuliza tena.

"Hapana, hakuja" Tukajibu. Kisha akasema:

❁

"Swala hizi mbili (Alfajiri na swala ya usiku) ndizo zilizo ngumu zaidi kwa wanafiki. Lau mngelijua malipo na faida zinazopatikana kutokana na swala hizi, mngelitembelea magoti na kujiburuza ili kwenda kujiunga na jamaa. Safu ya kwanza ni kama safu ya malaika. Lau mngelijua ubora wake, mngelishindana ili kuswali katika safu hiyo. Swala ya mtu aliyeswali na mtu mwingine ni bora zaidi na ina malipo zaidi ya swala aliyoswali peke yake. Swala ya watu wawili ni nzuri na bora zaidi ya swala ya mtu mmoja. Kadri idadi ya watu inavyoongezeka, ndivyo Mwenyezi Mungu

aliye juu zaidi anavyoiridhia zaidi". (Abu Dawud, Salat, 47/554; Nasai, Imamet, 45).

❁

Abdullah bin Mas'ud ﷺ ana kifuatacho cha kusema:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu, sijapata kumuona mtu mwingine zaidi ya mnafiki, ambaye unafiki wake umejulikana kwa watu wote tofauti na mtu aliyepuuzia swala yake. Naapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba hata kama mtu angelikuwa mgonjwa angeliletwa katika swala hata kama angelikuwa anapepesuka na huku ameshikiliwa na watu wawili, na angelikuwa katika safu kati ya wale watu wawili kama msaada kwake" (Muslim, Masajid, 256-257).

❁

"Siku moja Abdullah bin Omar ﷺ alikuwa anatembea sokoni, muda wa swala ukafika. Akawaona wakifunga maduka na mazizi yao mara tu baada kusikia mwito wa swala na kuelekea msikitini. Alipoona haya akasema:

"Hawa ni wale ambao Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amewatukuza kama ifuatavyo:

"Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu, na kushika Sala, na kutoa Zaka. Wanaihofu Siku ambayo nyoyo na macho yatageuka" (An Nur, 24:37) (Ibn-i Kathir, Tafsir, III, 306; Haythami, VII, 83).

❁

Shifa bint- Abdillah ﷺ anasimulia kuwa:

"Siku moja Omar bin Khattab ﷺ alikuja kutuona. Alipoona watu wawili wa familia yetu wamelala akauliza:

"Hawa watu wana tatizo gani mpaka wakashindwa kujumuika katika jamaa?"

"Ewe kiongozi wa waumini! Hawa waliswali pamoja waumini wengine jioni-tukio hili lilitokea katika mwezi wa Ramadhani-kisha wakaendelea kuswali mpaka asubuhi. Baada ya hapo wakaswali swala ya alfajiri na kwenda kulala" Nikasema.

Omar akajibu kama ifuatavyo:

"Kuswali swala ya alfajiri katika jamaa ni bora kwangu kuliko kuswali mpaka asubuhi" [50].

❁

Wakati fulani Othman bin Affan ﷺ alikuwa ameenda kwenye swala ya usiku. Alipoona mkusanyiko umetawanyika akalala nyuma ya msikiti huku akiwasubiri watu wengine wafike.

Wakati ule Ibn-i Abi Amri ﷺ akafika na kukaa karibu na Othman. Othman akamuuliza yeye ni nani. Akajitambulisha kwake. "Unajua kiasi gani katika Qur-an?" Akamuuliza. Alipojibu hili Othman akasema:

"Ewe mtoto wa kaka yangu! Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akisema:

"Mtu anayeswali swala ya usiku pamoja na watu (katika jamaa) ni kama mtu aliyetumia nusu ya usiku akiswali. Mtu anayeswali swala ya alfajiri katika jamaa ni kama mtu aliyetumia usiku mzima akiswali" (Muwatta, Salatu'l Camaa' 7; Muslim, Masajid, 260).

Thabit bin Hajjaj anasimulia hadith ambayo inawagusa wale ambao hawashiriki katika swala ya jamaa:

"Siku moja Omar bin khattab ﷺ alikuja msikitini kwa ajili ya swala. Akawageukia watu na kumuamuru mpiga adhana asome adhana, kisha akasimama na kusema:

50.Abdurrazak, al Musannaf, Beirut 1970, I, 526; Muwatta, Salatu"l Jamaa, 7

"Hatutamsubiri mtu katika kuswali" Alipomaliza kuswali akawageukia watu na kusema:

❁

"Watu fulani wana tatizo gani mpaka wanashindwa kuswali katika jamaa na kusababisha wengine wasiswali. Naapa kwa Mwenyezi Mungu nilitamani kuwatuma watu waende wakawashike hao watu na kuwaleta hapa ili niwausie wajiunge na swala" (Abdurrazzak, 1, 519).

Ummu-d Darda ﵂ anasimulia kuwa:

"Siku moja Abu-d Darda ﵁ alikuja kwangu akiwa na hasira. Nikamuuliza:

"Ni kipi kilichokukasirisha?". Akatoa jibu lifuatalo:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu sijui kingine juu ya watu wa Muhammad ﷺ zaidi ya kuwa wanaswali katika jamaa. (Kwanini hawa watu wanapuuzia swala?)" (Bukhari, Adhan, 31).

Pale Abdullah bin Omar ﵁ alipokosa swala ya jamaa alikuwa akifanya ibada mpaka swala inayofuata. Pia alifanya hivi katika swala za usiku. Yaani alikuwa akifanya ibada mpaka asubuhi. (Ibni Hajar, Isabe, II, 349).

❁

Mmoja wa maswahaba waliobarikiwa aitwae Harith bin Hassan ﵁ alikuwa ndiyo punde ameoa. Wakati ule ilikuwa ni desturi kwamba mtu ambaye ndiyo ametoka kuoa haruhusiwi kutoka nyumbani kwa siku kadhaa, Hivyo hakuhudhuria swala ya alfajiri. Hata hivyo alihudhuria swala ya alfajiri siku iliyofuata. Akaulizwa na baadhi ya watu:

"Umeoa jana usiku, inakuaje umeondoka nyumbani kwako" Jibu lake lilikuwa:

"Naapa kwa jina laMwenyezi Mungu! Ubaya ulioje wa mke ambaye angelinizuia kuswali swala ya alfajiri katika jamaa" (Haythami, II, 41).

Siku moja Ibn-i Jurayj alimuuliza Ata' (q.a) ambaye alikuwa ni miongoni mwa wanavyuoni maarufu katika kipindi cha *tabi'een*:

"Kama mtu anaswali swala ya faradhi nyumbani kwake kisha akasikia (miongoni mwa) adhana mbili, je akate swala yake na kwenda msikitini?"

❁

"Kama ana matumaini ya kupata hata sehemu ya swala ile, basi afanye hivyo" Ata akajibu.

"Vipi kama nitasikia adhana ya pili, je nije msikitini kama ambavyo ningelifanya ninaposikia adhana ya kwanza?" Ata akajibu "Ndiyo". (Abdurrazzak, I, 514).

Vivo hivyo siku moja Ibn-i Omar (Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) aliswali swala mbili za faradhi zenye rakaa nne nyumbani kwake, aliposikia adhana ya pili haraka akaenda msikitini. (Abdurrazzak, I, 514-515).

Amir bin Abdullah alikuwa juu ya kitanda alichofia. Pumzi zake zilikuwa za kuhesabu na watu waliomzunguka walikuwa wakilia. Aliposikia adhana ya swala ya adhuhuri akawaambia wale waliomzunguka:

"Ninyanyueni".

"Kuna nini, unataka kwenda wapi?" Wakamuuliza.

"Kwenda msikitini" Akasema. Wale waliomzunguka wakamuuliza kwa mshangao:

"Katika hali hii?"

Akasema kwa ujasiri mkubwa:

❁

"Subhanallah! (Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu). Je nisikie adhana na nisijibu? Je hili linawezekana? Ninyanyueni!"

"Alienda msikitini huku akisindikizwa na wale walio karibu naye na baada ya kuswali rakaa moja pamoja na imamu akakata roho akiwa kwenye sijda".

Uzuri ulioje wa hadith: "Namna unavyoishi ndivyo utakavyokufa" Kwa rehema za Mwenyezi Mungu mja ambaye aliweka umuhimu mkubwa katika kuswali katika jamaa amefariki akiwa katika sijda.

Ata bin Thabit (q.a) anasimulia:

"Tulisikia kuwa mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu aitwae Abdullah-i Sulami ni mgonjwa. Tukafikiria kwenda kumtembelea. Wakatuambia kuwa anaishi msikitini. Tukaona lile ni jambo geni kwetu. Kuishi msikitini wakati ana kitanda nyumbani kwake, likawa ni jambo geni kwetu. Tulipoenda msikitini tukamkuta anaswali. Tulipoona anapata shida kupumua tukaogopa na tukasema:

❁

"Ewe Shaykh! Je si ungelikuwa na utulivu kama ungelibaki kitandani nyumbani kwako?"

Akatupa jibu lifuatalo:

"Kutokana na hadith iliyonifikia, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitujulisha kuwa kuswali katika jamaa ni bora. Nilitamani roho yangu ichukuliwe wakati naswali msikitini"

Muhammad bin Sammad alikuwa ni mtu mwenye kufanya ibada sana. Alikuwa makini sana lilipokuja suala la kuswali katika jamaa. Anasema:

"Siku zote ninaswali katika jamaa. Kamwe sijawahi kukosa *takbir* ya kufungulia swala kwa miaka arobaini sasa. Siku moja tu nilikuwa nimeshughulishwa na msiba wa mama yangu nikakosa rakaa ya kwanza. Nikaiswali hii swala mara 25 kwa matumaini ya kupata ujira wa swala ya jamaa. Usiku ule ndani ya ndoto niliambiwa:

"Ewe Muhammad! Umeswali swala yako mara 25, ni vipi utaweza kufidia pale malaika wanaposema Amin katika swala ya jamaa?". (Kandevli, Fazail'i A'mal, uk. 275).

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

"Imam atakapomaliza kusoma surat Fatha na maamuma waitikie 'amin'. Kwani kama neno hili la mkusanyiko litakutana na 'amin' ya wale walio mbinguni, basi mtu huyu atasamehewa madhambi yake madogo yaliyopita". (Bukhari, Adhan, 113).

Kutokana na masimulizi, Siku ya kiama Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atauliza:

"Wako wapi majirani zangu?"

Malaika watauliza:

"Nani anaweza kuwa jirani yako ewe Mola?"

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atasema:

"Wale wanaostawisha misikiti yangu (hawa ni wale wanaoendelea kuswali katika jamaa)". (Ali al Muttaki, VII, 578/20339).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Msikiti ni nyumbani kwa wale wote walio wema. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amewaahidi utulivu, huruma, kuwapitisha kwenye daraja la Sirat mpaka peponi na kuwaridhia wale wanaofanya misikiti kuwa nyumbani kwao" [51]

Mmoja wa wanahistoria wa Uthmainiyya aitwae Asik Pashazade alisema:

"Familia hii ya Uthmainiyya inatoka kwenye ukoo wenye kuheshimika. Hakujawahi kuonekana kwao kitendo kilichoharamishwa. Walijitahidi kujizuia na mambo yote yaliyosemwa na wanavyuoni wao kuwa ni ya dhambi"

Tabia zao zilizokwishatajwa ndizo zilizopelekea Shaykhu'l Islam, Molla Fenari apate ujasiri wa kukataa ushahidi wa Yildirm Bayazit mahakamani kwa sababu hakuwa (akiswali) katika jamaa. Alipoulizwa na Sultani sababu iliyompelekea akatae ushahidi wake alijibu kwa uwazi:

"Sultani wangu! Sikuoni katika jamaa, wakati wewe kama kiongozi wa taifa hili ungelikuwa katika safu ya kwanza. Kwa maneno mengine unatakiwa uwe mtu mwenye vitendo vizuri... Kama hujumuiki na watu katika jamaa basi utakuwa ni mfano mbaya kwa watu wako, jambo ambalo litazuia ukubalike kuwa shahidi..."

Baada ya tukio hili, na katika masimulizi mengine kama shukrani kutokana na ushindi wa Nigbolu, Yildirim Bayazid alijenga msikiti maarufu uitwao Ulu ndani ya Bursa na akawa anaswali katika jamaa mara tano kwa siku.

Kwa kifupi swala ya jamaa inaonyesha ukomavu wa imani ya watu. Vilevile Mtume ﷺ anasema:

51. Taberani, Al Mu'jemu'l abir, tah. Hamdi Abdulmecid as Salafi, Beirut, Daru Ihyai't turasi'l Arabi, VI, 254/6143; Ali al Muttaki, VII, 580/20349

"Ukimuona mtu anaswali katika msikiti mara kwa mara basi utakuwa shahidi wa imani yake" na kisha akasoma Aya ifuatayo:

"Hakika wanaoamirisha misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na wakashika Sala, na wakatoa Zaka, na wala hawamchi ila Mwenyezi Mungu. Basi huenda hao wakawa katika waongofu" (Tawba, 9:18)(Tirmidhi, Iman, 8/2617).

Marafiki wa Mwenyezi Mungu wameelezea faida za msingi zinazopatikana kwa kuswali jamaa msikitini kama ifuatavyo:

-Kufaidika kutokana na mafanikio na neema ambazo Mwenyezi Mungu ameziweka katika msikiti na kusimamisha ujamaa ndani ya moyo wa muumini.

-Kuswali kwa wakati, hasa wakati wake wa mwanzo.

-Kupata dua, kuombewa msamaha na kushuhudiwa na malaika.

-Kuwa mbali na shetani.

-Kupata malipo makubwa kwa kuwepo katika takbira ya kufungulia swala.

-Kutakaswa kutokakana na kujiona na katika matendo ya mtu.

-Kufaidika na dua na utajo wa Mwenyezi Mungu unaofanywa kwa pamoja.

-Kutoa uhakika wa muendelezo wa mahusiano miongoni mwa waislamu.

-Kusaidiana katika masuala ya utii na ibada.

-Kujifunza kanuni za usomaji wa Qur-an katika swala inaposomwa Qur-an kwa sauti.

-Kuswali kwa ukamilifu na amani.

Kuswali katika jamaa kuna faida nyingi. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi na Mtume wake kipenzi mara kwa mara wamewaamrisha waumini kuswali misikitini na kuendelea kuswali katika jamaa.

c. Ibada za usiku

Ni furaha isiyoelezeka kwa mja kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu mtukufu ndani ya vina vya usiku. Pia ni chanzo cha rehema zisizo na kifani, msamaha na baraka, kwani Mwenyezi Mungu anapendezwa na kuridhia jambo hili. Qur'an tukufu inaeleza:

"Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumwomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyowaruzuku". (As Sajda, 32:16).

Siri, hekima na ustawi ambao Mola wetu ameuweka juu ya usiku unakuwa wazi katika moyo wa mtu. Fadhila hizi tukufu ambazo zinapandisha daraja la mja zinapatikana katika vina vya usiku, hivyo mja hana budi kuzipa uzito nyakati hizi ndani ya siku.

Usiku ni baraka ya kipekee kwa waumini wanaotamani kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kutokana na utuluvu na ustawi unaopatikana usiku.

Tunaelezwa katika *hadith*:

"Kuna muda ndani ya usiku ambao kama muislamu ataomba jambo lolote jema ndani ya dunia hii au kesho akhera Mwenyezi Mungu atampa. Muda unapatikana kila usiku". (Muslim, Musafirin, 166)

Khaja Ali Ramiteni (q.a) anasema:

"Haja ya muumini itakidhiwa endapo nyoyo tatu zitaungana; moyo safi wa muumini, moyo wa Qur'an ambao ni surat Yasin na

moyo wa usiku ambao ni muda mfupi kabla ya alfajiri. Wale ambao wanatambua thamani ya baraka hii wanakuwa wamepata wakati muhimu kwa ajili ya dua, ibada na kujikurubisha kwa Mola wao, wakati viumbe wengine wamelala na kuna utuluvu wa hali ya juu duniani kote. Mwenyezi Mungu mtukufu amewatukuza waja hao wenye furaha kama ifuatavyo:

"Walikuwa wakilala kidogo tu usiku na kabla ya alfajiri wakiomba maghfira". (Az Zariyat 51:17-18).

Usiku ni muda wa kuacha utamu wa kitanda kwa dhumuni pekee la kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Usiku ni muda wa kuingia kwenye utukufu wa Mwenyezi Mungu kutokana na furaha na mapenzi ya mja kwa Mola wake. Haya yanapelekea swala zinazoswaliwa nyakati tulivu za usiku, Qur'an inayosomwa na utajo unaofanywa kuwa na umuhimu mkubwa katika kutafuta ukaribu na Mwenyezi Mungu. Ibada inayofanywa nyakati za usiku ni sawa na kukutana na kipenzi chako na kuongea naye. Kubakia macho wakati watu wengine wamelala, na kuingia kwenye rehema za Mwenyezi Mungu ambaye ndiye Mlinzi wetu, ni jambo ambalo linamuwezesha muumini kuwa miongoni mwa waja maalum wenye mapenzi na rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Uharaka wa kufanya ibada za usiku unaendana na kiwango kikubwa cha furaha na mapenzi ya Mwenyezi Mungu ndani ya moyo. Baadhi ya wafanya ibada za usiku ambao wameonja raha na utukufu wake wanasema: "Siogopi kifo, mpaka kije kati yangu na swala zangu za usiku".

Unakuwaje mtu ambaye anadai anampenda Mola wake kikweli kweli, analala mpaka asubuhi bila kujali?Ndiyo maana kuamka kabla ya alfajiri ni jambo linalodhihirisha mapenzi ya kweli na heshima kubwa aliyonayo mja kwa Mola wake. Kwa upande mwingine usiku uliopita bila mazingatio yoyote unachukuliwa kuwa usiku usio na faida, kama mvua iliyonyesha jangwani.

Hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimshauri Abdullah bin Amr

Ibn As ﷺ kama ifuatavyo:

❁

"Abdullah! Usiwe kama yule. Kwani ingawa alikuwa akiendelea kufanya ibada za usiku, kwa sasa ameacha". (Bukhari, Tahajjud, 19).

Hivyo kuacha *tahajjud* usiku ni hasara kubwa na ni chanzo cha uharibifu.

❁

Kufaidika kutokana na ibada za usiku kunaanza kwa "Kuomba msamaha" ; na kunaendelea kwa kujiingiza kwenye ukanda wa kiroho wa tawheed, kumswalia Mtume (*salawat-i sherif*) na kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Kumkumbuka Mwenyezi Mungu katika nyakati kabla ya alfajiri ni sawa na makutano ya mja na Mlinzi wake, jambo ambalo linauhuisha moyo. Hii ni nafasi ya kipekee ambayo haistahiki kupotezwa na ni hitajio lisiloweza kupuuzwa. Kama miili yetu inavyohitaji kunawiri ndivyo ambavyo roho zetu zinavyohitaji kustawishwa kiimani. Mwenyezi Mungu mtukufu ameweka thamani kubwa kwenye utajo unaofanywa kabla ya alfajiri ukilinganisha na nyakati nyingine. Imeelezwa katika Qur'an:

"Na usiku msujudie Yeye, na umtakase usiku, wakati mrefu. Kwa hakika watu hawa wanapenda maisha ya kidunia, na wanaiacha nyuma yao siku nzito". (Man, 76:26-27).

Amr bin Abasa ﷺ anasimulia:

Nilimuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Je kuna muda ulio bora zaidi mwingine ambao unamkurubisha zaidi mja kwa Mwenyezi Mungu?"

Akajibu:

"Ndiyo, muda ambao mja yuko karibu zaidi na Mola wake ni katikati ya sehemu ya mwisho ya usiku. Kama utaweza kuwa miongoni mwa wale wanamkumbuka Mwenyezi Mungu katika muda huo, fanya hivyo. Kwani swala itakayoswaliwa wakati huo inashuhudiwa (malaika huwa pamoja nao)". (Nasai, Mawakit' s Salat, 35).

Kwa ufupi, kama muumini atatumia vizuri usiku kama alivyoshauriwa na Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake na kufaidika kutokana na kumkumbuka yeye, usiku wake utang'aa zaidi ya mchana. Vivo hivyo Bayazid-i Bistami anasema:

❁

"Hakuna siri zilizodhihirishwa kwangu mpaka nilipofanya nyakati zangu za usiku kuwa nyakati zangu za mchana"

Kwa wale wanaojua thamani ya usiku ambao umejaa fadhila kubwa na hivyo kuuhuisha kwa njia nzuri, imani ya kabla ya alfajiri itaenea siku nzima. Kutokana na haya ili kufaidika zaidi kutokana na mafanikio ya kiimani yaliyopatikana usiku hatuna budi kuendelea na misingi hii katika masiku yetu na kujizuia na madhambi.

Matukio ya wema

Juu ya kufaidika kutokana na mafanikio ya usiku, Mwenyezi Mungu mtukufu anamuamrisha kipenzi chake kama ifuatavyo:

"Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya sunna hasa kwako wewe. Huenda Mola wako Mlezi akakunyanyua cheo kinachosifika". (Isra, 17: 79).

❁

Tangu amri hii tukufu itolewe kamwe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakuacha kuswali wakati wa usiku ambao umebarikiwa na wenye mafanikio, wala hakuacha kuomba msamaha, kusoma Qur'an na kuomba dua nyingine. Alifanya haya hata zile siku alizokuwa mgonjwa na kudhoofika kiasi cha kushindwa kusimamia miguu yake. Hakupuuzia swala yake ya tahajjud na hivyo alihuisha nyakati zake za usiku hata kama ni kwa kukaa. (Abu Dawud, Tatavvu", 18/1307).

Mke wa Mtume, Aisha رضي الله عنها anatufahamisha kuwa:

❁

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kamwe hajawahi kuswali zaidi ya rakaa 11 katika swala za usiku, ikiwa ni ndani ya Ramadhani au wakati mwingine wowote. Kwanza alikuwa akiswali rakaa nne zilizokuwa ndefu na nzuri. Kisha aliswali rakaa nne zaidi. Usiulize uzuri na urefu wake (kwani ni ngumu kuzielezea). Kisha aliswali rakaa mbili zaidi. Wakati fulani nilimuuliza:

❁

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Je utalala bila ya kuswali swala ya *witr*?"

"Aisha! Macho yangu yanalala lakini moyo wangu haulali kamwe" Alijibu. (Bukhari, Tahajjud 16, Tarawih 1; Muslim, Musafirin 125).

Hadith hii inaonyesha ni namna gani moyo wa Mtume ulikuwa pamoja na Mwenyezi Mungu mtukufu, si wakati wa ibada tu bali wakati wote.

Hudhayfa ﷺ anaelezea hali ya Mtume ilivyokuwa wakati wa ibada siku moja alipokuwa nyuma yake katika swala ya sunnah:

❁

"Siku moja nilisimama kuswali pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Akaanza kusoma surat Baqara ndani ya Qur'an. *"Nadhani atarukuu akifika aya ya mia moja"* Nikajisemea mwenyewe. Alipofikia aya ya mia moja akaendelea kusoma. *"Labda ataswali rakaa mbili kwa sura hii"* Nikafikiria. Akaendelea kusoma. *"Atarukuu akimaliza sura"* Nikafikiria. Hata hivyo bado hakumaliza. Akaanza kusoma surat *Al-i Imran*[52]. Alikuwa akisoma taratibu sana. Alipokuwa akifika kwenye aya yenye kutukuza alisema "S*ubhanallah* (Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu). Alipofika kwenye aya ya dua, alikuwa akiomba dua. Alipofika kwenye aya ya kujikinga kwa Mwenyezi Mungu, alijikinga kwa Mwenyezi Mungu. Kisha akarukuu. Akaanza kusema "S*ubhana Rabbiya'l a'zim*" (Utukufu ni wa Mola wangu, Aliye Mkuu) Rukuu yake ikawa ndefu kama kilivyokuwa kisimamo chake. Kisha akasema "S*ami Allahu liman hamida. Rabbena laka'lhamd*" (Mwenyezi Mungu anasikia wanaomtukuza. Utukufu wote ni wako ewe Mola wetu) na kunyooka. Akabakia katika kisimamo kama alivyokuwa ametulia katika rukuu. Kisha akasujudu. Akasema "S*ubhana Rabbiya'l ala*" *(Utukufu ni wa Mola wangu, aliye juu zaidi).* Sijda yake ikawa ndefu kama kilivyokuwa kisimamo chake" (Muslim, Musafirin, 203).

Aisha ﷺ anasema:

"Usiku mmoja niligundua kuwa Mjumbe wa Mwenyezi hakuwa pembeni yangu. Nikadhani ameenda kwa mke mwenzangu.

52. Kutokana na maelezo ya hadith hii, Mtume ﷺ alisoma kwanza Baqara, kisha An Nisaa, kisha Al Imran. Usomaji katika utaratibu huu sio sawa na mpangilio wa sasa wa Qur'an, ambao ni Baqara, Al Imran, An Nisaa. (Wachambuzi) wa hadith wanaelezea hekima yake kwa namna mbili: Kwanza, wakati ule hakukuwa na mpangilio maalum wa sura. Pili, inaruhusiwa kusoma sura katika mpangilio huu.

Nikaanza kumtafuta. Baada ya muda niliporudi nikamkuta ama amerukuu au yuko kwenye sijda huku anasema yafuatayo:

سُبْحَانَكَ وَبِحَمْدِكَ لَا اِلٰهِ اِلاَّ اَنْتَ

"(Ewe Mwenyezi Mungu!) Naomba unisamehe madhambi yote na nakutukuza wewe. (Mola wangu Mlezi!) Hakuna mungu mwingine isipokuwa Wewe. Kutokana na haya nikamuambia (kwa uchokozi):

"Mama yangu na baba yangu watolewe kafara kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!Nilikuwa najisumbua nini na wewe uko hapa.". (Muslim, Salat, 221).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitamani umma wake wote uswali swala ya *tahajjud*, ambayo ni moja ya njia muhimu za kuongeza imani ya mtu. Alianza kuwazoesha wale walio karibu naye. Usiku mmoja aligonga kwenye mlango wa mkwe wake na binti yake, Ali رضي الله عنه na Fatma رضي الله عنها na kuwaambia: *"Hamuendi kuswali?"* Aliwasisitizia jambo hili ili wafaidike na mafanikio ya kiimani yanayopatikana usiku.

❁

Kwa maswahaba wengine aliwaambia:

"Fanyani juhudi kuamka usiku. Kwani huo ulikuwa ndiyo mwenendo wa watu wema waliotangulia na ni njia ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. (Ibada ya namna hii) itawazuia kufanya madhambi, ni fidia kwa makosa yenu, na itaondoa tabu katika miili yenu". (Tirmidhi, Daawat, 101/3549). Kwa kuwaambia haya, aliwashawishi wawe macho katika kipindi kabla ya alfajiri.

Nabii Suleiman عليه السلام, ambaye ni mtoto wa nabii Daudi aliambiwa na mama yake:

"Mwanangu mpendwa! Usilale sana usiku. Kwani kulala sana usiku kutamfanya mtu awe dhaifu siku ya kiama". (Ibn-i Majah, Ikamat'us Salah, 174).

Ibn-i Omar ﷺ anasimulia tukio lifuatalo ambalo linathibitisha kuwa swala ya *tahajjud* itamuweka mtu mbali na adhabu ya moto wa jahannam:

"Katika kipindi cha maisha ya Mtume mtu yeyote aliyekuwa akiota ndoto alikuwa akimsimulia. Nikatamani sana kuota ndoto ili nimsimulie Mtume.

❁

Wakati ule nilikuwa kijana ambaye sijaoa na nilikuwa nikilala msikitini.

Wakati fulani katika moja ya ndoto zangu, malaika wawili walinichukua na kunipeleka motoni. Nikaona mihimili miwili iliyojengwa kama kuta za kisima. Nikastaajabu kuwaona watu ninaowajua wakiwa ndani ya moto. Nikaanza kuomba kwa sauti:

"Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na moto wa jahannam. Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na moto wa jahannam". Wakati ule malaika mwingine akaja na kuniambia:

"Usiogope, hakuna kitakachokupata"

Nikamsimulia ndoto hii dada yangu mkubwa aitwae Hafsa ﷺ na yeye akamsimulia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Kisha Mtume akasema: *"Uzuri ulioje na wema alionao Abdullah! Lau kama angeliswali usiku pia..."*

Tokea siku ile, Abdullah ﷺ akatumia sehemu kubwa ya usiku kwa ajili ya ibada na kulala kidogo sana. (Bukhari, Ashabu'n Nabi, 19).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika hadith tukufu amewasifu wale waumini ambao wanatoa kwa siri na ambao wanaamka usiku kwa ajili ya swala ya *tahajjud* na wanajitahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

"Kuna watu wa aina tatu ambao Mwenyezi Mungu anawapenda. Na kuna watu wa aina tatu ambao Mwenyezi Mungu anawachukia. Inapokuja kwenye watu ambao Mwenyezi Mungu anawapenda:

Mtu analiendea kundi la watu na kuwaomba kitu, si kwa kuwa anajuana nao bali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hawampi anachotaka. Mtu mmoja miongoni mwa mkusanyiko huu anajisogeza nyuma bila ya mtu yeyote kujua na kwa siri anampa huyu mtu anachotaka. (Anafanya hivi kwa siri) kiasi kwamba Mwenyezi Mungu na yule mtu aliyesaidiwa ndiyo wanaojua.

❁

(Inapokuja kwenye mtu wa pili): Kundi la wasafiri limekuwa likitembea usiku kucha. Kisha wanachoka sana kiasi kwamba kulala kunakuwa muhimu kwao zaidi ya kitu kingine chochote. Wanasimama mahali kwa ajili ya kulala. (Wote wanalala). Mtu mmoja tu kati yao anaamka na kuniomba kwa unyenyekevu na kusoma aya zangu.

(Wa tatu ni kama ifuatavyo): Mtu amejiunga na msafara wa kijeshi. Wanakutana na maadui lakini wanakutana na upinzani mkubwa. Mtu huyu tu ndiye anayesogea mbele na kuendeleza mapambano mpaka anauawa au anaibuka mshindi.

Watu watatu ambao Mwenyezi Mungu anawachukia ni mzee ambaye anafanya uzinzi, masikini mwenye kiburi na tajiri ambaye ni dhalimu". (Tirmidhi, Jannah, 25/2568; Nasai, Zakat, 75).

Kutokana na masimulizi ya Ali ﷺ, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Kuna aina fulani za majumba ndani ya pepo. Ukiwa ndani unaweza kuona nje na ukiwa nje unaweza kuona ndani". Aliposikia haya Bedui akasimama na kuuliza:

"Haya majumba ni kwa ajili ya nani ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Mtume akajibu:

"Ni kwa ajili ya wale wanaoongea maneno mazuri na matamu, ambao wanaongea kwa ulaini, ambao wanapenda kuwalisha wengine, ambao wanaendelea kufunga na ambao wanaswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wakati watu wote wamelala". (Tirmidhi, Birr, 53/1984).

❁

Mwalimu wetu mwenye kuheshimika aitwae Musa (q.a) ametujulisha mwenendo wa kiongozi mkubwa aitwae Mahmud Sami Ramazanoglu. Anaongelea mwenendo wake mzuri katika kumfahamu Mwenyezi Mungu, kumtumikia Yeye na namna alivyokuwa akihuisha nyakati zake za usiku kama ifuatavyo:

"Ingawa uso uliobarikiwa wa Mahmud Sami Ramazanoglu ulikuwa ukitabasamu wakati wote, moyo wake kwa ndani ulikuwa ukilia. Alikuwa akitoa machozi kwa ajili ya jamii ya Waislamu na kuwaombea wawe huru kutoka kwenye mikono ya madhalimu. Alikuwa akilia kwa kuomba wenye madhambi waongolewe na kusamehewa na

machozi yake yalikuwa yakimiminika ndani kwa ndani. Wakati Qur'an ikisomwa alikuwa akisikiliza kwa heshima na wakati mwingine machozi yalimiminika mashavuni mwake. Katika kipindi cha hijja wakati anapita kati ya Madina na Makka, machozi yake yalionekana yakichuruzika kutoka machoni mwake

mithili ya lulu wakati wenzake wamelala chini ya mbalamwezi. Tukio hili lilikuwa ni lenye uzuri kiasi kwamba washairi na waandishi wanapata ugumu kulielezea"

Hamasa ya ibada za usiku kwa hayati Musa Topbas inaweza kulinganishwa na kitambo kisichoelezeka na shauku aliyokuwa nayo mpenzi anayetarajia kukutana na kipenzi chake. Hali hii iliendelea mpaka katika zile siku alizokuwa mgonjwa na mwili wake ukiwa unataabika, lakini aliendelea kubakia katika kilele cha mapenzi. Baada ya kufanyiwa upasuaji wa jicho na kuamka baada ya nguvu ya nusukaputi kuisha swali la kwanza kuwauliza wale waliomzunguka lilikuwa ni:

"Saa hizi ni saa ngapi?"

Alipoambiwa "Bwana! Saa hizi ni takriban saa 9", akasema:

"Ibada za usiku ni muhimu zaidi" na kwa msaada wa wale waliomzunguka akachukua udhu kwa udongo mkavu (*tayammum*) na kana kwamba amesahau maumivu aliyokuwa nayo, akaugeuza moyo wake kwa Mola wake na kuswali rakaa mbili za swala ya *tahajjud* (kwa kutikisa macho yake). Alifanya hivi kwa furaha na shauku kubwa, na kisha akaanza kumtaja na kumtukuza Mwenyezi Mungu kama kawaida yake. Hali yake hii ilikuwa ni kama ufafanuzi wa fumbo la Aya ifuatayo:

"Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumwomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyowaruzuku". (As Sajda, 32:16).

Siku moja Ibrahim bin Edham aliambiwa:

"Siwezi kuamka kwa ajili ya ibada za usiku, nifundishe tiba ya jambo hili"

Akapokea jibu lifuatalo:

"Usimuasi Mwenyezi Mungu wakati wa mchana na Yeye atakuruhusu uwe mbele yake wakati wa usiku. Kuwa mbele yake wakati wa usiku ni heshima kubwa. Wafanyaji madhambi hawastahiki heshima hii!"

Ibada za usiku ni njia muhimu sana katika kupata afya ya kiroho na kiwiliwili[53]. Ibada za usiku zinaepusha maradhi na kuimarisha roho na kiwiliwili, zinaleta busara na utukufu. Namna gani tukio lifuatalo linatahadharisha:

Wakati wa vita vya Yarmak wakati majeshi mawili yamekaribiana, Kiongozi wa kigiriki alituma mpelelezi ili kujua hali ya askari wa kiislamu. Baada ya yule mpelelezi kumaliza upelelezi wake akaulizwa:

"Waislamu wakoje? Wanafanya nini? Yule mpelelezi akawaambia alichokiona kama ifuatavyo:

بِاللَّيْلِ رُهْبَانٌ وَبِالنَّهَارِ فُرْسَانٌ

"Wao ni taifa ambalo linafanya ibada nyakati za usiku na ziko tayari kupigana mchana wake"

Kutokana na haya kiongozi wao akatoa jibu lifuatalo:

"Kama unayoyasema ni kweli, basi kuwa chini ya ardhi (yani kufa) ingelikuwa ni bora zaidi kuliko kupigana nao juu ya ardhi"

Tukio lifuatalo linaendana na lililopita:

Hakuna adui aliyeweza kuwashinda maswahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika vita. Kiongozi wa jeshi la Kigiriki lililoshindwa ambaye ni shujaa wao, aliliambia jeshi lake yafuatayo kwa hasira:

53.Angalia Tirmidhi, Deavat, 101/3549

"Hamuoni aibu! Je watu mnaopigana nao si binadamu kama nyinyi?"

"Kwa hakika wao ni binadamu kama sisi", walijibu:

"Vizuri, je nyie mko wengi, au wao?" akauliza.

"Bwana, Sisi tunawazidi kwa kila kitu" walijibu.

"Sasa mna tatizo gani kila mnapokutana nao mnashindwa vibaya mno?" Kutokana na haya mzee mmoja mwenye busara miongoni mwa wazee wa Kigiriki akasimama na kutoa uchambuzi ufuatao:

"Wanapitisha nyakati zao za usiku kwa ibada, wanafunga nyakati za mchana, wanatekeleza ahadi zao, wanaamrisha mema na kukataza mabaya na wanashirikiana katika kila kitu... (hii ndiyo sababu hatuwezi kuwashinda)"

Kutokana na haya huyu shujaa akasema:

"Umesema ukweli" [54]

Kwa kuhitimisha ni kwamba usiku ni wakati wa kipekee wa kutuliza moyo na akili, kunoa utambuzi, hisia, muonekano na kuimarisha kumbukumbu. Ni njia nyepesi na ya haraka katika kustawisha imani na kiwiliwili. Wakati wa usiku ni fursa ambayo haitakiwi kupotezwa na wale wanaokabiliwa na majukumu makubwa wakati wa mchana. Ni wakati wa kuendeleza mwenendo wa watu wema na watu wenye utambuzi, ambao wanafanya harakati za kuijenga jamii. Fadhila za usiku uliojaa amani wanapewa waumini wa kweli tu, hawa ni wale ambao wanaweza kuhuisha nyakati zao za usiku kwa kuzidisha ibada. Nyoyo za wale wenye desturi hizi zinaweza kufikia upana wa mbingu na ardhi na hujaa utukufu wa Mwenyezi Mungu na hutafuta kumjua Mwenyezi Mungu.

54.Ibn-i Asakir, Tarihu Dimask, ts., II, 97

Ewe Mola wetu! Tunusuru na kupoteza nyakati zetu za usiku kwa ujinga na hasara ya maisha haya mafupi yenye kupendeza. Tujaalie baadhi ya fadhila za usiku! Zinyeshelezee nyoyo zetu mafanikio yanayopatikana katika nyakati za usiku. Tujaalie tufikie asubuhi ya kesho Akhera kutoka kwenye dunia hii ambayo ni kama usiku mfupi, katika hali ya mapenzi ya kweli na fadhila kutoka kwako na jaalia nyoyo zetu zionje furaha ya kukutana na Wewe... Amin!

d. Swala na Dua

Wakati mja anakutana na ukuu na utukufu wa Mwenyezi Mungu uso kwa uso, ni lazima akubali madhaifu yake. Kisha atafute msaada na neema Zake kwa unyenyekevu na utii. Hii ndio maana ya swala na dua.

Kuomba dua kwa kupitia swala ni jambo muhimu sana katika dini kwani linaonyesha uhitaji wa mtu na ni dalili ya mtu kutafuta msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee.

❁

Mja hana budi kuomba dua kwa Mwenyezi Mungu mtukufu, si kwa maneno tu, bali kwa moyo safi. Swala ni lazima zitekelezwe wakati roho ipo kati ya 'khawf na raja', yani 'hofu na matumaini'. Swala ni lazima itoke moyoni; moyo ni lazima usisimke kutokana na maana ya maneno ya swala. Kama mtu anaomba msamaha kwa ajili ya dhambi fulani, hana budi kukiri na kujuta juu ya dhambi hiyo. Jalaluddin al Rumi anasema:

" Ombeni dua na msamaha wakati macho yenu yamegubikwa na machozi na moyo unawaka kwa majuto. Kwani maua huchanua pale penye joto na unyevunyevu".

Kwa namna yoyote ile muumini hana budi kuwa katika hali ya unyenyekevu kwa Mola wake ikiwa ni sharti mojawapo la kuwa mtumwa wake. Lengo la mafunzo ya dini ni kuifanya roho ya muumini iwe katika hali ya kuendelea kuomba dua. Kwani dua ndiyo ufunguo wa mlango wa moyo ambao unamuongoza mja kwa Mwenyezi Mungu. Qur'an inaeleza:

"Na waja wangu watakapo kuuliza habari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba". (Baqara, 2:186).

❁

Kadri dua zinavyorudiwa mara kwa mara ndivyo zinavyozama ndani ya moyo wa muumini kwa hisia nzuri zenye kupelekea kuwa ndiyo mwenendo wake. Hii ndiyo sababu inayowafanya watu wema waendelee kuishi katika hali ya kuomba dua.

❁

Kuomba dua ni kuelekea kwa Mwenyezi Mungu mtukufu, ambaye ndiye mmiliki wa nguvu kuu, ukiwa na utambuzi wa kweli juu ya uhitaji wetu na kuinamisha vichwa vyetu mbele yake kwa unyenyekevu na utulivu. Kuanza dua zetu kwa kukiri uhitaji wetu na makosa yetu kunakaribisha huruma ya Mwenyezi Mungu na hivyo kuna mchango mkubwa katika kupokelewa dua zetu.

Mtume ﷺ ametufundisha namna bora ya kuomba dua. Licha ya swala zake ambazo aliziswali huku akibubujikwa na machozi na mpaka vifundo vyake vya miguu vikavimba, pia alikuwa akijikinga kwa Mwenyezi Mungu wakati wote kwa hisia za uhitaji. Alipendelea dua nzuri na fupi na hakuomba ila dua za namna hii[55]. Alikuwa akitushauri yafuatayo:

55.Abu Dawud, Vitir, 23/1482

"Sehemu ambayo mja yupo karibu zaidi na Mola wake ni katika sijda. Kwa sababu hii ombeni dua zaidi mnapokuwa katika sijda". (Muslim, Salat, 215).

Mbali na kushikamana na dua, muumini hana budi kufanya juhudi kupata dua za ndugu zake katika imani, masikini, madhaifu na wahitaji. Kwani Mtume ﷺ anasema:

"Hakuna dua inayokubalika kwa haraka zaidi ya dua ya muislamu anayomuombea muislamu mwenzake wakati hayupo" (Tirmidhi, Birr, 50/1980).

❁

Jalaluddin Al Rumi anasema yafuatayo:

"Tafuta kujitolea nafsi yako, utajiri wako na mali zako kwa ajili ya kuwaridhisha watu. Hii itapelekea dua zao kuwa taa na kukumulikia wakati upo kwenye kiza cha kaburi..."

Matukio ya wema

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

"Muislamu akiomba jambo kwa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atamkidhia haja yake au atamuondolea jambo baya kulingana na ombi lake, hali yakuwa haombi jambo la haramu na hakati udugu"

Mmoja wa maswahaba zake alisema:

"Kama ni hivyo tunahitaji mambo mengi kutoka kwa Mwenyezi Mungu". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akajibu kama ifuatavyo:

"Neema za Mwenyezi Mungu ni nyingi kuliko vitu mnavyomuomba". (Tirmidhi, Deavat, 115/3573; Ahmad, II, 18).

Mwenyezi Mungu mtukufu hakatai dua zilizoombwa kwa moyo safi. Hata hivyo Hakubali maombi ambayo yanaenda kinyume na qadari, hata kama yamefanywa kwa moyo safi. Hata hivyo mja asikate tamaa kamwe bali aendelee kuomba. Kwani maombi kama hayo yameahirishwa mpaka siku ya kiama. Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Mola wenu anasema, 'Niiteni nitakuitikieni'." (Mu'min, 23:60).

❁

Mtume Muhammad ﷺ anasema:

"Dua ya mja itajibiwa hali ya kuwa haijaombwa kwa jambo lenye kupelekea kupata dhambi au kuathiri udugu na kama ana subira katika kusubiri majibu"

Aliulizwa:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Inamaanisha nini kwa mtu kukosa subira (juu ya majibu)?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

"Mja anasema: "Naendelea kuomba lakini Mola wangu hajibu dua zangu". Anakata tamaa haraka ikiwa dua zake hazijibiwi upesi na anaacha kuomba. (Hivi ndivyo anavyokosa subira)". (Muslim, Zikir, 92).

Vivo hivyo nabii Zakaria عليه السلام aliomba "Mola wangu mlezi, Usiniache peke yangu..." . (Anbiya, 21:89).

❁

Baada ya kusema hayo akaomba mtoto wa kiume kwa lengo la kuimarisha dini, lakini dua yake ikajibiwa miaka 40 baadae kwa kupewa nabii Yahya عليه السلام.

Wakati fulani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimuona mtu akiwa kwenye swala ya faradhi, lakini hakumswalia Mtume kabla ya kuomba dua. Kutokana na haya akasema:

"Mtu huyu hakuwa na subira (kutokana na haraka)". Kisha akamuita yule mtu na kumuambia yafuatayo kama tahadhari kwa umma wote:

"Yeyote kati yenu atakayeomba dua na amtukuze Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi kwanza, kisha aniswalie mimi. Kisha aombe chochote anachotaka". (Tirmidhi, Deavat, 64/3477).

Mtume Muhammad ﷺ ameshauri kwamba muumini amuombee dua ndugu yake katika imani, ama akiwa naye au asipokuwa naye. Omar رضي الله عنه alipomuomba ruhusa ya kutekeleza umra alisema:

"Ndugu yangu, tujumuishe katika dua zako, usitusahau". (Tirmidhi, Deavat, 109/3562).

Omar رضي الله عنه anaelezea namna alivyojisikia aliposikia maneno yale:

"Kama ningepewa dunia nzima nisingelikuwa na furaha kama ile niliyokuwa nayo niliposikia maneno haya". (Abu Dawud, Vitir, 23/1498).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

" Dua ya muislamu juu ya ndugu yake katika imani wakati hayupo itakubaliwa. Pale mtu atakapomuombea wema ndugu yake, malaika aliye katika zamu pembeni yake anamuombea: "Mwenyezi Mungu akubali dua yako na akupe sawa na ulichokiomba". (Muslim, Zikr 87, 88; Ibn-i Majah, Manasik, 5).

Hivyo tuwaombee ndugu zetu waislamu na tuwaombe watuombee na sisi.

Kikubwa tunachohitaji katika dunia hii yenye kulaghai kuliko kitu kingine chochote ni *taqwa* (uchamungu), hivyo hili ndilo jambo tunalostahiki kuliomba katika dua zetu. Siku moja mtu mmoja alimjia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nitaka kusafiri, tafadhali niombee"

Mtume akajibu:

"Mwenyezi Mungu akujaalie uchamungu". Yule mtu akasema:

"Niombee tena kidogo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema:

"Mwenyezi Mungu akusamehe madhambi yako". Yule mtu akasema:

"Kidogo tena, baba yangu na mama yangu watolewe kafara kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu"

Mtume ﷺ akasema:

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akujaalie wepesi katika kufanya wema popote pale utakapokuwa" (Tirmidhi, Deavat, 44/3444).

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisoma maneno yafuatayo kutoka kwa nabii Ibrahim عليه السلام na dua ya nabii Isa عليه السلام:

Baada ya hapo akanyanyua mikono yake huku anatokwa na machozi na kutuombea:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Ulinde umma wangu, urehemu umma wangu". Kutokana na haya Mwenyezi Mungu mtukufu akasema:

"Ewe Jibril! Ingawa ninajua zaidi (lakini kwa ajili ya watu kuelewa), nenda kwa Muhammad na umuulize kwa nini analia".

Jibril akamuendea, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamjibu kuwa alikuwa analia kwa kuhofia umma wake. Jibril aliporudi kutoa hizi habari Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akasema:

❁

"Ewe Jibril! Nenda kwa Muhammad na umpe habari njema kwamba: "Tutakufanya uridhike juu ya umma wako na Kamwe Hatutokusababishia huzuni" (Muslim, Iman, 346).

Hivyo ndivyo Mtume alivyokuwa akiujali na kuuhurumia umma wake. Na sisi hatuna budi kuitafakari kiundani hii hadith na kujiuliza ni kwa kiwango gani tunampenda na kama tunampenda hatuna budi kujiuliza na kwa kiwango gani tumeziingiza sunnah katika maisha yetu na ni kwa kiwango gani tumeiga mwenendo wake.

Ibn-i Abbas رضي الله عنه anasimulia:

"Siku moja nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiomba dua ifuatayo baada ya swala ya usiku:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Ninakuomba unijaalie rehema ambayo kwayo utauongoza moyo wangu, utatengeneza mambo yangu, na kunirekebishia mapungufu yangu. Na unijaalie imani thabiti, na unijaalie kutenda matendo mema na kusafisha matendo yangu, na uniongoze katika njia unayoiridhia, na utajaalie kupata marafiki ambao tutaendana nao na ambao watatulinda kutokana na mambo maovu.

Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie imani na hukumu ambayo haitawanufaisha makafiri. Nijaalie rehema ambayo kwayo nitanufaika hapa duniani na kesho Akhera, na ambayo unairidhia.

Ewe Mwenyezi Mungu! Ninakuomba uongofu katika hukumu yako kutokana na rehema zako. Ninakuomba unipandishe daraja

kama la mashahidi (walio karibu yako), Ninakuomba unijaalie maisha ya furaha na utulinde kutokana na maadui zetu.

Ewe Mwenyezi Mungu! Licha ya uelewa wangu kuwa finyu na amali zangu kuwa chache, ninakuletea mlangoni kwako (mahitaji ya hapa duniani na kesho akhera) unikidhie. Ninahitaji rehema zako, na ninakuletea haja yangu.

Ewe Mola wangu Mlezi ambaye unahukumu mambo yote na kuyamaliza na ambaye unayaona mahitaji ya nyoyo na kuzitibu. Ninakuomba uniweke mbali na moto kama ulivyotenganisha bahari. Ninakuomba unilinde kutokana na maangamizi na adhabu za kaburini.

❁

Ewe Mwenyezi Mungu! Kama kuna wema katika yeyote miongoni mwa waja wako au neema ambayo umeviahidi viumbe vyako na mimi nimeshindwa kuzitambua au sikuziweka katika akili yangu na hivyo kuwa nje ya maombi yangu, Ewe Mola wa walimwengu wote, ninakuomba unisogezee na kunipatia kutokana na rehema zako.

Ewe Mwenyezi Mungu! Ewe mmiliki wa kamba imara na njia ya haki (kama Qur'an na dini). Katika siku ya kiama ambayo umewaahidi makafiri moto, ninakuomba unilinde kutokana nao, na katika siku ambayo maisha ya milele ndiyo yanaanza ninakuomba pepo pamoja na malaika walio mbele yako, pamoja na wale waliorukuu na kusujudu kwa wingi hapa duniani, na ambao wametekeleza ahadi zao. Wewe ni mmiliki wa rehema zisizo na mwisho, Wewe ni mmiliki wa upendo usio na mwisho, Unafanya ulitakalo (licha ya waombaji wengi kukuomba na licha ya uwezo wako mkubwa wa kuwajibu maombi yao). Ewe Mwenyezi Mungu! Tufanye tuwe wale ambao hatujapotea wala hatujawapoteza wengine na tufanye kuwa viongozi wa uongofu kwa wale waliopata

uongofu. Tufanye kuwa wahamasishaji wa amani miongoni mwa marafiki zetu na maadui kwa maadui zetu. Tunawapenda wale wanaokupenda kutokana na mapenzi yao kwako. Tuna uadui na wale wanoaenda kinyume na wewe kutokana uadui wao kwako.

❁

Ewe Mwenyezi Mungu! Haya ni maombi yetu. Ni juu yako kuyakubali kutokana na rehema zako. Hii ndiyo jitihada yetu na Wewe ndiyo wa kutusaidia.

Ewe Mwenyezi Mungu! Jaza nuru kwenye moyo wangu na kaburi langu; niwekee nuru mbele yangu na nyuma yangu; niwekee nuru kushotoni mwangu na kuliani mwangu; niwekee nuru juu yangu na chini yangu; niwekee nuru kwenye masikio yangu na macho yangu, na pia kwenye nywele zangu na ngozi yangu, na pia kwenye nyama yangu na damu yangu na mifupa yangu.

Ewe Mwenyezi Mungu! Nizidishie nuru, nijaalie nuru juu ya mambo yote niliyoyataja na ambayo sikuweza kuyataja.

Utukufu ni wake yule aliyetukuka na ambaye amewataka watu wamjue kutokana na utukufu wake. Utukufu ni wake Yule aliye mkuu na ambaye kwa sababu hii anaendelea kuwapa waja wake neema nyingi. Utukufu ni wake yule ambaye ni yeye tu wa kutukuzwa na kufadhilishwa. Utukufu ni wake yule mwenye kumiliki utukufu na rehema. Utukufu ni wake yule mwenye kumiliki utukufu na wema. Yeye ametakasika na kila udhaifu". (Tirmidhi, Deavat, 30/3419).

Wakati fulani watu walimlalamikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ juu ya ukosefu wa mvua. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akaagiza aletewe mimbari. Mimbari iliwekwa sehemu ambayo watu hukusanyika kwa ajili ya swala za eid na swala za maiti (*Musalla*). Ikapangwa siku ya watu kukutana. Mtume ﷺ akaelekea kule pale wekundu wa jua ulipoanza kujitokeza. Aka-

wasili (kwenye *musalla*) na kupanda kwenye mimbari. Akatoa *takbir* kwa kusema "*Allah Akbar*", akamsifu Mwenyezi Mungu na kisha akasema:

"Mmelalamika kuwa mji wenu upo kwenye ukame na mvua haijanyesha katika nyakati zake za kawaida na hivyo imechelewa. Mwenyezi Mungu (mtukufu) amewaamuru mumuombe. Ameahidi kujibu maombi yenu" na kisha Mtume akaendelea kwa kuomba dua ifuatayo:

"Sifa zote njema anastahiki Mola wa walimwengu wote. Yeye ni mwingi wa rehema, na Mwenye kurehemu. Yeye ndiyo Mmiliki wa siku ya kiama. Hakuna mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu. Anafanya atakalo. Ewe Mola wetu Mlezi! Wewe ni Mwenyezi Mungu, na hakuna mungu mwingine isipokuwa Wewe. Wewe ni tajiri. Sisi ni masikini. Tuteremshie mvua. Jaalia kitakachoteremka kituongezee nguvu na uimara. Jaalia iendelee kwa kitambo kirefu".

Baada ya kuomba dua hii akanyanyua mikono yake. Alinyanyua mikono yake kiasi kwamba weupe wa kwapa zake ukaonekana. Kisha akawageukia watu wakati mikono yake bado ipo juu. Kisha akaondoka kwenye mimbari na kuswali rakaa mbili. Mara Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akawatumia mawingu. Kukatokea Ngurumo na radi. Mvua ikaanza kunyesha kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu. Mvua ikawa inazidi kumwagika kabla ya Mtume kurudi msikitini. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipowaona watu wanaharakisha kutafuta pa kujificha akatabasamu na kusema:

"Nashuhudia kwamba Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kila jambo na kuwa mimi ni mja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu" (Abu Dawud, Istiska, 2/1173).

Baada ya Mtume kuomba mvua kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi, aliswali swala maalum ya 'kuomba mvua', hivyo aligeukia swala ya sunnah ili akubaliwe dua yake.

❁

Mke wa Mtume, Aisha ﵂ anasema:

"Usiku mmoja niliamka na kukuta Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hayupo pembeni yangu (kitandani). Nilidhani ameenda kwa wake zake wengine. Mikono yangu ilipogusa miguu yake nikaanza kupapasa. Nikagundua kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesujudu. Nikasikiliza na kumsikia akilia huku anaomba yafuatayo:

اَللَّهُمَّ أَعُوذُ بِرِضَاكَ مِنْ سَخَطِكَ وَبِمُعَافَاتِكَ مِنْ عُقُوبَتِكَ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْكَ
لاَ أُحْصِى ثَنَاءً عَلَيْكَ أَنْتَ كَمَا اَثْنَيْتَ عَلَى نَفْسِكَ

"Ewe Mwenyezi Mungu! Najikinga kwako kutokana na hasira zako. Najikinga na adhabu zako kutokana na msamaha wako. Ewe Mwenyezi Mungu najikinga kwako pekee na si kwa yeyote mwingine. Siwezi kukusifu kisawa sawa. Wewe ni kama ulivyojisifu mwenyewe" (Muslim, Salat, 222; Tirmidhi, Deavat, 75/3493).

❁

Omar ﵁ anasimulia:

"Katika siku ya Badr, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaangalia washirikina na kuona kuwa wamefikia idadi ya watu elfu moja. Maswahaba zake walikuwa 313[56]. Upesi akageukia Ka'aba na kunyanyua mikono yake kwa ajili ya dua. Akaanza kumuomba Mola wake kwa sauti kama ifuatavyo:

56. Angalia Bukhari, Megazi, 6; Tirmidhi, Siyer, 38/1598

"Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie kile ulichoniahidi. Ewe Mwenyezi Mungu, Nijaalie ushindi. Ewe Mwenyezi Mungu, kama utaangamiza kundi hili la waislamu hakuna yeyote atakayebakia katika mgongo wa ardhi kukuabudu"

Akaendelea kuomba huku amenyanyua mikono yake mpaka joho lake likavuka mabega yake. Abu Bakar ﷺ alipoona hili akamuendea na kulipandisha mabegani mwake na kisha akamuambia:

❁

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Dua yako kwa Mwenyezi Mungu inatosha. Kwa hakika Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atatekeleza ahadi yake kwako"

Mpaka pale Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi, Mwenye kuheshimiwa na kutukuzwa alishusha Aya ifuatayo:

"Mlipokuwa mkimuomba msaada Mola wenu Mlezi, naye akakujibuni kuwa: Kwa yakini Mimi nitakusaidieni kwa Malaika elfu wanaofuatana mfululizo". (Anfal, 8:9).

Pia katika siku ile Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi alituma malaika kwenda kuwasaidia waumini. (Muslim, 58; Bukhari, Megazi, 4).

Kulikuwa na swahaba aitwae Abu Mi'lak ambaye alijihusisha na biashara kwa kushirikiana na wengine. Alikuwa ni mtu mwema na mwenye upole. Siku moja aliondoka kwa ajili ya safari wakati njiani kumezuiwa na jambazi mwenye silaha. Jambazi huyu akasema:

"Toa kila ulichonacho, nitakuua"

"Kama lengo lako in kuchukua mali zangu basi zichukue" Abu Mi'lak alisema.

"Nataka uhai wako tu" jambazi akasema. Abu Mi'lak akasema:

"Kama ni hivyo, naomba ruhusa niswali". Yule jambazi akamuambia:

"Swali kadri upendavyo". Baada ya kumaliza swala akaomba dua ifuatayo:

يَا وَدُودُ يَا ذَاالْعَرْشِ الْمَجِيدِ يَافَعَّالاً لِمَا يُرِيدُ أَسْاَلُكَ بِعِزَّتِكَ الَّتِى
لاَ تُرَامُ وَمُلْكِكَ الَّذِى لاَ يُضَامُ وَبِنُورِكَ الَّذِى مَلأَ اَرْكَانَ عَرْشِكَ
اَنْ تَكْفِيَنِى شَرَّ هَذَا (اللِّصِّ) يَا مُغِيثُ اَغِثْنِى

"Ewe kipenzi cha nyoyo! Ewe mmiliki wa kiti kitukufu cha enzi. Ewe Mwenyezi Mungu ambaye unafanya chochote utakacho. Kwa heshima ya utukufu na ufalme usio na mipaka na nuru inayomulika kiti chako cha enzi, nakuomba unilinde kutokana na ubaya wa jambazi huyu. Ewe Mwenyezi Mungu ambaye unatoa msaada kwa watu, naomba unisaidie"

Abu Mi'lak alirudia dua hii mara tatu. Muda mfupi baada ya kumaliza dua yake alitokea muendesha farasi akiwa ameshika mkuki usawa wa masikio na kumuua yule jambazi. Yule swahaba aliyeokolewa kutokana na rehema za Mwenyezi Mungu, akamuambia yule muendesha farasi:

"Wewe ni nani? Mwenyezi Mungu amekufanya unisaidie"

Muendesha farasi akajibu:

❁

"Mimi ni mkazi wa mbinguni kutoka mbingu ya nne. Ulipoomba dua mara ya kwanza nilisikia milango ya mbingu inapasuka. Katika dua yako ya pili nilisikia makelele ya wakazi wa mbinguni. Ulipoomba kwa mara ya tatu kulisikika: "Kuna mtu yuko kwenye matatizo anaomba msaada". Niliposikia haya nilimuomba Mwenyezi Mungu anichague nije kumuua huyu jambazi. Mwenyezi

Mungu aliye juu zaidi akakubali ombi langu ndiyo nikaja. Jua kwamba, yeyote atakayechukua udhu na kuswali rakaa nne na kuomba dua atakubaliwa dua yake ama akiwa kwenye tatizo au la". (Ibn-i Hajar, al isaba, IV, 182).

Siku moja mke wa Mtume aitwae Ummu Salamah ﵂ aliulizwa:

"Ewe mama wa waumini! Ni dua ipi ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliisoma kwa wingi akiwa na wewe" Akajibu:

"Muda mwingi alikuwa akiomba:

يَا مُقَلِّبَ الْقُلُوبِ ثَبِّتْ قَلْبِى عَلَى دِينِكَ

"Ewe Mwenyezi Mungu mwenye kugeuza nyoyo za watu! Jaalia moyo wangu uwe na msimamo katika dini" (Tirmidhi, Deavat, 89/3522; Ahmad, IV, 182, VI, 91).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliomba dua nyingi kwa ajili ya ulinzi wa umma wake. Aliomba dua ifuatayo kwa ajili ya ulinzi wa watu wa Yemen "Ewe Mwenyezi Mungu! Zigeuzie nyoyo zao kwetu" (Tirmidhi, Menakib, 71/3934). Watu wa Taif wakamfukuza nje ya mji kwa mawe na matusi ya kila namna na wakaendelea kuwadhuru Waislamu kutokana na upinzani wao mkubwa mpaka ulipofikia mwaka wa tisa wa *hijrah*. Bado aliwaombea watu hawa kwa Mwenyezi Mungu na kuomba ulinzi kutoka kwake: "Ewe Mola wangu mlezi! Walinde watu wa Thaqif. Walete kwetu".

Mtume ﷺ alipomtuma Ali kwenda Yemen kuwa hakimu wao aliweka mkono wake kwenye kifua cha mpwa wake, akihofia majukumu na mzigo aliompa, kisha akamuombea kama ifuatavyo:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Uongoze moyo wake kuelekea kwenye ukweli, na ujaalie ulimi wake usimamie haki"

Baadaye Ali ﵁ akasema:

"Baada ya dua hii kamwe sikusita nilipotakiwa kuhukumu baina ya watu wawili" (Ibn-i Maja, Ahkam, I).

❁

Wakati Mtume ﷺ amesimama kwa ajili ya Hijja, alishika kamba ya ngamia wake kwa mkono mmoja na akanyanyua juu mkono wake mwingine na kuomba dua ndefu iliyoonyesha utumishi wake na ulaini wa moyo wake. Sehemu ya dua yake nzuri ni hii ifuatayo:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Sifa zote njema ni zako kama ulivyojisifu mwenyewe na zaidi ya tunavyoweza kukusifu. Ewe Mwenyezi Mungu! Swala zangu, ibada zangu, uhai wangu na kifo changu, vyote ni kwa ajili yako. Marejeo yangu ni kwako pekee.

Ewe Mwenyezi Mungu! Najikinga kwako kutokana na adhabu za kaburini, kutokana na miito ya shetani inayoufunika moyo, na kutokana na kuharibika mambo yangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Najikinga kwako kutokana na madhara ya majanga yanayosababishwa na upepo mkali.

Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie nuru katika macho yangu, masikio yangu na moyo wangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Kunjua kifua changu. Nirahisishie kazi yangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Najikinga kwako kutokana na afya ambayo inageuka kuwa maradhi, kutokana na adhabu yako ambayo inaweza kuja ghafla na kutokana na ghadhabu zako kwa ujumla. Ewe Mwenyezi Mungu! Niongoze katika njia iliyonyooka. Nisamehe (madhambi) yaliyopita na yajayo.

❁

Ewe Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi, ambaye unapandisha madaraja na ambaye unatoa neema. Ndimi mbalimbali zinanyanyuliwa juu yako kukuomba wewe. Matakwa yangu

kwako ni: katika uwanja huu wa mtihani, wakati watu wa hapa duniani wamenisahau nakuomba wewe unikumbuke.

Ewe Mwenyezi Mungu! Unasikia maneno yangu. Unaniona nilipo. Unajua kila kitu kuhusu mimi, vyote vya dhahiri na vya siri. Hakuna jambo langu lililofichikana kwako. Mimi ni mhitaji na dhaifu. Nakuomba unisaidie na kunirehemu. Nina hofu. Ninakiri makosa yangu. Kama mhitaji anavyokuomba, na mimi pia ninakuomba. Kama mwenye madhambi anavyokuomba, na mimi pia ninakuomba. Na kama mja wako anavyoinamisha kichwa chake mbele yako, machozi yakimtiririka, akijitolea kila kitu ili kutafuta radhi zako, anavyoweka paji lake la uso chini na kukuomba, na mimi pia nakuomba. Ewe Mola wangu Mlezi! Usininyime kwa kutonijibu maombi yangu. Nihurumie Ewe mbora wa wanaoombwa na mbora wa wale wanaotoa" [57]

Uzuri na uzito ulioje wa dua hii ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ambaye hakuwa na dhambi. Dua hii inaonyesha namna ambavyo moyo unatakiwa uwe mbele ya Mwenyezi Mungu mtukufu...

Sehemu ya dua iliyoombwa na watu wema waliotangulia (*salaf-i salihin*) katika siku ya Arafat ni kama ifuatavyo:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Nani anaweza kujisifu mbele yako? Ewe Mwenyezi Mungu! Ulimi wangu umekwama kwenye madhambi na sina amali njema wala mwingine wa kuniombea, zaidi ya kutumaini rehema zako ambazo zitanifikisha kwako. Ewe Mwenyezi Mungu! Najua kutokana na makosa yangu sina nafasi kwako na naona haya kukuomba msamaha. Hata hivyo Wewe ni Mkarimu wa wakarimu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hata kama sistahili kupata

57. Angalia Ibn-i kathir, al Bidaya, V, 166-8; Haysami, III, 252; Ibn-i Kayyum, Zadu"l Mead, Beirut 1995, II, 237

rehema zako, tafadhali jaalia rehema zako zinifikie hivyo hivyo. Kwani rehema zako ni pana sana kiasi cha kuwafikia wote. Ewe Mwenyezi Mungu! Hata makosa yangu yakiwa makubwa kiasi gani, ni madogo ukilinganisha na msamaha wako. Naomba unisamehe Ewe mmiliki wa ukarimu.

Mola wangu. Kama unawasamehe waja wako watiifu pekee, wakosefu watamkimbilia nani?

Mola wangu. Kama unaonyesha huruma na upendo kwa waja wako wema, wapotevu watamkimbilia nani awasaidie?

Ninakuhitaji Wewe kila wakati. Kwa upande mwingine Wewe hunihitaji mimi. Wewe Muumba wangu pekee ndiye unayeweza kunisamehe. Nijaalie nirudi kwako huku mahitaji yangu na matakwa yangu yakiwa yametimia.

Ewe Mwenyezi Mungu, ewe mmiliki wa mahitaji ya wale wanaoomba. Ewe Mwenyezi Mungu, ambaye unajua yaliyo vifuani mwa wale walio kimya. Ewe Mwenyezi Mungu, ambaye kinyume na Wewe hakuna Mlezi mwingine wa kukimbiliwa kwa ajili ya msaada. Ewe Mwenyezi Mungu, ambaye kinyume na Wewe hakuna Muumbaji mwingine wa kuhofiwa. Ewe Mwenyezi Mungu ambaye kinyume na Wewe hakuna muombezi wa kukimbilia kwake wala hakuna mlinda mlango ambaye anaweza kupewa rushwa. Ewe Mwenyezi Mungu, ambaye ukarimu na wema wako vinaongezeka kadri mahitaji yanavyoongezeka. Ewe Mwenyezi Mungu! Wewe ni mkarimu kwa wageni wako wote wanaokutembelea. Na sisi pia ni wageni wako. Tuingize katika pepo yako.

Ewe Mwenyezi Mungu! Kila kundi linapewa zawadi na waombaji wote wanapewa wanachoomba; wageni wote wameandaliwa zawadi zao. Na kila mtu anayezitumaini atapewa zawadi hizo. Tumekuja kama kundi moja kwenye nyumba yako tukufu. Tumes-

imama mbele ya hii madhabahu yako tukufu[58]. Tupo sehemu hizi takatifu. Lengo letu ni kupata malipo makubwa na mapenzi yako. Usipuuzie matumaini yetu ewe Mwenyezi Mungu![59]

Abu Umama ﷺ anasimulia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisoma dua nyingi lakini hatukuweza kukariri hata moja. Siku moja tukamwambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Umesoma dua nyingi lakini hatukuweza kuzikariri hata moja". Kisha Mtume akasema:

"Niwafundishe dua ambayo inajumuisha dua hizo zote? Semeni kama ifuatavyo:

اَللّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِ مَاسَأَلَكَ مِنْهُ نَبِيُّكَ مُحَمَّدٌ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
وَنَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَااسْتَعَاذَكَ مِنْهُ نَبِيُّكَ مُحَمَّدٌ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
وَأَنْتَ الْمُسْتَعَانُ وَعَلَيْكَ الْبَلَاغُ وَلاَ حَوْلَ وَلاَ قُوَّةَ إِلاَّ بِاللهِ

"Ewe Mwenyezi Mungu! Tunakuomba mambo yote mazuri ambayo Mtume wako Muhammad ﷺ amekuomba na tunakuomba ulinzi dhidi ya mabaya yote ambayo Mtume wako Muhammad ﷺ amekuomba ulinzi dhidi yake. Wewe ndiye Msaidizi pekee ambaye unaombwa msaada. Wewe ndiye utakayemuwezesha mtu kufikia malengo yake katika dunia hii na kesho akhera. Hakuna nguvu ya kujizuia na madhambi wala nguvu ya kufanya ibada ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee!"

Anas ﷺ anasimulia:

58. Katika kiarabu masha'ir, lenye maana ya madhabahu kwa ajili ya sherehe za hijja.
59. Angalia Ghazalli, Ihya Ulumi"d- Din, Beirut, 1990, I, 337-8; Beyhaki, ShuAbu'l Iman, II, 25-6

"Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimtembelea mgonjwa ambaye alikuwa amepoteza nguvu nyingi na kumuuliza:

"Je uliomba dua juu ya chochote kutoka kwa Mwenyezi Mungu?" Yule mgonjwa akajibu:

"Ndiyo. Nimekuwa nikimuomba "Ewe Mwenyezi Mungu! Nipe adhabu sasa ambayo ungelinipa kesho akhera!"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

"Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu! Huna nguvu ya kuihimili. Kwa nini usingeliomba kama ifuatavyo:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

" ... Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema, na Akhera mema, na utulinde na adhabu ya Moto!" (Baqara, 2:201).

Kisha yule mtu akasoma dua hii na kuponywa. (Muslim, Zikr, 23; Tirmidhi, Deavat, 71/3487).

Hivyo hatuna budi kuwa makini na tunachokiomba kwa Mwenyezi Mungu na hatuna budi kuzingatia sifa za dua. Daima tumuombe Mwenyezi Mungu mambo ya heri na afya njema.

❁

Kutokana na masimulizi kutoka kwa Ali رضي الله عنه mtumwa mmoja alimjia na kumwambia:

"Siwezi kukulipa deni langu, nisaidie". Akamwambia:

"Je nikufundishe dua ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alinifundisha? Ikiwa utaendelea kuisoma, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atakusaidia kulipa deni lako hata kama ni kubwa kama mlima wa Thabir" na kisha akasoma dua ifuatayo:

اَللّٰهُمَّ اكْفِنِي بِحَلاَلِكَ عَنْ حَرَامِكَ وَاغْنِنِي بِفَضْلِكَ عَمَّنْ سِوَاكَ

"Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie riziki ya halali na unilinde kutokana na haramu! Kwa rehema zako usinifanye nimtegemee mwingine kinyume na Wewe" (Tirmidhi, Deavat, 110/3563).

Sultani Murad alipoingia kwenye nyanda za Kosovo alifikiwa na dhoruba kubwa ambayo iliacha athari za vumbi. Hakuna kitu kilichoweza kuonekana. Usiku ule ulikuwa ni usiku wa Beraat (msamaha). Baada ya kuswali rakaa mbili, Murad Han aliomba dua ifuatayo huku machozi yakimtiririka mashavuni mwake:

"Ewe Mola wangu Mlezi! Kama dhoruba hii imekuja kwa sababu ya madhambi ya mja wako huyu dhaifu basi naomba usiwaadhibie askari wangu wasio na hatia. Ewe Mwenyezi Mungu! Wamekuja hapa kwa lengo pekee la kulitukuza jina lako na kuutangaza Uislamu.

Ewe Mola wangu Mlezi! Hukuninyima ushindi kwa miaka yote hii. Daima umekuwa ukijibu dua zangu. Kwa mara nyingine tena narejea kwako, naomba ukubali dua zangu. Tuteremshie mvua. Ijaalie iondoe dhoruba hii ya vumbi. Tujaalie tuzione vizuri nyuso za makafiri na utujaalie tupambane nao uso kwa uso"

Ewe Mola wangu Mlezi! Vyote utajiri na mja wako huyu ni vyako. Mimi ni mja dhaifu. Unajua vyema nia yangu na siri zangu. Nia yangu si utajiri wala mali. Nataraji kupata radhi zako tu.

Ewe Mola wangu Mlezi! Usiwaangamize hawa askari waumini na kuwafanya washindwe mikononi mwa makafiri. Wajaalie ushindi ambao utawafanya Waislamu wote washerehekee. Na kama ukitaka mfanye mja wako huyu awe kafara kwa ajili sherehe hiyo.

Ewe Mola wangu Mlezi! Usinifanye niwe sababu ya maangamizi ya askari wengi wa kiislamu. Wasaidie na uwape ushindi. Niko tayari kutoa uhai wangu kwa ajili yao kama itakuwa ndiyo

sababu ya kunikubalia kuingia kwenye kundi la mashahidi. Niko tayari kusalimisha roho yangu kwa ajili ya askari hawa wa kiislamu... Umenijaalia kuwa askari. Nijaalie kufa shahidi sasa kwa rehema zako na utukufu wako... Amin!"

Baada ya maombi haya ya dhati yule Sultani akaanza kusoma Qur'an kwa upole wa hali ya juu. Haikuchukua muda kabla mawingu ya rehema hayajajitokeza. Mvua kubwa ikashuka kwenye tambarare za Kosovo. Upepo ukaacha kuvuma. Vumbi likatoweka...

Adui akashambuliwa. Mapambano yaliyochukua masaa nane yakaisha kwa kupata ushindi.

Wakati Murad Han anatembea kati ya majeruhi na mashahidi wa vita, Askari mmoja wa Kiserbia aliyejeruhiwa alisimama na kusema:

"Niacheni niende. Naenda kwa sultani kumbusu mkono wake na kuwa muislamu". Yule askari wa Kiserbia ambaye alikuwa akijifanya amejeruhiwa alijifanya anataka kuubusu mkono wa sultani Murad. Mara akatoa upanga aliokuwa ameuficha chini ya mkono wake na kuungiza kwenye kifua cha sultani. Na pale dua ya sultani Murad ikawa imejibiwa katika njia nzuri zaidi na akawa amebarikiwa kwa kufa shahidi...

Kwa kukihitimisha, ni kwamba dua ina nafasi muhimu katika maisha ya kiibada na utumishi. Kwani moja ya mambo ambayo Mwenyezi Mungu anapendezwa nayo ni kwa mja kutambua uhitaji wake na kunyanyua mikono yake na kupeleka jambo lake kwa Mola wake kwa kumuomba na kujikinga kwake. Hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anamuadhibu yule anayekataa kujishusha na kuomba na hanyenyekei anapoomba jambo lolote.

Qur'an tukufu inasema:

"Sema: Mola wangu Mlezi asingekujalini lau kuwa si kuomba kwenu" (Furqan, 25:77).

Hivyo dua ni funguo ya milango ya rehema, ndiyo silaha ya muumini, ndiyo nguzo ya dini na nuru ya mbingu na ardhi. Yeyote aliyefunguliwa milango ya dua pia atakuwa amefunguliwa milango ya wema, hekima na rehema. Ambaye anataka dua zake zikubalike katika nyakati za shida na ugumu hana budi kuomba dua sana nyakati za utulivu na amani. Watu wema ni wale wanaoishi katika hali ya kuomba daima.

e. Unyenyekevu na utulivu (*khushu*)

Khushu inaashiria hali ya moyo kujaa mapenzi na hofu ya Mwenyezi Mungu na viungo vingine kupata amani na utulivu kutokana na hisia hizi.

Khushu, ambayo kiini chake ni moyoni lakini dhahiri yake inaonekana katika mwili, ina vipengere viwili:

Kipengere cha moyo pale unapotambua udhaifu wake mbele ya utukufu na ukuu wa Mola Mlezi. Hivyo *nafs* inanyenyekea kwenye maamrisho ya Mwenyezi Mungu na kufikia kwenye daraja la tabia njema, heshima na utii. Kipengere cha pili ni cha nje ya moyo, ambapo athari za hisia hizi zinasababisha upole na utulivu katika viungo vya mwili. Kwa mfano kutuliza macho na kuangalia pale unaposujudia wakati wa swala...

❁

Mfano bora wa namna ya kutekeleza khushu katika maisha ya mtu na ibada zake unaweza kuonekana katika maisha ya Mtume ﷺ na maswahaba zake waliobarikiwa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakutathmini hatua yoyote ya maisha yake bila kuilinganisha na maisha ya kesho Akhera. Aliweka umakini juu ya umuhimu wa

kujiweka katika hali ya kiimani wakati wa ibada kama ambavyo ungelikuwa wakati wa pumzi yako ya mwisho.

Siku moja swahaba alimjia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kusema:

❁

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nipe ushauri, ufanye uwe mfupi na mzuri". Juu ya hili Mtume ﷺ akasema:

"Tekeleza swala yako (omba) kama mtu anayeyaaga maisha yake. Usitoe neno lolote ambalo litakubidi uombe msamaha. Usione wivu juu vitu walivyonavyo watu wengine" (Ibn-i Majah, Zuhd, 15; Ahmad, V, 412).

Ibada itakuwa yenye thamani pale itakapotekelezwa katika hali ya umakini, utulivu (*khushu*) na mazingatio. Ubora wa maswahaba waliobarikiwa na wale waumini wema waliowafuata ulitokana na mwenendo huu nyoyoni mwao.

❁

Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alikuwa akiwaambia marafiki zake:

"Mnaswali na kuwajibika zaidi ya maswahaba. Lakini bado wao ni bora zaidi yenu"

Alipoulizwa:

"Ni kipi kilichowafanya wawe bora zaidi yetu?" akajibu:

"Wao waliipa mgongo dunia na kuzingatia maisha ya kesho akhera kuliko nyie". (Ibnu'l Jawzi, Sifatu's Safwe, Beirut 1979, I, 420).

❁

Utulivu wakati wa swala ni jambo muhimu mno kiasi kwamba uokovu wa mja unapatikana kwa kupitia mlango huu. Qur'an tukufu inasema yafuatayo katika surat *Mu'minun*:

"Hakika wamefanikiwa Waumini: ambao ni wanyenyekevu katika Swala zao" (Mu'minun, 23:1-2).

Mtume wetu anatufahamisha namna ambavyo mja atachukuliwa kutokana na namna nzuri atakavyoitekeleza swala yake:

❁

"Mja anaswali, hata hivyo, moja ya kumi tu au moja ya tisa, au moja ya nane, au moja ya saba, au moja ya sita, au moja ya tano, au moja ya nne, au moja ya tatu au nusu yake ndiyo anayoandikiwa". (Abu Dawud, Salat, 123-4/796).

Inamaanisha kuwa kuna malipo kwa mja mwenye kuswali ikiwa atatekeleza swala yake kwa umakini na heshima kubwa.

Mola wetu Mlezi anaelezea tena namna ambavyo muumini anaweza kuswali kwa unyenyekevu kama ifuatavyo:

"Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kusali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu, Ambao wana yakini kuwa hakika watakutana na Mola wao Mlezi na ya kuwa hakika watarejea kwake" (Baqara, 2:45-6).

❁

Hivyo mtu atafikia khushu ya kweli au unyenyekevu wa hali ya juu ikiwa ataswali kwa kujua kwa hakika kuwa siku moja atasimama mbele ya Mola wake na kuwajibika kwa kila jambo alilolitenda.

Hali hii ya hofu katika swala ikiendelea itafikia mahali imegubika maisha yote ya muumini. Ndiyo maana Jalaluddin Al Rumi (q.a) anafafanua Aya **"Isipokuwa wanaoswali, ambao wanadumisha Swala zao"** (Ma'arij, 70:22-3) kama ifuatavyo:

"Hali yako baada ya swala lazima iwe sawa na hali yako ndani ya swala".

❁

Ili kufikia hali hii hakuna budi kumuiga Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa kunufaika kutokana na mwenendo wake bora na kumuingiza moyoni kwa ujumla. Kama alivyosema:

" ... Mwenyezi Mungu anampenda mtu ambaye moyo wake umejaa hofu, huzuni na huruma na ambao unafundisha watu mambo mema na kuwaita kwenye utii wa Mwenyezi Mungu. Na anamchukia mtu ambaye moyo wake umezungukwa na mambo ya upuuzi, na ambaye anautumia muda wake wa usiku kwa kulala ingawa hajui kama roho yake itarudishwa, na anamkumbuka Mwenyezi Mungu kidogo mno" (Deylemi, I, 158).

❁

Matukio ya wema

Abdullah bin Shihhir رضي الله عنه anatufahamisha unyenyekevu wa hali ya juu aliokuwa nao Mtume kama ifuatavyo:

"Wakati fulani nilienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Alikuwa anaswali huku analia na ilisikika kana kwamba kifua chake kinachemka" (Abu Dawud, Salat, 156-7, 904; Ahmad, IV, 25, 26).

Ni muhimu sana kwa mtu kuzingatia kanuni za msingi (*fiqh*) za swala. Hata hadith zinatuelekeza kuchukua tahadhari juu imani zetu. *Fiqh* inamuandaa mja juu ya twahara, udhu na usafi, wakati twahara ya moyo au *khushu* (utulivu) inamuwezesha muumini kupata amani na utambuzi wa moyo na "Makutano matukufu".

Mtume ﷺ alionyesha umuhimu wa kuswali katika hali ya hofu na kumuomba Mwenyezi Mungu mtukufu kama ifuatavyo:

"Swala inaswaliwa kwa mizunguko (rakaa) miwili miwili. Katika kila mwisho wa rakaa muumini anakaa kwa ajili ya tashah-

hud [60]. *Swala ni staha ya hali ya juu na ni ishara ya unyenyekevu na udhalili mbele ya Mwenyezi Mungu. (Mwishoni) unanyanyua mikono yako kwa Mola wako Mlezi huku viganja vimegeukia uso wako na unaita: "Ewe Mola wangu Mlezi! Ewe Mola wangu Mlezi! . Swala ya mtu asiyefanya hivi ni pungufu"*. (Tirmidhi, Salat, 166/385)

Aisha ﵂ anasimulia:

"Siku moja Abu Jahm ﵁ alimletea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ zawadi ya nguo nzuri na iliyonakshiwa ambayo aliitumia kwa kuswalia. Alipomaliza akasema:

"Mrudishie nguo hii Abu Jahm. Macho yangu yalishughulishwa na nakshi zake. Zilikuwa zinakaribia kunitoa katika swala". (Muwatta, Salat, 67; Bukhari, Salat, 14).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwafundisha watu wake kanuni za Hijja kwa kuzitekeleza yeye mwenyewe wakati wa Hijja ya kuaga. Alielezea kuwa ni muhimu kuwa mnyenyekevu wakati wa Hijja kama inavyokuwa katika ibada nyingine.

Pia ilikuwa hivyo hivyo wakati Mtume anarudi Muzdalifa kutoka Arafa katika siku ya Arafa. Aliwasikia watu nyuma yake wanatoa sauti za juu na kupiga ngamia wao kiasi cha kunguruma kwa maumivu. Akawanyooshea fimbo yake na kuwaambia:

❁

"Enyi watu! (Punguzeni mwendo) Kuweni wapole. Hamtapata malipo ikiwa mtaharakisha" (Bukhari, Hajj, 94; Muslim, Hajj, 268).

Ali ﵁ anasimulia:

"Mtume alimuona mtu akichezea ndevu zake wakati wa swala. Kisha akamuambia:

60. Tashahhud ni sehemu ya swala ya faradhi ambayo muumini anakaa na kuisoma hiyo tashahhud.(Maelezo ya mfasiri).

"Kama moyo wake ungelikuwa na khushu (utulivu wa hali ya juu) vivo hivyo viungo vyake vingine vingelikuwa nayo" (Ali al-Muttaki, VIII, 197/22530).

Aisha ﵂ anasimulia kwamba wakati fulani mama yake, Ummu Ruman ﵂ alimuambia:

"Siku moja wakati ninaswali nilikuwa nikiyumbayumba. Abu Bakar aliponiona ninafanya vile akanikaripia sana kiasi cha kutaka kuvunja swala yangu, baada ya kusema:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anasema:

"Yeyote atakayesimama kwa ajili ya kuswali na atulize kila kiungno chake na anyenyekee. Asiyumbeyumbe kama mayahudi. Kwani utulivu wa viungo ni kipengere kimojawapo cha kukamilisha swala" (Alusi, Ruhu'l Ma'ani, Beirut ts. , XVIII, 3).

❁

Pamoja na nabii Suleiman ﷺ kupewa utajiri mkubwa na ufalme, lakini bado aliweza kuung'oa moyo wake kwenye hadaa za kidunia na kuishi maisha ya utumishi, na kuendelea kuishi katika hali ya staha, unyenyekevu na hamasa. Mwenendo wake huu umeelezwa kama ifuatavyo:

" Pamoja na nabii Suleiman kupewa utajiri, lakini kamwe hakuacha kunyanyua kichwa chake na kukielekezea mbinguni kwa unyenyekevu aliokuwa nao kwa Mwenyezi Mungu" (Ibn-i Abi Shayba, al Musannaf, Beirut, Daru'l-Fikr 1989, VIII, 118).

❁

Abdullah bin Abu Bakr ﵁ anasimulia:

"Siku moja Abu Talha alikuwa akiswali kwenye bustani yake. Ndege aitwaye 'Dubsi' alijaribu kuruka nje ya bustani na kutafuta njia ya kutokea. Jambo hili likamfurahisha Abu Talha, hivyo

macho yake yakamfuatilia ndege yule kwa sekunde. Kisha akarudi kwenye swala yake lakini akawa amesahau idadi ya rakaa alizokwisha swali. Kwa kuona kuwa ndege huyu amekuwa sababu ya kumshughulisha na kumharibia unyenyekevu wake akaenda kwa Mtume na kumuambia kilichotokea:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ! Natoa huyu ndege wangu kama sadaka. Unaweza kumtumia utakavyo au kumpa yeyote umtakaye" (Muwatta, Salat, 69).

❁

Uzuri ulioje wa tukio lifuatalo ambalo linaonyesha unyenyekevu wa hali ya juu wa maswahaba wakati wa swala.

"Wakati fulani Mtume alipokuwa anarudi Madina baada ya msafara aliousimamisha njiani. Aliwageukia maswahaba zake na kuwauliza:

"Nani atalinda leo usiku?"

Ammar bin Yasir رضي الله عنه kutoka kwa wahamiaji na Abbad bin Bashir رضي الله عنه kutoka kwa wasaidizi, upesi wakaitikia:

"Sisi tutafanya hivyo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu"

Kisha Abbad رضي الله عنه akamuuliza Ammar رضي الله عنه:

"Sehemu gani ya usiku unataka kulinda; mwanzoni au mwishoni" Ammar رضي الله عنه akajibu:

❁

"Ningelipenda kulinda sehemu ya mwisho" na kisha akaenda kulala upande wake. Kisha Abbad akaanza kuswali. Wakati ule mshirikina akatokea. Alipoona kitu cheusi kimesimama akafikiria lazima atakuwa ni mlinzi hivyo akamuelekezea mshale. Ule mshale ukamchoma Abbad. Abbad akauchomoa ule mshale na kuendelea kuswali. Yule mtu akamlenga kwa mara ya pili na ya tatu na zote

zilimpata. Mara zote Abbad alikuwa akisimama juu na kuuchomoa mshale na kuendelea na swala. Kisha akarukuu na kusujudu. Baada ya kumaliza swala alinyanyuka na kuwaamsha marafiki zake na kusema:

❁

"Amkeni. Nimejeruhiwa"

Ammar akaamka upesi. Yule mshirikina aliwaona akajua kuwa ameonekana hivyo akakimbia. Ammar alipomuona Abbad anatokwa na damu nyingi akasema:

"Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu! Kwa nini hukuniamsha pindi uliporushiwa mshale wa kwanza?"

Abbad akatoa jibu lifuatalo lenye mvuto ambalo lilionyesha upendo wake na shauku ya swala na unyenyekevu wa hali ya juu katika ibada zake:

❁

"Nilikuwa ninasoma sura ndani ya Qur'an. Sikutaka kusitisha swala yangu bila ya kuimalizia. Lakini mishale ilipokuwa inaendelea kuja niliacha kusoma na kurukuu. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu lau kama si kuhofia kupoteza nafasi niliyopewa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu bora ningelikufa kuliko kukatisha hii sura"

Siku moja Asma ﵂, binti wa Abu Bakar ﵁ aliulizwa na mjukuu wake, Abdullah:

❁

"Bibi! Maswahaba wa Mtume walikuwa wanafanyaje walipokuwa wanasikiliza Qur'an?"

Asma ﵂ akajibu:

"Machozi yalikuwa yakiwamiminika machoni mwao na miili yao ilikuwa ikitetemeka kama ilivyotajwa ndani ya Qur'an" (Bayhaki, ShuAbu'l Iman, II, 365).

Mwenyezi Mungu mtukufu anawaelezea waja wake ambao wanasoma Qur'an kwa unyenyekevu kama ifuatavyo:

"Na huanguka kifudifudi na huku wanalia, na inawazidisha unyenyekevu" (Isra, 17:109).

❁

"Husisimua kwacho ngozi za wenye kumhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu" (Az Zumar, 39:23).

Wakati fulani Ali ﷺ akiwa kwenye vita mshale ulimchoma mguuni. Hawakuweza kuuchomoa kutokana na maumivu. Ali aliwaambia:

"Ngojeni niswali, kisha mtauchomoa"

Wakafanya kama alivyowaambia. Hapo waliweza kuuchomoa kwa wepesi bila ya ugumu wowote. Ali, ambaye hakuhisi maumivu, baada ya kumaliza swala aliwauliza:

"Mlifanya nini?"

Wakajibu:

"Tuliuchomoa mshale"

Siku moja Veysel Karani aliulizwa na mama yake:

"Mwanangu. Unawezaje kufanya ibada usiku kucha mpaka asubuhi? Unawezaje kuvumilia?"

Yule rafiki mkubwa wa Mwenyezi Mungu akajibu:

"Ewe mama yangu mpendwa! Ninafanya ibada zangu kwa umakini na usahihi mkubwa. Kutokana na unyenyekevu wa hali ya juu moyo wangu unakunjuka kiasi kwamba sihisi kuchoka, Nahisi kutengana na dunia na hisia za mwili wangu. Na kabla ya kujitambua, mara asubuhi imefika..."

"Ni *khushu* ya namna gani hii?"

"K*hushu* ni pale ambapo mwili hauhisi hata mkuki unapoutoboa"

Kutokana na masimulizi ni kwamba kila Zayn al Abideen aliponyanyuka kuchukua udhu uso wake ulisawajika na kila alipoanza kuswali miguu yake ilikuwa ikitetemeka. Alipoulizwa sababu alisema:

"Je hamtambui mahala ninapoingia?" (Abu Nuaym, Hilya, III, 133).

Wakati fulani alipokuwa anaswali nyumba yake ilishika moto. Hata hivyo hakulijua hilo. Alipomaliza kuswali na kuambiwa kuhusu tukio lile, walimuuliza:

"Ni kipi kilichokufanya ushindwe kugundua kuwa nyumba yako imeshika moto?"

Zayn al Abideen akajibu:

"Moto unaomsubiri mwanadamu kesho akhera umenifanya niusahau moto wa hapa duniani"

Swala ya Muslim bin Yasir ilikuwa na hali sawa na hiyo ya Zayn al Abideen. Wakati fulani alikuwa akiswali msikitini ndani ya mji wa Basra. Mara msikiti ukaanza kuporomoka. Hata hivyo Muslim bin Yasir hakutambua kinachoendelea na hivyo aliendelea na swala yake. Alipomaliza wakamuuliza:

"Msikiti ulikuwa unaporomoka lakini wewe hukusogea hata inchi moja. Ni hali gani hii?"

Muslim bin Yasir akauliza katika hali ya kustaajabu:

"Ni kweli msikiti umeporomoka?" kama ushahidi kuwa kweli hakuhisi chochote wakati anaswali.

Rafiki wa Mwenyezi Mungu anasimulia:

"Siku moja nilikuwa ninaswali swala ya mchana nyuma ya Zunnun-i Misri. Yule mtu aliyebarikiwa aliposema "Allahu Akbar (Mwenyezi Mungu ni mkubwa), neno "Allah" lilikuwa na mguso mkubwa kwake kiasi kwamba kiwiliwili chake kikawa kama kimekufa. Aliganda na kuendelea kusimama pale alipokuwa. Aliposema neno "Akbar" moyo wangu ukapasuka vipande vipande kutokana na utukufu wa neno lile.

Amir bin Abdullah alipokuwa akisimama kuswali alikuwa akikata mawasiliano na (nje) ya dunia moja kwa moja.

"Ni bora mikuki itoboe mwili wangu kuliko kusikiliza maongezi na mishughuliko ya watu ninapokuwa ndani ya swala".

Bahauddin Nakshiband ﷺ siku moja aliulizwa:

"Mja anawezaje kupata unyenyekevu wa hali ya juu akiwa ndani ya swala". Akajibu:

"Kuna masharti manne:

7. Riziki yake lazima iwe ya halali.

8. Ajiweke mbali na upuuzi wakati wa kuchukua udhu.

9. Hana budi kutambua uwepo wake (mbele ya Mwenyezi Mungu) katika takbira ya kwanza.

10. Kamwe asimsahau Mwenyezi Mungu nje ya swala. Inamaanisha kuwa hali yake ya kuwa mbele ya Allah, utulivu na kujiweka mbali na maasi haina budi kuendelea baada ya kumaliza swala yake".

Kwa kifupi, *khushui* ni kutekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu na kujizuia na yale aliyoyakataza. *Khushui* (utulivu wa hali ya juu), taqwa (kumuogopa Mwenyezi Mungu), ikhlas (usafi wa moyo) na ihsan (wema) ni sawa kihali na kimaana. Chanzo cha haya yote ni mapenzi kwa Mwenyezi Mungu.

Mapenzi kwa Mwenyezi Mungu ni kiashirio cha ulivyo moyo wa muumini. Hali hii ya kiroho inajidhihirisha yenyewe kwa kupitia ibada ambazo zinafanywa kwa unyenyekevu wa hali ya juu na usafi wa matendo ya mtu.

Hatuna budi kujaza nyoyo zetu unyenyekevu wa hali ya juu katika kila kipengele cha maisha yetu na kila tunapotekeleza ibada zetu zote, hasa swala. Na unyenyekevu huu hauna budi kuonekana kwa watu wanaotuzunguka, kutokana na matendo yetu yanayopelekea amani na utulivu.

7. Kuifahamu Qur'an tukufu

Qur'an tukufu ni mwalimu wa uongofu ambaye anatuonyesha njia ya haki. Ni rehema kwa waumini na ponyo kwa maradhi ya moyo. Wakati huohuo Qur'an ndiyo ambayo inamtoa mwandamu kwenye kiza na kumleta kwenye nuru na kumkumbusha juu ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake.

Qur'an tukufu ni uongofu ambao unamtaarifu mwanadamu lengo la kuumbwa viumbe vyote. Inaonyesha hekima juu ya uumbaji wa mwanadamu na kuamrisha kuishi kulingana na utaratibu wa Mwenyezi Mungu duniani kote.

Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Mwenyezi Mungu ameteremsha hadith nzuri kabisa, Kitabu chenye kufanana na kukaririwa; husisimua kwacho ngozi za wenye kumhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Huo ndiyo uwongofu wa Mwenyezi Mungu, na kwa huo humwongoa amtakaye. Na ambaye ameachwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi hapana wa kumwongoa". (Azzumar, 39:23)

Aya hii inaonyesha aina ya mahusiano yanayotakiwa kuwepo katika nyoyo zetu na Qur'an.

Kiwango cha taqwa tuliyonayo kinalinganishwa na mwangwi wa Qur'an ambao unajidhihirisha katika hali ya mwenendo wa Qur'an uliojaa usafi wa moyo katika ibada zetu, uzuri wa tabia zetu, na upana wa nyoyo zetu.

Qur'an ndiyo kishiko cha pekee ambacho mtu anaweza kukishikilia. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amewapelekea wale waja wake ambao wanataka kupata radhi zake na kuokolewa kutokana na maovu na hivyo adhabu za siku ya kiama. Wale ambao watashikamana nayo wataokolewa na kupandishwa daraja na kusifiwa; wale watakaoikataa watadharauliwa na kuwekwa mbali na njia iliyonyooka.

Qur'an tukufu ni dhifa ya kiroho ambayo Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ameiandaa kama zawadi kwa waja wake. Wale wanaokubali mwaliko huu kutoka kwa Mola wao na kuufanyia kazi wataonja raha ya neema zisizo na mwisho, ambazo zitapelekea kupatikana kwa amani na furaha.

Utu na heshima ya kweli kwa mwanadamu vinategemea ni kwa kiwango gani anatekeleza maamrisho yake na kujipamba na tabia zake. Inamaanisha kwamba mwanadamu ataweza kupata heshima inayoendana na lengo la kuumbwa kwake iwapo ataikumbatia Qu'ran na kutii maamrisho yake matukufu. Mwenyezi Mungu mtukufu anatuamrisha kuishi kulingana na Qur'an kwa kuifahamu vilivyo. Hivyo akili ambayo inaweza kuwa chanzo cha vyote furaha na kuridhika inahitaji muongozo unaopatikana ndani ya Qur'an.

Kama Qur'an haijatufungulia mlango wa kutafakari, basi tutakosa kujua mambo mengi. Kwa kutafakari kiundani juu ya

yaliyomo ndani ya Qur'an kutatuwezesha kugundua njia nyingi za wema.

Hakuna budi kuifahamu Qur'an vizuri na kujiweka nayo karibu ili kujifunza vizuri mwenendo wa kiislamu.

Tumeelezwa katika hadith kwamba:

"Ikiwa mmoja wenu anapenda kuomba na kuzungumza (kumsihi na kuongea) na Mola wenu, basi na asome Qur'an wakati moyo wake umetulia na kuzingatia" (Suyuti, I, 13/360).

"Someni Qur'an! Kwani siku ya kiama Qur'an itakuja kumuombea yule anayeisoma" (Muslim, Musafirin, 252, 253; Ahmad, V, 249, 251).

"Siku ya kiama taji litawekwa juu ya vichwa vya wazazi wa wale wanaoisoma Qur'an na kuifanyia kazi. Nuru inayotoka kwenye taji hili ni nzuri zaidi ya nuru ya jua ambayo inaangazia nyumba iliyo chini yake. Kwa namna hiyo, je unaweza kuwazia itakavyokuwa nuru ya yule anayeifanyia kazi Qur'an?" (Abu Dawud, Vitir, 14/1453).

Kushikamana barabara na Qur'an ni amali njema ambayo Mwenyezi Mungu anapendezwa nayo na kuiridhia. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anapendezwa na si chochote zaidi ya usomaji wa Qur'an uliofanywa na Mtume kwa sauti nzuri, ya juu na kwa teganni[61]*"* (Bukhari, Fadailu'l Qur'an 19, Tawheed 32; Muslim, Musafirin 232-234).

61. Teganni ina maana zifuatazo za kuipamba Qur'an, maneno yaliyo mazuri kabisa, katika namna ambayo inafaa na kwa sauti nzuri. Linatumika kusisitiza furaha na huzuni katika sauti ya mtu wakati wa kuisoma na pia kuisoma vizuri na kwa sauti ya juu. Kwa maelezo zaidi angalia M.Yasar Kandemir, Ismail Lutfi Cakan, Rasit Kucuk, Riyadhu-s Saliheen – Translation and Commentary, Istanbul 2001, V, 118.

"Mwenyezi Mungu hasikilizi chochote zaidi ya anavyomsikiliza mja wake ambaye anaswali rakaa mbili za usiku na ambaye (anasoma Qur'an). Rehema za Mwenyezi Mungu zinasambaa kwenye kichwa cha mja kwa kipindi chote atakachokuwa kwenye swala. Mja kamwe hatomkurubia Mwenyezi Mungu zaidi ya pale anaposoma Qur'an" (Tirmidhi, Fadhailu'l Qur'an, 17/2911).

Imeelezwa kuwa wale watu wanaosahau sura za Qur'an walizozihifadhi kutokana na kutozipitia mara kwa mara, wanapata dhambi kubwa (Abu Dawud, Salat, 16/461). Mtu asiye na hata kiasi kidogo cha Qur'an moyoni mwake ni sawa na nyumba tupu[62].

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Nyoyo zinashika kutu kama chuma kinavyoshika kutu". Maswahaba zake wakauliza:

"Ni kipi kifutio cha kutu hii ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

"Kwa kusoma sana kitabu cha Mwenyezi Mungu na kumkumbuka sana Mwenyezi Mungu" (Ali al-Muttaki, II, 241).

Pia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwashauri maswahaba zake kama ifuatavyo:

❁

"Yapeni haki macho yenu kutokana na ibada"

"Ipi haki ya macho yetu ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" wakamuuliza.

Mtume akajibu:

62. Tirmidhi, Fadai'ul Qur'an, 18/2913; Darimi, Fadail'ul Qur'an, 1

"Kusoma Msahafu (kurasa za Qur'an), kutafakari yaliyomo na kuchukua mafundisho yaliyomo katika maudhui zake" (Suyuti, I, 39).

❁

Wakati mwingine Mtume ﷺ alisema:

"Kwa hakika miongoni mwa watu kuna wale ambao wapo karibu na Mwenyezi Mungu"

Alipoulizwa:

"Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni nani hao?" akajibu:

"Hao ni watu wa Qur'an, watu wa Mwenyezi Mungu, na waja maalum wa Mwenyezi Mungu" (Ibn-i Majah, Mukaddima, 16).

Mtume Muhammad ﷺ alikuwa akipendezwa zaidi pale watu walipokuwa wakikusanyika pamoja katika juhudi ya kuisoma na kuielewa Qur'an. Aliwazungumzia watu hawa:

" ... Kundi la watu litakapokusanyika pamoja ndani ya moja ya nyumba za Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kusoma kitabu cha Mwenyezi Mungu, kukijadili na kujaribu kukielewa na kukizingatia, litashukiwa na namna fulani ya utulivu na kufunikwa na huruma ya Mwenyezi Mungu. Malaika watawazunguka. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anawataja katika mkusanyiko uliomzunguka. Na yule aliyebaki nyuma (kwa kutojali matendo yake), nasaba yake haitomsaidia..." (Muslim, Zikir, 38; Ibn-i Majah, Mukaddima, 17).

❁

Hivyo hatuna budi kuzishikamanisha zaidi nyoyo zetu na Qur'an kwa ajili ya furaha ya hapa duniani na kesho Akhera. Hatuna budi kuisoma, kuielewa, kuimakinisha nyoyoni mwetu na kujitahidi kutekeleza mafundisho yake kwa nyoyo safi.

Matukio ya wema

Mtume ﷺ alikuwa akisoma Qur'an tukufu kwa namna inavyotakiwa na kutafakari kiundani maana yake na kufuata maamrisho yake bila kuchelewa. Alikuwa akiisoma Qur'an kwa moyo wake wote, akiitafakari na kuifanyia kazi. Wakati anasoma, akifikia Aya inayomtukuza Mwenyezi Mungu alikuwa akimtakasa Mwenyezi Mungu kutokana na mapungufu na madhaifu kwa kusema '*SubhanAllah*' (Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu). Alipofikia Aya zenye dua alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu. Alipofikia Aya zilizotaja kuomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu, upesi aliomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu. (Angalia Muslim, Musafirin, 203; Nasai, Kıyamu" l Layl, 25).

Mtume ﷺ alikuwa akisoma Qur'an mara kwa mara kila siku[63]. Aws bin Hudhayfa ؓ ambaye anatoka katika kabila la Thakif ambaye alikuja Madina anasimulia kuwa:

"Usiku mmoja, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alichelewa kutoka nje baada ya swala ya usiku.

❁

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa nini umekaa muda mrefu hivyo kabla ya kutoka nje?" Tulimuuliza. Mtume ﷺ akajibu:

"Nimejiwekea jukumu la lazima kwangu la kusoma hizb (1/60) ya Qur'an kila siku, sikutaka kutoka nje mpaka niwe nimemaliza".

Ilipofika asubuhi tuliwauliza maswahaba:

"Huwa mnaigawanyaje Qur'an? Wakajibu:

"Sura tatu za kwanza tunaziita *hizb*, kisha sura tano zinazofuta ni *hizb* ya pili, kisha saba zinazofuata, kisha tisa , kisha kumi na moja, na kumi na tatu zinazofuata kila moja ni *hizb*. Mwishoni

63. Muslim, Musafirin, 142; Ahmad, IV, 9İ Ibn-i Majah, Salat, 178

surat kahf na sura zinazoifuata ni *hizb* nyingine. Hivyo tunaisoma Qur'an katika sehemu saba" (Ahmad, IV, 9; Ibn-i Majah, Salat, 178).

❁

Abdullah ibn-i Mas'ud ﷺ anasimulia kuwa:

"Siku moja Mtume ﷺ aliniambia:

"Ewe ibn Mas'ud nisomee Qur'an" Nikajibu:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nitakusomeaje Qur'an wakati imeshushwa kwako?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema:

"Ninapenda kusikia Qur'an ikisomwa na mwingine".

Kisha nikaanza kusoma kuanzia surat Nisaa. Nilipofikia Aya inayosema: "Basi itakuwaje pindi tukiwaletea kutoka kila umma shahidi, na tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?" (An Nisaai, 4:41).

"Hilo litafanyika".

Wakati ule nikaona machozi kama lulu yakitiririka machoni mwake" (Bukhari, Tafsir, 4/9; Muslim, Musafirin, 247).

Uzuri ulioje wa tukio hili ambalo linaonyesha huruma aliyokuwa nayo Mtume juu ya umma wake...

Siku moja wakati Aisha ﷺ amechelewa kurudi kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, alimuuliza sababu ya kuchelewa kwake. Aisha akajibu kuwa alitaka kusikiliza Qur'an ndiyo maana alichelewa:

❁

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kulikuwa na mtu msikitini, ambaye Kamwe sikuwahi kusikia mtu akisoma Qur'an vizuri kama yeye". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akaenda msikitini na kukuta yule mtu ni Salim ﷺ. Akasema:

"Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu kwa kuwepo mtu kama huyu miongoni mwa watu wangu" (Ibn-i Majah, Ikamah, 176; Ahmad, VI, 165; Hakim, III, 250/5001).

Siku moja swahaba alimuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni amali ipi ambayo inapendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu?" Mtume mpendwa akajibu:

"Amali za *hal* na *murtahil*"

"Na ni nini *hal* na *murtahil*?" Swahaba akauliza. Mtume akajibu:

"Kusoma Qur'an kuanzia mwanzo mpaka mwisho na baada ya kumaliza kuanza tena mwanzo" (Tirmidhi, Kiraat, 11/2948).

Sasa hivi ni jambo la kawaida kwamba pindi Qur'an yote inapokuwa imesomwa, kisha mtu anasoma sura tatu za mwisho za Qur'an na kisha anaanza tena kwa kusoma sura ya ufunguzi, *al Fatiha*, na kisha anasoma Aya tano za mwanzo katika sura inayofuata, *Baqara*. Hili linafanywa ili kufikia ubora uliotajwa katika hadith hii.

❁

Hivyo usomaji mwingine unaanzwa na amali njema inayokubaliwa zaidi na Mwenyezi Mungu inakuwa imefanywa.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliipa Qur'an umuhimu mkubwa na aliwapenda wale maswahaba zake waliokuwa kama yeye.

❁

Wakati fulani Mtume alikuwa anataka kutuma kikosi chenye idadi kubwa ya watu. Aliwaamuru wasome Qur'an. Kila mmoja

wao alisoma kadri alivyohifadhi Aya za Mwenyezi Mungu. Mtume alimsogelea aliyekuwa mdogo miongoni mwa maswahaba na kumuuliza:

"Ewe fulani, Umehifadhi nini?" Akajibu:

"Nimehifadhi sura hizi na surat Baqara". Mtume akasema:

"Je umehifadhi surat Baqara?"

Alipojibu "Ndiyo" akasema:

"Utaenda. Wewe ni kiongozi wao. Sura hii inabeba takriban dini nzima"

Mmoja wa viongozi katika kikosi kile akasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hofu yangu ya kushindwa kuyafanyia kazi yaliyomo ndani ya surat Baqara imenipelekea kushindwa kuihifadhi".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

"Jifunze Qur'an, isome, wausie wengine waisome na kuifanyia kazi. Kwani yeyote anayejifunza Qur'an, anayeisoma na kuifanyia kazi, ni sawa na chupa ya miski ambayo inasambaza harufu yake kila mahali. Yule anayejifunza Qur'an, lakini analala (yani haifanyii kazi) ni sawa na chupa ya miski iliyofungwa kwa kizibo chake" (Tirmidhi, Fadailu'l Qur'an, 2/2876).

❁

Tukio hili linaonyesha manufaa ya mtu anayesoma na kuishi kulingana na surat *Baqara*. Pia katika *hadith* hii Mtume ﷺ anatangaza wajibu wa waumini kuifahamu na kuifundisha Qur'an.

Maswahaba walipokuwa wamejifunza Aya kumi kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hawakukimbilia kuhifadhi nyingine kumi kabla ya kuelewa maamrisho yake na hekima zake vizuri na

kuzifanyia kazi katika maisha yao. Waliufanyia kazi ujuzi uliopatikana ndani ya Qur'an na walipanda daraja kwa kupitia hekima zilizomo ndani yake. (Ahmad, V, 410).

Omar ﷺ anasema:

"Nilimaliza kuisoma surat Baqara ndani ya miaka kumi na mbili na nikachinja ngamia kama shukurani juu ya hilo" (Kurtubi, al-Jami li- ahkami'l Qur'an, Beirut 1985, I, 40).

Abdullah bin Omar ﷺ alimaliza *Baqara* ndani ya miaka nane. (Muwatta, Qur'an, 11).

Kuisoma Qur'an kutakuwa na thamani pale tu itakapofanyiwa kazi na kuwafundisha wengine.

Wawakilishi wa kabila la Thaqif, ambao walikuja kumuona Mtume walimuacha Othman bin Abi'l kuwaangalizia wanyama kwa kuwa alikuwa mdogo miongoni mwao. Wale wawakilishi waliporejea na kulala kutokana na jua la mchana, Othman ﷺ akaenda kwa Mtume ﷺ na kumuuliza maswali yanayohusu dini, na kusikiliza Qur'an na kujifunza. Kwa kupitia njia hii aliweza kusoma na kuhifadhi baadhi ya sura kutoka kwa Mtume.

❁

Othman ﷺ ambaye alifanya makubaliano na Mtume kwa siri na ambaye aliingia kwenye Uislamu kabla ya wale marafiki zake wawakilishi, alikuwa akienda kusoma Qur'an, na kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakuwepo alikuwa akienda ama kwa Abu Bakr, au Ubayy bin Ka'b na kuwauliza ni kipi aulize na kujifunza.

Jambo hili lilimpendezea sana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ambaye alimpenda sana. Wale wawakilishi wa Thaqif walipotaka kurejea nchini kwao walisema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Je unaweza kutuchagulia mmoja wetu kuwa kiongozi?"

Mtume akamchagua Othman bin Abi'l kuwa kiongozi wao ingawa alikuwa ni mdogo miongoni mwao. (Ibn-I Sa'd, V, 508; Ibn-I Hisham, IV, 185; Ahmad, IV, 218).

Aya za Qur'an ambazo zilishushwa kwa sababu mbalimbali moja baada ya nyingine, zilikuwa ndiyo chanzo cha furaha kubwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na maswahaba zake, na zili-waongezea utambuzi na kufanya nyoyo zao zizidi kushikamana na Mwenyezi Mungu. Walijawa na huzuni kubwa pale ufunuo ulipo-koma kutokana na kufa kwa Mtume.

Tunaweza kuuona mfano huu wenye mguso juu mapenzi ya Qur'an katika tukio lifuatalo:

❁

Baada ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ Abu Bakar alimuambia Omar:

"Simama twende kwa Ummu Ayman, ambaye alikuwa akim-pendwa na aliyekuwa karibu mno na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Tumtembelee kama Mtume alivyokuwa akifanya"

Walipowasili kwa Ummu Ayman, akaanza kulia.

❁

Wakamuuliza:

"Kwa nini unalia? Kwani hujui kuwa fadhila za Mwenyezi Mungu kwa Mtume ni bora zaidi?"

Ummu Ayman akajibu:

"Hiyo sio sababu inayonifanya nilie. Bila shaka ninajua kuwa fadhila za Mwenyezi Mungu kwa Mtume aliyebarikiwa ni bora zaidi. Ninalia kwa sababu ufunuo umefikia mwisho"

❁

Maneno haya yanayoonyesha mapenzi juu ya ufunuo mtakatifu yaliwagusa Abu Bakar ﷺ na Omar ﷺ na wao wakaanza kulia pamoja na Ummu Ayman ﷺ. (Muslim, Fadailu's Sahabe, 103).

Maswahaba wa Mtume walikuwa wakisoma Qur'an mara kwa mara, na hawakukubali siku ipite bila ya wao kuisoma au kupitisha macho katika kurasa zake. Waliianza siku kwa Qur'an na waliwashauri wale waliokuwa na matatizo ya macho wapitishe macho yao juu ya kurasa zake. (Haythami, VII, 165).

Othman, ambaye aliheshimiwa na kuitwa '*Jami'ul Qur'an*', au mkusanyaji wa Qur'an kutokana na huduma yake juu ya Qur'an, alizichakaza chapa mbili kutokana na kufungamana nazo mno" (Kettani, Nizamu'l Hukumeti'n Nabawwiyya, (at- Teratibu'l Idariyye), Beirut 1996, II, 197).

Usayd bin Hudayr ﷺ anasimulia:

"Usiku mmoja nilikuwa nikisoma surat *Baqara*. Farasi wangu alikuwa amefungwa karibu yangu. Wakati fulani akanyanyuka kwa miguu yake miwili ya nyuma. Nikasitisha kusoma; farasi akatulia. Nikaanza kusoma tena, na yule farasi akanyanyuka tena. Kwa kweli nilihofia kwamba farasi angemkanyaga mtoto wangu Yahya, hivyo nikamkaribia. Wakyati ule nilipoangalia juu nikaona vitu kama mishumaa. Kisha vikapaa angani na kutoweka.

Ilipofika asubuhi nikamuambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kilichotokea. Akasema:

"Soma ewe Usayd, soma"... Kisha akasema:

"Ewe Usayd, unajua ni nini ulichokiona?"

❁

"Hapana" Nikajibu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema:

"Walikuwa ni malaika waliokuja kusikiliza Qur'an. Kama ungeliendelea kusoma wangeliendelea kusikiliza mpaka asubuhi. Wangeliweza kuonekana na watu ambao hawakuweza kuwaona" (Bukhari, Fadailu'l Qur'an, 15, Menakib 25; Muslim, Musafirin 241-242).

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuambia yafuatayo kipenzi cha Qur'an, Ubayy bin Ka'b:

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ameniamuru nikuambie usome sura "Lam yakunilladhina kafaru"

Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه akauliza:

"Je Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ametaja jina langu?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

"N*dio*"

Ubayy bin Ka'b aliguswa mno na nafasi hii tukufu mpaka akaanza kutoa machozi kwa wingi. (Bukhari, Menakibu'l Ansar 16, Tafsir 98/1, 3; Muslim, Misafirin, 246).

Ubayy bin Ka'b alikuwa juu katika orodha ya hafidh (wale walioihifadhi Qur'an yote). Alikuwa ni mmoja wa wale watu wanne waliobahatika ambao juu yao Mtume alisema *"Jifunzeni Qur'an kutoka kwa mmoja miongoni mwa hawa wanne"*. Alikuwa ni mtu aliyekuwa akiisoma Qur'an vizuri mno na mara kwa mara. (Bukhari, Fedail'ul Qur'an, 8). Hivyo ufahamu huu wa Ubayy juu ya Qur'an ndio uliompelekea kupata neema hii, heshima na utukufu ambao haupatikani ila kwa watu wachache sana waliochaguliwa kinyume na mitume; pia ndio ulimpelekea kupata nafasi tukufu. Heshima iliyoje, furaha iliyoje...

Kama yalivyo mambo mengine, maswahaba walifuata nyayo za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu walipotakiwa kuishi kwa mujibu wa Qur'an kwa kushikamana na Qur'an na yaliyomo ndani yake. Kinana al Adawi رضي الله عنه anasimulia:

"Wakati fulani Omar bin Khattab ﷺ alimuandikia barua kiongozi wake wa jeshi kama ifuatavyo:

"Watambue wale waliohifadhi Qur'an na unijulishe ili niwasifu na kuwafadhilisha na kuwasambaza ili wakawafundishe wengine"

Abu Musa al Ashari alimjulisha Omar kuwa ana mahafidh zaidi ya 300. Ifuatayo ni sehemu ya ushauri kutoka kwenye barua ambayo Omar alikuwa anawahutubia wale mahafidh:

"Jueni kuwa Qur'an ni hazina ya heshima na zawadi kwenu. Shikamaneni nayo na msiifanye iwafuate nyinyi. Watakaoifanya Qur'an iwafuate wao wataanguka na kwenda moja kwa moja motoni. Yeyote anayeshikamana na Qur'an, ataingizwa kwenye pepo ya *Firdaws*. Kama unaweza ifanye Qur-an iwe muombezi wako na usiiache ikawa adui yako. Kwani yule ambaye ataombewa na Qur-an ataenda peponi wakati yule ambaye atashitakiwa nayo ataenda motoni. Jueni kwamba Qur-an ndio chanzo cha uongofu na ndio njia sahihi ya elimu. Ni kitabu cha mwisho ambacho kimekuja kutoka kwa mwingi wa rehema. Kwa kupitia kitabu hiki macho yasiyoona, masikio yasiyosikia na nyoyo zilizofungwa vyote vinafunguliwa... (Ali al Muttaki, II, 285-6/4019).

Mja mwerevu wa mjumbe wa Allah, Anas bin Malik ﷺ kila alipomaliza kusoma Qur-an, aliikusanya familia yake na kusoma dua ya *hatim* (dua isomwayo baada ya kumaliza kusoma Qur-an). (Ibn-I Abi Shayba, al Musannaf (Hut), Riyadh, 1409, VI, 128).

Omar bin Khattab alikuwa akimuambia Abu Musa mara kwa mara; ni nani aliye na sauti nzuri na ambaye anaweza kuisoma Qur-an kwa usahihi zaidi:

"Ewe Abu Musa! Njoo utukumbushe kuhusu Mola wetu". Kisha Abu Musa alikuwa akiwasomea Qur-an .

Wakati fulani alimwambia Abu Musa al-Ashari:

"Ndugu yangu! Tuongezee ari juu ya Mola wetu".

Kisha akaanza kusoma Qur-an. Baada ya kusoma kwa muda, wakamwita Omar kwenye swala, Khalifa ambaye alikuwa akisikiliza Qur-an kwa umakini, upesi akaja na kuuliza:

"Si tulikuwa kwenye swala muda si mrefu?" (Ibn-I Sa'd, IV, 109).

Siku moja Nafi, mtumwa aliyeachiwa huru na Abdullah bin Omar, aliulizwa:

"Abdullah alikuwa akifanya nini nyumbani kwake?"

Nafi akajibu:

"Watu wengine hawawezi kufanya alichokuwa akifanya. Alikuwa akichukua udhu mpya katika kila swala na kufungua Qur-an na kuisoma mfululizo baina ya nyakati hizi". (Ibn-I Sa'd, IV, 170).

Wale watu waliokariri Qur-an kiukweli, ambao wameshikamana nayo, wanapata fadhila nyingi hapa duniani na kesho Akhera. Mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu, Mahmud Sami Ramazanoglu ﷺ ametufahamisha kuhusu maiti ya hafidh ambaye alimuona yeye binafsi.

Hafidh huyu alikufa miaka 50 iliyopita akiwa Adana. Kaburi lake lilitaka kufukuliwa ahamishiwe sehemu nyingine ili kupisha ujenzi wa barabara. Kaburi lake lilipofukuliwa aliiona maiti yake iko vilevile na sanda yake inang'aa.

Imeelezwa katika hadith:

"Hamil-i Qur-an (mwenye kuhifadhi Qur-an ambaye ameishi kulingana na mafundisho yake na amechukua mwenendo wake na kujipamba na hekima zake) atakapokufa, Mwenyezi Mungu anaiamuru ardhi isiule mwili wake, na ardhi inajibu:

"Ewe Mola wangu! Nitaulaje mwili wake wakati amebeba maneno yako kifuani mwake?..." (Daylami, I, 284/1112; ali al- Muttaki, I, 555/2488).

Hatuna budi kuwa makini na waangalifu katika matendo yetu na kuiheshimu Qur-an tukufu ambayo ni maneno ya Mola wetu. Hayo ni kwa sababu tunaishi katika nyakati ambazo tunahitaji zaidi manufaa na maadili ya Qur-an.

Kwa mfano hatutakiwi kuisoma Qur'an wala kuruhusu isomwe wakati hatuna udhu. Aya ifuatayo inathibitisha hili kwa uwazi:

"Hapana akigusaye ila waliotakaswa" (Waqiah, 56:79)

Aya hii inaashiria hadathi ndogo, hadathi kubwa na kwa wanawake wakiwa kwenye hedhi au nifasi. Maimamu wote wanne wamekubaliana kuwa ni haramu kugusa (kurasa) za Qur-an bila kuwa twahara (kuwa na udhu). (Mavsuatu'l Fikhiyye, XVIII, 322).

"Sheria hii imekuwa ikitekelezwa kwa miaka 1400 hasa kuanzia kipindi cha Mtume aliyebarikiwa. Imeelezwa katika hadith:

"Mwanamke aliye katika hedhi au mtu aliye katika janaba hawaruhusiwi kusoma Qur-an." (Tirmidhi, Taharah, 98/131).

"Wasiiguse Qur-an ila wale walio twahara". (Hakim, I, 553/1447).

Kwa kuongezea ni kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipomtuma Amr bin Hazm kwenda Yemen alimwandikia tamko linaloelezea mambo ya fardh (lazima), sunnah (mwenendo wa mtume) na hukumu. Katika tamko lile Amr aliambiwa awafundishe watu Qur-an na pamoja na kuwafundisha maamrisho yake, hekima zake, lakini pia aliambiwa awakataze watu wasio twahara wasiiguse Qur-an. (Muwatta, Qur'an, I; Kattani, 216).

Imam Malik anasema:

"Kwa ambaye hayuko twahara haruhusiwi kuibeba Qur'an hata kama ipo ndani ya mfuko au shuka, kwani hili ni jambo lisilopendeza... Haya ni kwa sababu ya heshima na utukufu wa Qur'an" (Muwatta, Qur'an, 1).

Cha zaidi ni kwamba mtu hana budi kuonyesha heshima na unyenyekevu juu ya Qur'an ikiwemo kujizuia kuibeba chini ya kiuno, kuiruka, kuiwekea juu yake kitabu kingine na kutoenda nayo chooni. Haya ni lazima yafanyike pamoja na ibada na kuyapitisha kwa vizazi vijavyo. Kwani Qur'an tukufu ni alama muhimu mno ya Uislamu. Qur'an tukufu inatufahamisha yafuatayo:

وَمَن يُعَظِّمْ شَعَائِرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ

"Ndiyo hivyo! Na anayetukuza ibada za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo" (Hajj 22:32).

Kwa kifupi Qur'an ni kitabu kitakatifu kilichoshushwa kwa mpangilio maalum kwa ajili ya kumuwezesha mwanadamu kupata njia ya haki, kujifunza mambo ambayo angelishindwa kujifunza mwenyewe na kumuwezesha kuingia peponi. Hivyo kushikamana nayo na kuijali ndiyo njia sahihi ya kuifuata.

Manufaa ya kushikamana na Qur'an yanaelezewa katika hadith ifuatayo:

"Qur'an ni sawa na kamba imara, upande mmoja yupo Mwenyezi Mungu na upande mwingine uko mikononi mwako. Ishike kwa nguvu, hutapotea wala kuharibikiwa". (Haythami, IX, 164).

Kadri tunavyonufaika na Qur'an ndivyo imani zetu zinavyoongezeka. Wale wanaoshikamana na Qur'an na kupata radhi za Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake, wako kwenye fadhila kubwa

isiyoelezeka. Mwenyezi Mungu atujaalie sisi sote kupata fadhila hizo na aturahisishie kila mmoja wetu kufikia daraja hili. Amin!...

8. Dhikrullah[64] na *Swalawat-i Sharifa*[65]

Neno la kiarabu kwa mwanadamu, '*insan*', linafikiriwa na baadhi ya watu kuwa linatokana na mzizi wa neno '*nisyan*' linalomaanisha 'kusahau'. '*Nisyan*', ambalo ni kinyume na '*dhikr*' (kukumbuka) linamaanisha usahaulifu ambao ndiyo udhaifu mkubwa wa mwanadamu. Ili kufidia madhara yanayosababishwa na hii '*nisyan*', ambayo ni sehemu ya asili ya mwanadamu, anahitaji *dhikr* ili wakati wote kumuweka '*Allah*' na utambuzi binafsi kama 'mtumishi' kichwani mwake. Kwani marudio yanaimarisha utambuzi na uelewa wa jambo linalorudiwa.

Neno '*dhikr*' limejirudia zaidi ya mara 250 ndani ya Qur'an, ikiashiria umuhimu wake wa kipekee kwa mja. Mja anahitajika kuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu mtukufu katika maana halisi ya neno na afikie daraja la '*marifatullah*' (kumfahamu Mwenyezi Mungu). Lakini jambo hili litawezekana pale tu moyo utakapofaidika kutokana na ukumbukaji huu. Ndiyo maana Mola wetu Mlezi akasema:

"Na mkumbuke Mola Mlezi wako nafsini kwako kwa unyenyekevu na hofu, na bila ya kupiga kelele kwa kauli, asubuhi na jioni. Wala usiwe miongoni mwa walio ghafilika" (A'raf 7:205).

64. Dhikrullah ni kumtaja Mwenyezi Mungu. Dhikr inatekelezwa kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kutaja jina lake na maneno mengine yaliyopo katika sheria. (Maelezo ya mfasiri).
65. Swalawat-i Sharifa ni jina linalowakilisha namna tunavyomtakia Mtume Muhammad ﷺ baraka pindi jina lake linapotajwa. Kumtumia Mtume baraka kuko kwa namna nyingi lakini iliyozoeleka ni yenye kifupi cha "saw' ambayo imetumika katika kitabu hiki.(Maelezo ya mfasiri).

"Soma uliyofunuliwa katika Kitabu, na ushike Sala. Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyatenda" (Ankabut 29:45).

"Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto" (Al'i imran 3:191).

Pindi moyo, ambao ndiyo kiongozi wa mwili, utakapohuishwa kwa kupitia utajo wa Mwenyezi Mungu, na ukawa safi zaidi kiasi cha kutofautisha ukweli na uongo, unakuwa kama dira inayouongoza mwili kuelekea kwenye haki na wema. Utatoa maelekezo sahihi kwa washirika wengine wa mwili ambao wako chini yake. Mwishoni utafikia utumishi ambao Mwenyezi Mungu anauridhia.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaelezea faida za utajo wa Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

"Ulingano kati ya mtu anayemtaja Mwenyezi Mungu na mtu asiyemtaja, ni sawa na tofauti kati ya uhai na mauti" (Bukhari, Dawat, 66).

Vile vile wale walio mbali na utajo wa Mwenyezi Mungu pia wapo mbali na kuwa wapokeaji wa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na hivyo wako katika tishio kubwa. Qur'an tukufu inasema:

"Enyi mlioamini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndiyo waliokhasiri" (Munafikun 63:9).

"Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole

wao wenye nyoyo ngumu zisizomkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri" (az Zumar, 39:22).

"Anayeyafanyia upofu maneno ya Rahmani tunamwekea Shetani kuwa ndiye rafiki yake" (az-Zuhruf, 43:36).

"Nenda kwa Firauni; kwani hakika yeye amepindukia mipaka" (Twaha, 20:24).

Kutokana na hatari kubwa ya kupuuzia kufanya *dhikrullah* (kumkumbuka Mwenyezi Mungu) Mwenyezi Mungu mtukufu amekuwa akirudia mara kwa mara kuwaonya waja wake kuhusu jambo hili. Katika moja ya maonyo yake anasema:

"Je! Wakati haujafika bado kwa walioamini zikanyenyekea nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyoteremka? Wala wasiwe kama waliopewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa wapotovu" (Hadid 57:16).

Aya hii ilishushwa kama onyo kwa baadhi ya maswahaba ambao, kutokana na kuishi kwao maisha ya shida na tabu walipokuwa Makka, walianza kuzembea baada ya kupata neema ya riziki na fadhila nyinginezo walipohamia Madina. (Angalia Suyuti, Lubab, II, 151-52).

Ingawa Musa na Harun (amani iwe juu yao) wote walikuwa mitume, lakini bado Mwenyezi Mungu mtukufu aliwaonya alipowatuma kwenda kumpa mawaidha Firauni kama ifuatavyo:

"Nenda, wewe na ndugu yako, pamoja na ishara zangu, wala msichoke kunikumbuka" (Taha 20:42).

Kwa namna hii kwa kuwaonya hata hawa mitume kutojitenga na *dhikr*, Alitaka liwe somo na mfano (kwa wanadamu).

Katika kuongelea umuhimu wa kuwa katika hali ya *dhikrullah na murakaba* (kuwa macho), Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

❁

"Msijiingize katika maongezi yasiyo ya lazima na kumsahau Mwenyezi Mungu. Kwani kukithirisha maongezi pamoja na kumfanya mtu amsahau Mwenyezi Mungu lakini pia kunaufanya moyo kuwa mgumu. Na yule aliye mbali zaidi na Mwenyezi Mungu ni yule mwenye moyo mgumu". (Tirmidhi, Zuhd, 62/2411).

Namna nyoyo za waumini zinavyoweza kufikia umakini ambao utawafanya wawe huru kutokana na tatizo la kupuuzia mambo na kupata radhi za Mwenyezi Mungu, ni kwa kumtaja Mwenyezi Mungu wakati wote. Hili si jambo la muda mfupi, bali ni la kipindi chote cha uhai, hili litawezekana kwa kufanya *dhikrullah* katika kila pumzi, kwani hii ndiyo njia pekee ya kuamsha imani ya mtu.

Mke wa Mtume, Aisha رضي الله عنها anasema:

"Kila hali ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ilikuwa ni ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu" (Muslim, Hayz, 117).

Ibn-i Abbas رضي الله عنه anasema yafuatayo kuhusu Aya:

"Enyi mlioamini! Mdhukuruni Mwenyezi Mungu kwa wingi wa kumdhukuru" (Ahzab, 33:41).

❁

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ameweka mpaka katika kila jambo la ibada aliyomfaradhishia mja wake. Amekubali dharura za wale waliosamehewa (Kwa sababu yeyote ile). Lisilo la dharura ni *dhikr*. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi hakuweka mpaka katika *dhikr*. Hakubali dharura ya yeyote anayeacha kumkumbuka Mwenyezi Mungu, isipokuwa yule asiye na akili timamu. Mwenyezi

Mungu mtukufu amewaamuru watu wawe katika hali ya *dhikr* katika hali zote" (Taberi, Jamiu'l Beyan an Te'vili Ayi'l Qur'an, Beirut, 1995, XXII, 22; Kurtubi, XIV, 197).

Katika kuwahamasisha watu juu ya *dhikr* na kuwa pamoja na watu wa *dhikr,* Mtume Muhammad ﷺ anasema:

"Kukaa pamoja na kundi la watu wanaomtaja Mwenyezi Mungu kuanzia swala ya asubuhi mpaka jua lichomoze, kunapendeza zaidi kwangu kuliko kuwanusuru watumwa wanne kutoka kabila la watoto wa Ismail. Vilevile kukaa pamoja na watu wanaomtaja Mwenyezi Mungu kuanzia baada ya swala ya adhuhuri mpaka jua linapozama, kunapendeza zaidi kwangu kuliko kuwaacha huru watu wanne" (Abu Dawud, Ilim, 13/3667).

❁

Kwa kuongezea ni kwamba tunayoyasema wakati wa kumswalia Mtume ni miongoni mwa maneno ya *dhikr*.

Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamswalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu" (Ahzab, 33:56).

Mtume ameelezea thamani ya swala hizi kama ifuatavyo:

"Yeyote anayeniswalia mara moja, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi humrehemu mara kumi zaidi[66], anamfutia makosa kumi na kumpandisha daraja mara kumi" (Nasai, Sahv, 55)

"Watu watakaokuwa karibu zaidi na mimi siku ya kiama ni wale wanaonitumia salamu na baraka nyingi zaidi" (Tirmidhi, Vitir, 21/484).

❁

66. Muslim, Salat, 70

Kwa kuongezea ni kwamba, matendo ya ibada kama vile kuswali, tasbih (kutukuza), tahmiid (kusifu), tahlil (kumpwekesha Mwenyezi Mungu), istighfar (kuomba msamaha) na kusoma Qur'an na kuzingatia Aya zake, pia yanachukuliwa kuwa ni *dhikr*.

Matukio ya wema

Mke wa Mtume, Aisha رضي الله عنها anatujulisha kwamba pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipoamka usiku kwa ajili ya ibada, aliswali na kuomba dua kwa kusema "Alhamdulillah" (Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu) "S*ubhanallahi wa bihamdih*" (Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu mwenye kuhimidiwa) mara kumi kila moja na kisha alisema yafuatayo mara kumi:

اَللّٰهُمَّ إِنِّى أَعُوذُ بِكَ مِنْ ضَيقِ الدُّنْيَا وَ ضَيقِ يَومِ القِيَامَ

"Ewe Mwenyezi Mungu! Ninajilinda kwako kutokana na dhiki ya hapa duniani na kesho akhera"

❁

Kisha Mtume alianza kuswali" (Abu Dawud, Adab, 101/5085).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipendelea *dhikr* na dua ambazo ni fupi lakini zenye maana kubwa. Siku moja mke wa Mtume , Juwayriya رضي الله عنها aliswali swala ya alfajiri na kisha akakaa pale pale aliposwalia. Mtume ﷺ akaondoka nyumbani mapema na aliporudi baadaye akamkuta Juwayriya bado amekaa pale pale alipomuacha.

"Je umekaa hapa ukifanya *dhikr* tokea muda niliokuacha?" Akamuuliza. Alipojibu ndiyo, Mtume ﷺ akasema:

❁

"Kama sentensi nne nilizozisema mara tatu kila moja kabla ya kukuacha zingelipimwa na kulinganishwa na dhikr zako zote ulizozifanya tokea asubuhi utakuta kuwa malipo yake ni sawa:

"Ametakasika Mwenyezi Mungu kutokana na kila udhaifu na ninamsifu kwa idadi ya viumbe vyake, mpaka aridhike, kwa kiasi cha kufikia uzito wa dunia na idadi ya maneno yasiyoisha" (Muslim, *dhikr*, 79)

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Kuna maneno ambayo ni mepesi katika ulimi, lakini ni mazito yakipimwa kwenye mizani ambayo inapendeza kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema:

سُبْحَانَ اللهِ وَبِحَمْدِهِ عَدَدَ خَلْقِهِ وَرِضَا نَفْسِهِ وَزِنَةَ عَرْشِهِ وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ

"Ametakasika Mwenyezi Mungu na sifa zote njema anastahiki Yeye. Ametakasika Mwenyezi Mungu aliye mkuu" (Bukhari, Dawat 65, Ayman, 19, Tawheed 58; Muslim, Zikr, 31).

Mwenyezi Mungu mtukufu anapenda moyo wa mja wake uwe pamoja naye kila wakati. Katika aya ifuatayo watu hawa wameelezwa kuwa wale **"Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala."** (Al-Imran, 3:19)

سُبْحَانَ اللهِ وَبِحَمْدِهِ سُبْحَانَ اللهِ العَظِيمِ

Hadith zilizopita zinaonesha ubora wa hizi *tasbihat* (dua za kutukuza) zinazofanywa, na wingi wa malipo yake. Kwa upande mwingine ni kwa ajili ya kutia moyo na kushawishi. Hata hivyo tusiishie kumtaja Mwenyezi Mungu kwa *tasbihat* pekee bali hatuna budi kuwa katika hali ya kuendelea kufanya *dhikr*. Jambo hili ni muhimu sana kwa mujibu wa Qur'an na sunnah.

Abdullah bin Busra ﷺ anasimulia:

"Mabedui wawili walikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kumuuliza maswali. Mmoja wao akauliza:

"Ewe mjunbe wa Mwenyezi Mungu ni yupi mtu bora?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akajibu:

"Ni yule mwenye umri mrefu na matendo mema".

Mwingine akauliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hukumu za Uislamu zimekuwa nyingi mno, niambie amali moja ambayo nitashikamana nayo"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akajibu:

"Ufanye ulimi wako wenye unyenyekevu wakati wote kwa kumtaja Mwenyezi Mungu" (Ahmad, IV, 188).

Mtume aliposema kuwa katika hali ya kufanya *dhikr* wakati wote ni kwa kuwa kunamletea muumini ulinzi dhidi ya kupuuzia na kusahau utajo wa Mwenyezi Mungu. Ni njia ya kumuongezea mtu utii na unyenyekevu kwenye maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu. Hivyo kwa upande mwingine *dhikr* ni njia ya mafanikio na ukuaji wa imani ambao unamuongezea muumin shauku ya kutekeleza hukumu za dini.

Swahaba mmoja alimjia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kumuuliza:

"Ni jihad ipi yenye malipo makubwa zaidi?"

Mtume akajibu:

"Jihad ya yule mwenye kumtaja Mwenyezi Mungu zaidi" Kisha yule swahaba akauliza tena:

"Ni funga ipi yenye malipo makubwa zaidi?" Mtume akajibu:

"Funga ya mwenye kumkumbuka Mwenyezi Mungu zaidi"

Baada ya hapo yule swahaba akauliza swali lile lile juu ya mtu anayeswali, anayetoa sadaka, anayekwenda kuhiji na anayetoa zaka. Jibu lilikuwa sawa kwa maswali yote haya:

"Mtu anayemkumbuka Mwenyezi Mungu zaidi"

Kutokana na hayo Abu Bakar ﷺ alimwambia Omar ﷺ:

"Ewe Omar! wale wanaomtaja Mwenyezi Mungu wamechukua mgao wote wa wema" Kisha Mtume ﷺ akawageukia na kusema:

"Ndiyo, hilo ni kweli." (Ahmad, III, 438; Haythami, X, 74).

Hivyo kwa namna yoyote ile kama tutajifunza kuwa katika hali ya *dhikr* wakati wote tutanufaika.

Muadh bin Jabal ﷺ amesimulia kuwa:

"Siku moja nilimwambia Mtume ﷺ:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nipe ushauri"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaniambia:

"Muogope Mwenyezi Mungu kadiri uwezavyo, mkumbuke Mwenyezi Mungu popote utakapokuwa, iwe pembezoni mwa jiwe au mti na kwa dhambi uliyoitenda kwa siri , omba msamaha kwa siri, lakini uliyoitenda kwa uwazi, basi omba msamaha kwa uwazi" (Haythami, X, 74)

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiwaambia maswahaba zake ubora wa mikusanyiko ya *dhikr*:

"Mnapokuja kwenye mabustani ya peponi hakikisheni mnafaidika nayo vizuri"

"Unamaanisha nini unaposema mabustani ya peponi ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" wakamuuliza.

Mtume ﷺ akajibu:

"Mikusanyiko ya dhikr" (Tirmidhi, Deavat, 82/3510).

Kila wakati Abdullah bin Rawaha رضي الله عنه anapopita karibu na mmoja wa maswahaba alikuwa akisema:

"Njoo ndugu yangu! Tukae kidogo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na tusafishe imani zetu juu ya mola wetu mlezi (tufanye *dhikr*)".

Swahaba mmoja ambaye hakuelewa maana ya jambo hili alimwendea Mtume na kumjulisha hali ilivyokuwa. Mtume akamwambia:

"Mwenyezi Mungu amrehemu Abdullah bin Rawaha. Anapenda watu wa dhikr ambao wanasifiwa na malaika" (Ahmad, III, 265).

Abdullah bin shaddad رضي الله عنه amesimulia kuwa:

"Watu watatu kutoka kabila la bani Uzra walimjia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kusilimu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akauliza:

"Nani atawahudumia hawa?"

Talha رضي الله عنه akasema:

"Mimi nitafanya hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu".

❁

Walipokuwa pamoja na Talha, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alituma kikosi kidogo cha askari. Mmoja kati ya wale watu watatu akajitolea kuwepo katika kile kikosi, akafa shahidi. Kisha akatuma kikosi kingine kidogo, mtu mwingine wa pili akajitolea

kuwepo katika kikosi hiki, na yeye akafa shahidi. Baadaye mtu wa tatu akafa akiwa kitandani.

Talha anasimulia:

"Niliwaona hawa watu watatu tukiwa pamoja nao peponi. Yule aliyekufa kitandani kwake alitangulia mbele, kisha yule shahidi wa pili na mwisho akafuata yule shahidi wa kwanza. Nilistaajabishwa na kuchukizwa kidogo na jambo hili. Upesi nikamwambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu nilichokiona. Akasema:

"Hili si jambo la kushangaa. Hakuna aliye bora zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu zaidi ya muumini anayemtukuza Mwenyezi Mungu wakati wote, anafanya takbir, tahlil na ambaye anaishi kulingana na Uislamu" (Ahmad, I, 163).

Siku moja Uftade alienda nje ya mji pamoja na wanafunzi wake kwa ajili ya mazungumzo. Kutokana na maagizo ya mwalimu wao wanafunzi wote wakazungukia sehemu nzuri za maeneo yale na kumletea mwalimu wao kichanga cha maua. Hata hivyo mikononi mwa kadhi wa zamani wa Busra, Mahmud Efendi, ambaye baadaye alipata umaarufu na kuitwa Aziz Mahmud Hudayi, alirudisha ua lililonyauka na huku shina lake limevunjika... Baada ya wenzake kuwasilisha maua yao kwa furaha, Mahmud Efendi aliwasilisha ua lake lililonyauka na kuvunjika kwa Uftade huku amejiinamia. Wanafunzi wenzake wakiwa na shauku juu ya jambo lile, Uftade aliuliza:

❁

"Mwanangu Mahmud! Kwa nini, wakati kila mmoja ameleta lundo la vichanga vizuri vya maua, lakini wewe umeleta ua lililonyauka?"

Mahmud akainamisha kichwa chake chini kwa unyenyekevu mkubwa na kujibu:

"Mwalimu! Chochote ambacho nitakuletea hakitatosha kamwe. Kwani kila ua nililoliinamia kwa ajili ya kulichuma, nililikuta katika hali ya kumtaja Mola wake, likisema '*Allah*, *Allah*'. Moyo wangu ulishindwa kuzuia utajo huu wa Mola wao. Kwa udhalili nilipelekewa kukuletea ua hili ambalo halikuweza kuendelea na *dhikr*".

Kwa wale wenye nyoyo nyepesi, kila atomu duniani ina cha kujifunza. Vitu vyote, ikiwa ni hai au visivyo hai vinafanya *dhikr* kwa Mwenyezi Mungu. Imeelezwa katika Aya ya Qur'an:

"Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa sifa zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye maghfira" (Isra, 17:44).

Hivyo mtu hana budi kutambua ukweli huu wa jukumu lake kwa kuchukua mazingatio kwenye mazingira yake ndani ya ulimwengu huu na asipuuzie kumtaja Mola wake.

Dhikr iliyo bora miongoni mwa *dhikr* zetu ni *salawat-i sharif*. Muumini atanufaika kiimani kiasi cha kufikia kumtumia salamu na baraka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Kwani thamani ya Mtume wetu mbele ya Mwenyezi Mungu ni kubwa zaidi.

❁

Kwanza kabisa Mola wetu binafsi amemtumia salamu Mjumbe wake ﷺ na kumpandisha daraja kwa kupitia rehema zake na radhi zake na amemteremshia neema kadhaa.

Moja ya nyakati ambazo tunamtumia salamu Mtume ﷺ ni wakati wa swala, tunaposoma *Atahiyyatu*[67]. Kutokana na mapokezi Mtume alisema:

67. Haya ni maneno yanayosemwa katika swala wakati umekaa. (Maelezo ya mfasiri).

"Kwenye usiku wa miraji nilimuona Mola wetu kwa jicho la moyo wangu. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akaniambia:

"Ongea na Mimi ewe kipenzi!"

Nilipigwa na bumbuwazi. Kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akajaalia moyo wangu useme maneno yafuatayo:

اَلتَّحِيَّاتُ لِلّٰهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ

"Maamkizi yote ni ya Mwenyezi Mungu, na swala zote, na mambo yote mazuri"

Kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akasema:

لَسَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللّٰهِ وَبَرَكَاتُهُ

"Amani iwe juu yako iwe Mtume, na rehema za Mwenyezi Mungu na baraka zake"

Nikajibu:

اَلسَّلَامُ عَلَيْنَا وَ عَلَى عِبَادِ اللّٰهِ الصَّالِحِينَ

"Amani iwe juu yetu, na juu ya waja wako wema"

Kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akasema:

"Ewe Mtume wangu! Nimemuondoa kati yetu hata Jibril. Hujauondoa umma wako kati yetu".

Baada ya kusikia maneno haya nikasema:

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللّٰهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

"Ninashuhudia kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu pekee. Na ninashuhudia kuwa

Muhammad ni mja wako na Mjumbe wako" (Angalia Qurtubi, III, 425).

Ubayy bin Ka'b ﷺ anasimulia:

❁

"Siku moja ilipopita theluthi ya usiku Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliamka kisha akasimama na kusema:

"Enyi watu! Mkumbukeni Mwenyezi Mungu! Mkumbukeni Mwenyezi Mungu! Baragumu la kwanza likipulizwa litaihamisha dunia kutoka sehemu moja hadi nyingine. Kisha baragumu la pili litapulizwa. Mauti yatakuja na kushambulia kwa kishindo kikubwa. Mauti yatakuja na kushambulia kwa kishindo kikubwa".

Nikamuuliza Mtume:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ninakuswalia kwa wingi, lakini nashangaa, je nizidishe? [kiasi gani kinatosha]?"

"Fanya kwa wingi kadri utakavyo", alisema.

"Nikitenga sehemu ya nne ya swala yangu kukuswalia, je hapo itatosha?" Niliuliza.

"Tenga muda mwingi kadri upendavyo. Lakini ukifanya zaidi, itakuwa bora kwako" alisema.

"Kama ni hivyo nitatenga nusu ya dua yangu kukuswalia" Nikasema.

"Fanya mara nyingi kadri upendavyo. Lakini ukifanya zaidi, itakuwa bora kwako" alisema.

"Kama ni hivyo je theluthi mbili itatosha?" Nikauliza.

"Fanya mara nyingi kadri upendavyo. Lakini ukiongeza, itakuwa bora kwako" alisema.

Niliposema:

"Kama ni hivyo vipi nikitenga dua yangu yote kukuswalia?", akajibu:

"Hapo Mwenyezi Mungu atakuondolea magumu yako na kukusamehe madhambi yako". (Tirmidhi, Qiyamah, 23/2457).

❁

Siku moja Mtume ﷺ alimuona mmoja wa maswahaba zake akianza dua yake kwa kumsifu Mwenyezi Mungu na kumswalia Mtume, akamsifu na kusema:

"Ewe unayeomba dua! Omba dua (ikiwa utaanza dua yako kwa kumsifu Mwenyezi Mungu na kuniswalia), na dua zako zitajibiwa" (Tirmidhi Dawat, 64, 3476).

Omar bin Khattab ؓ alisema:

"(Binafsi), dua unayoomba inabakia kati ya mbingu na ardhi. Ikiwa humswalii Mtume, hakuna dua yako hata moja itakayopanda kwa Mwenyezi Mungu" (Tirmidhi, witr, 21/486).

Ka'b bin Ujra ؓ anasimulia kwamba siku moja walimuambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Tumejifunza kukutakia amani, lakini hatufahamu namna ya kukutakia rehema". Akajibu:

Semeni maneno haya:

اَللَّهُمَّ صَلِّى عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى (إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى)
آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ اَللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا
بَارَكْتَ عَلَى (إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى) آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

"Ewe Allah! Teremsha rehma juu ya Muhammad na familia yake kama ulivyoteremsha rehma juu ya Ibrahimu na familia yake.

Hakika Wewe ndiwe Mwenye kuhimidiwa na kutukuzwa. Ewe Mwenyezi Mungu teremsha Baraka juu ya Muhammad na familia yake kama ulivyombariki Ibrahimu na familia yake. Hakika Wewe ndiwe Mwenye kuhimidiwa na kutukuzwa" (Bukhari, Daawat, 32, Tirmidhi, Witr, 20; Ibn-I Majah, Iqama, 25)...

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

"Siku bora miongoni mwa masiku ni ijumaa... Hivyo, niswalieni kwa wingi katika siku hii, siku ambayo zitawasilishwa kwangu".

Kisha maswahaba wakauliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni vipi salat-u salam zitawasilishwa kwako wakati umeshakufa na hakuna hata nyayo zako". Mtume akajibu:

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ameiharamisha ardhi kuozesha miili ya mitume". (Abu Dawud, Salat 201/1047, Witr, 26).

Ali رضي الله عنه anasema yafuatayo kuhusu ubora wa kumswalia Mtume kwenye siku ya ijumaa:

"Yeyote atayemswalia Mtume mara mia moja siku ya ijumaa, atajitokeza kwenye mkusanyiko wa siku ya kiama akiwa na uso mzuri na wenye kung'aa. Watu wataulizana: "Nastaajabu huyu mtu alikuwa akifanya amali gani". (Bayhaki, ShuAbu'l Imam, III 212).

Ka'b bin Ujra رضي الله عنه anasimulia:

"Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alituambia tusogee kwenye mimbari. Tukafanya vile. Alipanda kwenye ngazi ya kwanza, kisha akasema "Amin". Akapandisha ngazi ya pili na kusema "Amin". Akapanndisha ngazi ya tatu na kusema vilevile "Amin".

Aliposhuka kwenye mimbari tukamuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Leo tumesikia mambo kutoka kwako ambayo hatujawahi kuyasikia. (Ni ipi hekima yake)".

Akajibu:

"Jibril alinijia na kuniambia: Yule anayeufikia mwezi wa Ramadhani na madhambi yake yasifutwe awe mbali na rehema za Mwenyezi Mungu". Nikasema "Amin". Nilipopanda ngazi ya pili, akasema:

"Yule anayesikia jina lako na asikuswalie awe mbali na rehema za Mwenyezi Mungu". Nikasema "Amin". Nilipopanda ngazi ya tatu akasema:

"Yule ambaye ameshindwa kupata pepo wakati mama yake na baba yake, au wote wamefikia uzee akiwa nao lakini akashindwa kuwafanyia wema. Nikasema: amin". (Hakim, IV, 170/7256; Tirmidhi, Deawat, 100/3545).

Kumesimuliwa na mtu mwema kuwa:

"Nilikuwa na jirani ambaye alikuwa akizalisha chapa za vitabu vya wanavyuoni kwa kuviandika yeye mwenyewe. Alipokufa nilimuona kwenye ndoto. Nikamuuliza:

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amekufanyia nini?".

Akasema:

"Amenisamehe".

"Ni amali gani iliyokupelekea kufikia haya" Nikamuuliza.

"Kila nilipokuwa nikiandika jina tukufu la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika kitabu nilikuwa siachi kumswalia. Hivyo Mola wangu amenijaalia fadhila ambazo hakuna jicho lililopata kuona, hakuna sikio lililopata kusikia, na hakuna mtu aliyewahi kufikiria". (Nebhani, Saadet'ul Dareyn, pg 101).

Imesimuliwa kuwa mtu mmoja ambaye alishindwa kushikamana na mwenendo wa Mtume ﷺ alimuona kwenye ndoto usiku mmoja. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akampuuzia. Akauliza kwa huzuni:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Je umenikasirikia?"

"Hapana".

"Hivyo kwa nini unanipuuzia?"

"Sikujui"

"Hilo linawezekanaje ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Mimi ni miongoni mwa umma wako. Wanavyuoni wanasema kwamba unaweza kuwatambua watu wa jamii yako vizuri zaidi ya mama anavyomtambua mtoto wake mwenyewe..."

"Hilo ni kweli. Hata hivyo sioni hata chembe ya mwenendo wangu kwako. Kwa kuongezea, hakuna rehema wala amani zilizonijia kutoka kwako. Jua kwamba ninawatambua watu wa umma wangu kutokana na kiwango chao cha kushikamana na mwenendo wangu".

Alipoamka kutoka kwenye usingizi mzito alihuzunika, kisha muumini huyu akatubu madhambi yake yaliyopita na kushikamana na mwenendo mtukufu wa Mtume. Alitumia muda wake mwingi kumswalia Mtume. Baada ya muda mfupi akamuona tena Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwenye ndoto kwa mara nyingine. Wakati huu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimuambia:

"Sasa ninakutambua na nitakuombea shifaa..."

Kwa kifupi Mtume ﷺ anasema:

"Mtu atakuwa pamoja na yule anayempenda". (Bukhari, Adab, 96). Kanuni inasema "Mpenzi anapenda kila kitu anachopenda kipenzi chake", hatuna budi kumfuata Mtume katika matendo

yetu yote na hali zetu zote. Kwani mapenzi katika jambo hili ni kama uti wa mgongo wa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Mapenzi yote kinyume na haya yamekatazwa ndani ya Qur'an na *sunnah*.

Njia pekee ya kumfikia Mwenyezi Mungu mtukufu, yaani kukutana naye ni kwa kupitia mapenzi juu ya kipenzi chake Mtume ﷺ.

Dhikrullah na *swalawat-i sharif* ni virutubisho vya imani zetu na kutuhakikishia furaha ya milele. Ubora wa nyoyo na roho zetu unakamilika kwa *dhikr* (kumkumbuka Mwenyezi Mungu). Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndiyo nyoyo hutua!" (Ar Rad, 13:28).

Njia ya kufikia utumishi wa Mwenyezi Mungu ni kufanya dhikr (kumkumbuka Mwenyezi Mungu) wakati wote. Ni kwa kupitia njia tu ndiyo maisha yetu yanaweza kupata furaha na utamu wa imani. Mwenyezi Mungu atujaalie wote tuyapate hayo. Amin...

9. Hofu na maandalizi ya kifo na maisha ya Akhera

Mtu anapoangalia utaratibu wa ulimwengu kwa jicho la utambuzi atagundua kuwa jambo la kuzingatia zaidi ni mauti.

Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Kila kilichoko juu yake kitatoweka" (Ar Rahman, 55:26).

"Kila nafsi itauonja umauti" (Anbiya, 21:35).

Inastaajabisha kwamba watu-wageni katika dunia hii kwa siku mbili au tatu lakini bado wanajidanganya. Ingawa wanaona matukio ya vifo kila siku, lakini bado wanaona mauti yapo mbali nao. Wanadhani wao ni wamiliki wa hii dunia yenye kudanganya

ambayo wataiacha muda wowote. Wakati kila mtu anapoingia hapa duniani, moyo wake unakuwa umefunikwa ndani ya mwili na anawajibika kusafiri kuelekea kwenye mauti. Ameingia kwenye maandalizi ya safari hiyo lakini hakumbuki. Kisha siku inafika ambapo roho yake inatengana na kiwiliwili. Anaingizwa katika kaburi ambalo ndiyo mlango wa kuelekea Akhera, na kuanza safari nyingine kubwa. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anasema:

"Na tunayemzeesha tunamrudisha nyuma katika umbo. Basi je! hawazingatii?" (Yasin, 36:68).

Lengo la maisha ya hapa duniani kwa wanadamu ni kuishi maisha ya utumishi ambao Mwenyezi Mungu anauridhia ili baadaye kupata furaha ya milele. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anasema:

"Mtu mwenye akili ni yule ambaye hafanyi mambo kwa matamanio ya nafsi yake na ambaye anajiandaa kwa maisha ya baada ya mauti..." (Tirmidhi, Qiyamah, 25/2459).

Uzuri ulioje namna marehemu Najip Fazil alivyoelezea jambo hili:

❁

"E*we (mfanya biashara) bahili, jishonee begi lingine la fedha*".

Na fukia fedha yote unayoitafuta kaburini!"...

Maisha ni kama matone yanayojaza bilauri ya maji. Ubora wa bilauri unategemea ulivyo usafi wa matone. Tone la mwisho kujaza bilauri ni pumzi ya mwisho ya mtu.

Imeelezwa katika hadith:

❁

"Yeyote ambaye maneno yake ya mwisho wa uhai ni '*La ilaha illallah*' ataingia peponi". (Abu Dawud, Janaiz, 15-16/3116; Hakim, I, 503).

Inamaanisha kuwa, mtu atakayeondoa moyoni mwake mambo ya upuuzi, tamaa na mawazo mabaya na kuujaza mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kuendelea na hali hii ya kuishi maisha ya kiimani mpaka mwisho wa uhai wake ataingia peponi. Kwani ni vigumu sana kwa mtu ambaye anafuata njia nyingine kusema '*la ilaha illallah*" katika pumzi yake ya mwisho. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Mtu anakufa kulingana na alivyoishi na atafufuliwa kulingana na alivyokufa". (Angalia Muslim, Jannah, 83; Munawi, V, 663).

❁

Pumzi ya mtu ya mwisho ni sawa na kioo kisicho na ukungu. Mtu atajijua vizuri zaidi katika pumzi yake ya mwisho. Akaunti ya maisha yake italetwa mbele ya moyo wake na macho yake. Ndiyo maana hakuna tukio lenye kuonya kama wakati wa kifo.

Mtume ﷺ anasema:

"Kutokana na amali za mtu, kaburi litakuwa bustani miongoni mwa mabustani ya pepo au shimo miongoni mwa mashimo ya moto". (Tirmidhi, Qiyamah, 26/2460).

Hivyo ni muhimu kuandaa pumzi zetu zenye kuhesabika kwa ajili ya pumzi yetu ya mwisho kama tunataka kuondoka hapa duniani tukiwa waja wema na kufanya makaburi yetu kuwa mabustani miongoni mwa mabustani ya peponi. Ili kuwa na maisha ya furaha baada ya kufa hatuna budi kuishi kwa kufanya amali njema na kufuata muongozo wa Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

"Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini". (Hijr, 15:99).

Wale waja maalum ambao wanaishi kwa namna hii, kwa mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake na ambao

wanayapamba kwa amali njema- kwa rehema za Mwenyezi Mungu- mwishoni wataondoka wakiwa na amani ndani ya nyoyo zao, imani inayotokana na 'maneno ya shahada'[68]. Kwa upande mwingine wale walio na bahati mbaya ambao wanadanganywa na mapambo ya dunia hii yenye kupita na kudhoofisha nyoyo zao, mara nyingi hufa kulingana na walivyoishi na atakuwa amepata hasara na udhalili na kufukiwa ardhini kwa udhalili.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema yafuatayo kama onyo kwa umma wake:

"Hakuna mtu atayekufa bila kujuta"

"Ni majuto gani hayo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" aliulizwa.

❁

Mtume akajibu:

"Kama mtu atakayekufa ni mwema (mwenye mazuri na mema) atajuta kwa kutoongeza mema yake; kama atakuwa ni mtu mbaya, atajuta kwa kutoachana na mabaya yake na kubadilika". (Tirmidhi, Zuhd, 59/2403).

Mwenyezi Mungu mtukufu anawaonya waja wake juu ya suala hili katika Aya ifuatayo:

"Enyi mlioamini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndiyo waliokhasiri. Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema? Wala Mwenyezi Mungu hataiakhiri-

68. Maneno ya shahada ni kama ifuatavyo: Nashuhudia kwamba hakuna Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. (Maelezo ya mfasiri).

sha nafsi yoyote inapo fika ajali yake; na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda" (Munafiquun, verses 9-11).

Kwa kifupi mauti yetu na maisha yetu kaburini ambayo yataendelea mpaka siku ya kiama yataendana na namna tulivyoishi hapa duniani na namna matendo yetu yalivyokuwa.

Uzuri ulioje namna Jalaluddin Al Rumi alivyolielezea jambo hili:

"Mwanangu, mauti ya mtu ni kiashirio cha namna alivyo. Kwa wale wanaochukia mauti na kuyafanyia uadui, wasijue kuwa mauti yanapelekea kurudi kwa Mwenyezi Mungu, kwao kifo kitakuwa kama adui mwenye kuogopesha. Kwa wale ambao ni marafiki wa mauti, yatakuwa rafiki yao.

Ewe roho mwenye kuogopa na kuyakimbia mauti! Ukweli ni kwamba huyakimbii mauti bali unahofia nafsi yako.

Kwani yale unayoyaona na hivyo kuyahofia na kutetemeka mbele ya kioo cha mauti siyo taswira ya mauti bali ni muonekano wako mbaya. Roho yako ni kama mti. Na mauti kama majani ya mti huo. Kila jani linalingana na aina ya mti (ulilolibeba)..."

Hivyo mauti yatamvutia mtu kulingana na namna alivyoyapamba maisha yake kwa amali njema.

Matukio ya wema

Abdullah bin Omar ﷺ anasimulia: "Siku moja nilikuwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Mtu mmoja kutoka *Ansar* alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, alimsalimia na kumuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni nani mbora zaidi miongoni mwa waumini?" Mtume akajibu:

"Ni yule mwenye tabia njema zaidi". Yule mtu akauliza tena:

"Sawa, ni nani mwenye akili zaidi miongoni mwa waumini?" Mtume akajibu:

"Ni yule anayeyakumbuka zaidi mauti na akafanya maandalizi mazuri kwa ajili ya atakayokutana nayo baada ya mauti. Hiyo ndiyo akili ya kweli." (Ibn-i Majah, Zuhd, 31).

Bara ﷺ anasimulia:

"Siku moja tulikuwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika swala ya maiti. Mtume ﷺ akakaa karibu na kaburi na kuanza kulia kiasi kwamba eneo lililomzunguka likaloana kwa machozi yake. Kisha akasema:

❁

"Enyi ndugu zangu! Jiandaeni vizuri na mauti (ambayo yatatufika sote)". (Ibn-Majjah, Zuhd, 19).

Omar ﷺ alimuamuru mmoja wa watumishi wake kumkumbusha maneno yafuatayo kila siku:

"Ewe Omar! Usighafilike na kifo". Hata hivyo nywele nyeupe zilipojitokeza kwenye ndevu zake, alimwambia mtumishi wake:

"Hizi zitasaidia. Kwa sasa ndevu zangu nyeupe zitakuwa ni kikumbusho changu cha mauti kila wakati".

Ukweli ni kwamba hatuna budi kutosahau mauti. Lazima tuyakumbuke mauti ili tuweze kuyamiliki matashi ya nafsi zetu.

Mtume Muhammad ﷺ ametujulisha baadhi ya matukio ya kaburini, siku ya kiama na maisha ya Akhera ili tutafakari na kuchukua mazingatio na kujiandaa kwa ajili ya pumzi yetu ya mwisho, mauti na yatakayofuata baada ya mauti. Baadhi yake ni haya yafuatayo:

"Muislamu anapoingia kwenye maumivu ya mauti, malaika wa rehema wakiwa wamevalia vazi jeupe la hariri wanamtokea na kusema:

"Toka kwenye kiwiliwili chako, huku ukimridhia Mola wako na Mola wako akikuridhia. Kutana na rehema za Mwenyezi Mungu na harufu iliyo nzuri zaidi na Mola wako asiye na ghadhabu na wewe".

Kisha roho inaondoka kwenye kiwiliwili ikifuatana na harufu nzuri ya miski. Malaika wanapokezana mpaka inafikia milango ya mbinguni na kutasemwa:

"Ulioje uzuri wa harufu hii uliyokujanayo kutoka duniani". Kisha wataipeleka kwenye roho nyingine za waumini. Roho hizi za waumini zitafurahia mno kuja kwake kama mtu anavyofurahia kwa kukipata kitu alichokuwa amekipoteza. Watamuuliza:

"Nini kimempata fulani na fulani? Nini kimempata fulani na fulani?" Wanaulizia kuhusu wale walioachwa duniani. Baadhi ya roho zinajibu (kuhusu mmoja miongoni mwa wale walioouliziwa):

"Achana naye. Amejizika mwenyewe kwenye wasiwasi wa dunia". Kisha roho ambayo ndiyo imefika itauliza:

"Fulani amekufa, je hakuja kwenu?" Watajibu:

"Amekufa kweli? Kama ni hivyo, amepelekwa sehemu anayostahiki kwenda, amepelekwa motoni.

Kafiri akiingia kwenye mahangaiko ya mauti, malaika wa adhabu wanamtokea wakiwa na vazi baya lililotengenezwa kwa vinywele vyembamba na kusema:

"Kiache kiwiliwili, kasirika na huku umebeba ghadhabu za Mwenyezi Mungu nenda upesi kwenye adhabu ya Mwenyezi Mungu".

Kisha roho inaondoka huku inatoa harufu mbaya mno. Malaika wanaipeleka kwenye mlango wa ardhi na kusema:

"Ubaya ulioje wa harufu hii!" Kisha wanaipeleka kwenye roho nyingine za makafiri". (Nasai, Janaiz, 9).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ametujulisha yafuatayo:

"Siku ya kiama mwanadamu ataletwa kama mwanakondoo na kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu na kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atamuambia:

"Nilikujaalia neema nyingi na mali nyingi. Nilikushushia hizo fadhila na baraka, umefanya nini katika kurudisha fadhila?" Atasema:

❁

"Ewe Mola wangu! Nilizizidisha, nimeziacha katika kiwango kikubwa mno tofauti na zilivyokuwa. Niruhusu nirudi duniani ili nizirudishe kwako".

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atasema:

"Kwanza nionyeshe ulichotanguliza kwa ajili ya maisha ya Akhera". Atasema tena:

"Ewe Mola wangu! Nilizidisha, nimeziacha katika kiwango kikubwa mno tofauti na zilivyokuwa. Niruhusu nirudi duniani ili nizirudishe kwako".

Haya ni kwa sababu mja huyu hakuwa ametanguliza chochote kizuri. Ndiyo maana atatupwa motoni". (Tirmidhi, Qiyamah, 6/2427).

Hivyo wale waliochezea maisha ya dunia hii kwa upuuzi na hawakufanya maandalizi yoyote kwa ajili ya Akhera watakuwa na mwisho wenye kuhuzunisha. Mwenyezi Mungu mtukufu anatujulisha haya katika Qur'an kama ifuatavyo:

"Na ama atakayepewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake, basi huyo ataomba kuteketea. Na ataingia Motoni. Hakika alikuwa furahani kati ya jamaa zake. Huyo hakika alidhani kuwa hatarejea tena" (Inshiqaq, 84:10-14).

❁

Mfano mwingine wa mwisho mbaya kwa wale waliojiegemeza kwenye utajiri wa dunia, vyeo na madaraka na kuwapelekea kuwa mafedhuli, wenye majivuno na kujiona ni wa Qarun. Mwenyezi Mungu mtukufu anatujulisha kisa chake kilichojaa maonyo kama ifuatavyo:

"Hakika Qaruni alikuwa katika watu wa Musa, lakini aliwafanyia dhulma. Na tulimpa hazina ambazo funguo zake zinawatopeza watu wenye nguvu kuzichukua. Walipomwambia watu wake: Usijigambe! Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanao jigamba. Na utafute, kwa aliyokupa Mwenyezi Mungu, makazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi. Akasema: Kwa hakika nimepewa haya kwa sababu ya elimu niliyonayo. Je! Hakujua kwamba Mwenyezi Mungu keshawaangamiza, katika vizazi vya walio kabla yake, watu waliokuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye, na wenye makundi makubwa zaidi kuliko yake. Na wakosefu hawataulizwa habari ya dhambi zao. Basi akawatokea watu wake katika pambo lake. Wakasema wale waliokuwa wanataka maisha ya duniani: Laiti tungelikuwa tunayo kama aliyopewa Qarun! Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa. Na wakasema wale waliopewa elimu: Ole wenu! Malipo ya Mwenyezi Mungu ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda mema. Wala hawatapewa hayo isipokuwa wenye subira. Basi tukamdidimiza yeye na nyumba yake katika ardhi; wala halikuwepo kundi lolote la

kumnusuru kwa Mwenyezi Mungu, wala hakuwa miongoni mwa wanao jitetea" (Qasas, 28:76-81).

❁

Kisa cha Qarun ni mfano mzuri wa mwisho wa wale wasio wasikivu ambao wanategemea na kutosheka na utajiri wao na madaraka yao hapa duniani na ambao wanasahau kuwa siku moja wao pia watakufa.

Siku moja Mtume ﷺ aliulizwa:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Je tutaweza kumuona Mola wetu siku ya kiama?" Mtume akawauliza:

"Je mmewahi kupata ugumu katika kuliona jua mchana wa siku isiyo na mawingu?"

Walipojibu "Hapana" akawauliza tena:

"Je mnahitaji kusukumana na kupigana vikumbo wakati mnataka kuungalia mwezi katika usiku usio na mawingu?"

❁

Maswahaba hawa walipojibu tena "Hapana, Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu", akasema:

"Naapa kwa yule ambaye roho yangu iko mikononi mwake kwamba hakutakuwa na kusukumana na kupigana vikumbo wakati wa kumuona Mola wenu. Kama msivyohitajika kusukumana na kupigana vikumbo wakati wa kuona jua na mwezi. Hapo mja atakutana uso kwa uso na Mola wake. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atauliza:

"Ewe fulani. Je sikukufadhilisha? Je sikukufanya kuwa bwana wa viumbe vyote? Je sikukupa mke? Je sikuwafanya farasi na ngamia kukunyenyekea? Je sikukufanya kiongozi ili uchukue moja ya nne ya mali kutokana na ngawira?" Mja atajibu:

"Ndiyo Ewe Mola!"

Kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atauliza:

"Kwa hiyo haukufikiria kamwe kuwa utakutana na Mimi?"

Mja atajibu:

"Hapana Ewe Mola"

Kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atasema:

"Kama ni hivyo sasa ni mimi ninayekupuuza. Kama wewe ulivyonisahau duniani"

Kisha mja wa pili atajitokeza mbele ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atamuuliza maswali yale yale. Kisha atamuuliza mja wa tatu maswali yale yale. Kila wakati mja atalazimishwa kukiri kile anachoulizwa na Mola wake.

Kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atasema:

"Je haikukujia kichwani kamwe kuwa utakuja kukutana na Mimi?" Mja atajibu:

"Ewe Mola wangu! Nilikuamini Wewe, vitabu vyako na mitume wako. Niliswali, nilifunga, nilitoa zaka!" Ataendelea kutaja sifa za Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi kadri ya uwezo wake. Mwenyezi Mungu mtukufu na mkuu anasema:

"Kama ni hivyo achia hapo! Kwa sasa shahidi dhidi yako atakuja". Mja atajifikiria mwenyewe:

"Ni nani atakuwa shahidi dhidi yangu?" Kinywa cha mja kitafungwa. Mfupa wake wa paja, nyama yake na mifupa yake itaambiwa: "Sasa ongeeni". Mfupa wake wa paja, nyama yake na mifupa yake itaongea na kutoa ushuhuda wa kila kitu alichowahi kukifanya yule mja. Kwa namna hii mja hawezi kutoa udhuru wowote.

Huyu ni mnafiki ambaye amekutana na ghadhabu za Mwenyezi Mungu". (Muslim, Zuhd, 16).

Mja atawezaje kuficha madhambi yake mahakamani ambapo viungo vyake vyote na ardhi vitakuwa shahidi dhidi yake? Hivyo hatuna budi kuishi kwa umakini mkubwa na uangalifu kama hatupendi kupata aibu siku hiyo.

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Mja atakapowekwa kaburini na watu wake wa karibu kuondoka- akiweza kusikia sauti za hatua zao (wanapoondoka)- malaika wawili watamtokea. Watamkalisha na kumuuliza:

"Ulikuwa ukimfikiriaje Muhammad ﷺ?" Kama aliyeulizwa ni muumini atajibu kama ifuatavyo:

❁

"Nashuhudia kuwa yeye ni mja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!" Watamuambia:

"Angalia sehemu yako motoni. Mwenyezi Mungu ameibadilisha kuwa bustani kutoka peponi". Yule mtu ataangalia na kuona sehemu zote mbili. Kisha Mwenyezi Mungu atafungua dirisha katika kaburi lake ambalo linatazamana na pepo.

Kama mtu aliyeulizwa ni kafiri au mnafiki, atajibu swali la malaika kama ifuatavyo:

"Simjui mtu mnayemuongelea. Mara chache sana nilikuwa nikirudia waliyokuwa wakiyasema wengine". Ataambiwa:

"Hukuelewa na hukufuata". Kisha atapigwa kwa chuma kati ya masikio yake. Atapiga kelele kutokana na maumivu (ya kile chuma) kiasi kwamba viumbe vyote karibu yake (isipokuwa watu na majini) vitamsikia". (Bukhari, Janaiz, 68, 87; Muslim, Jannah, 70).

Siku moja nabii Suleiman , mtoto wa nabii Daudi عليه السلام alipita karibu na mkulima aliyekuwa akilima shamba. Yule mkulima akasema:

"Bila shaka familia ya Daudi imepewa mamlaka makubwa kabisa"

❁

Upepo ukasafirisha maneno haya mpaka kwa Suleiman ambaye upesi alishuka kwenye mnyama wake na kumfuata yule mkulima:

"Nimekusogelea ili usitamani jambo ambalo huliwezi". Kisha akaendelea kuongea:

"Utukuzaji uliofanywa na mja na kukubaliwa na Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi bila shaka ni bora kuliko mali zote na mamlaka iliyopewa familia ya Daudi".

❁

Ukweli ni kwamba, ndani ya dunia hii yenye kupita amali njema tunazofanya kwa moyo safi ndiyo mtaji wetu na furaha katika maisha ya Akhera. Imeelezwa katika Aya tukufu kuwa :

"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie inayo yatanguliza kwa ajili ya Kesho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo habari ya mnayoyatenda". (Hashr, 59:18).

Hakuna namna ya kukimbia mauti. Njia pekee ni kujiandaa nayo. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Nabii Daudi عليه السلام alikuwa na mapenzi katika juhudi zake za dini na heshima yake ilikuwa ya kipekee. Kila alipotaka kuondoka nyumbani kwake alihakikisha anafunga mlango wake vizuri kiasi kwamba hakuna mtu atakayeweza kuingia mpaka arudi. Siku

moja alifunga mlango wake na kuondoka... Aliporudi alimuona mtu amekaa katikati ya nyumba yake. Akamsemesha:

❁

"Wewe ni nani?" Yule mtu akajibu:

"Mimi ni yule asiyemuogopa mfalme, wala hakuna kizuizi kinachoweza kunizuia". Baada ya kusikia haya, Daudi akasema:

"Kwa maana hiyo wewe ni malaika wa mauti. Karibu kwa amri ya Mwenyezi Mungu".

Baada ya muda mfupi roho yake ikachukuliwa na malaika..." (Ahmad, II, 419).

Hivi ndivyo wale walio tayari kwa mauti wanavyomsalimia malaika wa mauti, Izrail...

Uzuri ulioje namna marehemu Najip Fadhil alivyolielezea jambo hili:

(Katika kipindi) ambacho mashuka yanapanda na kushuka (mwenye ufahamu) hana budi kusema "Karibu Izrail".

Hatuna budi kuzitumia neema alizotujaalia Mwenyezi Mungu kwa ajili ya maisha ya akhera wakati bado tuna nafasi na tufanye maandalizi kwa ajili ya tabu za siku ya kiama. Maneno yafuatayo ya hekima kutoka kwa Abu Dharr ﵁ ni muhtasari wa umuhimu na njia ya kujiandaa na mauti na yanayofuatia baada yake:

❁

"Kuna wanahisa watatu katika kipande chochote cha mali. Wa kwanza ni mmiliki, ambaye ni wewe. Wa pili ni mwisho wako. Haukuambii ikiwa utakuletea wema au ubaya kama vile balaa au mauti. Wa tatu ni mrithi wako. Anakusubiri kwa shauku ulaze kichwa chako chini haraka iwezekanavyo, (yani ufe) kisha achukue

mali yako ambayo utaulizwa juu yake. Kama unaweza usiwe dhaifu zaidi miongoni mwa hawa wanahisa!"

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anasema:

لَن تَنَالُواْ الْبِرَّ حَتَّى تُنفِقُواْ مِمَّا تُحِبُّونَ

"Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda". (Al'i Imran, 3: 92).

Hii ndiyo mali ninayoipenda... huyu ngamia. Ili kukutana naye tena peponi, ninamtanguliza (ninamtoa kama sadaka)" (Abu Nuaym, Hilya, I, 163).

Wakati fulani kulikuwa na mwanachuoni maarufu aliyeitwa Ucbas Nureddin Hamza Efendi[69] ambaye alikuwa katika kipindi cha Uthmainiyya. Alikuwa akihifadhi fedha zake kwa sababu alikuwa hawezi kuzitumia. Alikuwa hafungi farasi wake na alikuwa akivaa nguo na viatu vikuukuu. Kwa njia hii alikuwa akihifadhi fedha zake. Ndiyo maana alijulikana miongoni mwa watu kama "Hodja mpenda fedha".

Hodja huyu alijenga Ucbas Madrasa ndani ya Karagumruk na baadaye Ucbas Masjid kwa kutumia fedha alizohifadhi. Aliweka vyumba kwa ajili ya kuishi wanavyuoni na masikini na alitoa vitu vingi kuwa wakfu. Wale waliomfahamu waliposikia haya wakastaajabu na kumdhihaki kwa kusema:

"Hodja, utawezaje kuondoka na mali zako ambazo unazipenda mno?"

Hodja akatoa jibu zuri lifuatalo:

69. Hodja huyu alipewa jina la ukoo kama Ucbas kwa sababu alizaliwa katika kijiji cha Ucbas ambacho ni sehemu ya Karasu. Anatoka kwa wanavyuoni (na alikuwa hakimu). Alikufa mwaka 948/1541. Ili kujua maisha yake na mambo mengine angalia Taskopruzade, As Shaiku'n Numaniyye (thk. A. Suphi Furat), uk 540-541).

"Rafiki zangu wapendwa! Mnasema kweli. Ni Kweli ninapenda fedha. Ndiyo maana sikuweza kuziacha hapa duniani. Hivyo nimezitanguliza kesho Akhera".

❁

Ali ﷺ anasema:

"Dunia imetupa mgongo na inaondoka. Akhera ipo mbele yetu na inatusubiri. Kila moja ina watoto wake (wafuasi). Kuweni wafuasi wa Akhera, na si wa dunia. Leo ni wakati wa kufanya amali njema, wakati hakuna hesabu. Kesho ni wakati wa hesabu, wakati ambao hakutakuwa na nafasi nyingine ya kufanya mambo mema". (Bukhari, Rikak, 4).

Kama inavyokuwa kwa mwanafunzi ambaye anaondoka kwenye chumba cha mtihani ambapo hawezi tena kujibu maswali zaidi wala hawezi kujiongezea daraja...

Kutokana na kunufaika kwa maneno ya Ali, baadhi ya marafiki wa Mwenyezi Mungu wanasema yafuatayo:

" Dunia imetupa mgongo na inaondoka wakati Akhera inakuja kwetu. Kustaajabisha kulikoje kwa yule ambaye anakifuata kile kilichompa mgongo na kuondoka, lakini bado yeye anaendelea kukifuata na kupuuzia kile kinachomfuata..."

❁

Abu Darda ﷺ alikuwa akisema:

"Nahofia kuwa mtamezwa na neema ambazo zinampenda mtu na kuchukuliwa na matamanio ya siri. Matamanio haya yanaongezeka unapojaza tumbo kwa chakula ingawa una njaa ya elimu. Mbora wenu ni yule anayemshauri rafiki yake kama ifuatavyo:

"Tufunge kabla hatujafa"

Mbaya miongoni mwenu ni yule anayemuambia rafiki yake:

"Njoo tujifurahishe kabla ya kufa. Tule, tunywe na kufurahia maisha kadri tuwezavyo..." (Abu Nuaym, Hilya, I, 218).

❁

Mgongo wa Sufyan-i Sevri ulipinda akiwa na umri mdogo. Alikuwa akiwaambia yafuatayo wale waliotaka kujua sababu:

"Nilikuwa na mwalimu ambaye nilikuwa nikijifunza kutoka kwake. Ingawa nilijaribu kumshawishi aseme agano la imani wakati anakufa lakini hakuweza kulisema. Nilipoona hali hii mgongo wangu ukapinda".

Tofauti na mitume, hakuna mwenye uhakika na mwisho wake. Nabii Yusuf عليه السلام alimuomba Mwenyezi Mungu mtukufu:

" ... (Ewe Mwenyezi Mungu!)... Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na nichanganyishe na watendao mema" (Yusuf, 12:101).

Yusuf kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu kunaonyesha kuwa hata mitume walikuwa wakihofia mwisho wao. Ndiyo maana muumini hana budi kufanya juhudi kwa matumaini na hofu na kuipa Akhera kipaumbele.

Siku moja Shakik-i Belhi alipopita karibu na makaburi aliyaangalia kwa tahadhari na kuwaambia wale waliokuwa pamoja naye:

"Wengi miongoni mwa hawa sasa wamegundua kuwa dunia iliwadanganya..."

"Kwa nini?" walimuuliza. Akajibu:

"Kwani hawafikirii kuwa wakati wanaishi walikuwa na mali, utajiri, nyumba, vipando, ndugu, mabustani na mashamba? Lakini sasa mnaona kuwa hayo si ya kweli..."

❁

Tukio lifuatalo kutoka kwa rafiki wa Mwenyezi Mungu, Rabi bin Haysem (q.a) ni mfano mzuri unaoonyesha namna mtu anavyotakiwa mara kwa mara kuiihesabu *nafsi* yake ili kujiandaa na kifo na Akhera:

Siku moja Rabi bin Haysem alichimba kaburi nyuma ya kitalu chake. Inapofika wakati akahisi kuwa moyo wake umekuwa mgumu, anaingia kwenye hili kaburi na kulala kwa muda mfupi. Alikuwa akitafakari kuwa siku moja ataiacha hii dunia na kuachwa katika hali ambayo atahitaji msaada na kukubali kutoa sadaka wakati yupo ndani ya kaburi. Alitafakari kuwa angelitakiwa kuyahesabu matendo yake kwa ajili ya Akhera, kisha alianza kuomba msamaha.

Kisha alikuwa akisoma Aya ifuatayo:

حَتَّى إِذَا جَاء أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ارْجِعُونِ لَعَلِّي أَعْمَلُ صَالِحاً فِيمَا تَرَكْتُ

"Mpaka yanapomfikia mmoja wao mauti, husema: Mola wangu Mlezi! Nirudishe. Ili nitende mema sasa badala ya yale niliyoyaacha. Wapi! Hii ni kauli aisemayo yeye tu. Na nyuma yao kipo kizuizi mpaka siku watapofufuliwa" (Mu'minuun, 23:99-100).

Alikuwa akitoka kwenye lile kaburi anajiambia mwenyewe:

"Ewe Rabi! Angalia, leo umerudishwa kwenye uhai. Itafikia wakati ambao ombi lako hili halitakubaliwa na hivyo hutarudishwa tena duniani. Chukua tahadhari sasa na ongeza amali zako njema, harakati zako za dini na maandalizi yako kwa ajili ya Akhera..."

Uzuri ulioje wa ushauri ufuatao kutoka kwa Imam Ghazzali:

"Kila siku baada ya kuswali swala ya Alfajiri na kabla ya kuanza siku mpya, kila muumini hana budi kukutana uso kwa uso na roho yake mwenyewe na kufunga nayo baadhi ya mikataba na

kuweka nayo makubaliano juu ya masharti kadhaa. Kama mfanya biashara anavyomuachia mtaji mwenzake na kuingia naye mkataba. Lakini haachi kumtahadharisha juu ya baadhi ya mambo. Pia mwanadamu hana budi kuitahadharisha roho yake yafuatayo:

❁

"Mtaji wangu ni uhai wangu. Uhai wangu ukiniondokea, mtaji wangu utakuwa umeisha na faida itakuwa imefikia kikomo. Hata hivyo hii ni siku mpya. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amenifadhilisha na kunipa hii siku. Kama angekuwa amechukua uhai wangu ningelitamani nirudishwe na kupewa angalau siku moja ili niweze kufanya amali njema. Sasa fanya kana kwamba uhai wako ulichukuliwa na sasa umerudishwa. Hivyo leo usifanye maasi wala matendo mabaya na usitumie vibaya siku hii. Kwani kila pumzi ni baraka usiyoilipia.

❁

Jua vizuri kwamba siku ina masaa 24 kwa usiku wake na mchana wake. Siku ya kiama, Masanduku 24 yaliyofungwa kwa ajili ya kila siku yatawekwa mbele ya mtu. Moja miongoni mwake litakapoletwa mbele na kufunguliwa, mja ataliona limejaa nuru kama malipo kwa matendo yake mema aliyoyafanya ndani ya lisaa lile. Atayafurahia sana yale malipo aliyolipwa na Mwenyezi Mungu na kufikiria kuwa kama furaha ile ingeligawanywa na kupewa watu wa motoni wasingelihisi maumivu (yake). Sanduku la pili litakapofunguliwa na kukutwa limejaa kiza na harufu mbaya, saa hili ni lile mja alilopitisha kwa kibri. Mja atahuzunika mno kiasi kwamba kama huzuni hii ingeligawanywa miongoni mwa watu wa peponi wasingelihisi furaha yake kutokana na huzuni yake. Sanduku la tatu litafunguliwa na kukutwa liko tupu. Hili linaonyesha muda ambao mja aliutumia kwa kulala au kufanya mambo ya halali. Hata hivyo siku hiyo ambayo kutakuwa na hitajio la malipo hata kutokana na amali ndogo kabisa, mja ataumia kwa majuto, atau-

mia zaidi ya mfanyabiashara ambaye amepoteza faida kubwa ingawa ana vitega uchumi tele na atapata maumivu zaidi kwa kuupoteza muda ule bila ya faida yoyote.

Hivyo, ewe nafsi unayeamrisha maovu! Jaza sanduku lako vizuri wakati bado una nafasi na usithubutu kuliacha tupu. Usijiingize kwenye uvivu usije ukaanguka kwenye kina kirefu kuliko vyote!"

Halid-i Baghdadi, ambaye alifikia kilele cha sayansi ya ndani na nje aliishi maisha yake yote akiwa na shauku juu ya pumzi yake ya mwisho. Ameandika yafuatayo katika *Maktubat* yake:

❁

"... Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi kuwa siamini kuwa nimewahi kufanya amali njema hata moja ambayo inakubalika mbele ya Mwenyezi Mungu kuanzia siku niliyozaliwa na mama yangu mpaka leo. (Bado ninaomba rehema za Mola wangu). Kama huioni roho yako kama iliyofilisika wakati unafanya matendo mazuri, basi hicho ni kilele cha ujinga..." [70]

Kipande kifuatacho kutoka kwenye barua aliyomtumia rafiki yake ni kielelezo cha shauku ya kujiandaa na pumzi yeke ya mwisho:

"... Natumaini utafungamana na mambo yatakayohitajika wakati wa pumzi ya mwisho, kwamba unatekeleza mambo yako kulingana na mwenendo wa Mtume, kwamba huegemei mambo yenye kuvutia ndani ya dunia hii yenye kupita, na kwamba husahau kumuombea mja huyu dhaifu. Muombee awe na mwisho mwema na wenye manufaa kwa kumjaalia imani moyoni mwake na kuishi kulingana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu". (Mektubat-I Mawlana Halid, p 175).

❁

70. Halid-I Baghdadi, Mektubat-I Mawlana Halid, Istanbul, 1993, pg 178).

Hivyo marafiki wakubwa wa Mwenyezi Mungu kamwe hawakutegemea amali zao na hivyo walitafuta rehema na msamaha wa Mwenyezi Mungu walipozingatia pumzi yao ya mwisho. Hivyo, hatupaswi kutegemea ufahamu wetu au matemdo yetu, bali tunapaswa wakati wote kumuomba Mwenyezi Mungu mtukufu atujaalie mwisho mwema.

Wakati fulani kulikuwa na mtu aliyekuwa akiendesha duka ambalo lipo kwenye lango la kutokea nje ya mji. Kila mazishi yanapopita katika lango lile huyu mtu alikuwa akitumbukiza mbegu ndani ya birika lililokuwa karibu naye na mwisho wa mwezi alikuwa akihesabu mbegu zile na kusema:

"Mwezi huu, watu wengi kiasi hiki wametumbukia kwenye birika hili".

Na ni siku ile ile ambayo na yeye alifariki. Baada ya muda mfupi rafiki yake, ambaye hakuwa na taarifa juu ya kifo chake alikuja kumtembelea. Alipomkosa aliwauliza majirani zake:

"Nini kimempata mmiliki wa duka hili?"

Wakasema:

"Na yeye pia ametumbukia ndani ya birika"...

Tunapata mafunzo gani... Tusisahau kuwa kila mtu ataingia ndani ya birika la mauti... Huwa watu wanawaangalia wenzao wakielekea kwenye maisha ya milele mmoja baada ya mwingine, lakini wanapuuzia na kuona kuwa vifo vyao viko mbali, mbali sana...

Mtumishi wa Yavuz Sultan Selim Han, Hasan Can anasimulia:

"Kila Sultan Yavuz alipotokwa na jipu mgongoni mwake, jipu hilo liliongezeka ndani ya muda mfupi na kusababisha tundu kubwa. Liliongezeka kiasi kwamba tuliweza kuona ini lake kwa kupitia tundu hilo. Alikuwa akipata maumivu makubwa mno.

Alikuwa kama simba aliyejeruhiwa. Lakini hakukubali udhaifu wake na hivyo aliendelea kutoa amri na maelekezo kwa askari wake. Nikamsogelea na akaniuliza yafuatayo huku anaashiria hali yake:

"Hassan Can, hii ni hali gani?"

Nikahisi kuwa safari yake ya mauti imefika na anakaribia kuanza maisha ya Akhera. Ndiyo maana kwa huzuni kubwa, na maumivu ya utengano yakiunguza moyo wake, nikamwambia:

"Sultan wangu, Nafikiri muda wa kukutana na Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi umefika".

Sultan akanigeukia kwa kustaajabu na kusema:

"Hassan, Hassan! Unadhani nilikuwa na nani mpaka wakati huu? Je umeona kasoro yoyote (katika uhusiano) wangu na Mwenyezi Mungu mtukufu?"

Huku nikihisi aibu kutokana na maneno haya nikasema:

"(Mwenyezi Mungu aharamishe hayo) Sultan wangu! Sikumaanisha hayo. Nilikuwa najaribu kukushauri, kama tahadhari kuwa muda huu ulionao unaweza kuwa tofauti na nyakati nyingine".

Huyu Sultan mkubwa, akiwa amezama kwenye ulimwengu mwingine, akanihutubia yafuatayo kwa mara ya mwisho:

"Hassan! Soma surat *Yasin*".

Huku macho yangu yakiwa yamejawa na machozi nikaanza kusoma. Nilipofika kwenye Aya "Salam (amani)" roho njema ya Sultan ikaenda kwa Mola wake.

Kwa ujumla, wale wasio karibu na Mwenyezi Mungu katika maisha yao hawahusiki katika fadhila za aina hii katika pumzi zao za mwisho. Ndiyo maana hatuna budi kuishi kwa malengo ili kufa vizuri.

Sultan Murad II alikuwa ni mtu asiyefikiria matashi yake binafsi bali kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Alikuwa na msimamo mkubwa na kujitambua kiasi kwamba hakusita kupoteza uhai wake kwa ajili ya mwisho mwema. Jambo kubwa kwake lilikuwa ni kutoa pumzi yake ya mwisho akiwa na imani moyoni mwake na kuweza kupelekwa mbele ya Mwenyezi Mungu katika siku ya kiama akiwa hana lawama wala madhambi. Baada ya kupata mtoto wa kiume na wa kike akamuambia kiongozi wake, Candarli Ibrahim Pasha:

"Ewe Candarli! Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu tuliye naye, kwa mapenzi yake, amewashughulikia watoto wetu hapa duniani. Kilichobaki kwetu ni kuiaga hii dunia tukiwa na imani nyoyoni mwetu..."

Afisa Muzaffer, ambaye alionyesha mafanikio makubwa katika vita kwa ajili ya Dardanelles, baadaye alienda upande wa mashariki ambapo alipambana kwa matumaini makubwa. Alipokuwa akipambana ndani ya vita hivi alijeruhiwa vibaya mno. Katika nyakati zake za mwisho ambapo sauti yake haikuweza kutoka tena, alichukua bahasha kutoka kwenye mfuko wake. Kisha akaokota kijiti na kukichovya kwenye damu iliyokuwa ikitiririka kutoka kwenye jeraha lake na kuanza kuandika yafuatayo:

"Qibla (uelekeo wa Makka) kiko upande upi?"

Kwa kugundua kuwa anakaribia kukata roho, wale waliomzunguka walikubaliana na ombi lake na kumuelekezea *Qibla*. Wakati wa kifo chake, kama jitihada zake za mwisho, Afisa aliwapa askari wake waliokuwa mashujaa ujumbe ufuatao. Upande mmoja, furaha ya kuungana na Mola wake ilikuwa imejaa uso wake na kwa upande mwingine alikuwa na mfadhaiko na wasiwasi juu ya jukumu tukufu alilopewa la kuilinda nchi yake:

"Kikosi cha askari kiendelee kwenye Jihad kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; Msifanye kifo changu kikawa ni hasara..."

Alikuwa akitaka kuandika ujumbe wake wa tatu lakini muda wake ulikuwa umeisha. Akawa amekufa kwa ajili ya Mola wake.

Ni ujasiri ulioje uliomfanya achukua damu kutoka kwenye mishipa yake wakati ulimi wake umeshindwa kuongea, ili aelezee hitajio lake la kuelekea Makka wakati roho yake inatoka. Na hivyo mwisho wa maisha ya mtu aliyeishi kwa kufuata njia ya Mwenyezi Mungu unakuwa mwema na uliobarikiwa.

Hali ya mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu, Mahmud Sami Ramazanoglu, katika nyakati zake za mwisho ni mfano mwingine mzuri kwetu. Sami Efendi alikuwa ni rafiki wa Mwenyezi Mungu ambaye moyo wake ulikuwa umejaa mapenzi ya Mtume. Kama inavyokuwa kwa mtu anayetembea kwenye theluji anavyoacha alama zake za miguu kwenye theluji; na kisha mtu anayejaribu kutafuta njia yake akafuata alama zile, ndivyo Sami Efendi alivyoishi, aliishi kwa imani huku akifuata nyayo za Mtume. Kwa kuonyesha haya alibarikiwa kwa kufa kama Mtume, ambaye alitumia muda wote wa maisha yake kumfuata kwa mapenzi na shauku. Wakati wa kifo chake ulikuwa ni wakati ambao mwito wa swala ya *tahajjud* (swala ya usiku) ulisomwa. Wale waliokuwa naye katika nyakati zile za mwisho walisikia maneno yafuatayo kutoka kinywani mwake:

"Allah, Allah, Allah!"...

Haikuwa ulimi wake tu, bali mwili wake wote, pamoja na seli zake na roho yake viliendelea kuita "Allah"...

Kwa kifupi, ili mja kuwa na mwisho mwema, yaani kuvuta pumzi yake ya mwisho akiwa na imani moyoni mwake, kwanza hana budi kutwaharisha roho yake na moyo wake. Lazima avitoe kwenye mambo mabaya na kuvifanya vipambwe kwa tabia njema

na kudhihirisha majina mazuri ya Mwenyezi Mungu mtukufu. Kwa moyo kufikia hali hii ya uchamungu ni zawadi nzuri mno ya uongofu katika safari hii ya maisha. Mistari ifuatayo kutoka kwa Jalaluddin al Rumi inaelezea chanzo cha usafi wa moyo:

"Makaburi yenu hayatengenezwi kwa mawe wala pamba wala mikeka. Hamna budi kuchimba makaburi yenu wenyewe ndani ya nyoyo zenu zisizochafuliwa na ndani ya usafi wa ndani ya dunia yenu, ili msiwe na malalamiko yoyote mbele ya Mwenyezi Mungu mtukufu".

Hivyo ni muhimu kujiandaa kwa ajili maisha ya Akhera katika njia bora kadri iwezekanavyo, na kwa roho iliyotakasika, kwa ibada, utii, kutenda mambo mema na kutoa.

Katika pumzi ya mwisho ya mja, Mwenyezi Mungu mtukufu anampa bishara njema ikiwa ni mja aliyeyapamba maisha yake kwa amali njema na ambaye kamwe hakumsahau Mola wake katika maisha yake yote:

"Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa" (Fussilat 41:30).

Mwenyezi Mungu atubariki sisi sote kwa kutujaalia kuwa wapokezi wa bishara hizi njema. Amin!...

FOR FREE IN PDF FORMAT

ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT

1350 BOOKS IN **60 LANGUAGES** FOR FREE

Islamic books in different languages are waiting
for you in PDF format at the web site
www.islamicpublishing.org

ERKAM PUBLICATIONS | islamicpublishing.org |